

# Sifa Ya SWALAH YA MTUME

صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

Kutoka Mwanzo Mpaka Mwisho Kama Kwamba  
Unaiona

*“Swalini Kama Mliyoniiona Nikiswali”*  
[Al-Bukhaariy]

صِفَةُ صَلَاةِ النَّبِيِّ  
صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ  
مِنَ التَّكْبِيرِ إِلَى التَّسْلِيمِ كَأَنَّكَ تَرَاهَا

Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy

Mfasiri:

Abu ‘Abdillaah Muhammad Saalim Sa’iyd  
Baawazir

## # صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Sifa ya Swalah ya Mtume

---

Tafsiri ya Kitabu

*Swifat-us Swalatin-Nabbiy صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Min At-Takbiyr Ilaa At-Tasliym Ka-anaka Taraaha*

©Abu 'Abdillaah Muhammad Saalim Sa'iyd Baawazir

Chapa Ya Nne

Nakala 5,000

Kimefasiriwa Kutoka Kiarabu Na:

Abu 'Abdillaah Muhammad Saalim Sa'iyd Baawazir

**يوزع مجاناً ولا يباع Kinagaiwa Bure Hakiuzwi**

Haki Zote Zimehifadhiwa, Hairuhusiwi Kupiga Chapa Kitabu Hiki Kwa Jinsi Yoyote Ile Bila Idhini Ya Mfasiri Na Wachapaji Kwa Maandishi.

YALIYOMO

Utangulizi Wa Chapa Ya Nne .....	12
Utangulizi Wa Mfasiri .....	13
Historia Fupi Ya Shaykh Al-Albaaniy .....	17
Kuzaliwa Na Kukua Kwake .....	18
Kujifunza Kwake Elimu Ya Hadiyth.....	19
Wanafunzi Wake Maarufu .....	22
Vitabu Vyake.....	23
Fadhila Na Mema Yake .....	25
Elimu Yake Na Athari Yake Kwa Watu .....	26
Sifa Njema Walizotoa Ma’ulamaa Kwa Mujaddid Wa Zama Hizi Shaykh Muhammad Naaswir-Ud-Diyn Al-Albaaniy (Allaah Amrehemu).....	27
Shaykh ‘Abdul-‘Aziyz Bin Baaz [Aliyekuwa Mufti Wa Saudi Arabia] (Allaah Amrehemu).....	27
Mwanachuoni Shaykh Muhammad Ibn Swaalih Al-‘Uthaymiyn (Allaah Amrehemu).....	28
Mwanachuoni Mfasiri Shaykh Muhammad Al-Amiyn Ash-Shanqiyytwiy (Allaah Amrehemu).....	29
Shaykh ‘Abdul-Muhsin Al-‘Abaadiy (Allaah Amhifadhi).....	29

Mufti Wa Zamani Wa Saudia Mwanachuoni Shaykh Muhammad Bin Ibraahiym Aal Shaykh (Allaah Amrehemu)	30
Mwanachuoni Shaykh Muqbil Al-Waadi'iy (Allaah Amrehemu) .....	30
Mwanachuoni Wa Hadiyth India, Shaykh 'Abdus-Swamad Sharafud-Diyn (Allaah Amrehemu) .....	31
Waziri Wa Masuala Ya Kiislamu, Al-Awqaaf, Ulinganio Na Uongozi Shaykh Swaalih Bin 'Abdil-'Aziyz Bin Muhammad Aali Shaykh .....	31
Kipindi Cha Mwisho Cha Maisha Yake Na Kifo Chake.....	32
Utangulizi.....	34
Sababu Za Kuandika Kitabu Hiki Na Baadhi Ya Vipengele Vyake .....	39
Manhaj Ya Kitabu Hiki .....	42
Kauli Za Maimaam Wanne Kuhusu Kushikamana Na Sunnah Na Kuacha Kufuata Rai Zao .....	45
Wasemavyo Maimaam.....	45
1- Abu Haniyfah (رحمه الله) .....	45
2- Maalik Bin Anas (رحمه الله).....	48
3- Ash-Shaafi'iy (رحمه الله).....	50
4- Ahmad Bin Hanbal (رحمه الله) .....	54

Wafuasi Wa Maimaam Wanatakiwa Kuacha Rai Zao (Maimaam) Ikiwa Zinapingana Na Sunnah .....	57
Shubuhaat (Mambo Yenye Utata) Na Majibu Yake .....	60
1- Baadhi Yao Wanasema: .....	61
Nitalijibu Swali Hili Kwa Pande Mbili:.....	61
Kwanza: .....	61
2- Shub-ha Ya Pili, Wengine Wanasema:.....	63
3- Shub-ha Ya Tatu, Wengine Wanadai: .....	72
4- Shub-ha Ya Nne:.....	74
Tanbihi Ya Mfasiri .....	78
Swalah Ya Mtume (صلى الله عليه وسلم).....	79
Kuelekea Ka'abah.....	80
Kusimama Katika Swalah.....	83
Swalah Ya Mgonjwa Katika Hali Ya Kukaa .....	84
Swalah Ndani Ya Meli (Chombo Cha Baharini) .....	86
Kukaa Na Kusimama Katika Swalah Ya Usiku (Tahajjud) ....	86
Swalah Kwa Kuvaa Viatu Na Maamrishi Ya Kufanya Hivyo87	
Swalah Juu Ya Minbar.....	89

<i>Sutrah</i> Na Kuwajibika Kwake .....	89
Yanayokata (Yanayovunja) Swalah.....	93
Swalah Kulielekea Kaburi.....	93
<i>Takbiyrah</i> .....	94
Kunyanyua Mikono .....	95
Kuweka (Kufunga) Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kushoto Na Kuamrisha Kwake .....	96
Kuweka Mkono Juu Ya Kifua .....	96
Kutazama Mahali Pa Kusujudu Na Khushuu (Unyenyekevu) .....	98
Du'aa Za Kufungulia .....	98
Kisomo ( <i>Tilaawah</i> ) .....	108
Kusoma Aayah Moja Moja .....	109
Ulazima (Ufaradhi) Wa <i>Al-Faatihah</i> Na Fadhila Zake .....	111
Kufutwa Kisomo Nyuma Ya Imaam Katika Swalah Za <i>Jahriyyah</i> (Swalah Za Kunyanyua Sauti) .....	114
Kuwajibika Kusoma Katika Swalah Za <i>Sirriyyah</i> .....	116
(Swalah Za Kimya) .....	116
Aamiyn, Imaam Kunyanyua Sauti Anapoileta.....	117

Kisomo Chake (صلى الله عليه وآله وسلم) Baada Ya <i>Al-Faatihah</i> ...	119
Kuchanganya Kwake (صلى الله عليه وآله وسلم) Baina Ya Surah Zinazofanana Na Nyinginezo Katika Rak'ah.....	122
Ruhusa Ya Kusoma <i>Al-Faatihah</i> Pekee .....	124
Kunyanyua Sauti Na Kusoma Kimya Kimya Katika Swalah Tano Na Nyenginezo .....	126
Aliyokuwa Akisoma (صلى الله عليه وآله وسلم) Katika Swalah Mbali Mbali .....	128
1- Swalah Ya Alfajiri .....	129
Kisomo Katika Sunnah Ya Alfajiri .....	132
2- Swalah Ya Adhuhuri .....	133
Kisomo Chake (صلى الله عليه وآله وسلم) Cha Aayaat Baada Ya <i>Al-Faatihah</i> Katika Rak'ah Mbili Za Mwisho .....	135
3- Swalah Ya Alasiri .....	137
4- Swalah Ya Maghrib.....	138
Kisomo Katika Sunnah (Baada Ya Swalah) Ya Magharibi ...	139
5- Swalah Ya 'Ishaa.....	140
6- Swalah Ya Usiku .....	142
7- Swalah Ya Witr .....	148

8 - Swalah Ya Ijumaa.....	150
9 - Swalah Za 'Tyd Mbili.....	152
10 -Swalah Ya Janaazah .....	153
Kusoma Kisomo Vilivyo Na Kuitengeneza Sauti Unaposoma .....	153
Kumsahihisha Imaam.....	157
Kujikinga Na Shaytwaan Kwa Kutema Mate Kidogo Wakati Wa Swalah Ili Kuondosha Wasiwasi.....	157
Kurukuu .....	158
Sifa Ya Rukuu.....	159
Ulazima Wa Kutulia Katika Rukuu.....	160
Adhkaar Za Rukuu.....	162
Kuirefusha Rukuu .....	166
Kukatazwa Kusoma Qur-aan Katika Rukuu .....	166
Kusimama (Kuitadili) Kutoka Katika Rukuu Na Anachokisema Ndani Yake .....	167
Kurefusha Kisimamo Hiki Na Wajibu Wa Kutulia Ndani Yake .....	174
Kusujudu.....	176



Kwenda Chini Kusujudu Kwa (Kutanguliza) Mikono .....	176
Wajibu Wa Kutulia Katika <i>Sujuud</i> .....	181
Adhkaar Za <i>Sujuud</i> .....	182
Kukatazwa Kusoma Qur-aan Katika <i>Sujuud</i> .....	186
Kurefusha <i>Sujuud</i> .....	187
Fadhila Za <i>Sujuud</i> .....	188
Kusujudu Juu Ya Ardhi Na Juu Ya Jamvi 0.....	189
Kuinuka Kutoka Kwenye <i>Sujuud</i> .....	190
Kikao Baina Ya <i>Sajdah</i> Mbili (Kikao Cha <i>Iftiraash</i> ) .....	192
<i>Al-Iq'aa</i> u (Kusimamisha Miguu Huku Umekalia Visigino) Baina Ya <i>Sajdah</i> Mbili .....	192
Wajibu Wa Kutulia Baina Ya <i>Sajdah</i> Mbili .....	193
Adhkaar (Utajo) Baina Ya <i>Sajdah</i> Mbili .....	193
Kikao Cha Mapumziko .....	195
Kuitegemea Mikono Miwili Katika Kuinuka .....	196
Ulazima Wa Kusoma Suratul - Faatihah Katika Kila Rak'ah .....	196
Tahiyaatu ( <i>Tashahhud</i> ) Ya Kwanza.....	197

Kutikisa Kidole Katika <i>Tashahhud</i> .....	199
Wajibu Wa <i>Tashahhud</i> Ya Kwanza Na Hukumu Ya Du'aa Ndani Yake.....	201
Matamshi Mbali Mbali Ya <i>Tashahhud</i> .....	202
Kumswalia Mtume Pahala Pake Na Matamshi Yake Mbali Mbali .....	208
Faida Muhimu Za Kumswalia Mtume Wa Ummah 'Swalaatu 'Alan Nabbiy .....	214
Faida Ya Kwanza.....	214
Faida Ya Pili .....	219
Faida Ya Tatu .....	224
Faida Ya Nne.....	230
Faida Ya Tano .....	231
Faida Ya Sita .....	231
Kusimama Kwa Ajili Ya Rak'ah Ya Tatu, Kisha Ya Nne.....	232
<i>Qunuu</i> t An-Naazilah Katika Swalah Tano ( <i>Qunuu</i> t Wakati Waislamu Inapowafikia Janga, Au Maafa) .....	233
<i>Qunuu</i> t Katika Swalah Ya Witr.....	235
<i>Tashahhud</i> Ya Mwisho.....	237
Wajibu Wa <i>Tashahhud</i> Hii.....	237

## # صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ Sifa ya Swalah ya Mtume

---

Wajibu Wa Kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) .....	238
Wajibu Wa Kujikinga Kutokana Na Mambo Manne Kabla Ya Kuomba Du'aa.....	238
Kuomba (Du'aa) Kabla Ya Kutoa Salaam Na Aina Zake .....	239
<i>Tasliym</i> (Kutoa Salaam) .....	247
Wajibu Wa <i>Tasliym</i> (Kutoa Salaam).....	250
Hitimisho.....	250
Vitabu Alivyotumia Mwandishi Kwa Marejeo.....	252

## Utangulizi Wa Chapa Ya Nne

Baada ya kumalizika chapa za mwanzo za kitabu hiki bila kutosha kukidhi mahitaji ya Ummah wa wanaozungumza lugha ya Kiswahili sehemu nyingi duniani, na kuonekana kinahitajika zaidi na zaidi na maombi ya wengi waliopenda mafunzo haya yaenee sehemu mbalimbali zaidi, tumeonelea tena tukichape nakala nyingi zaidi katika chapa hii ya nne.

Kwa Tawfiyq ya Allaah (سبحانه وتعالى) kumetokeza wahisani na wapendao mafunzo sahihi ya Dini hii kuenea, wakaomba wajitolee kuchapa nakala zaidi kwa gharama zao ili kujaribu kutekeleza maombi na mahitaji ya wengi hususan walio nje ya Afrika Mashariki ambao ni nadra sana kwao kupata mafunzo ya Dini yao kwa lugha hii huko walipo maeneo ya Bara la Amerika, Ulaya na Asia.

Si rahisi kukidhi kiu na mahitaji ya Waislamu walio Afrika Mashariki, lakini tutajitahidi zaidi ya nusu ya chapa hii kuwafikia wao hususan walio maeneo ya nje ya miji ambao hawawezi kumudu gharama za ununuzi wa vitabu na ambao upatikanaji wa maandiko ya Dini ni haba kwao.

## Utangulizi Wa Mfasiri

Hakika shukurani ni Zake Allaah (سبحانه وتعالى), tunamshukuru Yeye, na kumtaka msaada, na tunamuomba Yeye msamaha. Tunamuomba Allaah (سبحانه وتعالى) Atulinde na shari za nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu. Anayeongozwa na Allaah (سبحانه وتعالى) hakuna wa kumpoteza, na anayepotezwa na Allaah (سبحانه وتعالى) basi hakuna wa kumuongoza.

Na nashuhudia kuwa hakuna apasaye kuabudiwa ila Allaah (سبحانه وتعالى), Ni Mmoja tu Asiye na mshirika. Na nashuhudia kuwa Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) ni mja Wake na ni Mjumbe Wake. Rahma na Amani za Allaah zimshukie yeye, jamaa zake, Swahaba zake, na wote waliotangulia kwa wema hadi siku ya mwisho.

Ama ba'ad,

Namshukuru tena Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii kwa Lugha ya Kiswahili, kazi ambayo naamini sana kuwa itawanufaisha sana Waislam wazungumzaji wa lugha hii na kuweza kuwasaidia kupata mafunzo sahihi ya 'Ibaadah hii adhimu ambayo itakuwa ni jambo la kwanza kabisa kwa mja kuulizwa kwalo siku ya Hesabu.

Umuhimu wa kitabu hiki ni mkubwa sana, haswa kwa kuwa ni kitabu kilichoelezea 'Ibaadah hii ya Swalah kwa mapana na marefu na kwa dalili sahihi zilizothibiti kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Ni kitabu kwa mwenye kutaka kujua ilivyokuwa Swalah ya kipenzi chetu (صلى الله عليه وآله وسلم) kama alivyosema: **((Swalini kama mlivyoniwa nikiswali))**.<sup>1</sup> Basi anapaswa kuwa nacho kwenye nyumba yake.

---

<sup>1</sup> Al-Bukhaariy

Hiki ni kitabu cha Swalah kilichoenea na kuuzika kwa wingi sana labda kuliko vitabu vyote vya Swalah vilivyowahi kuandikwa. Ni kitabu chenye mauzo makubwa katika nchi za Kiarabu kwa mujibu wa wachapishaji wa kitabu hicho. Hali kadhalika kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza na kimeuzwa na kinaendelea kuuzika kwa wingi katika nchi za Ulaya na haswa Uingereza. Nimeonelea manufaa hayo yasiwaenee tu wenye kuzungumza Kiarabu na Kiingereza pekee, bali na jamii yetu ya wazungumzao Kiswahili.

Swalah ina fadhila kubwa sana, hivyo kukosa kuswali ni kosa kubwa. Swalah ni 'amali ya kwanza itakayokaguliwa Siku ya Qiyaamah na ndio ufunguo wa Pepo. Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

((**'Amali ya mwanzo atakayoulizwa Muislamu Siku ya Qiyaamah kuwa kaitekeleza-na kaitekeleza vilivyo-ni Swalah. Ikiwa aliitekeleza vilivyo basi kunatarajiwa atafaulu. Ikiwa hakuitekeleza au kaitekeleza, lakini sivyo ndivyo, basi itatazamwa Swalah za Sunnah, kama alizitekeleza vilivyo. Ama ikiwa hana hata Sunnah au kaitekeleza sivyo ndivyo, basi keshapata khasara**))<sup>2</sup>

Amesema tena (صلى الله عليه وآله وسلم):

((**Funguo za kufungulia milango ya Peponi ni Swalah**))<sup>3</sup>

Ubaya wa kuacha Swalah ni mkubwa sana kwani Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema:

﴿ خَلْفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهْوَاتِ فَسَوْفَ

يَلْقَوْنَ غِيًّا ﴾

---

<sup>2</sup> Ahmad, Abu Daawuud, at-Tirmidhiy, an-Nasaaiy na Ibn Maajah.

<sup>3</sup> Muslim.

**((Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Swalah, na wakafuata matamano. Basi watakuja kuta adhabu ya moto))<sup>4</sup>**

Na kadhalika Anasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kutaja habari za wasioswali pindi watakapoulizwa sababu yao ya kuwepo motoni:

﴿ مَا سَلَكَكُمْ فِي سَقَرٍ ﴿٤٢﴾ قَالُوا لَمْ نَكُ مِنَ الْمُصَلِّينَ ﴿٤٣﴾ ﴾

**((Ni nini kilichokupelekeni motoni? Waseme: Hatukuwa miongoni waliokuwa wakiswali))<sup>5</sup>**

Na Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**((Kizuizi kilichoko baina ya mtu na ukafiri ni Swalah))<sup>6</sup>**

Kadhalika akaeleza ubaya wa mtu kutokuswali na kumfananisha na kafiri:

**((Tofauti baina yetu Waislamu na wasio Waislamu ni Swalah))<sup>7</sup>**

Baada ya kujua masuala hayo muhimu kutoka katika Kitaab na Sunnah, ndivyo vilevile tutaona umuhimu wa kuijua 'Ibaadah hiyo vilivyo ili tuweze kuitekeleza ipasavyo. Na kwa mintarafu hiyo, tutaona kuna ulazima wa kupata mafunzo hayo kutoka katika chanzo kilichokamilika kwa dalili thaabit kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na Maswahaba zake. Na ndio nikakichagua kitabu hiki kukitafsiri ili kumuwezesha Muislam mwenye kusoma Kiswahili anufaike na aweze kuinoa na kuiboresha Swalah yake ili aweze kufikia makusudio yaliyotajwa katika Aayah na Hadiyth mbalimbali

---

<sup>4</sup> Maryam 19: 59.

<sup>5</sup> Al-Muddaththir 74: 42-43.

<sup>6</sup> Muslim.

<sup>7</sup> Abu Daawuud, an-Nasaaiy na Ibn Maajah.

Nisiwe mbakhili wa fadhila na mchache wa shukurani kwa wale waliotoa mchango wao mkubwa kabisa katika kazi hii tukufu. Nawaombea wote malipo kamili kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى) yanayotokana na kazi hii, bila kukosa thawaab za wale wote watakaonufaika kutokana na 'amali hii.

Shukurani zangu za dhati na du'aa zangu ni kwa dada yangu Ummu Iyyaad ambaye kwa juhudi zake zisizo mithali kazi hii imeweza kukamilika na pia ushirikiano wake mkuu wa dhati. Vilevile namshukuru al-Akh 'Abdullaah Mu'awiyah, al-Akh Muhammad 'Abdullaah al-Ma'awy, al-Akh Tawakkal, al-Akh Shams 'Ilm, al-Akh Muhammad 'Umar na al-Akh Fayswal 'Abdul-'Aziyz, kwa kujitolea wakati mkubwa kuipitia kazi hii. Pamoja na ndugu yangu mpenzi Sa'iyd Baawazir kwa kupitia vilevile na kuchangia maoni mbalimbali. Bila kusahau mchango mkubwa wa upitiaji na mawazo wa al-Akh Muhammad Faraj As-Sa'ay (Allaah Amrehemu). Hali kadhalika al-Ukht Ummu 'Abdir-Rahmaan ambaye ana mchango mkubwa katika ushauri na nasaha.

Na shukurani nyingi kwa tashji'i kubwa na uvumilivu wa hali ya juu kutoka kwa mke wangu Ummu 'Abdillaah ambaye amenisaidia kwa kiasi kikubwa na amenipa fursa ya kutosha ya kushughulika na majukumu haya matukufu bila kuchoshwa wala kuvunjika moyo. Namuomba Allaah (سبحانه وتعالى) Amlipe yeye na wote duniani na Akhera. Aamiyn

Abu 'Abdillaah Muhammad Saalim Sa'iyd Baawazir  
Dhul-Hijjah 1432 H - Oktoba 2011 M



## Historia Fupi Ya Shaykh Al-Albaaniy

(Historia hii fupi ya Shaykh nimeitoa katika kitabu nilichoandika kuhusu maisha ya Shaykh kiitwacho Shaykh Al-Albaaniy – Mwanachuoni Wa Karne Ambacho kinapatikana katika tovuti ya [www.alhidaaya.com](http://www.alhidaaya.com) na karibuni kitachapishwa in shaa Allaah)

**Abu ‘Abdillaah Muhammad Saalim Sa’iyd Baawazir**

**Al-Imaam, Al- Muhadith, Shaykh Muhammad  
Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy**

**1332 H-1420 H – 1914 M-1999 M**

**Jina Lake:** Muhammad Naaswir-ud-Diyn bin Nuuh An-Najaatiy

**Nasaba Yake:** Al-Albaaniy (Kajulikana kwa jina la Al-Albaaniy kwa sababu asili yake ni mtu wa Albania)

**Kun-Yah Yake:** Abu ‘Abdir-Rahmaan (Baba ya ‘Abdur-Rahmaan’)

**Wake Zake:** Alioa wake wanne; watatu wa mwanzo walimzalia watoto, na wa nne ‘Ummu Al-Fadhwl’ hakujaaliwa kuzaa, na ndiye aliyeishi naye hadi alipofariki dunia.

**Watoto Wake:** Aliruzukiwa watoto 13; 7 wa kiume na 6 wa kike. Wa kiume ni: ‘Abdur-Rahmaan, ‘Abdul-Latwiyf, ‘Abdur-Razzaaq, ‘Abdul-Muswawwir, ‘Abdul-Muhaymin, Muhammad na ‘Abdul-A’alaa. Wa kike ni: Aniyah, Aasiyah, Salaamah, Hassaanah, Sakiynah na HibatuLlaah.

Mwanachuoni Shaykh Muhammad Naaswir-ud-Diyn bin Nuuh An-Najaatiy Al-Albaaniy ni mmoja kati ya Ma’ulamaa wakubwa wa

Kiislam katika zama hizi. Anahesabika kuwa ni Mwanachuoni wa Hadiyth maarufu kabisa katika fani ya elimu ya *Jarh na Ta'adiyl*.<sup>8</sup>

Shaykh Al-Albaaniy vilevile ni hoja katika elimu ya *Mustwalahul-Hadiyth*.<sup>9</sup> Na Wanachuoni wamemsifu na kuelezea kwamba kwa elimu yake hiyo, karejesha kumbukumbu za zama za kina Imaam Ibn Hajr Al-'Asqalaaniy, Ibn Kathiyr na Wanachuoni wengine wakubwa wa fani hiyo.

Alikuwa na kumbukumbuku ya hali ya juu katika kuhifadhi vitu kichwani na mengine mengi. Kumbukumbu inayotukumbusha wema waliotangulia kama kina Ibn 'Abbaas, Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu 'anhum) na waliofuatia kama Imaam Al-Bukhaariy, Imaam Ash-Shaafi'y, Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah, Imaam Ibn Kathiyr, Imaam An-Nawawiy na wengine (Allaah Awarehemu wote).

## Kuzaliwa Na Kukua Kwake

Alizaliwa mwaka 1332 H – 1914 M katika mji wa Ashkoderia ambao kwa wakati huo ulikuwa mji mkuu wa Albania huko Ulaya Mashariki na ukoo wake ulikuwa maskini. Baba yake aliyeitwa Shaykh Nuuh An-Najaatiy alihitimu katika chuo cha Shari'ah huko Istanbul, Uturuki, na kurejea kwao akiwa Mwanachuoni. Lakini baada ya mfalme Ahmad Zogo kutwaa madaraka ya nchi na kuendesha utawala wa nchi hiyo kikomunisti ikabidi baba yake (Shaykh Al-Albaaniy) ahamie Damascus, Syria. Wakati huo Shaykh Al-Albaaniy alikuwa na umri wa miaka tisa.

---

<sup>8</sup> Ni fani ya Hadiyth inayohusiana na uaminifu wa wasimulizi wa Hadiyth na inakusanya habari zao zinazothibitisha uaminifu au udhaifu wa hao wasimulizi.

<sup>9</sup> Sayansi ya Hadiyth

Imaam Muhammad Naaswir-ud-Diyn Al-Albaaniy alianza masomo yake ya awali katika madrasah ya Al-Is'aaf Al-Khayriyah hapo Damascus na kuendelea hadi alipomaliza na kuwa msimamizi wa chuo hicho hadi yalipoanza mapinduzi dhidi ya Ufaransa nchini humo. Madrasah hiyo ikakumbwa na maafa ya moto yaliyosababishwa na vurugu na machafuko katika vita hivyo. Baba yake akaamua kumuachisha masomo na akaanza kumsomesha yeye mwenyewe. Alimwekea ratiba kali ya masomo ambayo ni; Qur-aan, Tajwiyd, Swarf, Fiqh (ya Kihanafi, yaliyokuwa madhehebu ya baba yake aliyekuwa Mwanachuoni mkubwa wa madhehebu hayo). Shaykh Al-Albaaniy alijifunza pia masomo mbalimbali ya Dini na lugha kutoka kwa Wanachuoni wakubwa na Mashaykh waliokuwa marafiki wa baba yake kama vile Shaykh Sa'iyd Al-Burhaaniy ambaye alimsomesha masomo ya balaaghah na lugha.

### **Kujifunza Kwake Elimu Ya Hadiyth**

Alitunukiwa shahada ya juu ya elimu ya Hadiyth kutoka kwa Shaykh Raaghib At-Twabbaakh, Mwanachuoni mkubwa wa Halab katika wakati huo. Hapo ni wakati alipokutanishwa naye kupitia Shaykh Muhammad Al-Mubaarak ambaye alimjulisha Shaykh At-Twabbaakh umahiri wa kijana huyo (Al-Albaaniy) katika elimu ya Hadiyth. Baada ya Shaykh At-Twabbaakh kumjaribu na kuthibitisha hilo mwenyewe, akamtunuku shahada (*Ijaazah*). Shahada hiyo si pekee, bali pia alipata kwa Wanachuoni wengine wakubwa wa Hadiyth kama Shaykh

Bahjatul Baytaar (ambaye isnaad yake inafika hadi kwa Imaam Ahmad bin Hanbal).<sup>10</sup>

Aliingia kwenye fani ya Hadiyith akiwa na umri wa miaka ishirini. Aliathirika sana na tafiti mbalimbali za Shaykh Muhammad Rashiyyd Ridhwaa, Mwanachuoni wa Misr wakati huo. Tafiti hizo zilikuwa katika jarida la Al-Mannaar. Anasema Imaam Al-Albaaniy: “Nilichokimulika mwanzo miongoni mwa vitabu, ni vile vya visa vya lugha ya kiarabu, kama vile; Adh-Dhwaahir, ‘Antarah, Maalik as-Sayf na vinginevyo kama hivyo. Kisha nikazama katika vitabu vya visa vya kijasusi vilivyotarjumiwa katika lugha ya Kiarabu. Siku moja nikapita katika vibanda vya kuuza vitabu na macho yangu yakaangaza kwenye jarida moja liitwalo Al-Mannaar na katika kupekuapekua ndani yake nikakutana na makala ya kitafiti ya mwandishi akikielezea kitabu cha *‘Ihya’ Uluum ad-Diyn’* cha Abu Haamid al-Ghazaaliy, akitaja mazuri yaliyomo ndani ya kitabu hicho na kasoro zake. Kwa mara ya kwanza nikakutana na aina kama hii ya uchambuzi wa kielimu. Nilivutika sana na uchambuzi sampuli hiyo na ukanifanya nisome toleo zima la makala hiyo. Kisha nikawa nafuatilizia maudhui za uchambuzi wa Hadiyith wa Mwanachuoni Al-Haafidh Al-‘Iraaqiy alioufanya kwa Hadiyith zilizomo ndani ya kitabu *‘Ihya’ Uluum ad-Diyn’*. Sikutosheka hadi ikabidi nimuombe muuza duka aniazime jarida hilo kwa kuwa sikuwa na uwezo wa fedha wa kulinunua!

Hapo ndipo ilipoanza safari ndefu ya kusoma vitabu mbalimbali. Nikatoa nakala ya maudhui hiyo iliyofanyiwa uchambuzi wa kina katika jarida hilo”

---

<sup>10</sup> *Hayaatul Al-Albaaniy*, Muhammad Ash-Shaybaaniy. Al-Albaaniy mwenyewe anayaeleza hayo pia kwenye vitabu vyake *‘Mukhtaswar Al-Uluww’* na *‘Tahdhiyrus-Saajid’*.

Shaykh Al-Albaaniy alijifunza pia kwa baba yake elimu ya kutengeneza saa hadi akawa fundi mzuri maarufu kwa kazi hiyo. Ikawa ndiyo kazi iliyompatia rizki yake. Alikuwa fundi na hapo hapo mtafutaji elimu. Hali hiyo ikaendelea hivyo hadi alipoamua kutenga siku mbili tu za kufanya kazi ya kutengeneza saa, na siku zote zilizobaki zikawa ni za kutafuta elimu. Elimu hiyo alikuwa akiichukulia katika maktaba kubwa ya mji huo wa Damascus iliyoitwa Adh-Dhwaahiriyah ambapo alikuwa akitumia siku nzima kusoma na kutafiti. Alishughulishwa mno na kusoma hadi akawa anasahau hata kula. Kilichokuwa kinakatisha utafiti na masomo yake ni vipindi vya Swalah tu. Mwishowe, wahusika wa maktaba hiyo wakamuamini na kuamua kumpa funguo zake awe anatumia maktaba wakati wa ziada, na akawa daima ni mtu wa mwisho kutoka na kufunga mwenyewe.

Hadiyth za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) zilikuwa zina athari kubwa sana katika maisha ya Shaykh kielimu na kiutendaji. Zikamuelekeza katika *Manhaj* (Njia, mwenendo) Sahihi; ambao ni kuchukua kutoka kwa Allaah (Qur-aan) na Mtume Wake (Sunnah) tu. Akipata usaidizi wa ufahamu wa vyanzo hivyo viwili vikuu kutoka kwa Maimaam Wanachuoni katika wema waliotangulia (*As-Salafu Asw-Swaalih*) bila kuwa na *ta'aswub* (kasumba) ya kumshabikia yeyote miongoni mwao au kumponda yeyote, bali msimamo wake ulikuwa ni kuchukua haki popote ipatikanapo na kutoka kwa yeyote.

Kwa sababu hiyo, aliyaacha na kuyaweka pembeni madhehebu ya Kihanafi aliyokulia nayo na aliyosomeshwa na baba yake. Baba yake (Allaah Amrehemu), alikuwa akivutana naye sana juu ya masuala hayo ya kimadhehebu, kwani baba yake alikuwa ameshikilia kwa nguvu sana msimamo wa Kihanafi na hataki kusikia mwingine hata iliyokuwa sahihi katika masuala mengine. Shaykh alijaribu sana kumfahamisha baba yake kuwa anapaswa kufanyia kazi Hadiyth za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) endapo

## Wanafunzi Wake Maarufu

Wanafunzi wake ni wengi sana na walio maarufu katika Mashaykh ni hawa ambao baadhi yao wako hai hadi leo:

Shaykh Muqbil bin Haadiy Al-Waadi'iy

Dkt. 'Umar Sulaymaan Al-Ashqar

Shaykh Saalim Al-Hilaaliy

Shaykh Hamdiy 'Abdul-Majiyd

Shaykh Muhammad 'Iyd 'Abbaasy

Shaykh Muhammad Ibraahiym Shaqrah

Shaykh 'Aliy Khushshaan

Shaykh Muhammad Jamiyl Zaynuu

Shaykh 'Abdur-Rahmaan 'Abdus-Swamad

## Vitabu Vyake

Maktaba za Kiislam zimeneemeka kwa vitabu vingi vya Shaykh hususan vile vikubwa vyenye mijalada mingi vya ‘*Silsilatul Ahaadiyith Asw-Swahiyhah*’ na ‘*Silsilatul Ahaadiyith adh-Dhwa’iyfah wal-Mawdhuw’ah*’ na kitabu chake cha Swalah kiitwacho ‘*Swiftatus Swalaatin Nabbiy’*<sup>11</sup> ambacho kimepokelewa kwa nguvu sana na wasomaji pande zote za ulimwengu, haswa vijana. Ni mojawapo ya vitabu vizuri na muhimu sana katika mafunzo ya Swalah kama ilivyoswaliwa na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).

Kadhaalika, Shaykh ana vitabu maarufu sana vya Hadiyith vyenye kuvifanyia sharh, tahkiki, na hata kubainisha yale ya sahihi na ya dhaifu ndani ya vitabu hivyo, kama alivyofanya kwenye vitabu *Sunan At-Tirmidhy*, *Sunan Ibn Maajah*, *Sunan Abi Daawuud* n.k. Vilevile ana mijalada mingi ya vitabu kama tutakavyoona hapo chini kwenye orodha fupi. Vilevile ameweza kutoa vitabu vya kufafanua na kusahihisha vitabu maarufu vya Wanachuoni wakubwa wa karibuni kama vitabu ‘*Tamaamul-Minnah Fiyt-Ta’aliyq ‘Alaa Fiqhis-Sunnah*’ kilichokuwa ni masahihisho ya Hadiyith zisizo sahihi katika kitabu cha Shaykh Sayyid Saabiq kitwacho ‘*Fiqhus-Sunnah*’, na ana kitabu cha ‘*Ghaayatul-Maraam Fiy Takhriyj Ahaadiyith Al-Halaal wal Haraam*’ ambacho ni usahihisho wa Hadiyith zilizomo katika kitabu cha Shaykh Yuusuf Al-Qaraadhwaawiy kiitwacho ‘*Al-Halaal Wal Haraam Fiy Islaam*’.

Kazi zake za uandishi kuhusu masuala ya Hadiyith zinazidi zaidi ya mia.

Baadhi Ya Vitabu Vyake Vilivyoenea Sana Ni:

---

<sup>11</sup> Kitabu hiki kimeshatafsiriwa na mwandishi kwa lugha ya Kiswahili na kinapatikana maeneo mbalimbali kwa jina “Sifa Ya Swalah Ya Mtume.”

- 1- *Silsilatul Ahaadiyth Asw-Swahiyhah* (Mijalada 1-11)
- 2- *Silsilatul Ahaadiyth Adhw-Dhwa'iyfah wal Mawdhuw'ah* (Mijalada 1-14)
- 3- *Al-Irwaa Al-Ghaliyl* (Mijadala 1-9)
- 4- *At-Targhiyb wa At-Tarhiyb* (Mijalada 1-4)
- 5- *Swahiyh wa Dhwa'iyf Sunan Abi Daawuud* (Mijalada 1-4)
- 6- *Swahiyh wa Dhwa'iyf Sunan At-Tirmidhiy* (Mijalada 1-4)
- 7- *Swahiyh wa Dhwa'iyf Sunan Ibn Maajah* (Mijalada 1-4)
- 8- *Mukhtaswar Swahiyh Al-Bukhaariy*
- 9- *Mukhtaswar Swahiyh Muslim*
- 10- *Sharhu Al-'Aqiydah Atw-Twahaawiyah*
- 11- *Ahkaam Al-Janaaiz*
- 12- *At-Tawaswul: Anwa'uhu wa Ahkaamuhu*
- 13- *Kitaabu As-Sunnah*
- 14- *Swalaatu At-Taarawiyh (Qiyaamu Ramadhwaan)*
- 15- *Tamaamul-Minnah Fiyt-Ta'aliyq 'Alaa Fiqhis-Sunnah*
- 16- *Ghaayatul-Maraam Fiy Takhriyj Ahaadiyth Al-Halaal wal-Haraam*



17- *Adaabu Az-Zafaaf*<sup>12</sup>

18- *Swifatu Asw-Swalaatin-Nabiy*<sup>13</sup>

### Fadhila Na Mema Yake

Shaykh Al-Albaaniy (Allaah Amrehemu) alikuwa ni mwenye kufuata mwenendo wa wema waliotangulia (*Salafus-Swaalih*), akifuata mwenendo wao na tabia zao, na yakawa macho yake yanafuata kilichosemwa na Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume Wake (صلى الله عليه وآله وسلم).

Alikuwa hastahi katika haki, akiitangaza haki katika vitabu na mihadhara yake. Hii ni sifa ya nadra sana kuipata katika ulimwengu wa leo, ambao wengi hawapendi kusema haki kwa kuchelea kuwaudhi wengine au kupoteza kukubalika. Shaykh alikuwa akijirudi pindi alipokutana na dalili sahihi inayokwenda kinyume na kauli yake, na aliacha kauli yake na kufuata dalili hiyo iliyosihhi bila kuangalia imetoka kwa nani. Kuna baadhi ya Hadiyith alizokuwa akiitakidi kuwa sahihi kwa elimu yake, na baadaye zikambainikia au akatanababishwa kuwa si sahihi, akawa anajirudi haraka na kukubali na kuzitaja katika vitabu vyake.

---

<sup>12</sup> Kitabu hiki kilishatafsiriwa na mwandishi wa Historia hii ya Shaykh na kinapatikana kwa jina “Adabu Za Ndoa Katika Sunnah Iliyotwaharika.” Chapa za mwanzo kimetawanywa bure na shukurani zote ni Zake Allaah.

<sup>13</sup> Kitabu hiki kimeshatafsiriwa na mwandishi kwa jina “Sifa Ya Swalah Ya Mtume” na chapa za mwanzo zimetawanywa bure na himidi zote Anastahiki Allaah.

## Elimu Yake Na Athari Yake Kwa Watu

Shaykh alikuwa katika daraja ya *Al-Haafidh* (Mwanachuoni wa Hadiyth aliyehifadhi Hadiyth laki moja (100,000) pamoja na mnyororo wa wapokezi wake na 'mutuun' zake (maneno ya kila Hadiyth). Hayo yanaelezwa na Shaykh 'Ashiysh aliyemuuliza suala hilo na Shaykh akakataa kumjibu kwa unyenyekevu na kutotaka kujifakharisha, alichojibu baada ya kukazaniwa sana swali hilo, alijibu kwa Aayah hii: **((Na neema yoyote mliyonayo inatoka kwa Allaah))**. [An-Nahl: 56].<sup>14</sup>

Katika wasia wake Shaykh alitoa hadiya maktaba yake ya vitabu na kazi zake za uandishi kukitunuku Chuo Kikuu Cha Madiynah Al-Munawarah kama alivyosema katika wasia wake: "Nimeiachia maktaba yangu - vyote vilivyomo, vikiwa ni vilivyochapishwa tayari, au nakala, au kazi nilizoziandaa kuchapishwa; kwa maandishi ya mkono wangu, au ya mwengine aliyeniandikia - kwa kuipa maktaba ya *Jaami'atul-Islaamiyah* (Chuo Cha Kiislam) kilichopo katika mji wa Madiynah Al-Munawarah. Kwa sababu ni kumbukumbu nzuri kwa chuo hicho wakati nilipokuwa huko nikifundisha, kwa kulingania kwake kwa msingi wa Kitaab (Qur-aan) na Sunnah kwa kufuata mwenendo (*Manhaj*) wa wema waliotangulia (*Salafus-Swaalih*)".<sup>15</sup>

Alikuwa mtu wa kawaida sana, mnyenyekevu asiye na makuu na asiyetofautishwa na watu wengine ila kwa vitendo na maongezi yake ya kielimu.

---

<sup>14</sup> Shaykh Husayn Al-'Awaashah, *Swafahaat Baydhwaa Min Hayaati Shaykhina Al-Albaaniy*, uk. 40.

<sup>15</sup> Samiyr bin Amiyn Az-Zuhayriy, *Muhadith Al-'Aswr*, uk.78.

Katika kipindi cha maisha yake, alifanya tafiti nyingi na kuzichambua taqriban silsilah 30,000 za wasimulizi wa Hadiyth (*isnaad*), akiwa ametumia kiasi cha miaka 60 ya umri wake kusoma na kupitia vitabu vya Sunnah na kuwa karibu navyo kwa muda wote huo, na mawasiliano ya nyanja hiyo, na pia kuwa karibu na Ma'ulamaa wa elimu hiyo.<sup>16</sup>

**Sifa Njema Walizotoa Ma'ulamaa Kwa Mujaddid Wa Zama Hizi Shaykh Muhammad Naaswir-Ud-Diyn Al-Albaaniy (Allaah Amrehemu)**

**Shaykh 'Abdul-'Aziyz Bin Baaz [Aliyekuwa Mufti Wa Saudi Arabia] (Allaah Amrehemu)**

Sikumuona mtaalamu wa Hadiyth za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika enzi yetu ya leo chini ya qubah la mbingu kama Mwanachuoni mkubwa Muhammad Naaswir-ud-Diyn Al-Albaaniy. Aliulizwa kuhusu Hadiyth ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) isemayo:

“Allaah Hutuma kwa Ummah huu Mwanachuoni katika kila miaka mia mtu wa kupiga msasa mambo ya dini Yake”.<sup>17</sup>

---

<sup>16</sup> Abu Hudhayfah: 20 Points Regarding Shaykh al-Albaanee

<sup>17</sup> Imepokewa na Abu Daawuud, na imeelezwa kuwa ni sahihi na Al-'Iraaqiy na wengineo.

Aliulizwa ni nani mpiga msasa wa karne hii? Akajibu: Ninadhani Shaykh Muhammad Naaswir-ud-Diyn Al-Albaaniy, ndiye mpiga msasa wa zama hizi. Na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.

### **Mwanachuoni Shaykh Muhammad Ibn Swaalih Al-Uthaymiyn (Allaah Amrehemu)**

Yale niliyoyajua kuhusu Shaykh na ambayo ni kidogo wakati nilipokuwa nakutana naye, ni kuwa yeye ana shime ya hali ya juu ya kutumia Sunnah na kupiga vita bid'ah; sawasawa katika 'Aqiydah au matendo. Ama kwa kusoma kwangu vitabu vyake, hakika nimemjua vyema kwa hayo. Ana elimu kubwa ya Hadiyth kwa upande wa Riwaayah na Diraayah. Allaah Amewanufaisha watu wengi kutokana na yale aliyoyaandika kwa upande wa elimu, mfumo na mwelekeo katika taaluma ya Hadiyth. Hii ni faida kubwa sana kwa Waislam. Himdi ni za Allaah. Ama kwa upande wa uhakiki wake wa kitaaluma katika fani ya Hadiyth, basi hayo hayasemekiki.

**Mwanachuoni Mfasiri Shaykh Muhammad Al-Amiyn  
Ash-Shanqiytwiy (Allaah Amrehemu)**

Shaykh ‘Abdul-‘Aziyz Al-Haddaah anasema:

“Hakika Mwanachuoni mkubwa Ash-Shanqiytwiy anamtukuza Shaykh Al-Albaaniy utukuzo wa kushangaza. Anapomuona anapita nailhali yeye yuko katika darsa yake katika Msikiti wa Madiynah, kasha husimamisha darsa lake, husimama na kumsalimia kwa ajili ya kumuheshimu”.

**Shaykh ‘Abdul-Muhsin Al-‘Abaadiy (Allaah Amhifadhi)**

Bila shaka Shaykh Al-Albaaniy, alikuwa ni katika Ma’ulamaa wa kipekee walioumaliza umri wao katika kuitumikia Sunnah, kuitungia vitabu, kulingania kwa Allaah Mtukufu, kuinusuru ‘Aqiydah ya kisalafiya, kuipiga vita bid'ah, na kutetea Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Yeye ni katika Ma’ulamaa wazuri wenye sifa za kipekee. Sifa zake zimeshuhudiwa na watu maalumu na wa kawaida. Hakuna shaka kwamba kumpoteza Mwanachuoni kama huyu, ni katika misiba mikubwa inayowapata Waislamu. Allaah Amlipe kheri nyingi kutokana na juhudi zake kubwa na Amweke katika Pepo Yake pana.

**Mufti Wa Zamani Wa Saudia Mwanachuoni Shaykh  
Muhammad Bin Ibraahim Aal Shaykh (Allaah  
Amrehemu)**

Amesema kuhusu Shaykh Al-Albaaniy (Allaah Amrehemu):  
“Yeye ni mwana Sunnah, mpiganiaji haki, na mwenye  
kupambana na watu wasiofuata haki”.

**Mwanachuoni Shaykh Muqbil Al-Waadi'iy (Allaah  
Amrehemu)**

Hakika katika taaluma ya Hadiyath, hakuna mtu kama Shaykh  
Muhammad Naaswir-ud-Diyn Al-Albaaniy. Na Allaah  
Amenufaisha kwa elimu yake na vitabu vyake mara nyingi  
zaidi kuliko yale wanayoyafanya wale wenye hamasa na Uislam  
pasi na elimu ya kutosha, na wasio na msimamo. Ninaloliamini  
na ambalo ni deni kwangu mbele ya Allaah ni kuwa, Shaykh  
Muhammad Naaswir-ud-Diyn Al-Albaaniy, ni katika waipigao  
msasa Dini na wanasadikishwa na neno la Mtume (صلى الله عليه  
وآله وسلم):

((Allaah Hutuma kwa Ummah huu mwanzoni mwa kila miaka  
mia mtu wa kupiga msasa mambo ya Dini Yake)).<sup>18</sup>

---

<sup>18</sup> Imepokewa na Abu Daawuud, na imeelezwa kuwa ni sahihi na Al-  
'Iraaqiy na wengineo.

**Mwanachuoni Wa Hadiyth India, Shaykh ‘Abdus-Swamad Sharafud-Diyn (Allaah Amrehemu)**

Katika moja ya barua walizokuwa wakiandikiana na Shaykh Al-Albaaniy katika masuala ya kitafiti ya Hadiyth, alikiri kuwa Shaykh Al-Albaaniy alikuwa Mwanachuoni mkubwa wa Hadiyth.

**Waziri Wa Masuala Ya Kiislamu, Al-Awqaaf, Ulinganio Na Uongozi Shaykh Swaalih Bin ‘Abdil-‘Aziyz Bin Muhammad Aali Shaykh**

Alisema: “Shukrani ni za Allaah kwa hukumu Zake na uwezo Wake ((Hakika sisi ni wa Allaah na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea)).<sup>19</sup> Hakuna shaka kwamba kumpoteza Mwanachuoni Mkubwa Shaykh Muhammad Naaswir-ud-Diyn Al-Albaaniy, ni msiba. Yeye ni katika Wanachuoni wakubwa wa Ummah na mabingwa wa Hadiyth. Kwa Ma’ulamaa hao (Shaykh Al-Albaaniy), Allaah Mtukufu Ameilinda Dini hii na Akaieneza Sunnah kupitia kwao...”

---

<sup>19</sup> Al-Baqarah: 156

## Kipindi Cha Mwisho Cha Maisha Yake Na Kifo Chake

Shaykh (Allaah Amrehemu) hakutulia kutafuta elimu hadi umri wa miaka 86, akisoma, akifundisha, akielimisha, akiandika vitabu, akiandika barua kwa Wanachuoni wenzake kuwapongeza, kuwanasihi, kuwakosoa makosa ya vitabuni mwao au fatwa zao. Hadi umri huo hakuwa akiacha kutafiti masuala ya Hadiyith, akipangua sahihi na dhaifu na za kutungwa, aliweza kugawa vitabu vingi vikubwa vya Hadiyith kama vya Maimaam Abu, Dawuud, Ibn Maajah, At-Tirmidhy, An-Nasaaiy na wengineo, akaweza kuvigawa Sahihi zake na Dhaifu zake na kuwasaidia kuwarahisishia wenye elimu na wanafunzi katika uandishi na tafiti zao.

Shaykh anakumbukwa sana kwa kazi hiyo iliyosaidia Ummah leo hii, na kuuamsha kujua Hadiyith sahihi na dhaifu na pia kuwafanya wengi wawe karibu na kuifuatilia elimu ya Hadiyith na sayansi yake. Aliyafanya yote hayo - kwa sababu moyo wake ulikuwa umefungamana nayo hayo kwa mapenzi ya juu - na hakuacha hadi taqriban miezi miwili ya mwisho ya maisha yake, alipokuwa dhaifu akiugua kitandani. Pamoja na magonjwa mazito yaliyomdhoofisha sana na kutotoka kitandani, hakuacha kusoma wala hakupoteza kumbukumbu zake, akiwa anamjua kila aliyekwenda kumtazama, akimuita kila mmoja kwa jina lake! Hadi Allaah (سبحانه وتعالى) Alipoirejesha roho yake na akamfisha katika nyakati za mwisho za Alasiri, siku ya Jumamosi, tarehe 22 katika mwezi wa Jumaadah Al-Aakhirah, mwaka 1420 H sawa na 10-02-1999 M huko 'Ammaan, Jordan.

Wanachuoni, watafuta elimu, wanafunzi, na watu wa kawaida wote waliathirika sana na kifo cha Shaykh. Taarifa za kifo chake zilipowafikia Waislam, majonzi yalienea pote na wengi kuhisi kuwa ile elimu na yule 'Mujaddid' (Mkarabati wa Dini) wa zama



hayupo nao tena. Mwaka huo ulikuwa ni mwaka wa huzuni, kwa kutanguliwa na kifo cha Mwanachuoni mkubwa wa zama hizo hizo ambaye alikuwa Mufti wa Saudia wa wakati huo, Shaykh Al-'Alaamah 'Abdul-'Aziyz bin 'Abdullaah bin Baaz, na baada yao kufuatiwa na kifo cha Mwanachuoni Shaykh Muhammad bin Swaalih Al-'Uthaymiyn, Mashaykh wengine wakubwa waliofariki katika mwaka huo ni, Shaykh Swaalih bin 'Aliy Ghaswuun, Shaykh 'Aliy Twantwawiy, Dkt. Mustwafaa Az-Zarqaa, Shaykh Mana'a Al-Qahtwaan na Shaykh 'Atwiyah bin Muhammad Saalim (Allaah Awarehemu wote hao na Awaweke katika pepo Yake Tukufu).

Abu 'Abdillaah (1432 H - 2012 M)

## بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

### Utangulizi

Sifa njema zote ni za Allaah Aliyefanya Swalah kuwa ni fardhi kwa waja Wake na kuwaamrisha kuitekeleza ipasavyo; Aliyeambanisha kufaulu na furaha kutokana na unyenyekevu katika Swalah; Aliyefanya kuwa ni kigezo cha Iymaan na kufr; na aliyeifanya ni kizuizi cha mambo machafu na vitendo viovu.

Rahma na Amani zimshukie Mtume Muhammad ambaye Amefunuliwa na maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴾



**((Na Tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao, wapate kutafakari))<sup>(20)</sup>**

Na ambaye ametekeleza kikamilifu kazi hii. Swalah ilikuwa ni jambo muhimu kabisa aliyowaeleza watu kwa kauli na vitendo, hata aliwahi kuswali mara moja katika minbar akisimama, akirukuu na kusujudu, kisha akasema: **((Nimefanya hivi ili mnifuate na mjifunze Swalah yangu))<sup>(21)</sup>**. Ametuwajibisha tumfuate anavyoswali kwa kusema: **((Swalini kama mlivyoniona nikiswali))<sup>(22)</sup>**. Amebashiria pia kuwa

---

<sup>20</sup> Suratun-Nahl: 16: 44

<sup>21</sup>Al-Bukhaariy na Muslim – itafuatia baadaye kikamilifu

<sup>22</sup>Al-Bukhaariy na Ahmad

atakayeswali kama anavyoswali, atakuwa katika ahadi ya Allaah kwamba Atamuingiza katika Pepo, akisema: **((Swalah tano ambazo Allaah (عزوجل) Amezifaradhisha. Atakayefanya wudhuu wake vizuri, akaziswali kwa wakati wake, na kutimiza rukuu zake, Sujuud zake na unyenyekevu, ana dhamana kutoka kwa Allaah kwamba Atamsamehe, lakini asiyetekeleza hana dhamana kutoka kwa Allaah, Akipenda Atamsamehe au Akipenda Atamuadhibu))**<sup>(23)</sup>

Rahma na Amani pia ziwafikie jamaa zake na Maswahaba zake Waswalihina waliotuletea 'Ibaadah yake (صلى الله عليه وآله وسلم), na Swalah, kauli na vitendo vyake na wakavifanya hivyo kuwa ni madhehebu na mfano bora kwao wa kufuata; na wale watakaofuata nyayo zao hadi siku ya Qiyaamah.

\*\*\*\*\*

Nilipomaliza kusoma kitabu cha Swalah katika At-Targhiyb wat-Tarhiyb cha Al-Haafidhw Al-Mundhiry (رحمه الله) na kuwafundisha ndugu zetu miaka minne iliyopita, ilidhihirika kwetu umuhimu wa nafasi ya Swalah katika Uislamu; na thawabu, neema na fadhila zinazowasubiri watakaoitekeleza na kuiswali sawa sawa; na kwamba yote inatofautiana, kutegemea ukaribu wa Swalah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Hii ndivyo ilivyoashiriwa katika usemi wake: **((Hakika mja huswali Swalah ambayo haandikiwi kitu ila sehemu ya kumi, au ya tisa, ya nane, ya saba, ya sita, ya tano, robo, thuluthi au nusu yake))**<sup>(24)</sup>. Hivyo nikawakumbusha ndugu kwamba

---

<sup>23</sup>Maalik, Abu Daawuud, An-Nasaaiy na Ibn Hibbaan. Hadiyth Swahiyh iliyobainishiwa kuwa Swahiyh na Maimamu wengi. Nimeitoa takhriyj yake katika Swahiyh Abi Daawuud (451, 1276)

<sup>24</sup>Swahiyh - Imekusanywa na Ibn Al-Mubaarak katika Az-Zuhd (10/21/1-2),

Lakini, maelezo kwa urefu juu ya vipengele vyote hivi vya Swalah sio wepesi kutekelezwa na watu wengi siku hizi, hata Maulamaa wengi kwa sababu ya kujihusisha na kujiwekea mipaka ya madhehebu fulani. Lakini kwa yeyote mwenye kujali na kusaidia katika ukusanyaji na utafiti wa Sunnah zilizotakasika, atajua kwamba katika kila madhehebu kuna Sunnah ambazo hazipatikani katika madhehebu mengine; juu ya hivyo, katika kila dhehebu kuna usemi na vitendo ambavyo havipatikani dalili za usahihi wake kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Mengi hayo hupatikana katika usemi tu wa Maulamaa waliofuatia<sup>(25)</sup>, wengi wao tunaona kwamba

---

Abu Daawuud na An-Nasaaiy ikiwa na isnaad nzuri; Nimetoa takhriy yake katika Swahiyh Abi Daawuud (761).

<sup>25</sup> Abul-Hasanaat Al-Laknawiy kasema katika *An-Naafi' Al-Kabiyir Liman Yutwaali' Al-Jaami' As-Swaghiyr* (Uk. 122.3) baada ya kuvikadiri vitabu vya Fiqh ya Hanafiy na kutaja vipi vya kutegemea na vipi visitegemewe: "Yote hayo tuliyosema kuhusu daraja zinazohusika za ukusanyaji huu unahusiana na yaliyomo katika mas-ala ya Fiqhi; lakini ama yaliyomo kuhusu Hadiyth za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), hazihusiki kwani vitabu vingi ambavo Mafuqahaa wanatagemea vimejaa uzushi wa Hadiyth, achilia mbali hukmu za Maulamaa. Ni dhahiri kwetu kutokana na uchambuzi mpana kwamba ingawa waandishi wake walikuwa ni mahodari lakini hawakuwa makini katika kunukuu usimulizi".

Moja ya uzushi na uongo wa Hadiyth ni zile zinazopatikana katika baadhi ya vitabu bora kabisa mfano wa Hadiyth hizo ni: "Atakayeswali Swalah ya

fardhi Ijumaa ya mwisho ya Ramdhaan itakuwa ni kadhaa ya Swalah zote alizoziacha maishani mwake hadi umri wa miaka sabini"! Laknawiy ( رحمه الله) kasema katika *Al-Aathaar Al-Marfuu'ah fil-Akhbaar Al-Mawdhwuu'ah* (Uk. 315) baada ya kutoka Hadiyth hii: "Aliy Al-Qaari kasema katika *Al-Mawdhwu'aat As-Suhgraa wa Al-Kubraa*: Huu ni uongo kabisa kwani inakwenda kinyume na Ijmaa' (rai za kuwafikiana) kwamba kitendo kimoja cha ibada hakiwezi kulipiza vitendo vilivyoachwa miaka mingi. Hiyvo hakuna maana kunukuu mwandishi wa *An-Nihaayah* wala wafasiri wengineo katika kitabu kiitwacho '*Al-Hidaayah*', kwani wao sio Maulamaa wa Hadiyth wala hawakutoa hizi Hadiyth kutoka kwa wakusanyaji wa Hadiyth".

Ash-Shawkaaniy pia alitaja Hadiyth hii katika *Al-Fawaa'id al-Majmuu'ah Fil Ahaadiyih al-Mawdhwuu'ah* ikiwa na maneno yaliyofanana, kisha akasema (Uk. 54): "Hii imezushwa bila shaka – sijaipata hata katika mkusanyo wa Hadiyth za Uzushi! Bali imekuwa ni maarufu baina ya wanafunzi wa Fiqh katika mji wa Sar'aa katika karne yetu, na wengi wameanza kuitekeleza. Sijui nani aliyewazushia. Allaah Awahizi waongo".

Laknawiy akaendelea kusema: "Kutegemea Hadiyth hii ambayo inapatikana katika vitabu vya uradi na du'aa ni uzushi, nimeandika insha fupi ya kitaalamu na dalili inayoitwa 'Kuwakanusha Ndugu Kutokana Na Uzushi Wa Ijumaa Ya Mwisho Ya Ramadhaan'. Humo nimetoa nukta ambazo zitamulika akili na zitazibua masikio, hivyo isome, kwani ni ya thamani katika maudhui hii na ni ya ubora wa hali ya juu.

Marudio ya Hadiyth za uongo kama hizo katika vitabu vya Fiqhi vimeharibu uaminifu wa Hadiyth nyinginezo ambazo hazikunukuliwa kutoka katika vitabu vya Hadiyth vinvayotegemewa. Maneno ya 'Aliy Al-Qaariy yameashiria haya. Muislamu lazima apokee Hadiyth kutoka kwa watu ambao ni wataalamu katika fani hii, kama usemi wa zamani wa Kiarabu unavyosema: "Watu wa Makkah wanajua njia za milima yao vizuri" na "Mwenye kumiliki anajua vyema vilivyomo nyumbani mwake".

<sup>26</sup> Maneno ya Imaam An-Nawawiy ( رحمه الله) katika *Al-Majmuu' Sharh Al-Muhadhdhab* (1/60) yanaweza kujumuishwa kama ifuatavyo: "Maulamaa watafiti wa Hadiyth na wengineo wamesema kwamba ikiwa Hadiyth ni dhaifu, haitotajwa kuwa: 'Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) kasema/katenda/kaamrisha/kakataza...' Au ibara yoyote nyingine inayotaja uhakika, bali itasemwa: 'Imeripotiwa/imenukuliwa/imesimuliwa kutoka kwa...' au ibara zingine zinazodokeza shaka. Wanasema kuwa ibara za uhakika huwa ni Swahiyh

---

na Hadiyth Hasan na ibara zenye shaka huwa ni nyinginezo. Hii ni kwa

Jambo hili limepuuzwa na Mafuqahaa wengi wa zama zetu, bali Maulamaa wengi wa nidhamu yoyote, isipokuwa Muhaddithiyn wenye ujuzi. Huu ni uzembe wa kuchukiza kabisa, kwani mara nyingi hutaja Hadiyth Swahiyh: 'Imeripotiwa kutoka kwake kwamba...' Na kuhusu Hadiyth dhaifu: 'Amesema' na: 'Fulani na Fulani ameripoti...' Hivi si sawa kabisa".

<sup>27</sup> Katika mlango huu, kuna kazi ya mwalimu wetu pia mwandishi wa *Irwaah'Al-Ghaliyl Fiy Takhriyj Manaar As-Sabiyl* katika Mijalada 9, na *Ghaayah Al-Maraam fiy Takhriyj Ahaadiyth Al-Halaal wal-Haraam*, takhriyj ya Ahaadiyth zinazopatikana katika kitabu cha Dkt. Yuusuf Al-Qaradhwaawiy 'Halali Na Haramu Katika Uislamu' (ambacho kina Hadiyth nyingi dhaifu) - **Mchapishaji**

## Sababu Za Kuandika Kitabu Hiki Na Baadhi Ya Vipengele Vyake

Kwa vile sijapata kuona kitabu chenye maarifa mengi kuhusu ma'uwadhui hii, nimehisi imeniwajibikia kutoa kitabu ambacho kitakusanya sifa nyingi za Swalah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa ajili ya manufaa ya ndugu zangu Waislamu wapendao kufuata uongofu wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika ibada zao, hadi iwe wepesi kwa yeyote mwenye kumpenda kweli Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aweze kutumia kitabu hiki kutimiza amri yake: **((Swalini Kama Mlivyoniona nikiswali))**.

Hivyo nikaianza kazi hii ngumu, na kufanya utafiti wa Hadiyith zinazohusika kutoka vyanzo mbali mbali za Hadiyith hadi kitabu hiki kilichokuwa mikononi mwako hivi sasa ni matokeo yake yote. Nikajiwekea masharti nafsini mwangu kwamba nitaziweka Hadiyith zilizokuwa na isnaad Swahiyh pekee kutokana na kanuni za msingi na sheria ya Sayansi ya Hadiyith. Nimepuuza Hadiyith yoyote ambayo imetegemewa na msimulizi asiyejulikana au dhaifu ikiwa imehusiana na maelekezo ya nje, adhkhaar, ubora n.k. wa Swalah. Hii ni kwa sababu naamini kwamba Hadiyith Swahiyh<sup>(28)</sup> zinatoshuleza, na hakuna haja ya zilizo dhaifu kwani zilizo dhaifu hazizidishi kitu isipokuwa dhana (makisio, mashaka) na makisio yasiyo sahihi ni kama Anavyosema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ﴾

---

<sup>28</sup> Istilahi ya 'Hadiyith Swahiyh' inajumuisha Swahiyh na Hasan mbele yamacho ya Muhaddithiyn, ikiwa ni Hadiyith Swahiyh lidhaatihi au Swahiyh lighayrihi, au Hasan lidhaatihi au Hasan lighayrihi.

**((Na dhana haisaidii chochote mbele ya haki))<sup>(29)</sup>**

Na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kasema: **((Tahadharini na dhana kwani dhana ni kauli ya uongo))<sup>(30)</sup>**

Kwa hiyo hatuwezi kumuabudu Allaah kwa kufuata Hadiyith zisizo Swahiyh, bali Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) ametukataza akisema: **((Jiepusheni na kusema yanayonihusu isipokuwa muyajuayo))<sup>(31)</sup>**. Kwa vile ametukataza kusimulia masimulizi dhaifu, basi pia haipasi kuzitekeleza.

Nimekigawa hiki kitabu katika sehemu mbili; kubwa na ndogo, matini kuu na matini ya kisaidizi/matini ndogo.

Matini kuu imejumuisha matini ya Hadiyith au ibara ilivyochukuliwa humo, pamoja na maneno yanayolingana kuunga pamoja ili kukifanya kitabu chepesi tokea mwanzo hadi mwisho. Nimekuwa makini kuibakisha matini ya kila Hadiyith kama ilivyopatikana katika vitabu vya Sunnah; ambako Hadiyith ilikuwa na maneno tofauti na nimechagua maelezo yaliyo bora kabisa yanayowafikiana na ufasaha, wepesi n.k. Lakini nimekusanya maneno mengine pamoja; hivyo: "(katika usemi kadha na kadhaa...)" au "(katika usimulizi kadhaa na kadhaa...)". Sikumtaja Swahaba aliyesimulia Hadiyith ila kwa nadra tu nimefanya hivyo, wala sikumtaja Imaam gani wa Hadiyith aliyekusanya Hadiyith, ili kufanya wepesi usomaji na marejeo.

Ama matini ya kisaidizi/ndogo ni maelezo kutokana na matini kuu. Humo nimefuatilia Hadiyith kutoka asili yake nikifumbua

---

<sup>29</sup> An-Najm: 53: 28

<sup>30</sup> Al-Bukhaariy Na Muslim

<sup>31</sup> Swahiyh - imekusanywa na At-Tirmidhiy, Ahmad na Ibn Abi Shaybah.



maelezo mbali mbali na njia za usimulizi. Pamoja nayo, nimetoa maelezo katika isnaad zao na usimulizi unaotilia nguvu, pamoja na tanbihi Swahiyh na zenye kutezwa kwa wasimulizi, ikiwa ni Swahiyh au dhaifu kutokana na hukumu za Sayansi ya Hadiyth. Aghlabu njia ya usimulizi moja huwa na nyongeza ya maneno ambayo hayapatikani katika njia nyingine, hivyo nimezitia hizi katika Hadiyth ya asili zilizotajwa katika matini kuu kila ilipowezekana bila ya kuharibu ufasaha, nikiweka nyongeza katika mabano ya mraba [...] bila ya kutaja chanzo gani kilichonacho nyongeza hiyo. Hii imefanywa ikiwa Hadiyth asili yake imetoka kwa Swahaba mmoja, au sivyo nimeitoa peke yake; mfano katika Du'aa za kufungulia n.k. Nyongeza hii ya maneno ziada ni manufaa makubwa ambayo hutoyapata katika vitabu vingi – Sifa njema zote ni za Allaah Ambaye Kwa Neema Zake Mema hutimia.

Kisha, nikataja katika matini ya kisaidizi/matini ndogo Madhehebu ya Maulamaa kuhusu Hadiyth tulizozitoa na dalili zake kila moja pamoja na hoja zake na kubainisha uzito na udhaifu wake. Kisha tukachagua rai iliyo sahihi ambayo tumeiweka katika matini kuu. Pia katika matini ya kisaidizi tumetoa baadhi ya mas-ala ambayo hakuna matini katika Sunnah, lakini imehitaji Ijtihad, na haikuja chini ya ma'uwduhui ya kitabu hiki.

Kwa vile kuchapishwa kitabu kuwekwa matini kuu na matini ya kisaidizi haiwezekani sasa kwa sababu mbali mbali, tumeamua kukichapisha kikiwa na matini kuu ya kitabu (pamoja na tanbihi fupi) kwa uwezo wa Allaah, na kukiita '*Swiffatus-Swalaht 'An-Nabbiyy'* (صلى الله عليه وآله وسلم) *Min At-Takbiyr ilaa At-Tasliym Kaannaka Taraaha'* (Sifa ya Swalah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) Kuanzia *Takbiyra Ya Mwanzo hadi Kumalizika kwa Salaam Kama Kwamba Unaiona*)"

Namuomba Allaah Ajaalie kazi hii iwe khaswa kwa ajili Yake, na iwasaidie ndugu zangu katika Iymaan kunufaika nayo kwani Yeye ni Mwenye Kusikia Aliye Karibu.

## Manhaj Ya Kitabu Hiki

Kwa vile lengo la kitabu hiki ni kubainisha uongofu wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kuhusu Swalah, imenipasa nijiwekee mipaka ya kufuata madhehebu fulani kwa sababu zilizotajwa nyuma. Kwa hiyo nimeweka tu yale yaliyothibitishwa kutoka kwake (صلى الله عليه وآله وسلم), na ndivyo ilivyo daima njia za Mualamaa wa Hadiyith<sup>(32)</sup> wakiwa wa zamani au wa kisasa<sup>(33)</sup> kama usemi mzuri usemao:

---

<sup>32</sup> 'Abdul-Hayy Al-Laknawiy amesema katika *Imaam Al-Kalaam Fiy Maa Yata'allaq bil-Qiraa'ah Khalf Al-Imaam* (Uk. 156) kama ifuatavyo:

"Yeyote mwenye kuzama katika bahari ya Fiqh na kanuni za falsafa ya shari'ah na asiyekuwa mwenye chuki au upendeleo na mtu, atatambua kwa yakini kwamba mas-ala mengi makuu na ya matawi ambayo Maulamaa wamekhitilafiana, madhehebu ya Maulamaa wa Hadiyith ni ya nguvu zaidi kuliko ya wengineo. Kila mara ninapoingia katika matawi ya rai zilizokhitilafiana, nakuta rai za Muhaddithiyn ziko karibu zaidi na haki - thawabu zao ziko kwa Allaah, na Kwake ni shukurani zao. Vipi wasiwe hivyo na hali wao ni warithi wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na ni manaibu wa shari'ah zake; Allaah Atujumuishe nao Atufishe tukiwa na mapenzi nao"

<sup>33</sup> Subki amesema katika *Al-Fataawa* (1/48)

"Jambo muhimu kabisa kwa Waislamu ni Swalah ambayo kila mmoja inampasa kuitilia hima na kuhakikisha inahifadhiwa kwa kuswaliwa na kutekelezwa ipasavyo. Yanayohusiana na Swalah ni mas-ala ambayo yamewafikiwa kwamba hakuna kujiepusha nay. Na mas-ala waliyokhitilafiana Maulamaa, muelekezo wake ni mambo mawili; Ima kujitoa katika shaka iwezenavyo katika mgogoro, au kutafuta yaliyothibitika kuwa Swahiyh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na

“Watu wa Hadiyth ni watu wa Mtume ingawa hawako naye, lakini wako na nyendo zake.”

Hivyo kitabu hiki In shaa Allaah kitakusanya yote yaliyohusiana na kila ma’uwdhui kutokana yaliyomo katika vitabu vya Hadiyth na vitabu vya ikhtilaaf za Madhehebu, ili hukmu sahihi itakayopatikana katika kitabu hiki, haitopatikana katika Dhehebu moja. Hivyo atakayefuata In shaa Allaah, atakuwa miongoni mwa wale Aliowaongoa Allaah:

﴿لِمَا اٰخْتَلَفُوْا فِيْهِ مِنَ الْحَقِّ بِاِذْنِهٖ ۗ وَاللّٰهُ يَهْدِيْ مَنْ يَّشَاءُ اِلَى صِرَاطٍ

مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٢١٣﴾

**((...walipokhitalifiana katika kwendea haki. Na Allaah Humuongoa Amtakaye kwenye Njia Iliyonyooka))<sup>(34)</sup>**

Nilipoziidhinisha hizi kanuni kwa nafsi yangu, yaani kuambatana na Sunnah Swahiyh na kuzitekeleza katika kitabu hiki na vinginevyo, nilijua hakika kwamba hii haitoridhisha kila kundi la watu au dhehebu; bali itasababisha kwa wengine, ikiwa sio wengi wao, kunituhumu na kunilaumu. Hili silijali

---

﴿فَمَنْ كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهٖ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهٖ اٰحَدًا﴾

**((Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake))** [Al-Kahf: 110]

Nasema: Muelekezo wa mwisho ni bora zaidi, bali ni wajibu; hii ni kwa sababu juu ya kwamba muelekezo wa mwanzo hauwezekani kwa mas-ala mengi, vile vile hautimizi amri ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) **((Swalini kama mlivyoniona nikiswali))** bali unamfanya mtu iwe Swalah yake tofauti na Swalah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).

<sup>34</sup> Al-Baqarah: 2:213

kwani pia natambua kwamba kuridhisha kila mtu ni jambo lisilowezekana na kwamba: **((Yeyote atakayeridhisha watu kwa kumghadhibisha Allaah, Allaah Atamuwakilisha kwa watu))** kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)<sup>(35)</sup>. Thawabu ziko kwa Allaah kwa yule Aliyesema:

“Sikuweza kujiepusha na kutuhumiwa

Hata ningelikuwa katika pango la mlima wenye mikunjokunjo

“Kwani nani atakayeweza kujiepusha na watu bila ya kudhuriwa

Hata akijifisha nyuma ya mbawa za tai”

Inanitosheleza kwangu kwamba naamini hii ndio njia sahihi zaidi ambayo Allaah Aameamrisha Waumini kufuata; ambayo Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) Bwana wa Mitume ameeleza. Hii ni njia waliofuatiliza Salafus Swaalih, Maswahaba, na Taabi'iyin pamoja na Maimaam wanne ambao Waislamu wengi leo wanafuata madhehebu yao. Wote wamekubaliana katika kuwajibikia kushikilia Sunnah na kuzirejea; kupuuza kila rai inayokwenda kinyume nazo, hata kama mwenye hizo rai ni mtukufu vipi, kwani utukufu wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ni bora zaidi na mifano yake ni ya kweli.

Kwa hivyo nimetekeleza kwa kufuata uongofu wao, nimefuata nyayo zao na kutekeleza amri zao kushikilia Hadiyith Swahiyh hata kama inapinga rai.

Amri hizi zao zimeniathiri sana katika usomi wangu wa njia hii na kukanusha kwangu kufuata taqliyd kwa upofu (kufuata rai). Namuomba Allaah (سبحانه وتعالى) Awajaze kheri.

---

<sup>35</sup> At-Tirmidhiy, Al-Qadhwaa'iy, Ibn Bushraan na wengineo

## Kauli za Maimaam Wanne Kuhusu Kushikamana na Sunnah na Kuacha Kufuata Rai Zao

"Imani yetu na ya kila mwenye kusema ya haki (mwenye kufanya 'Insaaf') juu ya Imaam

Itakuwa ni manufaa makubwa ikiwa tutazieleza baadhi ya kauli zao hapa, kwani huenda jambo hili litamuonya mtu au litawakumbusha wale ambao wanafuata rai za Maimaam au madhehebu maalum, bali wanaofuata kwa upofu wale Waalimu au Mashaykh na wale walio chini ya daraja ya hao Maimaam wanne wakubwa <sup>(36)</sup> wakishikilia madhehebu yao au rai zao kama kwamba zimeteremeshwa kutoka mbinguni! Na hali Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema:

﴿ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ ﴾

((Fuateni mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu, wala msifuate rafiki au walinzi wengine badala Yake))<sup>(37)</sup>

### Wasemavyo Maimaam

#### 1- Abu Haniyfah (رحمه الله)

Wa kwanza wao ni Abu Haniyfah Nu'maan bin Thaabit.

---

<sup>36</sup>Hii ni aina ya taqliyd (kufuata kwa upofu [kiujinga]) ambayo Imaam At-Twahaawiy alihusisha aliposema: "Hafuati rai ila ni mtu mkaidi au mjinga"

(kufuata kama kipofu)

<sup>37</sup> Al-A'raaf:3

Wafuasi wake wamesimulia kauli zake mbali mbali pamoja na maonyo tofauti ambayo yote lengo lake ni moja, nalo ni: Wajibu wa kuikubali Hadiyth na kuachilia mbali kufuata rai za Maimaam ambazo zinakhitilafiana nayo.

"Ikiwa Hadiyth imeonekana kuwa ni Swahiyh, basi hiyo ndiyo madhehebu yangu"<sup>(38)</sup>

"Hairuhusiwi"<sup>(39)</sup> kwa mtu yeyote kukubali rai zetu ikiwa hawatojua wamezipata kutoka wapi"<sup>(40)</sup>

---

<sup>38</sup> Ibnul-'Aabidiyn katika *al-Haashiyah* (1/63) na katika inshaa yake *Rasm al-Mufti* (1/4 kutoka Mkusanyiko wa Inshaa za Ibnul-'Aabidiyn). Shaykh Swaalih Al-Fulaaniy katika *al-Iyqaadhw al-Himaam* (uk.) na wengineo. Ibnul-'Aabidiyn amenukuu kutoka *Sharh al-Hidaayah* ya Ibn Al-Shahnah Al-Kabiyir, mwalimu wa Ibn Al-Himaam, kama ifuatavyo:

"Ikiwa Hadiyth iliyo kinyume na Madhehebu imeonekana kuwa ni Swahiyh basi mtu atende kwa kufuata hiyo Hadiyth na aifanye kuwa ni madhehebu yake. Kuifanyia kazi Hadiyth hakutombatilisha mtu kuwa sio mfuataji wa madhehebu ya Hanafi, kwani imeripotiwa kuwa Abu Haniyfah alisema: "Ikiwa Hadiyth imeonekana kuwa ni Swahiyh, basi hiyo ndiyo madhehebu yangu". Na hii imeelezewa na Imaam Ibn 'Abdil-Barr kutoka kwa Abu Haniyfah na kutoka kwa Maimaam wengine".

Hii ni sehemu ya ukamilifu wa elimu na ucha Mungu wa Maimaam, kwani wameonyesha kwa kusema kwamba wao hawakuwa na maarifa (elimu) kamili ya Sunnah zote. Na Imaam Ash-Shaafi'iy amefafanua wazi wazi (tazama mbele). Hutokea wanapokwenda kinyume na Sunnah huwa ni kwa sababu hawakuitambua. Ndipo walipotuamrisha tushikilie Sunnah na tuizingatie kuwa ni sehemu ya madhehebu yao. Allaah Awashushie Rahma Yake kwao wote.

<sup>39</sup> Sio halaal

<sup>40</sup> Ibn 'Abdil-Barr katika *Al-Intiqaa' fiy Fadhwaa'il Ath-Thalaathah Al-Aimmah Al-Fuqahaa* (uk.145), Ibn Al-Qayyim katika *I'laam Al-Muwaqi'iyin* (2/ 309), Ibn 'Aabidiyn katika tanbihi zake kwenye *Al-Bahr Ar-Raa'iq* (6/ 293) na katika *Rasm Al-Mufti* (uk. 29, 32) na Sha'raaniy katika *Al-Miyzaan* (1/ 55) pamoja na usimulizi wa pili. Usimulizi wa mwisho ulikusanywa na 'Abbaas Ad-Dawriy katika *At-Taariykh* ya Ibn Ma'iyn (6/ 77/1) ikiwa na *Isnaad Swahiyh* kutoka kwa Zafar, mwanafunzi wa Imaam Abu Haniyfah. Usimulizi uliofanana upo kutoka kwa wafuasi wa Abu Haniyfah; Zafar, Abu Yuusuf na 'Aafiyah bin Yaziyd; taz. *Al-Iyqaadhw* (uk. 52). Ibn Al-Qayyim alithibitisha kwa nguvu usahihi wake kutoka kwa Abu Yuusuf katika *I'laam Al-Muwaqi'yn* (2/ 344). Nyongeza ya usimulizi wa pili

Katika usimulizi mwengine: "Imekatazwa<sup>(41)</sup> kutokana na maneno yangu"

Usimulizi mwengine imeongezwa: "...Kwani sisi ni wanaadamu, tunasema jambo siku moja na kulirudisha (kulikataa) siku ya pili yake".

Na katika usimulizi mwengine: "Ole Ewe Ya'quub!<sup>(42)</sup> Usiandike kila kitu unachosikia kutoka kwangu kwani huwa natoa rai moja leo na kesho huikataa. Au hutoa rai moja kesho na kuikataa keshokutwa".<sup>(43)</sup>

---

unarejewa na mwandishi wa *Al-Iyqaadhw* (uk. 65) kwa Ibn 'Abdil-Barr, Ibn Al-Qayyim na wengineo.

Ikiwa hivi ndivyo wanavyosema kwa mtu asiyejua dalili zao, jibu lao litakuwa nini kwa yule anayetambua kuwa dalili zinapingana na kauli yao, lakini bado anatoa hukumu iliyopinga dalili? Kwa hiyo, fuata usemi huu, kwani pekee unatosheleza kuvunja ufuataji rai kwa ujinga. Ndio maana nilipomlaumu mmoja wa Mashaykh (*Muqallid*) wa madhehebu katika kutoa fatwa (hukm) kwa kutumia maneno ya Abu Haniyfah bila ya kujua dalili, aligoma kuamini kuwa hiyo ni kauli ya Abu Haniyfah!

<sup>41</sup> Haraam

<sup>42</sup> Mwanafunzi mashuhuri wa Imaam Abu Haniyfah, Abu Yuusuf (رحمه الله)

<sup>43</sup> Hii ni kwa sababu Imaam kawaida hutoa rai yake kutokana na *Qiyaas* (analojia). Kisha tena hupata analojia iliyo na nguvu zaidi, au Hadiyth ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) humfikia. Kwa hiyo huikubali hiyo na kuipuuza rai yake ya nyuma. Maneno ya Sha'araaniy katika *Al-Miyzaan* (1/) yamewekwa kwa mukhtasari kama ifuatavyo:

"Imani yetu na ya kila (mwenye kusema ya haki juu ya) wa Imaam Abu Haniyfah (رحمه الله) ni kwamba, aliishi hadi iliporikodiwa Shari'ah. Na safari za wahifadhi wa Hadiyth katika miji mbali mbali na mipakani kwa ajili ya kukusanya na kuzipata. Angeliipokea na kupuuza analojia zote ambazo alizozitumia, idadi za *Qiyaas* katika madhehebu yake zingelikuwa kidogo kama zilivyo katika madhehebu mengine. Lakini kwa vile dalili za Shari'ah zimetapakaa kwa Waliotangulia na waliowatangulia, na haizikukusanywa wakati wa maisha yake, ilihitajika kuwepo *Qiyaas* nyingi katika madhehebu yake kulingana na Maimaam wengine. Maulamaa wa baada ya hapo, kisha wakafanya safari kutafuta na kukusanya Hadiyth kutoka nchi mbali mbali na miji na wakaziandika. Hivyo baadhi ya Hadiyth za Shari'ah zimeelezea nyingine. Hii ni sababu ya kuweco idadi kubwa ya *qiyaas* katika madhehebu yake wakati kwenye madhehebu mengine ilikuwa ni idadi ndogo"

"Ninaposema jambo linalokhitilafiana na kitabu cha Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) au yaliyosimuliwa na Mtume (سبحانه وتعالى), basi mpuuze kauli yangu".<sup>(44)</sup>

## 2- Maalik bin Anas (رحمه الله)

Imaam Maalik bin Anas amesema:

"Hakika mimi ni mwanaadamu: Ninafanya makosa (mara nyingine) na ninakuwa sahihi (mara nyingine). Kwa hiyo, tazameni rai zangu: zote ambazo zinakubaliana na Kitabu (Qur-

---

Abul-Hasanaat Al-Laknawiy amenukuu maneno yake kikamilifu katika An-Naafi' Al-Kabiyir (uk. 135) akiandika na kupanua tanbihi zake. Kwa hiyo yeyote anayependa kutafuta maelekezo yake afanye humo.

Kwa vile hii ni uthibitishaji kuwa kwa nini Abu Haniyfah mara nyingine alikhitilafiana na Hadiyth zilizokuwa Swahiyh bila ya kukusudia na ni sababu barabara ya kukubaliwa, kwani Allaah Haikalfishi nafsi kwa yale isiyoweza kubeba. Hairuhusiwi kumtukana kwa sababu hiyo kama walivyofanya watu wajinga. Bali ni wajibu kumheshimu, kwani yeye ni mmoja wa Maimaam wa Waislamu ambao wameihifadhi hii Dini hadi ikafikishwa kwetu kutoka katika kila matawi yake. Na kwa vile yeye analipwa (Na Allaah سبحانه وتعالى) kwa hali yoyote ile; ikiwa kapata au amekosea kwa kutokusudia. Wala hairuhusiwi kwa wafuasi wake wapenzi kuendelea kushikilia kauli zake ambazo zinakhitilafiana na Hadiyth zilizo Swahiyh kwani kauli hizo sio madhehebu yake kama kauli zake hapo juu zilivyosema. Kwa hiyo hii ni mipaka miwili; ukweli na uongo katika yake. **((Na waliokuja baada yao wanasema: Mola wetu! Tughufirie sisi na ndugu zetu waliotutangulia kwa Imani, wala Usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walioamini. Mola wetu! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye Kurehemu))** [Al-Hashr 59:10]

<sup>44</sup> Al-Fulaaniy katika Al-Iyqaadhw Al-Himaam (uk.50), ikifuatilia kwa Imaam

Muhammad na kisha kusema: "Hii haimhusu Mujtahid, (mwenye kujitahidi

kwa elimu yake na kutoa hukmu) kwa vile hakujifunga katika rai zao, bali inamhusu Muqallid (mwenye kufuata).



aan) na Sunnah, zikubalini; na zote ambazo hazikubaliani na Kitabu (Qur-aan) na Sunnah, basi zipuuzeni".<sup>(45)</sup>

"Kila mmoja baada ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), atakuwa na kauli yake itakayokubaliwa na kukataliwa, isipokuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)".<sup>(46)</sup>

Ibn Wahb amesema: "Nilimsikia Maalik akiulizwa kuhusu takhliyl ya vidole vya miguu (kuvichanganua vidole ili kupitisha maji) wakati wa wudhuu. Akasema: "Watu si lazima kufanya hivyo". Sikumkaribia hadi zogo la watu lilipopunguka. Nilipomwambia: "Tunajua kuwa ni Sunnah kuhusu jambo hilo". Akasema: "Jambo gani hilo? Nikasema: "Layth bin Sa'd, Ibn Lahiy'a na 'Amr bin Al-Haarith wamesimulia kwetu kutoka kwa Mustawrid bin Shaddaad Al-Quraishiy ambaye amesema: "Nilimuona Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akisugua baina ya vidole vyake vya miguu kwa kidole chake kidogo". Akasema: "Hadiyth hii ni Hasan (njema); sikuwahi kuisikia abadan ila leo". Kisha

---

<sup>45</sup> Ibn 'Abdil-Barr katika *Jaami'ul Bayaan Al-'Ilm* (2/32), Ibn Hazm akinukuukutoka kwake katika *Uswuul-Al-Ahkaam* (6/149) na hali kadhaalika Al-Fulaaniy (uk. 72).

<sup>46</sup> Hii inajulikana sana miongoni mwa Maulamaa wa baadaye kuwa ni kauli ya Maalik. Ibn 'Abdil-Haadiy alikiri kuwa ni Swahiyh katika *Irshaad As-Saalik* (227/1); Ibn 'Abdil-Barr katika *Jaami'ul-Bayaan Al-'Ilm* (2/91) na Ibn Hazm katika *Uswuul Al-Ahkaam* (6/145, 179) alisimulia kama ni kauli ya Al-Hakam bin 'Utaybah na Mujaahid; Taqiyud-Diyn As-Subki alisimulia katika *Al-Fataawa* (1/148) kama ni kauli ya Ibn 'Abbaas akishangazwa kwa uzuri wake kisha akasema: "Haya maneno yameanzia kwa Ibn 'Abbaas na Mujaahid, na Maalik (رحمه الله) aliyachukua, na akawa mashuhuri kwayo". Inavyoelekea kwamba Imaam Ahmad kisha akachukua kauli hii kutoka kwao, kama Abu Daawuud alivyosema katika *Masaail* ya Imaam Ahmad (uk 276). "Nilimisikia Ahmad akisema: Kila mmoja anapokelewa na anakatiliwa katika rai zake, isipokuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)"

### 3- Ash-Shaafi'iy (رحمه الله)

Ama kutoka kwa Imaam Ash-Shaafi'iy, kauli zake zilizonukuliwa ni nyingi na nzuri mno.<sup>(48)</sup> na wafuasi wake walikuwa ni bora kabisa katika kufuata.

"Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) zinamfikia na kumkwepa kila mmoja wetu. Kwa hiyo kila ninapotaja rai yangu au nikiunda sheria, na ikiwa ipo dalili kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), inayopinga rai yangu, basi rai iliyo sahihi ni aliyosema Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na hiyo ndio rai yangu"<sup>(49)</sup>

"Waislamu wamekubaliana pamoja kwamba ikiwa Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) imebainishwa dhahiri kwa yeyote,

---

<sup>47</sup> Kutoka kwa Utangulizi wa *Al-Jarh wat-Ta'diyi* ya Ibn Abi Haatim (uk. 31-32)

<sup>48</sup> Ibn Hazm anasema katika *Uswuul al-Ahkaam* (6/118)

"Hakika, Mafuqahaa wote ambao rai zao zilikuwa zikifuatwa zilipingwa kwa *taqliyd* na waliwakataza wafuasi wao kufuata rai zao kijinga. Aliyekuwa mkali kabisa miongoni mwao ni Ash-Shaafi'iy (رحمه الله), kwani yeye alirudia kutilia mkazo zaidi kuliko yeyote mwengine kufuata usimulizi ulio Swahiyh na kukubali dalili yoyote iliyoamriwa. Vile vile alidhihirisha wazi na kujitenga kuwa hana hatia ikiwa atafuatwa yeye tu pekee na aliwatangazia hayo wale waliokuwa naye. Tunaomba hii immufaishe mbele ya Allaah na thawabu zake ziwe za juu kabisa kwani alikuwa ni sababu ya mema mengi".

<sup>49</sup> Imesimuliwa na Al-Haakim ikiwa ina isnaad ya kuendelea hadi kwa Ash-Shaafi'iy kama ilivyo katika *Taariykh Dimashq* ya Ibn 'Asaakir (15/1/3),

*I'laam Al-Muwaqi'iy*n (2/363,364) na *Al-Iyqaadhw* (uk. 100)

"Ukiona katika maandishi yangu jambo ambalo ni tofauti na Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), basi zungumza kwa kurejea Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na acha niliyoyasema mimi". Katika usimulizi mwengine: "...basi ifuate (Sunnah) na usitazame tena pembeni kufuata kauli ya mwengine yeyote"<sup>(52)</sup>

Hadiyith ikipatikana kuwa ni Swahiyh, basi hiyo ndiyo madhehebu yangu"<sup>(53)</sup>

---

<sup>50</sup> Halaal

<sup>51</sup> Ibn al-Qayyim (2/361) na Al-Fulaaniy (uk. 68)

<sup>52</sup>Al-Haraawiy katika Dhamm Al-Kalaam (3/47/1) Al-Khatiyb katika Al-Ihtijaaj bi Ash-Shaafi'iy (8/2), Ibn 'Asaakir (15/9/10), An-Nawawiy katika Al-Majmuu' (1/ 63), Ibn al-Qayyim (2/ 361), na Al-Fulaaniy (uk. 100) usimulizi wa pili ni kutoka *Hilyah Al-Awliyaa* ya Abu Nu'aym.

<sup>53</sup> An-Nawawiy katika Al-Majmuu' (1/ 63), Sha'raaniy (1/ 57), akitoa chanzo chake kama Al-Haakim na Al-Bayhaqiy na Al-Fulaaniy (uk. 107). Ash-Sha'raaniy kasema: "Ibn Hazm kasema: "Kwamba imeonekana ni Swahiyh naye au kwa Imaam mwengine". Kauli yake nyingine imethibitisha ufahamu huu.

An-Nawawiy amesema: "Wafuasi wetu walitenda kutokana na hili katika mambo ya tathwiyb (mwito wa Swalah baada ya adhana), shuruti za kutoka katika ihraam kwa ajili ya ugonjwa, na mambo mengine yaliyojulikana vyema katika vitabu vya madhehebu. Miongoni wafuasi wetu ambao wameripotiwa kuwa walitoa hukumu kutokana na chanzo cha Hadiyith (yaani kuliko kuchukua kauli ya Ash-Shaafi'iy) ni Abu Ya'quub Al-Buwiity na Abul-Qaasim Ad-Daarikiy. Wafuasi wa Muhaddithiyn (Wakusanyao Hadiyith), Imaam Abu Bakr Al-Bayhaqiy na wengineo walitenda kwa kufuata kauli hii. Wafuasi wengi wetu wa zamani, walipokumbana na jambo ambalo ilikuweco Hadiyith na madhehebu ya Ash-Shaafi'iy yalikuwa ni kinyume nalo, basi walitenda kwa kufuata Hadiyith na kutowa fatwa (hukmu) pia wakisema: "Madhehebu ya Ash-Shaafi'iy ni kila kinachokubaliana na Hadiyith". Shaykh Abu 'Amr (Ibn Asw-Swalah) alisema: "Yeyote miongoni mwa Ash-Shaafi'iy akiona Hadiyith inayopinga madhehebu yake, alichukulia kama

"Wewe (Imaam Ahmad)<sup>(54)</sup> ni mwenye elimu zaidi kuhusu Hadiyth kuliko mimi. Kwa hiyo Hadiyth ikiwa ni Swahiyh basi nijulishe, ikiwa ni kutoka Kufah, Basrah au Syria, ili nichukue rai ya Hadiyth madamu tu ni Swahiyh"<sup>(55)</sup>

---

alitimiza shuruti za Ijtihad kwa kawaida, au katika maudhui au jambo lile khaswa ambalo alikuwa huru kutenda kwa kufuata Hadiyth; kama sio. Lakini hata hivyo aliona vigumu kupingana na Hadiyth baada ya utafiti zaidi, hakuweza kupata uthibitishaji wa kukinaisha wa kupinga Hadiyth. Kwa hiyo, alibakia kutenda kwa kufuata Hadiyth ikiwa Imaam mwingine mwenye kujitegemea mbali na Ash-Shaafi'iy, basi alitenda kuifuata. Na hii huwa ni kithibitisho chake cha kuacha madhehebu ya Imaam wake katika jambo hilo". Alichosema (Abu 'Amr) ni Swahiyh na lililokubalika. Na Allaah Anajua zaidi.

Kuna uwezekano mwingine ambao Ibn *Asw-Swalaat* alisahau kutaja: Afanyeje mtu ikiwa hakumpata mtu yeyote ambaye alitenda kwa kufuata Hadiyth? Hii imejibiwa na Taqiyud-Diyn As-Subkiy katika makala yake 'Maana Ya Kauli ya Ash-Shaafi'iy: Ikiwa Hadiyth ikipatikana kuwa ni Swahiyh, basi ndio madhehebu yangu' (uk. 102, Mjalada 3). "Kwangu, lililo bora kabisa ni kufuata Hadiyth. Mtu na awaze kwamba yuko mbele ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kama vile ameisikia kutoka kwake, je, atakwenda demani (kufuata mweleko wa upepo) acheleweshe kutenda kwa kuifuata? Hapana! WaLLaahi, na kila mmoja anabeba jukumu kutokana na ufahamu wake".

Mjadala wake uliobakia umetolewa kuchambuliwa katika I'laam Al-Muwaqi'iyin (2/ 303, 370) na katika kitabu cha Al-Fulaaniy, (Kichwa cha habari kamili) Al-Iyqadhw Himam Uwl Al-Abswaar, Lil-iqtidaa Bisayyid Al-Muhaajiriyn Wal-Answaar, wa Tahdhiyrihim 'An Al-Ibitidaa' Ash-Shaa' fit-Quraa Wal-Amswaar, Min Taqlyid Al-Madhaahib Ma'a Al-Hamiyyat Wal-'Aswabiyyat Bayna Fuqahaa Al-A'swaar"

Kitabu hicho ni cha pekee katika maduhui hii, ambacho kila mpenda haki akisome kwa ufahamu na kutafakari.

<sup>54</sup> Akimwambia Imaam Ahmad bin Hanbal (رحمه الله)

<sup>55</sup> Imesimuliwa na Ibn Abi Haatim katika Aadaabu Ash-Shaafi'iy (uk. 94-5),

Abu Nu'aym katika Hulya Al-Awliyaa (9/ 106), Al-Khatwiyb katika Al-Ihtijaj Bish-Shaafi'iy (8/1) na kutoka kwake Ibn 'Asaakir (15/ 9/1), Ibn 'Abdil-Barr katika Al-Intiqaa' (uk. 75), Ibn Al-Jawziy katika Manaqqib Al-Imaam Ahmad (uk. 499) na Haraawiy (2/ 47/2) katika njia tatu kutoka kwa 'Abdullaah bin Ahmad bin Hanbal kutoka kwa baba yake kwamba Ash-Shaafi'iy alimhusisha nayo katika I'laam (2/325) kama alivyofanya

"Katika kila jambo, ambako wenye kusimulia wakipata ripoti kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ambayo ni kinyume na niliyoyasema, basi narudisha kauli yangu nyuma, ikiwa wakati wa maisha yangu au hata baada ya kufa kwangu"<sup>(56)</sup>

"Mkinisikia nasema kitu, na kinyume chake ni Hadithy Swahiyh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), basi tambua kuwa akili yangu imetoweka"<sup>(57)</sup>

"Kwa kila ninalosema, ikiwa upo usimulizi ulio Swahiyh, basi Hadiyth ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) inakuja mwanzo, kwa hiyo usifuate rai yangu"<sup>(58)</sup>

"Kila kauli kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ni rai yangu pia, japokuwa hujaisikia kutoka kwangu"<sup>(59)</sup>

---

Al-Fulaaniy katika Al-Iyqaadhw (uk. 152) na kisha akasema: "Al-Bayhaqiy amesema: "Hii ndio maana yeye, yaani Ash-Shaafi'iy alitumia Hadiyth sana, kwa sababu alikusanya elimu kutoka kwa watu wa Hijaaz, Syria, Yemen na Iraq. Kwa hiyo alikubali yote aliyoon kuwa ni Swahiyh bila ya kutegemea au kuangalia yale yaliyokuwa nje ya madhehebu ya watu wa nchi yake, wakati ukweli ulipodhihirika kwake kutoka sehemu nyingine. Wengineo kabla yake, walijiwekea mipaka kwa waliyoyakuta katika madhehebu ya watu wa nchi yao bila ya kujaribu kuhakikisha usahihi wa yale yaliyokuwa kinyume nayo. Allaah Atusamehe sote"

<sup>56</sup> Abu Nu'aym (9/ 107), Harawiy (47/ 1), Ibn al-Qayyim katika I'laam Al-Muwaqqi'iyin (2/ 363) na Fulaani (uk. 104)

<sup>57</sup> Ibn Haatim katika Al-Adaab (Uk. 93), Abul-Qaasim Samarqandi katika Al-Amaal, kama katika uchaguzi kutoka kwa Abu Hafsw al-Mu'addab (234/ 1), AbuNu'aym (9/ 106), na Ibn 'Asaakir (15/ 10/1) ikiwa ni sanad Swahiyh.

<sup>58</sup> Ibn Abi Haatim, Abu Nu'aym na Ibn 'Asaakir (15/ 9/2)

<sup>59</sup> Ibn Abi Haatim (uk. 93-4)

#### 4- Ahmad bin Hanbal (رحمه الله)

Imaam Ahmad alikuwa wa mbele miongoni mwa Maimaam kukusanya Sunnah na kuzishikilia sana hadi alichukizwa kuona kinaandikwa kitabu kilichokusanya mambo yaliyogeuzwa na mambo yaliyotegemea rai zaidi<sup>(60)</sup> kwa hilo akasema:

Msifuute rai yangu, wala msifuute rai ya Maalik, au Ash-Shaafi'iy au ya Awzaa'iy, wala Ath-Thawriy, lakini chukueni kutoka kule walikotoa"<sup>(61)</sup>

Katika usimulizi mmoja: "Msiige Dini yenu kutoka kwa mtu yeyote katika hawa, bali chochote kilichotoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na Maswahaba zake, chukueni, kisha kwa At-Taabi'iyn (Waliofuata) ambako mtu ana khiari".

Mara moja kasema: "Kufuata<sup>(62)</sup> ina maana kwamba mtu anafuata yaliyokuja kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na Maswahaba zake, ama baada ya At-Taabi'iyn (Waliofuata) anayo khiari"<sup>(63)</sup>

"Rai ya Awzaaiy, rai ya Maalik, rai ya Abu Haniyfah, zote ni rai, na ni sawa katika macho yangu. Lakini, dalili ni yale masimulizi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na Maswahaba zake"<sup>(64)</sup>

"Yeyote atakayekanusha kauli ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) basi yumo katika ukingo wa kuangamia"<sup>(65)</sup>

---

<sup>60</sup> Ibn Al-Jawziy katika Al-Manaaqib (uk. 192)

<sup>61</sup> Al-Fulaaniy (Uk. 113) na Ibn Al-Qayyim katika I'laam

<sup>62</sup> Ittiba'

<sup>63</sup> Abu Daawuud katika *Masaail* ya Imam Ahmad (uk. 276-7)

<sup>64</sup> Ibn 'Abdil-Barr katika *Jaami' Bayaan Al-'Ilm*

<sup>65</sup> Ibn Al-Jawziy (uk. 182)

Hizi ndizo kauli za wazi kabisa za Maimaam, Allaah (سبحانه وتعالى) Awe radhi nao, kuhusu kushikamana na Hadiyth na kukataza kufuata rai zao bila ya kuwa na dalili iliyo dhahiri kabisa.

Kwa hiyo, yeyote aliyeshikamana na lolote la Sunnah ambayo imeshuhudiwa kuwa ni Swahiyh hata kama imepinga kauli ya baadhi ya Maimaam, hatokuwa anapingana na madhehebu yao, wala hatopotoka katika njia zao, bali mtu huyo atakuwa anawafuata wote na atakuwa amekamata kile kilichoaminiwa zaidi akishika mkono ambao hautavunjika. Lakini hii haitakuwa hali ya yule anayeziweka kando Sunnah Swahiyh kwa sababu tu zimepingana na rai za Maimaam, bali mtu huyo atakuwa sio mtiifu kwao na amepingia kauli zao hizo za juu. Na tunaona Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema:

﴿ فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي

أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴾

((La! Naapa kwa Mola wako! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa.))<sup>66</sup>

﴿ فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ



((Basi na watahadhari wanaokhalifu amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu iumizayo))<sup>(67)</sup>

<sup>66</sup> An-Nisaa 4: 65

<sup>67</sup> An-Nuur 24: 63

Haafidhw Ibn Rajab Al-Hanbaliy (رحمه الله) amesema: "Kwa hivyo ni wajibu kwa mtu yeyote anayesikia amri ya Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) au kuijua, kuielezea kwa Ummah, kuwapa nasaha ya dhati na kuwaamrisha kufuata amri zake japo kama itakuwa ni kinyume na rai ya mtu mkubwa. Hii ni kwa sababu hukmu ya Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) ina haki zaidi kuheshimiwa na kufuatwa kupita rai za mtu yeyote mkubwa aliyekwenda kinyume bila ya kujua na amri za Mtume katika jambo lolote. Ndio maana Maswahaba na waliofuatia walimpinga yeyote aliyekwenda kinyume na Sunnah Swahiyh, mara nyingine wakiwa wakali katika kuwapinga kwao<sup>(68)</sup>, sio kutokana na kumchukia huyo mtu, bali alikuwa ni mpenzi wao na mwenye kuheshimiwa, lakini kwa sababu Mjumbe wa Allaah alikuwa mpenzi wao zaidi na amri zake zilikuwa juu ya amri za viumbe wengine. Hivyo inapokuwa amri ya Mtume na ya mtu mwengine zinapingana, amri ya Mtume huwa ndiyo ipasayo kutiliwa nguvu na kutekelezwa. Hakuna katika hili lingeliwazua wasimheshimu

---

<sup>68</sup> Japokuwa ni dhidi ya baba zao na walimu wao, kama Atw-Twahaawiy katika *Sharh Ma'aaniy Al-Aathaar* (1/ 372) na Abu Ya'laa katika Musnad yake (3/ 1317) wamesimulia, ikiwa na isnaad ya watu walioaminika kutoka kwa Saalim bin 'Abdillaah bin 'Umar (رحمه الله) ambaye amesema:

"Nilikuwa nimekaa na Ibn 'Umar (رضي الله عنه) msikitini siku moja, alikuja mtu kutoka Syria na akamuuliza kuhusu kuendeleza 'Umrah pamoja na Hajj (Inayojulikana kama ni Hajj At-Tamaattu'). Ibn 'Umar akajibu: 'Ni vizuri na jambo jema'. Kisha mtu akasema: 'Lakini baba yako (yaani 'Umar bIn Al-Khattwaab) alikuwa akikataza' Basi Akasema,' Ole wako! Ikiwa baba yangu alikuwa akikataza kitu ambacho Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akifanya na kuamrisha, je, utakubali rai ya baba yangu au amri ya Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم)?' Akajibu: 'Amri ya Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم)' Akasema: 'Basi nenda zako mbali na mimi' Ahmad (Namba 57000) amesimulia kama hivyo kama alivyosimulia At-Tirmidhiy (2/ 82) na amekiri kuwa ni Swahiyh.



Vipi wachukiwe hayo ikiwa wamewajibisha wafuasi wao kama ilivyo, na kama tulivyoona, kuwa wameamrisha waziache kando rai zao zinazokwenda kinyume na za Sunnah. Bali Imaam ash-Shaafi'iy (رحمه الله) aliwaambia Maswahaba zake kuzihusisha kwake Sunnah zilizo Swahiyh pia, japo kama hakuzitekeleza au katekeleza zilizo kwenda kinyume nazo. Hivyo mhakiki Ibn Daqiyq alipokusanya pamoja katika mjalada mzito, mas-ala ambayo kila mmoja katika kauli za madhehebu ya Maimaam wanne kuwa yamekwenda kinyume na Hadiyith Swahiyh, kama alivyoandika mwanzoni mwake: "Imekatazwa kuhusisha majibu haya kwa Maimaam waliojitahidi na ni fardhi kwa wanasheria wanaofuata rai zao kujua hizi ili wasije kuzinukuu wakawazulia"<sup>71</sup>

### Wafuasi Wa Maimaam Wanatakiwa Kuacha Rai Zao (Maimaam) Ikiwa Zinapingana na Sunnah

Kutokana na yote tuliyotaja, wafuasi wa Maimaam, **((Fungu kubwa katika wa mwanzo Na wachache katika wa mwisho))**<sup>(72)</sup> hawakubali rai za Imaam wao, bali wanazipuuzwa nyingi wanapotambua kuwa zinakwenda kinyume na za

---

<sup>69</sup> Bali atalipwa thawabu kwa sababu ya kauli ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم): ((Qaadhi akipitisha hukmu, akifanya juhudi (ijtihaad) na hukmu ikawa Swahiyh atapata thawabu mbili. Akifanya juhudi (ijtihaad) na akahukumu kimakosa, atapata thawabu moja)) [Imesimuliwa na Al-Bukhaariy, Muslim na wengineo]

<sup>70</sup> Imenukuliwa katika tanbihi za 'Iyqaadhw al-Himam' (Uk. 93)

<sup>71</sup> Fulaaniy (Uk. 99)

<sup>72</sup> Suratul Al-Waaqi'ah 56: 13-14

Sunnah. Hata Maimaam wawili Muhammad Ibn Al-Hasan na Abu Yuusuf (رحمهما الله) walikhitilafiana na Shaykh wao Abu Haniyfah 'Fiy Nahw thuluth al-madhhab'<sup>(73)</sup> kama vitabu vya masaail vinavyohibitisha. Imesemwa hivyo hivyo kuhusu Imaam Al-Muzaniy<sup>(74)</sup> na wafuasi wengineo wa Ash-Shaafi'iy na Maimaam wengine. Tungelianza kutoa mifano majadiliano yangeliendelea kuwa marefu na tungelitoka nje ya makusudio katika mas-ala utangulizi huu, hivyo tutajiwekea mipaka kwa mifano miwili:

1) Imaam Muhammad amesema katika Muwattwaa yake<sup>(75)</sup> (Uk. 158). "Ama Abu Haniyfah hakuona kuwa kuna Swalah ya kuomba mvua, lakini kauli yetu ni kwamba Imaam anaswali Rak'ah mbili na anaomba du'aa na anashika shuka yake..."

2) Tunaye 'Iswaam bin Yuusuf Al-Balkhiy mmoja wa wafuasi wa Imaam Muhammad<sup>(76)</sup> na mtumishi wa Imaam Abu Yuusuf<sup>(77)</sup> ambaye akitoa hukmu kinyume na Imaam Abu

---

<sup>73</sup> Ibn 'Aabidiyn Katika 'al-Haashiyah (1/ ) na Al-Laknawiy kaipa chanzo chake kutoka katika *An-Naafi' al-Kabiyr* (Uk. 93) ya Al-Ghazaaliy.

<sup>74</sup> Yeye mwenyewe amesema katika mwanzo wa 'Mukhtaswar Fiy Fiqhis-Shaafi'iy' (iliyochapishwa katika pembizo ya 'Al-Umm') "Kitabu hiki ni uchaguzi kutoka elimu ya Muhammad bin Idriys Ash-Shaafi'iy (رحمته الله) na kutokana na maana ya kauli zake kumsaidia yeyote anayekitaka akiwa anajua makatazo ya kufuata rai yake au ya yoyote mwengine ili mtu azingatie Dini yake"

<sup>75</sup> Ambako ameelezea kumpinga Imaam wake katika masaail ishirini (Namba 42, 44, 103, 120, 158, 169, 172, 173, 228, 230, 240, 244, 274, 275, 284, 314, 331, 338, 355, 356 kutoka *Ta'liyyq Al-Mummajjid 'alaa Muwattwa' Muhammad* (Tanbihi muhimu ya Muwattwa ya Muhammad)

<sup>76</sup> Ibn 'Aabidiyn amemtaja miongoni katika 'Al-Haashiyah' (1/ 74) na katika

*Rasm Al-Muftiy* (1/17). Qurayshi amemtaja katika 'Al-Jawaahiyir Al-Madhwiyyah fiy Twabaqaat Al-Haniyfah' (uk. 347) na akasema: "Alikuwa ni msimulizi wa Hadiyth wa kutegemewa. Yeye na kaka yake Ibraahiyim walikuwa Mashaykh wawili wa Al-Balakh katika zama zao".

<sup>77</sup> *Al-Fawaaid Al-Bahiyyah Fiy Taraajim Al-Hanafiyyah* (uk. 116)

Haniyfah kwa sababu hakujua ushahidi wake na ushahidi mwingine ulijitokeza kwake wenyewe hivyo alikuwa akiutolea hukmu:<sup>(78)</sup> . Hivyo alinyanyua mikono katika rukuu (kwenye Swalah) na anaponyanyuka<sup>(79)</sup> kama ilivyo mutawaatir Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) bali Maimaam wake watatu (yaani Abu Haniyfah, Abu Yuusuf na Muhammad) wamesema vinginevyo na hawakumzuia kutekeleza Sunnah. Huu ni mfano ambao kila Muislamu inampasa kuwa nao kwani tumeshaona kutokana na ushahidi wa Maimaam wanne na wengineo huko juu.

**Kuhitimisha:** Nina matumaini ya dhati kwamba hakuna mfuasi wa Imaam yeyote atakayekimbilia kushutumu kanuni za kitabu hiki na aache kunufaika na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) zilokuwemo kwa hoja kwamba ni kinyume na madhehebu yake. Bali natumai kwamba badala yake atakumbuka tuliyoyatanguliza miongoni mwa kauli za Maimaam katika kuwajibika kutekeleza Sunnah na kutojali kauli zao zinazopingana na Sunnah. Na atambue kwamba kushutumu kanuni hizi, ni kumshtumu Imaam yeyote anayemfuata miongoni mwao, kwani sisi tumechukua methodolojia/Manhaj kutoka kwao kama tulivyotangulia kubainisha. Basi atakayekengeuka kuwafuata katika njia hii yumo katika hatari kuu, kwani hivyo ni kuzikengeuka Sunnah. Na hali tumearishwa kuzirejea na kuzitegemea pale tunapokhitilafiana kama Anavyosema Allaah (سبحانه وتعالى):

---

<sup>78</sup> *Al-Bahr Ar-Raiiq* (6/ 93) na *Rasm Al-Muftiy* (1/ 28)

<sup>79</sup> *Al-Fawaaid* ... (uk. 116) kisha muandishi akaongeza tanbihi yenye faida: "Kutokana na hii inawezekana kutambulika ubatilifu wa usimulizi wa Makhuul kutoka kwa Abu Haniyfah: 'Kwamba mwenye kunyanyua mikono yake katika Swalah, Swalah yake itakuwa batili' ambayo Amiyar mwandishi wa *al-Itqaaniy* alivyohadaiwa kama ilivyotajwa kaitka historia yake. 'Iswaam Ibn Yuusuf, mfuasi wa Abu Yuusuf alikuwa akinyanyua mikono yake.

﴿ فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا

فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٥٠﴾

((La! Naapa kwa Mola wako! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utakayotoa, na wanyenyekee kabisa.))<sup>(80)</sup>

Namuomba Allaah (سبحانه وتعالى) Atujaalie miongoni mwa wale Asemao:

﴿ إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَنْ

يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا ۗ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥١﴾

((Hakika kauli ya Waumini wanapoitwa kwa [maneno ya] Allaah na Mtume Wake ili awahakumu baina yao, husema: "Tumesikia na Tumetii." Na hao ndio wenye kufaulu))<sup>(81)</sup>

## Shubuhaat (Mambo Yenye Utata) Na Majibu Yake

Hayo ndiyo niliyokuwa nimeyaandika tokea miaka kumi na tano katika utangulizi wa kitabu hiki. Na katika kipindi hiki, imetudhihirikia kuwa haya yana athari nzuri kwa vijana wa Kiislamu katika kuwaongoza kwenye wajibu wa kurejea katika chanzo halisi cha Uislamu (Qur-aan na Sunnah) katika Dini yao na 'Ibaadah zao. Hakika na himdi ni ya Allaah, idadi ya wanaoitekeleza Sunnah na wenye kufanya 'Ibaadah imeongezeka kati yao mpaka wamekuwa maarufu kwa hilo.

---

<sup>80</sup> An-Nisaa 4: 65

<sup>81</sup> An-Nuur 24: 51

Lakini pamoja na hivyo, nimelahidhi kuwa baadhi yao wameondokewa na ile hamasa ya kuyatekeleza hayo, si kwa kuwa wana shaka juu ya wajibu wa hilo baada ya kuwaletea Aayah na maelezo toka kwa Maimaam kuhusu wajibu wa kurejea kwenye Sunnah, bali ni kutokana na Shub-ha wanazozisikia toka kwa baadhi ya Mashaykh wafuataji bila dalili au hoja.

Kwa ajili hiyo, nimeona ni vyema kuliibua suala hili na kulijibu ili baadhi ya hao waliosita wahamasike katika kuifanyia kazi Sunnah pamoja na wenye kuifanyia kazi hata wawe ni katika kundi lililookoka kwa Idhini ya Allaah Ta'ala.

### 1- Baadhi Yao Wanasema:

“Hakuna shaka kuwa kurejea katika Uongofu wa Mtume wetu (صلى الله عليه وآله وسلم) katika masuala ya Dini yetu ni jambo la wajibu na hususan ikiwa linalohusika ni suala la kiibada tu lisilo na uwanja wa kutoa rai wala kufanya ijtihaad ndani yake, kwa vile ni masuala yaliyofungwa kwa matini (tawqiyfiah) kama Swalahah kwa mfano. Lakini mara kwa mara tunawasikia baadhi ya Mashaykh wafuataji bila dalili au hoja wakiliamuru hilo, bali tunawakuta wakikubali kuwepo makhitilafiano wakidai kuwa huo ni ukunjufu kwa ummah huku wakitoka dalili kwa Hadiyith ya:

(اختلاف أمتي رحمة) wanayoikariri mara kwa mara katika mnasaba kama huu wakiwajibu Answaar As-Sunnah. Hivyo inaonekana kwamba Hadiyith hii inakwenda kinyume na njia unayoilingania, na kitabu chako hiki na vinginevyo umevitunga juu ya njia hii hii. Je, unasemaje kuhusu Hadiyith hii?”

**Nitalijibu Swali Hili Kwa Pande Mbili:**

**Kwanza:**

Hadiyth si sahihi bali ni batili na haina asili. Al-'Allaamah As-Subkiy anasema:

“Sikuikuta ikiwa na sanad sahihi, au dhaifu, au hata mawdhu'u.”

Ninasema:

“Imepokelewa kwa tamko la:

(اختلاف أصحابي لكم رحمة)

Na:

(أصحابي كالنجوم فبأيهم اقتديتم اهتديتم)

Na Hadiyth zote hizi mbili si sahihi. Hadiyth ya kwanza haina maana wala msingi, na nyingine ni ya kutungwa. Nimehakiki yote hayo katika (*Silsilatul Ahaadiyth Adhw-Dhwa'iyfah wal-Mawdhwu'ah* “Mlolongo Wa Hadiyth Dhaifu Na Za Kutungwa” Nambari 58, 59 na 61).”

**Pili:**

Hadiyth pamoja na udhaifu wake, inakwenda kinyume na Qur-aan. Aayah zinazokataza makhitilafiano na kuamrisha maafikiano, ni mashuhuri kwa wote hata bila ya kuzitaja. Lakini pamoja na hivyo, hakuna ubaya tukizigusia hapa baadhi yake kwa njia ya mfano tu.

Allaah (سبحانه وتعالى) Anasema:

﴿ وَلَا تَنْزِعُوا عَنْهُمْ لُحْيَهُمْ وَتَحْكُمْ بِحُكْمِ اللَّهِ وَاصْبِرُوا إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴾



**((wala msizozane msije mkaharibikiwa na ikapotea nguvu zenu na vumilieni. Hakika Allaah Yu Pamoja na wanaovumilia))<sup>(82)</sup>**

---

<sup>82</sup> Al-Anfaal 8: 46

Na Anasema:

﴿ مِنَ الَّذِينَ فَرَّقُوا دِينَهُمْ وَكَانُوا شِيَعًا كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ

﴿ فَرِحُونَ ﴿۱۳﴾

((Miongoni mwa wale walioifarikisha Dini yao wakawa makundi makundi, kila kundi kinafurahia kilicho nacho))<sup>(83)</sup>

Na Anasema:

﴿ وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ﴿۱۱۸﴾ إِلَّا مَنْ رَحِمَ رَبُّكَ ﴿۱۱۹﴾

((Na hawataacha kukhitilafiana [watendelea tu] Isipokuwa ambaye Mola wako Amemrehemu))<sup>(84)</sup>

Na ikiwa waliorehemewa na Mola wako hawakhitilafiani, bali wanaokhitilafiana ni watu wa batili, basi vipi iingie akilini kuwa kukhitilafiana ni rehema?

Hivyo basi imethibiti kuwa Hadiyith hii si sahihi sawasawa kwa sanadi au kwa matini<sup>(85)</sup>. Na hapa inatubainikia kwa uwazi kuwa haijuzu kuifanya kuwa ni Shub-ha ili kuacha kuifanyia kazi Qur-aan na Sunnah kama walivyoamuru Maimaam.”

## 2- Shub-ha Ya Pili, Wengine Wanasema:

“Ikiwa makhitilafiano ni jambo lililokatazwa katika Dini, basi mnasemaje kuhusu makhitilafiano kati ya Maswahaba na

---

<sup>83</sup> Ar-Ruum 30: 32

<sup>84</sup>Huud 11: 118-119

<sup>85</sup>Mwenye kutaka maelezo zaidi, arejee kwenye chanzo tulichokitaja nyuma. (Juzuu ya kwanza ya ‘Silsilat Al- Ahaadiyith Adhwa-Dhwa’iyfah wal Mawdhwu’ah”. Chapa ya ‘Maktabatul Islaamiy.

Maimaam waliokuja baada yao? Na je, kuna tofauti kati ya kukhitalafiana kwao na kukhitalafiana kwa wengineo waliokuja baada yao?"

**Jibu:**

"Ndio, kuna tofauti kubwa kati ya makhitalafiano mawili. Na hili linabainika katika mambo mawili:

La kwanza ni sababu yake, na la pili ni athari yake.

Ama kukhitalafiana Maswahaba, hili bila shaka lilitokana na dharura na kutofautiana kimaumbile kati yao katika ufahamu, na wala si kwa chaguo lao. Hiyo ni pamoja na mambo mengi ambayo yalikuwepo katika zama zao yaliyopelekea kukhitalafiana kwao kisha yakaondoka baada yao<sup>(86)</sup>. Na kukhitalafiana kama hivi, hakuwezi kumalizika kabisa, na wala wenye kukhitalafiana hawawezi kupata lawama zilizotajwa katika Aayah zilizotangulia na mfano wa hayo, kwa vile sharti ya kuadhibiwa haipo, nayo ni kukusudia au kuwa na msImaamo usiobadilika.

Ama kutofautiana kwa wenye kufuata tu bila dalili au hoja, basi hao hawapewi udhuru, kwani inaweza kuwabainikia baadhi yao dalili ya wazi toka katika Qur-aan au Sunnah ikiunga mkono madhehebu mengine ambayo wao si wafuasi wake, kisha wakaipuuza, eti kwa vile iko kinyume na madhehebu yao, kana kwamba madhehebu kwao ndio asili na ndio Dini aliyokuja nayo Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم), na kuwa madhehebu mengine ni Dini nyingine iliyonasikhiwa.

---

<sup>86</sup> Rejea "Al-Ihkaam Fiy Uswuul Al-Ahkaam" cha Ibn Hazm, na "Hujjatu Allaah

Al-Baalighah" cha Ad-Dahlawiy, au risalah yake maalum katika utafiti huu iitwayo "Aqdu Al-Jayyid Fiy Ahkaam Al-Ijtihad wat Taqliyd".



Na wengine kati ya hao, wako kinyume na hivyo. Hawa wanayaona madhehebu haya - juu ya khitilafu pana - kama ni shari'ah nyingi tofauti.

Ndio kama walivyolieleza hilo baadhi ya wenzao waliokuja baada yao<sup>(87)</sup> wakisema:

“Hakuna ubaya kwa Muislamu kukifuata chochote akitakacho na kukiacha akitakacho, kwani yote ni shari'ah”.

Na hawa na wengineo wanaweza kutoa hoja ya kubakia katika makhitilafiano kwa kuitumia Hadiyith batili ya (اختلاف أمّتي رحمة). Na mara ngapi tunawasikia wakiitolea ushahidi wa hayo.

Baadhi yao wanabainisha kasoro ya Hadiyith hii na wanaiweka sawa wakisema:

“Makhitilafiano bila shaka yalikuwa ni rehma, kwani ndani yake kuna ukunjufu kwa umma”.

Pamoja na kuwa ubainishaji huu wa kasoro unakwenda kinyume na Aayah swariyh (zilizo wazi) zilizotangulia na makusudio ya maneno ya Maimaam yaliyotangulia, lakini hata hivyo, matini imerejeshwa na baadhi yao”.

Ibn Al-Qaasim anasema:

“Nimemsikia Maalik na Layth wakisema kuhusiana na kukhitilafiana Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم): Si kama walivyosema watu kuwa (kuna ukunjufu ndani yake) si hivyo, bali ni kukosea na kupatia”<sup>(88)</sup>.

Na Ash-hab anasema:

“Aliulizwa Maalik kuhusu mtu aliyechukua Hadiyith aliyohadithiwa na watu wa kuaminika toka kwa Maswahaba

---

<sup>87</sup> Tazama “Faydhw Al-Qadiyr” ya Al-Manaawiy (1/209) au “Silsilat Al-Ahaadiyith Adhw-Dhwa'iyfah” (1/76-77) chapa ya Maktab Al-Islaamiy.

<sup>88</sup> Ibn 'Abdil-Barr katika “Jaami' Bayaan Al-'Ilm” (2/81-82).

wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم): Je, unaona katika hilo ukunjufu?"

Akasema: "Hapana, naapa kwa Allaah mpaka aipatie haki. Haki haiwi ila moja, kauli mbili zenye kukhitalafiana zinakuwa sawa zote? Haiwi haki na sawa ila moja"<sup>(89)</sup>.

Al-Muzaniy anasema:

"Hakika Maswahaba wa Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) walikhitalafiana. Walipashana makosa wao kwa wao, na baadhi yao walizidadisi kwa kina kauli za wengine. Na lau yote wayasemayo yangelikuwa sawa kwao, basi wasingelifanya hilo. Na 'Umar bin Al-Khattwaab alighadhibika kutokana na makhitalafiano kati ya Ubayy bin Ka'ab na Ibn Mas'uud kuhusiana na suala la kuswali kwa nguo moja. Ubayy alisema: "Kuswali kwa nguo moja ni jambo jema zuri. Naye Ibn Mas'uud akasema: "Hakika lilikuwa hilo wakati nguo ni chache". Hapo 'Umar akatoka akiwa ameghadhibika akasema: "Watu wawili katika Maswahaba wa Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) wenye kutegemewa wamekhitalafiana. Na hakika Ubayy amesema kweli, na Ibn Mas'uud hakufanya taksiri. Na mimi sitaki kumsikia yeyote anakhitalafiana katika hilo baada ya makamu yangu haya, isipokuwa nitamfanya hivi na hivi"<sup>(90)</sup>.

Al-Muzaniy anasema tena:

"Aliyejuzisha makhitalafiano na akadai kuwa Maulamaa wawili wakifanya ijtihaad katika suala moja, na mmoja wao akasema ni halali, na mwengine akasema ni haramu, ya kuwa kila mmoja wao ameipatia haki katika ijtihaad yake, tunamuuliza: Je, unasema hili kwa kutumia asli au qiyaas? Akisema ni kwa kutumia asli, tutamuuliza: Vipi inakuwa asli nailhali Qur-aan inapinga makhitalafiano? Na akisema ni kwa qiyaas, tutamuuliza: Vipi usuul ikanushe makhitalafiano, na ijuzu

---

<sup>89</sup> Rejea iliyotangulia (2/82, 88-89)

<sup>90</sup> Rejea iliyotangulia (2/83-84)

kwako uifanyie kipimo cha kujuzu makhitilafiano? Hili halijuzu kwa mwenye akili sembuse Mwanachuoni”<sup>(91)</sup>.

Ikiwa mtu atasema: “Uliyoyaeleza kuhusu Imaam Maalik ya kuwa haki ni moja na haiwi nyingi yanakwenda kinyume na yaliyopo katika kitabu cha (المدخل الفقهي) cha Ustaadh Az Zarqaa (1/89):

(Na hakika Abu Ja’afar Al-Mansuur, kisha baada yake Ar-Rashid, waliazimia kuchagua madhehebu ya Maalik na kitabu chake (الموطأ) kuwa ndio kanuni ya kishari’ah. Lakini Maalik mwenyewe aliwakataza hilo akawaambia: “Hakika Maswahaba wa Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) walikhitilafiana katika furuu, wakasambaa miji mbalimbali, na wote wako katika haki).

Nami nasema:

“Kisa hiki ni maarufu na mashuhuri toka kwa Imaam Maalik (رحمه الله). Lakini kauli yake mwisho wa kisa hiki isemayo “na wote wako katika haki” ni kitu ambacho asli yake siujui kabisa toka kwenye riwaya au vyanzo nilivyovipitia<sup>(92)</sup> isipokuwa riwaya moja tu iliyotolewa na Abu Na’iym katika (الحلية) (6/332) kwa isnadi ambayo ndani yake yumo Al-Miqdaam bin Daawud ambaye Adh-Dhahabiy amemworodhesha katika kundi la (madhaifu). Pamoja na hivyo, tamshi lake: (na kila mmoja ana haki kwake mwenyewe), na neno (kwake mwenyewe), linaonyesha kuwa riwaya ya (المدخل) imeingiliwa. Na kwa nini isiwe hivyo nailhali inakwenda kinyume na yale yaliyopokelewa na watu wa kuaminika toka kwa Imaam Maalik kuwa haki ni moja na haiwi nyingi kama tulivyobainisha kabla?

---

<sup>91</sup> Rejea hiyo hiyo (2/89)

<sup>92</sup>Rejea “Al-Intiqaa” cha Ibn Al-Barr (41) na “Kashf Al-Mughatwaa fiy Fadhl Al-Muwatwaa” (Uk. 6-7) cha Al-Haafidhw Ibn ‘Asaakir, na “Tadhkirat Al-Haafidhw” cha Adh-Dhahabiy (1/195).

Ibn Abdul Barr (2/88) anasema:

“Lau kama haki iko katika nyuso mbili zenye kupingana, basi watangu wema wasingelikosoana katika ijtihaad zao, au hukumu zao au fatwa zao. Na mtizamo unakataa kitu na kinyume chake kuwa sawa chote. Hakika ametia fora aliyesema: “Kuthibitisha vinyume viwili kwa pamoja katika hali ni kubaya zaidi kunakoletwa katika yasiyowezezana”.

Ikiwa patasemwa: Ikithibiti kuwa riwaya hii ni batili toka kwa Imaam, basi ni kwanini Imaam alimkatalia Al-Mansuur kuwakusanya watu katika kitabu chake cha (الموطأ) na wala hakumjibu hilo?”

Ninasema:

“Pazuri zaidi nilipopapitia katika riwaya ni yale yaliyoelezewa na Al-Haafidh ibn Kathiyr katika (شرح اختصار علوم الحديث) (uk 31), ni kuwa Imaam alisema:

“Hakika watu wamekusanya na wameyaona mambo ambayo sisi hatukuyaona”.

Na hii ni katika ukamilifu wa elimu yake na uadilifu wake kama alivyosema ibn Kathiyr (رحمه الله).

Kwa hivyo basi, imethibiti kuwa makhitilafiano ni shari tupu, na wala si rehma. Lakini kuna makhitilafiano ambayo mtu hubebeshwa kwayo makosa kama makhitilafiano ya kasumba za kimadhehebu, na kuna mengine ambayo mtu habebeshwi kama makhitilafiano kati ya Maswahaba na Maimaam waliowafuata. Tunamwomba Allaah Atufufue katika kundi lao na Atuwezeshe kuwafuata”.

Na kwa hivi, inabainika kuwa makhitilafiano ya Maswahaba si sawa na makhitilafiano ya wafuataji bila dalili au hoja.

Na kwa kuhitimisha hayo:

Maswahaba walikhitalifiana kwa kulazimika. Lakini pamoja na hivyo, walikuwa wakipinga makhitilafiano na kuyakimbia pale mwanya unapopatikana.

Ama waigaji bila dalili au hoja – pamoja na kuweza kwao kumalizana na hilo ijapokuwa katika kundi kubwa kati yao – wao hawakubaliani, na wala hawalifanyii hilo juhudi, bali wanalikubali. Basi ni umbali ulioje kati ya makhitilafiano mawili. Na hii ni tofauti kwa upande wa sababu.

Ama tofauti kwa upande wa athari, basi hili liko wazi zaidi. Na hii ni kwa vile Maswahaba Allaah Awaridhie – pamoja na kukhitalifiana kwao kunakojulikana katika furuu – walikuwa wakilinda upeo wa kulinda picha ya umoja, na wakijiweka mbali iwezekanavyo na kila lile lenye kuparaganyisha neno na kupasua safu. Kwa mfano, walikuwepo wenye kuona kuwa inajuzu kusoma BismiLlaahi kwa sauti wakati ambapo wengine walikuwa hawaoni hivyo.

Walikuwepo wanaoona kuwa ni jambo mustahabu kunyanyua mikono, wakati wengine hawaoni hivyo. Lakini pamoja na hivyo, wote walikuwa wakiswali pamoja nyuma ya Imaam mmoja, na hakuna hata mmoja wao aliyeona inda kuswali nyuma ya Imaam anayetofautiana naye kimadhehebu.

Ama wafuataji bila dalili au hoja, hawa makhitilafiano yao yako kinyume kabisa na hivyo. Na hilo limeleta athari mbaya sana ya kuwaparaganyisha Waislamu katika Swalah ambayo ni nguzo kuu ya pili baada ya shahada mbili. Hawa wanakataa kuswali wote nyuma ya Imaam mmoja kwa hoja kuwa Swalah ya Imaam huyo ni batili au makruhu kwa uchache kwa yule mwenye kukhitalifiana na Imaam huyo kimadhehebu. Na bila shaka tushayasikia hayo, na tumeyaona kama walivyoyaona

wengineo<sup>(93)</sup>. Vipi isiwe hivyo nailhali baadhi ya vitabu vya madhehebu mashuhuri vimelieleza hilo kama ni karaha au ni batili? Na matokeo ya hayo ni kukuta mihrabu nne katika Msikiti mmoja wanaswali humo Maimaam wanne wakiandamana. Na utakuta watu wanamsubiri Imaam wao huku Imaam mwengine anaendelea kuswalisha.

Si hivyo tu, bali makhitalafiano yamefikia kugumu zaidi ya hapo kwa wafuataji bila dalili au hoja. Mfano wa hilo ni kuzuia kuoana kati ya wafuasi wa Hanafiy na Shaafi'iy. Kisha ikatolewa fatwa toka kwa mfuasi mashuhuri wa Kihanafi ajulikanaye kama (Mufti Ath-Thaqalayn). Yeye amejuzisha mwanamume wa Kihanafi kumwoa mwanamke wa Kishaafi'iy akilitolea sababu hilo akisema: “Kwa ajili ya kumteremsha (mwanamke) ngazi ya Ahlul Kitaab”<sup>(94)</sup>.

Na dhana ya hilo – na dhana za vitabu vya kuaminika kwao – ni kuwa haijuzu kinyume cha hivyo, nako ni mwanaume wa Kishaafi'iy kumwoa mwanamke wa Kihanafiy. Ni kama isivyojuzu kwa Myahudi au Mkristo kumwoa mwanamke wa Kiislamu.

Mifano hii miwili ni miongoni mwa mifano mingi inayompambanulia mtu yoyote mwenye akili nzuri athari mbaya iliyoletwa na ikhitalafu za watu waliokuja baadaye na kulishupalia kwao suala hili kinyume na Ikhitalafu za wale waliotangulia katika ummah yaani (Salafi) ambao kukhitalifiana kwao hakukuwa na athari mbaya kwa Ummah. Kwa hiyo wao (Salafi) wameokoka kuwa miongoni mwa wale wanaokatazwa kukhitalifiana katika Dini kinyume na watu wa mwisho (ambao

---

<sup>93</sup> Rejea Mlango wa nane wa kitabu “*Ma La Yajuuzu Fiyhi Al-Khilaaf*” (Uk, 65- 72) utakuta mifano mingi ambayo tumeashiria hapa, baadhi yao ikiwahusu Maulamaa wa Al-Azhar.

<sup>94</sup> “*Al-Bahr Ar-Raaq*”

wanaingia katika makemeo hayo). Namuomba Allaah Atuongoze sote katika njia yake iliyonyooka.

Laiti madhara ya kukhitalifiana kwao (watu wa mwisho) yangeishia kwa wao wenyewe tu basi ingekuwa nafuu lakini yanakwenda mbali zaidi hadi kwa watu wengine katika Ummah wa Ulinganiaji (Da'wah). Cha kusikitisha ni kuwa yameenda mbali zaidi hadi kuwafikia makafiri katika miji mingi na sehemu mbalimbali jambo lililowapelekea makafiri hao kutokuingia katika Dini ya Allaah makundi kwa makundi. Katika kitabu; *"Dhwalaamun Minal-Gharbi"* au *"Giza kutoka Magharibi"* cha Muhammad Al-Ghazaaliy, uk. 200 kuna maneno yanayosema:

"Palitokea katika mkutano uliofanyika katika chuo kikuu cha Princeton Marekani; mmoja kati ya wazungumzaji kuuliza swali ambalo mara nyingi huulizwa ndani ya makundi ya Mustashiriquuna (hawa ni watu wasiokuwa Waislamu wanaousoma Uislamu ili kutia shaka (Shub-ha) ndani ya Uislamu na ndani ya wale wanaoshughulika na mambo ya Kiislamu): "Ni kwa mafunzo gani Waislamu watautokea ulimwengu ili wakubaliane juu ya Uislamu wanaoulingania? Ni kwa kufundisha Uislamu kama wanavyoufahamu Masunni? Au ni kwa Uislamu kama wanavyoufahamu Mashia Imaamiyah au Zaydiyah? Kisha kila mmoja kati ya hawa na wale wanatofautiana kati yao.

Kundi moja hufikiri katika mas-alah fulani fikra ile ile ya zamani wakati jingine hufikiria katika mas-alah hayo fikra ya zamani lakini inayoendana na wakati. Kwa kifupi walinganiaji katika Uislamu huacha wanaowalingania katika kuchanganyikiwa kwani wao wenyewe wako katika kuchanganyikiwa.

Na katika utangulizi wa Risaala inayoitwa *"Risaalat As-Sultwaani Ilaa Muslimiy Bilaadi yaabaan"* ya mwanachuoni

mkubwa Muhammad Sultwaan Al-Ma'aswuumiy (رحمه الله), anaeleza kuwa liliulizwa swali na Waislamu wa Japan wanaokaa katika miji ya Tokyo na Osaka kuhusiana na Mashariki ya Mbali kama ifuatavyo: "Nini hakika ya Dini ya Kiislamu? Kisha ni nini maana ya Madhehebu? Na je, ni lazima kwa Muislamu kufuata moja kati ya madhehebu manne yaani awe ima katika Madhehebu ya Maalik, Hanafiy, Shafi'iy au mengine, au si lazima? Kwani kumetokea hapa Japan ikhitilafu na ugomvi mkubwa pale walipotaka makundi mbalimbali yenye fikra tofauti katika watu wa Japan kuingia katika Dini tukufu ya Uislamu na ili wapate utukufu wa Iymaan ya Kiislamu walipoiambia Jumuiya ya Waislamu iliyoko jijini Tokyo juu ya hili, wakasema wengi miongoni mwa Wahindi; wanapaswa wachague madhehebu ya Imaam Abuu Haniyfah kwani yeye ndio taa ya Ummah huu. Na wakasema watu wengi miongoni mwa watu wanaotoka katika sehemu ya Jawa, Indonesia wanatakiwa wawe Mashafi'iy. Wa-Japan waliposikia maneno yao walitahayari sana juu ya walichokusudia na hivyo mas-alah ya Madhehebu yakawa ndio sababu ya kuwafanya wasiingie katika Uislamu.

### **3- Shub-ha Ya Tatu, Wengine wanadai:**

Kuwa maana ya hichi mnacholingania katika kufuata Sunnah na kuacha kuchukua kauli za Maimaam zinazokhalifu Sunnah ni kuacha kuchukua kauli zao moja kwa moja na kufaidika na juhudi na rai zao mbalimbali.

#### **Nasema:**

Kauli hii iko mbali na lililo sawa bali ni batili ya wazi kama inavyoonekana wazi katika maneno yaliyotangulia ambayo yote yanaenda kinyume na kauli hii na kuwa kila tunachokilingania ni kuacha kuyafanya Madhehebu kuwa Dini na kuyanasibisha



pahala pa Qur-aan na Sunnah na kuyafanya kuwa ndio pa kurejelea panapotokea kukhitalifiana katika Dini au wakati wa kutaka kunyambua hukumu za Dini katika mambo yanayojitokeza kama wanavyofanya baadhi ya wasomi wa sasa ambao wameweka hukumu mpya zinazohusu hali za mtu binafsi (*Ahwaal-Shakhsiyah*), ndoa, na Talaka na mengineyo pasina kurejea katika Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume ili wajue la sawa ni lipi na lisilo sawa ni lipi na la haki ni lipi na batwili ni ipi, bali wanachofanya ni kupita katika njia ya (Ikhitilafu yao ni Rehma) na kufuata rukhsa na wepesi au Maslaha. Ni bora iliyoje kauli ya Sulaymaan Taymiy (رحمه الله) aliposema: “Ukichukua rukhsa ya kila msomi basi itakusanyika kwako shari yote”.

Amepokea maneno haya Ibn ‘Abdil Barr (2/91-92) na akasema ‘Uqbah: “Hii ni Ijmaa’ sijui kinyume nayo”.

Hichi ndicho tunachochukia na kama unavyoona kinawafikiana na Ijmaa’.

Ama kurejea katika kauli zao na kufaidika nazo na kuzitumia katika kujua haki katika yale waliyokhitalifiana katika lile ambalo halina dalili ya moja kwa moja kutoka katika Qur-aan au Sunnah au lenye haja ya kupambanuliwa zaidi, hili ni jambo ambalo hatulipingi bali tunalihimiza kwani kuna faida kubwa inayotarajiwa kupatikana kwa wale wenye kupita njia ya kufuata Qur’aan na Sunnah.

Amesema mwanachuoni mkubwa Ibn ‘Abdil Barr (رحمه الله) (2/172): “Ni juu yako ewe ndugu yangu kuhifadhi misingi na kuitilia umuhimu, na jua ya kuwa anayejishughulisha na Sunnah na hukumu zilizotajwa ndani ya Qur-aan na akaangaalia kauli za Wanachuoni na kuzifanya kuwa msaada kwake katika Ijitihaad yake na kuwa ni ufunguo wa njia za uoni na kuwa ni tafsiri ya ibara za Sunnah zenye kuwa na uwezekano wa maana zaidi ya moja na ikawa hakumfuata

Atakayeizuia nafsi yake na kuchunguza na akayapinga tuliyoyataja na akaipinga Sunnah kwa rai yake na akaikataa kwa upeo wa uoni wake basi huyu ni mpotevu tena mwenye kupoteza, na asiyeyajua yote hayo na akakomalia na kushupalia kutoa Fat'wa pasina elimu huyo ni kipofu zaidi na amepotea zaidi njia ya Haki.

Hii ndio hakiki isiyo na kificho niache na vijengo katika njia.

#### **4- Shub-ha Ya Nne:**

Kisha kuna utata ulioenea katika wale wenye kuiga ambayo huwazuia kufuata Sunnah ambayo inawabainishia kuwa madhehebu yako kinyume na Sunnah hiyo; nayo ni utata wao kuwa kufuata Sunnah kunalazimu kumkosoa mwenye madhehebu na kukosoa kwa mtazamo wao maana yake ni kumkosoa Imaam na kwa kuwa kumkosa Muislamu wa kawaida tu hakufai itakuwaje basi kumkosoa Imaam miongoni mwa Maimaam wao?

### Jawabu Ya Hili:

Ni kuwa maana hii ni batili na sababu yake ni kutokufahamu vizuri Sunnah, kama si hivyo basi Muislamu mwenye akili anawezaje kusema hivyo wakati Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) anasema: **((Anapohukumu hakimu akajitahidi akapatia katika hukumu yake basi hupata ujira mara mbili na anapohukumu hakimu akajitahidi akakosea katika hukumu yake basi hupata ujira mmoja))<sup>(95)</sup>.**

Hadiyth hii inapinga maana yao hiyo na inaweka wazi pasina utata wowote kwani kauli ya msemaji ya kuwa; “fulani amekosea” maana yake katika Shari’ah ni kuwa “amelipwa ujira mmoja” ikiwa ni mwenye kulipwa katika rai ya mwenye kumkosoa, vipi basi atadhanika kuwa kukosolewa kwake ni kutukanwa, hakuna shaka kuwa utata huu ni batwili na inampasa kila mwenye kuwa nayo aachane nayo la sivyo yeye ndiye atakayekuwa anawatukana Waislamu wote, yaani atakuwa hawatukani watu wa kawaida tu bali hata Maimaam wakubwa na hata Maswahaba na Matabi’iyna na waliokuja baada yao katika Maimaam wenye kujitahidi na wengineo kwani tunajua kuwa watu hawa watukufu walikuwa wanakosoana na wanajibizana<sup>(96)</sup>, kuna yoyote mwenye akili Imaam mwenye kusema kuwa kwa kufanya hivi walikuwa wanatukanana wakati imethibiti kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kuwa alimkosa Abu Bakr katika kuawili kwake ndoto fulani ambayo aliota mtu mmoja; Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akamwambia: “Umepatia sehemu yake na kukosea sehemu nyingine”<sup>(97)</sup>, je Mtume alimtukana au kumfedhehesha Abu Bakr kwa maneno haya?

Ajabu ya athari ya utata huu kwa watu wake ni kuwa unawazuia kufuata Sunnah yenye kupingana na madhehebu yake kwani kwa mtazamo wake kuifuata Sunnah inayopingana na madhehebu yake ni kumtukana Imaam wake, ama kumfuata kwake-hata kama kunapingana na Sunnah-maana yake ni kumheshimu na kumtukana,

---

<sup>95</sup> Al-Bukhaariy na Muslim

<sup>96</sup> Tazama maneno ya Imaam Al-Muzaniy yaliyotangulia nyuma (Uk, 36) na

maneno ya Al-Haafidhw Ibn Rajab yaliyotangulia (Uk, 29)

<sup>97</sup> Al-Bukhaariy na Muslim

kwa hiyo wanakomalia kumfuata ili kuondokana na utata huu wa kumtukana Imaam.

Hawa wamesahau wala sisemi kuwa wamejisahaulisha kuwa wao kwa sababu ya utata huu wameingia katika shari kubwa zaidi kuliko walichokikimbia kwani lau msemaji angewaambia; Ikiwa kumfuata kunamaanisha kumheshimu mwenye kufuatwa na kumkhalifu kunaonyesha kumtweza ni vipi basi mumezizujishia nafsi zenu kukhalifu mwendo wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na kuacha kuifuata Sunnah ya Mtume kutokana na kufuata Imaam wa madhehebu fulani yanayopingana na Sunnah ya Mtume ambaye amehifadhiwa na kulindwa na Allaah na kukosea yaani ni Ma'aswuum na kumtweza kusiwe ukafiri? Ikiwa kumkhalifu Imaam kwenu kunazingatiwa ni kumtukana Imaam basi kumkhalifu Mtume ni matusi ya wazi zaidi, bali ni ukafiri wa wazi Allaah Atulinde na hili-lau angewaambia msemaji juu ya hilo wasingeweza kujibu ila kwa neno moja tutumewahi kulisikia kutoka miongoni mwao-nayo ni kauli yao kuwa sisi tumeiacha Sunnah kutokana na kumuamini Imaam wa madhehebu yetu naye ni mjuzi zaidi wa Sunnah kuliko sisi.

Jibu letu kwa neno hili lina sura mbalimbali maneno yanarefuka katika utangulizi huu lakini nitatosheka na sura moja ambayo ni jawabu lenye upambanuzi In shaa Allaah kwa Idhini ya Allaah na ninasema:

“Si Imaam wa madhehebu yenu tu ndiye anayejua Sunnah kuliko nyinyi bali kuna makumi, na mamia ya Maimaam wanaojua Sunnah zaidi yenu inapokuja Sunnah sahihi yenye kupingana na madhehebu yenu- Na ikiwa aliyachukua mmoja kati ya Maimaam hao-kuyachukua na hali ndio hii, itakuwa ni jambo la lazima kwenu kwa sababu neno lenu lililotajwa halitoki hapa kwani mwenye kuwapinga naye atawaambia hali ya kuwa anawapinga: “Sisi tumeichukua Sunnah hii kwa kumuamini Imaam aliyeichukua, kwa hiyo kumfuata wetu ni bora kuliko kumfuata Imaam aliyeikhalifu. Na hii iko wazi wala haifichiki kwa yeyote In shaa Allaah.

### Kwa hiyo ninaweza kusema:

Kitabu chetu hiki kwa kukusanya kwake Sunnah zilizothibiti kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kutakuwa hakuna udhuru kwa yeyote kutokuzifanyia kazi kwani hakuna ndani yake chochote walichokubaliana Wanachuoni kukiacha Allaah Awaepushe na hilo, bali hakuna mas-alah yoyote ndani yake ila Wanachuoni wamesema chochote na ambaye hajasema chochote tunamchukulia udhuru na ni mwenye kulipwa kwani itakuwa hakufikiwa na dalili hiyo moja kwa moja au kafikiwa lakini kwa njia ambayo kwake haisimaami kuwa ni hoja au kwa udhuru wowote mwingine katika nyudhuru za Wanachuoni. Ama yule ambaye itathibiti kwake dalili baada yake atakuwa hana udhuru katika kufuata bali iliyo lazima kwake ni kufuata dalili iliyolindwa na kuhifadhiwa (Ma'aswuum) na hilo ndilo kusudio la utangulizi huu na Allaah Anasema:

﴿يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ<sup>ط</sup>

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ سَخُولٌ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٩٨﴾



**((Enyi mlioamini muitikieni Allaah na Mtume Wake Anapokuiteni katika yale yatakayokupeni uhai. Na jueni ya kuwa Allaah Huingia kati ya mtu na moyo wake. Na kwamba Kwake Yeye mtakusanywa))<sup>(98)</sup>**

Na Allaah Anasema kweli naye Anaongoza njia ya sawa Naye ni Mpenzi Aliyekuwa Mbora kabisa na Ndiye Mwenye kunusuru Aliye bora zaidi.

---

<sup>98</sup> Al-Anfaal 8: 24

Na Rehema na Amani za Allaah ziwe juu ya Muhammad na juu ya Ahli zake na Jamaa zake na sifa zote njema Anastahili Allaah Mola wa Ulimwengu.

20/5/1389 H.

Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy

### **Tanbihi Ya Mfasiri**

Baadhi ya Adhkaar na du'aa nimeziweka kwa matamshi yake pamoja na maana yake na kwengine matamshi pekee kwani katika hali nyingine, ni wepesi kwa mwenye kusoma lugha ya Kiswahili kutamka na kuhifadhi kirahisi kuliko kuweka maana pekee.

**SWALAH YA MTUME (صلى الله عليه وسلم)**

Imeelezwa Kutoka Mwanzo Mpaka Mwisho Kama

Kwamba Unaiona

**(Swalini Kama Mlivyoniwa Nikiswali)**

[Al-Bukhaariy]

## Kuelekea Ka'abah

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alipokuwa anasimama kuswali Swalah zote za Fardhi na za Sunnah alikuwa anaelekea upande wa Ka'abah<sup>(99)</sup>

Naye Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliliamrisha hilo kwa kumwambia "mtu aliyeswali vibaya"<sup>(100)</sup>: **((Unaposimama kuswali, fanya wudhuu sawasawa, kisha elekea Qiblah na upige Takbiyr))<sup>(101)</sup>.**

"Wakati yuko safarini, Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akiswali Swalah za Sunnah na Swalah ya Witr na huku amepanda mnyama popote alipoelekea. (Mashariki au Magharibi)<sup>(102)</sup>

Hilo ni kwa Neno Lake Allaah Mtukufu:

﴿فَأَيْنَمَا تُولُونَ فَثَمَّ وَجْهُ اللَّهِ﴾

**((Basi kokote mnakoelekea, huko kuna Wajihhi wa Allaah))<sup>103</sup>**

Kauli hii inahusiana na Hadiyith hiyo<sup>(104)</sup>.

“Wakati mwengine alipokuwa anataka kuswali Swalah zisizo za fardhi akiwa juu ya ngamia wake, alikuwa akimwelekeza

---

<sup>99</sup> Jambo hili halina shaka yoyote kutokana na mlolongo wa umashuhuri wake (*tawaatur*). Kwa hiyo, halihitaji maelezo zaidi ingawa baadhi ya dalili zitafuata.

<sup>100</sup> Tazama Kiambatisho 3.

<sup>101</sup> Imekusanywa na Al-Bukhaariy, Muslim na Siraaj.

<sup>102</sup> Imekusanywa na Al-Bukhaariy, Muslim na Siraaj. Takhriy yake imetolewa katika “Irwa’a Al-Ghaliyl” (289 na 588).

<sup>103</sup> Al-Baqarah: 115

<sup>104</sup> Muslim. At-Tirmidhiy amekiri kuwa ni Hadiyithi Swahiyh.



Qiblah, kisha akisema *Takbiyr* na akiswali kuelekea popote kule msafara unapoelekea.”<sup>(105)</sup>.

"Alikuwa akifanya rukuu na *Sujuud* huku amempanda mnyama kwa kuinamisha kichwa chake, na akiinamisha kichwa zaidi chini katika *Sujuud* kuliko alivyoinamisha katika rukuu.”<sup>(106)</sup>

"Alipotaka kuswali Swalah za fardhi alikuwa akiteremka kutoka kwa mnyama na akielekea Qiblah.”<sup>(107)</sup>

Ama katika Swalah ya mtaharuki wa vita vilivyopamba moto, Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliweka kwa ummah wake kanuni ya kuswali "wakiwa wamesimama na kutembea kwa miguu yao, au wakiwa wamepanda mnyama, wakielekea Qiblah au kutokuelekea”<sup>(108)</sup>. Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: **((Wanapokutana majeshi Swalah ni *Takbiyr* na kuashiria kwa kichwa tu))**<sup>(109)</sup>

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) pia alikuwa akisema **((Kilichokuweco baina ya Mashariki na Magharibi ni Qiblah))**<sup>(110)</sup>

Jaabir (رضي الله عنه) amesema,

---

<sup>105</sup> Abu Daawuud na Ibn Hibbaan katika "*Ath-Thiqaat*" (1/12) na Adh-Dhiyaa katika "*Al-Mukhtaarah*" ikiwa na sanad hasan. Ibn As-Sukn amekiri kuwa ni Swahiyh na pia Ibn al-Mulaqqin katika "*Khulaaswat Al-Badr Al-Muniyr*" (22/1) na kabla yao, 'Abdul-Haqq Al-Ishbiyli katika "*Ahkaamuh*" (Namba 1394 kwa uhakiki wangu). Ahmad ameitumia kama ni uthibitisho kama alivyoripti Ibn Haani kutoka kwake katika "*Masaailuh*" (1/67).

<sup>106</sup> Ahmad na At-Tirmidhiy ambao wamekiri kuwa ni Swahiyh.

<sup>107</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>108</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>109</sup> Al-Bayhaqiyy na Sanad inayoelekeana na mahitajio ya Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>110</sup> At-Tirmidhiy na Haakim wamekiri kuwa ni Swahiyh. Nimeitowa katika "Irwaa al-Ghaliyl fiy takhriyj Ahaadiyth manaar As-Sabiyl" (292). Uchapisho wake Allaah (سبحانه وتعالى) Ameufanya wepesi.

"Wakati mmoja tulikuwa na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika msafara au kikosi cha jeshi, na kulikuwa na mawingu, tukajaribu kutafuta Qiblah lakini tulikhitalafiana, kwa hiyo kila mmoja wetu akaswali kuelekea upande tofauti na kila mmoja wetu alichora mstari mbele yake ili kuweka alama mahali pake. Ilipofikia asubuhi, tukazitazama tukaona kwamba hatukuswali kuelekea Qiblah. Kwa hiyo tukamuelezea Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) lakini hakutuamrisha tuirudie (Swalah) na akasema:

**((Swalah yenu imetosheleza)).<sup>(111)</sup>**

Na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akiswali kuelekea Bayt Al-Maqdis (na Ka'abah ikiwa mbele yake) kabla ya kuteremshwa Aayah ifuatayo:

﴿ قَدْ نَرَى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَاءِ ط فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضَاهَا ء فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ء وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوا وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ ء



**((Kwa yakini tukiona unavyo geuzageuza uso wako mbinguni. Basi Tutakuelekeza kwenye Qiblah ukipendacho. Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu; na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo...))<sup>112</sup>**

Ilipoteremshwa Aayah hii alielekea Qiblah. Walikuwa watu katika msikiti wa Qubaa' wakiswali Swalah ya Alfajiri, alipokwenda mtu kuwaambia "Hakika Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) ameteremshiwa Aayah jana usiku na ameamrisha kuelekeza uso wake Ka'bah. Basi jueni na elekeeni huko". Nyuso zao zilikuwa zimeelekea Shaam kwa

<sup>111</sup> Ad-Daara Qutniy, Al-Haakim, Al-Bayhaqiy, At-Tirmidhiy, Ibn Maajah na At-Twabaraaniy. Imetolewa katika "Al-Irwaa" (296).

<sup>112</sup> Al-Baqarah 2: 144

## Kusimama Katika Swalah

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akiswali kwa kusimama katika Swalah za fardhi na za Sunnah kwa kufuata maamrisho ya Allaah (سبحانه وتعالى) kama Alivyosema:

﴿ وَقَوْمُوا لِلَّهِ قَنِينًا ﴾

**((...na simameni kwa ajili ya Allaah mkiwa wanyenyekevu))<sup>114</sup>**

Ama katika safari alikuwa akiswali Swalah za Sunnah na huku amempanda (mnyama).

Ameweka kanuni kwa ummah wake kuswali wakati wa khofu kubwa kwa kusimama juu ya mnyama. Na hili ni kwa Neno Lake Allaah Mtukufu:

﴿ حَفِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَىٰ وَقَوْمُوا لِلَّهِ قَنِينًا ﴾ فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ فَإِذَا أَمِنْتُمْ فَأَذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُمْ مَا لَمْ

﴿ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴾

**((Zilindeni Swalah, na khasa Swalah ya katikati,<sup>(115)</sup> na simameni kwa ajili ya Allaah mkiwa wanyenyekevu)) ((Ikiwa**

---

<sup>113</sup> Al-Bukhaariy, Muslim, Ahmad, As-Siraaj, At-Twabaraaniy (3/108/2) na Ibn Sa'ad (1/243). Pia iko katika "Al-Irwaa" (290).

<sup>114</sup> Al-Baqarah, 2: 238

<sup>115</sup> Yaani Swalah ya 'Alasiri kutokana na usemi ulio Swahiyhi wa Maulamaa wengi. Miongoni mwao ni Abu Haniyfah na wanafunzi wake wawili. Kuna

**mnakhofu [Swalini] na hali mnakwenda kwa miguu au mmepanda. Na mtakapokuwa katika amani, basi mkumbukeni Allaah kama Alivyokufunzeni yale mliyokuwa hamyajui))<sup>116</sup>**

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliswali kwa kukaa wakati alipokuwa akiumwa hata akafariki<sup>(117)</sup>.

Vile vile aliswali kwa kukaa kwa mara nyingine kabla ya hivyo wakati alipojeruhiwa, na watu waliokuwa nyuma yake waliswali kwa kusimama, akawaashiria wakae nao, wakakaa (na kuswali). Alipomaliza, akasema, **((Mlikuwa mnataka kufanya kama wa-Fursi na Warumi wanavyofanya, wanawasimamia wafalme wao waliokuwa wanakaa. Kwa hiyo msifanye hivyo tena, kwani Imaam ni kwa ajili ya kumfuata, anapofanya rukuu fanyeni rukuu, anaposimama simameni, anaposwali kwa kukaa na nyinyi swalini kwa kukaa [nyote]).<sup>(118)</sup>**

### Swalah Ya Mgonjwa Katika Hali Ya Kukaa

'Imraan bin Huswayn (رضي الله عنه) alisema: "Nilikuwa naumwa ugonjwa wa bawasili (futuru), nikamuuliza Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) naye akasema:

**((Swali kwa kusimama, ikiwa huwezi, swali kwa kukaa, ikiwa huwezi swali kwa kulala ubavu))".<sup>(119)</sup>**

---

Hadiyth kuhusu kauli hii ambayo Ibn Kathiyr ameiweka katika Tafsiyr yake ya Qur-aan.

<sup>116</sup> Al-Baqarah, 2: 238-239

<sup>117</sup> At-Tirmidhiy ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh na Ahmad.

<sup>118</sup> Muslim na Al-Bukhaariy na imetolewa katika kitabu changu Irwaa' Al-Ghaliyl katika Hadiyth 394.

<sup>119</sup> Al-Bukhaariy, Abu Daawuud na Ahmad.

'Imraan bin Huswayn pia amesema, "Nilimuuliza Mtume ( صلى الله عليه وآله وسلم) kuhusu Swalah ya mtu anayeswali kwa kukaa, akasema:

**((Anayeswali kwa kusimama ni bora, na anayeswali kwa kukaa, thawabu zake ni nusu ya anayeswali kwa kusimama, na anayeswali kwa kulala [na katika riwaya nyingine kwa kulala chali], basi atapata thawabu nusu ya yule mwenye kuswali kwa kukaa)).<sup>(120)</sup>**

Makusudio hapa ni mtu mgonjwa, kwani Anas amesema: "Mtume ( صلى الله عليه وآله وسلم) alitoka mbele ya watu waliokuwa wakiswali kwa kukaa kwa sababu ya ugonjwa, akasema:

**((Hakika Swalah ya mwenye kukaa ni [sawa] na nusu ya Swalah ya mwenye kuswali kwa kusimama)).<sup>(121)</sup>**

Siku moja Mtume ( صلى الله عليه وآله وسلم) alimtembelea mgonjwa na akamuona anaswali (huku ameegemea) juu ya mto. Akauchukua na akautupa (pembeni). Kisha mgonjwa akachukua kipande cha mti ili akiegemea katika Swalah yake. (Mtume) akakichukua akakitupa (pembeni) na akasema:

**((Swali juu ya ardhi ukiweza, na kama huwezi, basi fanya haRak'ahti kwa kichwa chako kwa kufanya *Sujuud* iwe ya kuinama chini zaidi ya ruku)).<sup>(122)</sup>**

---

<sup>120</sup> Al-Bukhaariy, Abu Daawuud na Ahmad. Al-Khatwaabiy amesema:

"Makusudio ya Hadiyth ya 'Imraan ni mgonjwa wa kukisiwa anayeweza kuchechemea na kusimama kwa tabu, na kwa hivyo, thawabu za mwenye kukaa zimefanywa nusu ya mwenye kusimama kwa ajili ya kumpa msukumo asimame ingawa inajuzu kwake kukaa." Al-Haafidhw Ibn Hajr amesema katika *Fat-h Al-Baariy* (2/468): "Nayo ni makisio yenye kukubalika."

<sup>121</sup> Ahmad na Ibn Maajah kwa sanad Swahiyh.

<sup>122</sup> At-Twabaraaniy, Al-Bazaar, Ibn As-Samaak katika "Hadiythih" (2/67) na Al-Bayhaaqiy. Sanad yake ni Swahiyh kama nilivyoeleza katika Silisilah Al-Ahaadiyth As-Swahiyhah (323).

## Swalah Ndani Ya Meli (Chombo Cha Baharini)

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliulizwa kuhusu Swalah katika meli, akasema: ((Swali ukiwa umesimama ila ukiogopa kuzama)).<sup>(123)</sup>

Alipokuwa mzee mtu mzima, alijiwekea kiguzo katika sehemu ya kuswali ili kukiegemea.<sup>(124)</sup>

## Kukaa Na Kusimama Katika Swalah Ya Usiku (Tahajjud)

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa (mara) akiswali usiku mrefu akiwa amesimama na (mara nyingine) akiswali usiku mrefu kwa kukaa. Na alikuwa anaposoma kwa kusimama, hurukuu kwa kusimama, na anaposoma kwa kukaa, hurukuu kwa kukaa.<sup>(125)</sup>

Na wakati mwengine, alikuwa anaswali kwa kukaa, na husoma hivyo hivyo huku amekaa. Na inapobakia katika kisomo chake kiasi cha Aayah thalathini au arubaini hivi, husimama na kuzisoma kwa kusimama, halafu hurukuu na kusujudu. Kisha hufanya hivyo hivyo katika Raka'ah ya pili.<sup>(126)</sup>

---

<sup>123</sup> Al -Bazaar (68), Ad-Daaraqutwniyy na Abdul-Ghaaniy Al-Maqdisi katika "As-Sunan" (2/82). Na Al-Haakim amekiri kuwa ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy ameikubali.

<sup>124</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambao wamekiri kuwa ni Swahiyh kama alivyokiri Adh-Dhahabiy. Nimeiweka katika "As-Swahiyhah" (319) na "Al-Irwaah" (383).

<sup>125</sup> Muslim na Abu Daawuud.

<sup>126</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

Bali aliswali *Aswubh* (Swalah ya Asubuhi)<sup>(127)</sup> kwa kukaa chini katika siku za mwisho za maisha yake alipokuwa katika umri mkubwa na na hilo ilikuwa kabla ya kufariki kwake kwa mwaka mmoja.<sup>(128)</sup>

Vile vile alikuwa akikaa kwa kukunja miguu (mkao wa chuoni).<sup>129</sup>

### Swalah Kwa Kuvaa Viatu Na Maamrishi Ya Kufanya Hivyo

"Alikuwa akisimama (katika Swalah) bila ya viatu wakati mwingine na kuvaa viatu wakati mwingine"<sup>(130)</sup>

Ameruhusu kufanya hivyo kwa Ummah wake na kusema:

**((Mmoja wenu anaposwali, basi avae viatu vyake au avivue baina ya miguu yake, na wala asimkere mtu kwa viatu hivyo)).<sup>(131)</sup>**

Aliwasisitizia kuswali na viatu wakati mwingine, na kusema:

**((Kuweni tofauti na Mayahudi, kwani wao hawaswali na viatu vyao wala na khufu [soksi za ngozi] zao)).<sup>(132)</sup>**

---

<sup>127</sup>Ni Swalah ya Sunnah (usiku au jioni) imeitwa hivyo kutokana na yaliyokuwemo humo ya tasbiyh (Kumtukuza Allaah).

<sup>128</sup>Muslim na Ahmad.

<sup>129</sup> An-Nasaaiy, Ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake (1/107/2), 'Abdul-Ghaaniy Al-Maqdisi katika Sunan yake (80/1) na al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh na adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>130</sup>Abu Daawuud na Ibn Maajah. Ni Hadiyth yenye mapokezi mengi (Mutawaatir) kama alivyotaja atw-Twahaawiy.

<sup>131</sup>Abu Daawuud na Bazaar (53, Az-Zawa'id), al-Haakim amekiri kuwa ni Swahiyh na adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>132</sup> Abu Daawuud na Bazaar

Mara moja moja alikuwa anavivua wakati anaswali na kisha akiendelea na Swalah yake kama alivyosema Abu Sa'iyd Al-Khudriy:

"Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliswali nasi siku moja. Alipokuwa yumo katika Swalah, alivua viatu vyake na akaviweka upande wa kushoto kwake. Watu walipoona hivyo, nao pia wakavua viatu vyao. Alipomaliza kuswali alisema: **((Kwa nini mmevua viatu vyenu?))** Wakajibu: "Tumekuona wewe unavua viatu vyako na sisi pia ndio tukavua viatu vyetu". Akasema: **((Hakika Jibriyl amekuja kwangu na kunijulisha kwamba kulikuwa na uchafu)) au kasema [kulikuwa na] kitu cha madhara)).** Katika riwaya nyingine **((uchafu/ najsi)), basi atazame viatu vyake. Akiona vina uchafu, au kasema kitu katika viatu vyangu, kwa hiyo nikavivua. Kwa hivyo, mmoja wenu anapokwenda msikitini akioona chenye madhara, na [katika riwaya nyingine] najsi, basi avifute kisha aswali navyo)).**<sup>(133)</sup>

"Alipokuwa akivivua, alikuwa akiviweka upande wa kushoto kwake."<sup>(134)</sup>

Na pia alikuwa akisema: **((Mmoja wenu anaposwali, asiweke viatu vyake upande wa kulia wala kushoto kwake, ambako vitakuwa katika upande wa kulia wa mtu, isipokuwa kama kutakuwa hakuna mtu upande wa kushoto, lakini aviweke baina ya miguu yake)).** <sup>(135)</sup>

---

<sup>133</sup>Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah na al-Haakim ambao wamekiri kuwa ni Swahiyh na adh-Dhahabiy na an-Nawawiy wamekubali. Ya kwanza imetolewa katika Irwaa.

<sup>134</sup> Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah na al-Haakim.

<sup>135</sup>Abu Daawuud, An-Nasaaiy na Ibn Khuzaymah (1/110/2) na kwa Sanadi iliyo Swahiyh.



## Swalah Juu Ya Minbar

Mara moja Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliswali juu ya Minbar (na katika riwaya nyingine: iliyokuwa na daraja (vijingazi) tatu<sup>(136)</sup>). Hivyo (akasmama juu yake na akapiga *Takbiyr* na watu nyuma yake wakasema *Takbiyr* wakati yuko juu ya Minbar), (kisha akarukuu juu ya Minbar), halafu akainuka na kushuka kinyume nyume mpaka akasujudu katika kitako cha Minbar. Kisha akarudi (na akafanya kama alivyofanya katika raka'ah ya mwanzo) mpaka akamaliza Swalah yake. Kisha akageuka kwa watu na kusema: **((Enyi watu! Nimefanya hivyo ili mnifuate na mjifunze Swalah yangu)).**<sup>(137)</sup>

## *Sutrah*<sup>(138)</sup> Na Kuwajibika Kwake

"Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akismama karibu na *sutrah*, ili iweko (umbali wa) dhiraatatu baina yake na ukuta"<sup>(139)</sup> na "baina ya sehemu ya *Sujuud* na ukuta (kulikuweko) nafasi ya kuweza kupita kondoo"<sup>(140)</sup>.

---

<sup>136</sup>Hii ni Sunnah kuhusu Minbar, kwamba iwe na daraja tatu, na sio zaidi. Kuwa na zaidi ya daraja tatu ni bid'ah iliyoanzishwa na Bani Umayyah. Ni mara nyingi safu hukatika. Na kuliepuka hilo kwa kuiweka pembezoni mwa upande wa Magharibi wa Msikiti au wa Mihraab, ni bid'ah nyingine. Vile vile ni (bid'ah) kuipandisha katika ukuta wa kusini kama roshani ambako mtu hupanda kwa ngazi zilizoshikanishwa na ukuta! Na uongofu mbora kabisa ni uongofu wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Tazama *Fat-h Al-Baariy* (2/331).

<sup>137</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Riwaya nyingine ni yake Muslim na Ibn Sa'd (1/253). Imetolewa katika "*Al-Irwaa*" (545).

<sup>138</sup>*Sutrah* - "Kinga ya kuzuia" katika Swalah, inakusudia kitu cha kuwekwa mbele ya sehemu ya kusujudu kuinga ili asipite mtu au chochote mbele yake kama ilivyoelezewa katika somo hili.

<sup>139</sup> Al-Bukhaariy na Ahmad.

<sup>140</sup> Al-Bukhaariy na Ahmad.

Alikuwa akisema,

**((Msiswali isipokuwa mbele ya *Sutrah*, na msimuachie mtu kupita mbele yenu, lakini kama mtu akiendelea [kujaribu kupita] basi mzuwieni kwani yuko pamoja na rafiki)) (yaani Shaytwaan).<sup>(141)</sup>**

Alikuwa akisema,

**((Mmoja wenu akiswali mbele ya *Sutrah*, basi awe karibu yake ili shaytwaan asiweze kuivunja Swalah yake)).<sup>(142)</sup>**

Mara nyingine "Alikuwa anaswali mbele ya nguzo ya msikiti."<sup>(143)</sup>

Alipokuwa anaswali (kwenye sehemu ya wazi ambako kulikuwa hakuna kitu cha kutumia kiwe *Sutrah*) alikuwa akiuchomeka mkuki ardhini mbele yake kisha akiswali kuuelekea na watu wakiwa nyuma yake.<sup>(144)</sup> Mara nyingine "alikuwa akiweka kipando chake (mnyama) kisha akiswali

---

<sup>141</sup>Ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake (1/93/1) na Isnaad iliyothibitika.

<sup>142</sup>Abu Daawuud, Bazaar (ukurasa 54 Zawaa'id) na Al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahaabiy na An-Nawawiy wameikubali.

<sup>143</sup>Al-Bukhaariy. *Sutrah* ni lazima kuweko kwa Imaam au mtu anayeswali peke yake hata katika msikiti mkubwa. Ibn Haani amesema katika Masaa'il yake kutoka Imaam Ahmad (1/66) "Abu 'Abdillaah (Imaam Ahmad Ibn Hanbal) aliniona siku moja wakati naswali bila ya *Sutrah* mbele yangu na nilikuwa katika (Swalah ya) Jama'ah (kubwa) msikitini, kwa hiyo akaniambia, "Weka kitu kama *Sutrah*". nikamfanya mtu kama *Sutrah*. Hii inaonyesha kwamba Imaam Ahmad hakutofautisha baina ya msikiti mkubwa au mdogo katika mas-ala ya *Sutrah*. Na hii hakika ni sahihi, lakini hili ni jambo ambalo limesharauliwa na watu wengi pamoja na ma-Imaam wa misikiti katika kila nchi nliyotembea pamoja na nchi za Arabuni ambazo nimeweza kutembea katika mwezi wa Rajab wa mwaka huu (1410). Kwa hiyo ma-Ulamaa waambie watu na kuwanasihhi jambo hili, na kuwafahamisha shari'ah yake na kwamba pia inahitajika kuweko katika misikiti miwili mitukufu.

<sup>144</sup>Al-Bukhaariy, Muslim na Ibn Maajah.

kukielekea kipando chake.<sup>(145)</sup> Lakini hii sio sawa na Swalah katika sehemu ya mapumziko ya ngamia<sup>(146)</sup> ambayo "ameikataza"<sup>(147)</sup> na mara nyingine "alikuwa akichukua tandiko lake (la ngamia) akiliweka kwa urefu kisha akiswali kuelekea nchani mwake."<sup>(148)</sup>

Na alikuwa akisema,

**((Mmoja wenu akiweka mbele yake kitu kama fimbo nchani [mwishoni] mwa tandiko la mnyama, basi aswali na asijali mtu yeyote atakayepita mbele yake)).<sup>(149)</sup>**

Mara moja "Aliswali akiuelekea mti"<sup>150</sup> na wakati mwengine "Alikuwa akiswali mbele ya kitanda ambacho Mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها) alikuwa amelala (akiwa amejifunika shuka)."<sup>151</sup>

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa haachii kitu chochote kupita baina ya *Sutrah* yake, kwa hiyo mara moja "alikuwa anaswali na kondoo alipokuja na kukimbia mbele yake alimkimbiza mpaka akalibonyeza tumbo lake katika ukuta (kisha akapita nyuma yake)."<sup>(152)</sup>

Vile vile mara moja "wakati anaswali Swalah ya fardhi, alikunja ngumi yake. Na alipomaliza (kuswali) watu walimwambia, "Ee Mjumbe wa Allaah, kuna jambo limetokea wakati wa Swalah?" Akasema, **((Hapana isipokuwa shaytwaan alitaka kupita**

---

<sup>145</sup>Al-Bukhaariy na Ahmad.

<sup>146</sup>Yaani ni sehemu yao ya kupiga magoti.

<sup>147</sup>Al-Bukhaariy na Ahmad.

<sup>148</sup> Muslim, Ibn Khuzaymah (92/2) na Ahmad.

<sup>149</sup>Muslim na Abu Daawuud.

<sup>150</sup>An-Nasaaiy na Ahmad kwa Isnaad Swahiyh.

<sup>151</sup>Al-Bukhaariy, Muslim na Abu Ya'laa (3/1107).

<sup>152</sup>Ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake (1/95/1) At-Twabaraaniy (3/140/3) na Al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy kaikubali.

mbele yangu, nikamkaba mpaka nikahisi ubaridi wa ulimi wake katika mkono wangu. Naapa kwa Allaah! Ingelikuwa sio ndugu yangu Sulaymaan kunitangulia<sup>(153)</sup>. Ningelimfunga [shaytwaan] katika nguzo moja ya msikiti ili watoto wa Madiynah waweze kutembea mbele yake. (kwa hiyo yeyote atakayeweza kuzuwia kitu kumingilia baina yake na Qiblah afanye hivyo)."<sup>(154)</sup>

Pia alikuwa akisema,

((Mmoja wenu anaposwali mbele ya kitu kama *Sutrah* baina yake na watu na mtu akitaka kupita mbele yake, basi amsukume kwa shingo yake)) (na amfukuze kadiri anavyoweza) [katika riwaya nyingine: ((amzuie mara mbili na

---

<sup>153</sup>Inakusudiwa Du'aa ifuatayo ya Nabii Sulaymaan (عليه السلام) ambayo alijibiwa na Allaah (سبحانه و تعالی) kama ilivyo katika Qur-aan. ((Akasema: Mola wangu! Nisamehe na unipe ufalme usio mwelekea yeyote baada yangu. Hakika Wewe ndiye Mpaji)) ((Basi Tukaufanya upepo umtumikie, ukenda kwa amri yake, popote alipotaka kufika)) ((Na ukayafanya maShaytwaan yamtumikie, wote wajenzi na wapiga mbizi)) ((Na wengine wafungwao kwa minyororo)) [Swaad,38: 35-38].

<sup>154</sup>Ahmad, Daaraqutwniyy na At-Twabariy kwa Isnaad ya Swahiyh na iliyo na maana kama hii ni Hadiyth inayopatikana katika Al-Bukhaariy na Muslim na wengineo kutoka kwa mapokezi ya Maswahaba mbali mbali. Na mojawapo ya Hadiyth ambayo kundi la Maqadiyani hawaiamini kwani hawaamini (ulimwengu wa) majini ambao wametajwa katika Qur-aan na Sunnah. Desturi yao ni kukanusha maandishi yaliyo mashuhuri sana. Kama kutoka kwenye Qur-aan wanabadilisha maana yake mfano, maneno ya Subhaana Wa Ta'ala ((Sema: Imefunuliwa wahyi kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza)) [72:1] wanasema kwamba ina maana "kikundi cha binaadamu" na kulifanya neno la 'majini' kuwa inakaribia na maana ya 'binaadamu'. Kwa hiyo wanacheza na lugha na Dini. Na kama kutoka katika Sunnah basi kama inawezeka kwao kubadilisha kwa tafsiyr ya uongo wanafanya hivyo, au sivyo wanaona ni wepesi kukiri kuwa ni uongo hata kama Maimaam wa Hadiyth wote na Ummah mzima kabla yao wamekubaliana na usahihi wake, (tunawaambia kuwa hilo wanalilikataa hapo) kuwa hapana, hiyo ni mutawaatir (imekuja kwa mapokei mengi haina shaka yoyote). Allaah Awahidi.

**akikataa)] (akishikilia kutaka kupita mbele) basi agombane naye kwani hakika huyo ni shaytwaan)).<sup>(155)</sup>**

Vile vile alikuwa akisema,

**((Ikiwa mtu aliyepita mbele ya mtu mwenye kuswali amejua (kuwa ni dhambi) juu yake (kufanya hivyo), basi ingelikuwa ni bora kwake kusubiri arubaini kuliko kupita mbele yake)).**

Na nyongeza katika riwaya nyingine yasema, (Abu An-Nadr kasema, "Sikumbuki khaswa kama alisema ni siku arubaini, au miezi au miaka").<sup>(156)</sup>

### **Yanayokata (Yanayovunja) Swalah**

Alikuwa akisema:

**((Swalah ya mtu inavunjika (inakuwa baatwil) kunapokuwa hakuna kitu kama ncha ya tandiko (la mnyama) mbele yake (vitu vitatu) mwanamke (baleghe)<sup>(157)</sup> punda au mbwa mweusi))** Abu Dharr akasema, "Nilisema, Ee Mjumbe wa Allaah, kwa nini mbwa mweusi na sio mwekundu?" Akasema, **((Mbwa mweusi ni shaytwaan)).<sup>(158)</sup>**

### **Swalah Kulielekea Kaburi**

Alikuwa akikataza kuswali kwa kuyaelekea makaburi akisema:

**((Msiswali kuelekea makaburi na msiyakalie)).<sup>(159)</sup>**

---

<sup>155</sup> Al-Bukhaariy na Muslim na riwaya zaidi ni kutoka kwa Ibn Khuzaymah (1/94/1).

<sup>156</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>157</sup> Ina maana baleghe, na maana ya 'inavunjika' ni kuwa 'haifai tena' (baatwil). Ama kuhusu Hadiyth "Hakuna kinachovunja Swalah" hiyo ni Hadiyth dhaifu na nimeionyesha katika Tamaam Al-Minna (Ukurasa 306).

<sup>158</sup> Muslim, Abu Daawuud na Ibn Khuzaymah (1/95/2).

<sup>159</sup> Muslim, Abu Daawuud na Ibn Khuzaymah.

## Niyyah<sup>(160)</sup>

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema:

**((Vitendo vinategemea (vinalipwa kwa) Niyyah na kila mtu atapata kwa mujibu wa kile alichokusudia)).<sup>(161)</sup>**

## Takbiyah

Kisha Yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akianza Swalah kwa kusema:

اللَّهُ أَكْبَرُ

'Allaahu Akbar'.<sup>(162)</sup>

Alimuamrisha 'mtu aliyeswali vibaya' afanye kama ilivyotajwa na akamwambia: **((Hakika Swalah ya mtu haikamiliki hadi awe ametawadha kwa wudhuu uliyokamilisha viungo vya mwili kisha akasema Allaahu Akbar)).<sup>(163)</sup>**

---

<sup>160</sup>An-Nawawiy amesema katika Radhwah Atw-Twaalibiyn (1/224 Iliyochapishwa na Maktab Al-Islaamiy): "Nia ni kusudio, kwa hiyo mtu anayetaka kuswali, hutia akilini tayari hiyo Swalah pamoja na yanayohusika nayo ya sifa zake, mfano kama ni Swalah ya kipindi kipi, je, ni Swalah ya faradhi n.k. ndipo huleta hivi vyote katika nia yake pamoja na *Takbiyr* ya mwanzo".

<sup>161</sup> Al-Bukhaariy na Muslim na wengineo. Imetolewa pia katika *Al-Irwaa* (Namba: 22).

<sup>162</sup>Muslim na Ibn Maajah. Hadiyth inaashiria kwamba hakuwa akianza (Swalah) kwa maneno ya baadhi ya watu: "Nawaytu Uswalliy... n.k" ambayo imekubalika kuwa ni bid'ah (uzushi). Bali wamekhitilafiana kama ni bid'ah njema au mbaya ambayo tunasema: Hakika bid'ah zote katika ibada ni upotofu, kutokana na kauli (صلى الله عليه وآله وسلم) **((...na kila bid'ah ni upotofu na kila upotofu ni motoni))**. Lakini hapa sipo mahali pa maelezo marefu ya mas-ala haya.

<sup>163</sup> Atw-Twabaraaniy ikiwa na isnadi Swahiyh.

Pia alikuwa akisema:

**((Ufunguo wa Swalah ni Twahara, inaharamishwa (inaanzwa) na Takbiyr na inahalalishwa (inamalizikia) na Tasliym)).<sup>(164)</sup>**

Pia "alikuwa akipandisha sauti yake kutamka *Takbiyr* hadi walio nyuma yake walimsikia"<sup>(165)</sup>. Lakini "anapoumwa, Abu Bakr alikuwa akipandisha sauti yake kutamka *Takbiyr* kwa niaba ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).<sup>(166)</sup>

Alikuwa akisema pia:

**((Imamu anaposema: Allaahu Akbar, basi sema: Allaahu Akbar)).<sup>(167)</sup>**

## Kunyanyua Mikono

Alikuwa mara nyingine akinyanyua mikono pamoja na *Takbiyr*.<sup>(168)</sup> Mara nyingine baada ya *Takbiyr*<sup>(169)</sup> na mara nyingine kabla yake.<sup>(170)</sup>

---

<sup>164</sup>Abu Daawuud, At-Tirmidhiy na Al-Haakim ambao wamekiri usahihi wake na Adh-Dhahaabiy amekubali. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (Namba: 301). Maana hasa ya 'inaharamishwa na *Takbiyr*', ni vitendo vyote ambayo Allaah Ameviharamisha wakati huo. 'na inahalalishwa na *Tasliym*' ni yote yaliyoruhusiwa nje ya Swalah. Kama vile Hadiyth ilivyothibitsha kuwa mlango wa Swalah umefungwa, hakuna mwenye kuabudu anaweza kufungua isipokuwa kwa Twahara, imethibitisha pia kuwa Swalah haiwezi

kufunguliwa (kuanzishwa) isipokuwa kwa *Takbiyr* na haiwezi kumalizika bila ya *Tasliym*. Hii ni rai iliyokubalika kwa wengi wa Maulamaa.

<sup>165</sup>Ahmad, Al-Haakim ambao wamekiri kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahaabiy amekubaliana.

<sup>166</sup>Muslim na An-Nasaaiy.

<sup>167</sup>Ahmad na al-Bayhaqiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>168</sup>Al-Bukhaariy na An-Nasaaiy.

<sup>169</sup>Al-Bukhaariy na An-Nasaaiy.

<sup>170</sup>Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

Alikuwa akiinyanyua kwa kuvinyosha vidole vyake (sio kwa kuvitawanya wala kuvibana pamoja)<sup>(171)</sup> na "alikuwa akiweka (mikono) sambamba na mabega yake"<sup>(172)</sup> ingawa kwa nadra, "alikuwa akiinyanyua hadi ifikie sawa na (ncha ya juu ya) masikio yake".<sup>(173)</sup>

### **Kuweka (Kufunga) Mkono Wa Kulia Juu Ya Mkono Wa Kushoto Na Kuamrisha Kwake**

"Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto"<sup>(174)</sup> na alikuwa akisema:

**((Sisi, Mitume, tumeamrisha kuharakisha kufungua Swawm, kuchelewa (kula) daku na kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto katika Swalah)).<sup>(175)</sup>**

Vile vile: "alimpitia mtu aliyekuwa akiswali aliyeweka mkono wake wa kushoto juu ya mkono wa kulia, akamvuta kuondosha kisha akauweka wa kulia juu ya kushoto"<sup>(176)</sup>

### **Kuweka Mkono Juu Ya Kifua**

"Alikuwa akiweka mkono wa kulia nyuma ya kitanga cha mkono wa kushoto, kiwiko na kigasha"<sup>(177)</sup> "na aliwaamrisha

---

<sup>171</sup>Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah (1//2, 64/1), Tammaam Na Al-Haakim ambao wamekiri ni Swahiyh na Adh-Dhahaabiy amekubaliana.

<sup>172</sup>Al-Bukhaariy na An-Nasaaiy.

<sup>173</sup>Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>174</sup>Muslim Na Abu Daawuud, pia imetolewa katika *Al-Irwaa* (352).

<sup>175</sup>Ibn Hibbaan na Adh-Dwiyaa ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>176</sup>Ahmad Na Abu Daawuud ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>177</sup>Abu Daawuud, An-Nasaaiy na Ibn Khuzaymah (1/54/2) ikiwa na isnaad Swahiyh na Ibn Hibbaan amekiri usahihi wake (485).



Maswahaba wake kufanya hivyo<sup>(178)</sup> na (mara nyingine) "akiushika mkono wa kushoto kwa mkono wake wa kulia"<sup>(179)</sup>

"Alikuwa akiweka juu ya kifua chake"<sup>(180)</sup>

Pia, alikuwa akikataza mtu kuweka mkono juu ya kiuno wakati wa Swalah na aliweka mkono wake juu ya kiuno (kuonyesha makosa hayo)<sup>(181)</sup> Na hii ndio hasa aliyokuwa akiikataza.<sup>(182)</sup>

---

<sup>178</sup> Maalik, Al-Bukhaariy na Abu 'Awaanah.

<sup>179</sup>An-Nasaaiy na Ad-Daraqutwniy ikiwa na isnaad Swahiyh. Katika Hadiyth hii kuna ushahidi kwamba kuishikilia ni Sunnah na katika Hadiyth nyingine, kuwekea tu, hivyo yote ni Sunnah. Ama kuunga baina ya kuweka na kushikilia ambayo baadhi ya Mahanafi waliotangulia wameona ni vizuri, hivyo ni bid'ah; mfumo wake ni kama walivyotaja kuwa ni kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto, kushikilia kiwiko kwa kidole kidogo na cha gumba, na kuviweka bapa vidole vitatu vengine, kama ilivyoelezewa katika tanbihi za Ibn 'Aabidiyn kwenye Durr Al-Mukhtaar (1/454) kwa hiyo usibabaike na wasemayo.

<sup>180</sup>Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake (1/54/2) Ahmad na Abu Shaykh katika Taariykh Iswbahaan (Uk.125), At-Tirmidhiy amekiri moja ya isnaad ni hasan (njema) na maana yake inapatikana katika Al-Muwattwaa na Swahiyh Al-Bukhaariy ikichukuliwa kwa makini. Nimenukuu isnaad kamili ya Hadiyth hii katika kitabu changu 'Ahkaam al-Janaaiz' (Uk. 118).

#### **Tanbihi:**

Kuiweka katika kifua ndivyo ilivyothibiti katika Sunnah, na kinyume chake ni aidha dhaifu au haina msingi. Na Imaam Is-haaq Ibn Raahawayh alifanya Sunnah hii kama alivyosema Al-Marwazy katika Masaail (Uk. 222). "Is-haaq alikuwa akiswali Witr pamoja na sisi ... alikuwa akinyanyua mikono yake katika *Qunuut* na akileta *Qunuut* kabla ya kurukuu na kuweka mikono yake kifuani mwake au chini yake". Ni sawa na usemi wa Qaadhwiy 'Iyaadh Al-Maalikiy katika Mustahabbaat *Asw-Swalaat* kitabu chake Al-I'laam (Uk. 15, chapa ya 3, Ar-Rabaatw) "Mkono wa kulia uwekwe juu ya mkono wa kushoto sehemu ya juu ya kifua". Na karibu na hii ni kama alivyohusisha 'Abdullaah bin Ahmad bin Hanbal katika Masaail yake (Uk.): "Niliona wakati wa kuswali, baba yangu akiweka mikono yake mmoja juu ya mwenziwe juu ya kitovu (chini ya kifua kidogo)" Tazama Kiambatisho 4.

<sup>181</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>182</sup> Abu Daawuud, An-Nasaaiy na wengineo.

## Kutazama Mahali Pa Kusujudu Na Khushuu (Unyenyekevu)

"Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiinamisha kichwa chake wakati wa Swalah na kukongomeza (kuyaelekeza) macho yake katika ardhi<sup>(183)</sup>

### Du'aa Za Kufungulia

Kisha alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akianza kusoma kwa aina nyingi za du'aa ambazo akimsifu na kumtukuza na kumuadhimisha Allaah (سبحانه وتعالى). Alimuamrisha "mtu aliyeswali vibaya" afanye hivyo akimwambia: **((Swalah ya mtu haikamiliki hadi atamke *Takbiyr*, amsifu Allaah (سبحانه وتعالى), amtukuze na amuadhimishe asome atakachoweza katika Qur-aan...))**<sup>(184)</sup>.

Alikuwa akisoma du'aa zozote katika hizi zifuatazo:

1.

---

<sup>183</sup>Al-Bayhaaqiy na al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh kama alivyosema. Pia ina Hadiyth iliyotilia nguvu iliyoripotiwa na Maswahaba kumi: iliyosimuliwa na Ibn 'Asaakir' (17/202/2) Taz. *Al-Irwaa* (354).

#### Tanbihi:

Hadiyth hizi mbili zinaonyesha kwamba Sunnah ni kukaza macho yake mtu mahali pa kusujudu ardhini, hivyo kufunga macho katika Swalah kama wafanyavo baadhi ya watu ni ukosefu wa uchaji Mungu, kwani uongofu bora kabisa ni uongofu wa Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم).

<sup>184</sup>Al-Bukhaariy, Muslim na Ibn Abi Shaybah (12/110/2) imetolewa katika A Irwaa (Namba 8)

اللَّهُمَّ بَاعِدْ بَيْتِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ، اللَّهُمَّ نَقِّنِي مِنْ  
خَطَايَايَ كَمَا يُنَقَّى الثَّوْبُ الْأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ، اللَّهُمَّ اغْسِلْنِي مِنْ خَطَايَايَ  
بِالْمَاءِ وَالتَّلْجِ وَالبَرْدِ.

*Allaahumma Baa'id bayniy wa bayna khatwaayaaya kama Baa'dta baynal-Mashriq wal-Maghrib. Allaahumma Naqqiniy min khatwaayaaya kamaa yunaqqath-thawbul abyadhwa minad-danas. Allaahumma-Ghsilniy bil-maai wath-thalji wal-baradi.*

"Ee Allaah! Niweke mbali na madhambi yangu kama Ulivyoweka mbali baina ya Mashariki na Magharibi, Ee Allaah! Nitakase na madhambi yangu kama vile inavyotakaswa nguo nyeupe na uchafu, Ee Allaah! Nisafishe na madhambi yangu kwa theluji na kwa maji na kwa barafu"<sup>(185)</sup>

(Na alikuwa akisema katika Swalah za fardhi):

2.

وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا (مُسْلِمًا) وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ،  
إِنَّ صَلَاتِي، وَنُسُكِي، وَمَحْيَايَ، وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، لَا شَرِيكَ لَهُ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ  
وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ . اللَّهُمَّ أَنْتَ الْمَلِكُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، سُبْحَانَكَ وَبِحَمْدِكَ، أَنْتَ رَبِّي  
وَأَنَا عَبْدُكَ، ظَلَمْتُ نَفْسِي وَاعْتَرَفْتُ بِذُنُوبِي فَأَعْفِرْ لِي ذُنُوبِي جَمِيعًا إِنَّهُ لَا يَغْفِرُ  
الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ . وَاهْدِنِي لِأَحْسَنِ الْأَخْلَاقِ لَا يَهْدِي لِأَحْسَنِهَا إِلَّا أَنْتَ، وَاصْرِفْ عَنِّي  
سَيِّئَهَا، لَا يَصْرِفُ عَنِّي سَيِّئَهَا إِلَّا أَنْتَ، لُبِّكَ وَسَعْدِيكَ، وَالْخَيْرُ كُلُّهُ فِي بِيَدِكَ،  
وَالشَّرُّ لَيْسَ إِلَيْكَ، وَالْمَهْدِيُّ مَنْ هَدَيْتَ، أَنَا بِكَ وَإِلَيْكَ، لَا مَنْجَا وَلَا مَلْجَأَ مِنْكَ إِلَّا  
إِلَيْكَ، تَبَارَكْتَ وَتَعَالَيْتَ أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ إِلَيْكَ

<sup>185</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana.

*Wajjahtu wajhiya lil-Lladhiy Fatwaras-samaawati wal-ardhwa Haniyfam-Muslimaw-wa maa ana minal-mushrikiyn. Inna Swalahatiy wa nusukiy wa mahyaaya wa mamaatiy lil-Laahi Rabbil-'aalamiyn. Laa shariyka Lahu wa bidhaalika umirtu wa ana awwalul Muslimiyn. Allaahumma Antal-Maliku laa ilaaha illa Anta, Subhaanaka wa bi Hamdika, Anta Rabbiy wa anaa 'abduka, dhwalamtu nafsiy, wa'taraftu bidhambiy, fa-Ghfir liy dhambiy jamiy'an innahu laa yaghfirudh-dhunuwba illa Anta. Wa-HDiniy liahsanil-akhlaaqi laa yahdiy liahsanihaa illa Anta, was-Swirif 'anniy sayyiahaa laa yaswriifu sayyiahaa illa Anta. Labbayka wa Sa'dayka, wal-khayru kulluhu fiy Yadayka wash-sharru laysa Ilayka wal-mahdiyyu man Hadayta. Ana Bika wa Ilayka laa manjaa walaa malja-a Minka illa Ilayka. Tabaarakta wa Ta'aalayta, astaghfiruka wa atuwbu Ilayka.*

“Nimeuelekeza uso wangu kwa yule Ambaye Ameumba mbingu na ardhi hali ya kumtakasia yeye Dini yangu, na sikuwa mimi ni katika washirikina, hakika Swalah yangu na kuchinja kwangu na uhai wangu, na kufa kwangu ni kwa Allaah Bwana wa viumbe vyote, Hana mshirika, na kwa hilo nimeamrisha, nami ni wa kwanza waliojisalimisha.<sup>(186)</sup> Ee Allaah! Wewe ndiye Mfalme, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, Wewe ndiye Bwana wangu na mimi ni

---

<sup>186</sup> Imesimuliwa katika usimulizi mwingi, katika mwengine, ‘*Wa Anaa Minal-Muslimiyn*’ (Mimi ni miongoni wa Waislamu). Inaweza kuwa ni kutokana na makosa ya usimulizi mmojawapo, na ushahidi mwingine unaelekeza hapo, kwa hiyo mwenye kuswali aseme: ‘*Wa Anaa Awwalul-Muslimiyn*’ (Nami ni Muislamu wa mwanzo). Hakuna makosa hivyo, kinyume na watu wanavyosema kwa uoni kwamba inamaanisha "Mimi ni Muislamu wa kwanza mwenye sifa hii, na watu wengine hawana sifa hii". Lakini sio hivyo, ibara hii inaashiria kushindana katika kutekeleza amri. Hii ni sawa na ((**Sema: Ingelikuwa ar-Rahmaan Ana mwana, basi mimi ningelikuwa wa kwanza kumuabudu**)) [Az-Zukhruf, 43: 81] na kauli ya Muusa ('Alayhis-Salaam) ((**na mimi ni wa kwanza wa Waumini**)) [Al-A'raaf 7: 143].

mtumwa (mja) Wako<sup>(187)</sup> Nimedhulumu nafsi yangu, na nimekiri madhambi yangu kwa hivyo nisamehe madhambi yangu yote, hakika hasamehe madhambi, ila Wewe. Na niongoze kwenye tabia nzuri, kwani haongozi kwenye tabia nzuri ila Wewe. Na Niepushe na tabia mbaya, kwani hakuna wa kuniepusha na tabia mbaya ila Wewe. Naitikia mwito Wako, na nina furaha kukutumikia.<sup>(188)</sup> Kheri zote ziko mikononi Mwako, na shari haitoki Kwako<sup>(189)</sup>, Na ameongoka yule Uliyemuongoa, mimi nimepatikana kwa ajili Yako, hapana penye uokovu wala wa pa kukimbilia isipokuwa Kwako, umetakasika, na umetukuka, nakutaka msamaha na ninarejea Kwako (kwa kutubia)."

---

<sup>187</sup>Al-Azhariy amesema kwamba, "Siabudu chochote kingine isipokuwa wewe"

<sup>188</sup>Labbayk: Niko thabiti na daima niko katika utiifu Wako. Sa'dayk: Furaha kubwa kuwa katika amri Yako na kufuata kwa dhati Dini Uliyoichagua.

<sup>189</sup>Yaani, Uovu haunasibishwi kwa Allaah (وتعالى سبحانه) kwa sababu hakuna chochote kibaya katika vitendo Vyake, kwani vyote ni vyema vikianza kutoka uadilifu, fadhila na hikma vyote ambayo ni kheri na havina shari ndani yake bila ya kuwa na shari ndani yake. Kwa sababu shari imekuwa shari kwa sababu hauwezi kurudia kwa Allaah. Ibn Al-Qayyim (Rahimahu-Allaah) amesema: "Yeye ni Muumba wa mema na maovu, lakini maovu yako katika baadhi ya viumbe Vyake, na sio katika kuumba Kwake na sio katika vitendo Vyake. Kwa ajili hiyo Ametakasika na dhulma ambayo asili yake ni kuweka kitu katika sehemu nyingine isiyopasa. Haweki kitu isipokuwa katika mahali panapostahiki ili yote yawe mema. Lakini uovu ni kuweka kitu mahali pasipostahiki. Kinapowekwa katika mahali panapostahiki, huwa si kiovu, kwa hiyo jua kuwa uovu hautoki Kwake. Lakini ikisemwa: Kwa nini Ameumba maovu? Nitasema: Ameumba, na vitendo Vyake ni vizuri sio viovu kwani kuumba na vitendo vinasimama na Allaah, haiwezekani uovu kufanywa au kuhusishwa na Allaah. Chochote kilichokuwa kiovu hakiwezi kurudishwa kwa Allaah, ama vitendo na Alivyoviumba vinaweza kuhusishwa Naye, na vinakuwa ni vyema". Majadiliano muhimu yaliyobakia na kimalizio chake kitapatikana katika kitabu chake *Shifaa Al-'Aliyl fiy Massail al-Qadhwaa wal-Qadar wat-Ta'liyl* - taz (uk. 178-206).

Alikuwa akisema hivyo katika Swalah za fardhi na za Sunnah<sup>(190)</sup>

3. Hii du'aa ni kama iliyo juu bila ya:

أَنْتَ رَبِّي وَأَنَا عَبْدُكَ

*Anta Rabbiy wa anaa 'abduka*

“Wewe Ni Mola wangu nami ni mja Wako...”

Hadi mwishoni pamoja na nyongeza ifuatayo:

اللَّهُمَّ أَنْتَ الْمَلِكُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، سُبْحَانَكَ وَبِحَمْدِكَ

*Allaahumma Antal-Maliku laa ilaaha illa Anta Subhaanaka wa bi Hamdika*

“Ee Allaah, Wewe Ni Mfalme, hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe, Kutakasika ni Kwako na Sifa njema zote ni Zako”<sup>(191)</sup>

4- Kama na Namba 2 hadi,

وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ

*Wa anaa awwalul-Muslimiyn*

“...nami ni Muislamu wa mwanzo”,

---

<sup>190</sup>Muslim, Abu 'Awaanah, Abu Daawuud, An-Nasaaiy, Ibn Hibbaan, Ahmad, Ash-Shaafi'iy na At-Twabaraaniy. Walioeleza kuwa ni Swalah za Sunnah wamekosea.

<sup>191</sup>An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

Na akiongeza,

اللَّهُمَّ اهْدِنِي لأَحْسَنِ الأَخْلَاقِ وَأَحْسَنِ الأَعْمَالِ لا يَهْدِي لأَحْسَنِهَا إِلا أَنْتَ، وَقِنِي  
سَيِّئَ الأَخْلَاقِ والأَعْمَالِ لا يَقِي سَيِّئَها إِلا أَنْتَ،

*Allaahumma-HDiniy liahsanil akhlaaqi wa ahsanil a'maali  
laa yahdiy liahsanihaa illa Anta, wa Qiniy sayyial-akhlaaqi  
wal-a'maali laa yaqiy sayyiahaa illa Anta*

“Ee Allaah, niongoze kwenye tabia njema (nzuri) na vitendo vyema haongozi kwenye uzuri wake ila Wewe. Niepushe na tabia mbaya na vitendo vibaya hakuna mwenye uwezo kuinga ubaya wake ila Wewe”.<sup>(192)</sup>

5-

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ وَتَبَارَكَ اسْمُكَ وَتَعَالَى جَدُّكَ وَلا إِلَهَ غَيْرُكَ

*Subhaanaka-Allaahumma wa bi-Hamdika wa Tabaaraka-  
Smuka wa Ta'aala Jadduka wa laa ilaaha Ghayruka*

“Kutakasika ni Kwako<sup>(193)</sup> Ee Allaah, na sifa njema zote ni Zako<sup>(194)</sup>, na limetukuka Jina Lako<sup>(195)</sup>, na Utukufu ni Wako<sup>(196)</sup>, na hapana apasae kuabudiwa kwa haki, asiyekuwa Wewe”<sup>(197)</sup>

---

<sup>192</sup>An-Nassaiy na Ad-Daaraqutwniy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>193</sup>Nakutukuza ina maana kwamba nazingatia kuwa Umetakasika na kasoro yoyote. Na ‘Sifa njema’ maana yake ni kuwa tumezijua vizuri sifa Zako. Na Kutakasika’ maana yake ni wingi wa kutakasika kwa jina Lako, kwa sababu

kila la kheri linapatikana katika kulitaja jina Lako. ‘limetukuka Jina Lako’ maana yake ni kuwa limenyanyuka juu jina Lako (utukufu wako).

<sup>194</sup>Tumeshikamana katika kukusifu.

<sup>195</sup>Baraka za Jina Lako ni kubwa, kwani makubwa yaliyo mazuri hutokanakukumbuka Jina Lako.

<sup>196</sup> Utukufu na Nguvu Zako.

Alisema (صلى الله عليه وآله وسلم) pia: ((Hakika maneno yanayopendwa kabisa na Allaah ni mja Wake anaposema: (سبحانك اللهم) Umetukuka Ee Allaah...<sup>(198)</sup>)

6- Kama ilivyo juu kwa kuongeza katika Swalah za usiku:

لا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

*Laa ilaaha illa Allaah*

“Hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah”

Mara tatu na

اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا

*“Allaah ni Mkubwa”*

Mara tatu

7-

اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا، وَسُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا

*Allaahu Akbar Kabiyyraa wal-HamduliLlaahi kathiyyraa wa-SubhaanaLlaahi bukrataw-wa aswiylaa*

---

<sup>197</sup>Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana. ‘Uqayl amesema (Uk. 103) "Hii imesimuliwa kupitia njia mbalimbali kwa isnaad Swahiyh". Imetolewa katika *Al-Irwaa* (Namba 341) Imesimuliwa na Ibn Mandah katika *At-Tawhiyd* (123/2) kwa isnaad Swahiyh na An-Nasaaiy katika *Al-Yawm wal-Laylah* ikiwa ni mawquuf na marfuu’ kama katika *Jaami’ Al-Masaaniyd* ya Ibn Kathiyr (Mj. 3 Kifungu 2. Uk. 235/2)

<sup>198</sup>Abu Daawuud na Atw-Twahaawiy kwa isnaad Swahiyh.



“Allaah Ni Mkubwa, Na sifa njema ni za Allaah kwa wingi, Ametakasika Allaah asubuhi na jioni.”

Mmoja wa Maswahaba alifungua Swalah yake kwa du’aa hiyo, Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alisema: ((Imenipendeza hiyo (du'aa) kwani kwayo milango ya Pepo imefunguliwa))(199)

8-

الْحَمْدُ لِلَّهِ حَمْدًا كَثِيرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيهِ

*AlhamdulillahLlaahi Hamdan khathiyran-twayyibam-Mubaarakan fiyhi*

“Sifa njema ni za Allaah, sifa nyingi, nzuri, zenye Baraka”

Mtu mwengine alifungua Swalah yake kwa du’aa hiyo, kisha Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: ((Nimewaona Malaika kumi na mbili wakishindana nani atakayeipeleka juu))(200)

9-

اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ نُورُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ، وَلَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ قَيِّمُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ، (وَلَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ فِيهِنَّ)، وَلَكَ الْحَمْدُ أَنْتَ الْحَقُّ وَوَعْدُكَ حَقٌّ، وَقَوْلُكَ حَقٌّ، وَلِقَاؤُكَ حَقٌّ، وَالْجَنَّةُ حَقٌّ، وَالنَّارُ حَقٌّ، وَالسَّاعَةُ حَقٌّ، وَالنَّبِيُّونَ حَقٌّ، وَمَحَمَّدٌ حَقٌّ، اللَّهُمَّ لَكَ أَسَلْتُ وَعَلَيْكَ تَوَكَّلْتُ، وَبِكَ آمَنْتُ، وَالْيَاكُفُورُ أَنْبَتُ، وَبِكَ خَاصَمْتُ، وَالْيَاكُفُورُ حَاكَمْتُ، (أَنْتَ رَبَّنَا وَالْيَاكُفُورُ الْمَصِيرُ، فَاعْفِرْ لِي مَا قَدَّمْتُ، وَمَا أَخَّرْتُ، وَمَا أَسْرَرْتُ، وَمَا أَعْلَنْتُ) (وَمَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي) أَنْتَ الْمُقَدِّمُ وَأَنْتَ الْمُؤَخِّرُ، (أَنْتَ الْهَيَّ) لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ.

<sup>199</sup>Muslim Na Abu Awaanah; At-Tirmidhiy kasema ni Swahiyh. Kadhalika AbuNa’iyam ameisimulia katika ‘Akhbaar Aswbahaan’ (1/210) kutoka kwa Jubayr bin Mutw-am ambaye alimsikia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akiisoma kwenye Swalah ya Sunnah.

<sup>200</sup> Muslim na Abu ‘Awaanah

*Allaahumma Lakal-Hamdu Anta Nuwrus-samaawaati wal-ardhwi waman fiyhinna, wa Lakal-Hamdu Anta Qayyumus-samawaatil wal-ardhwi waman fiyhinna, wa Lakal-Hamdu Anta Malikus-samaawati wal-ardhwi wa man fiyhinna, wa Lakal-Hamdu Antal-Haqqu, wa-Wa'duka Haqqu wa-Qawluka Haqqu, wa Liqaauka Haqqu, wal-Jannatu Haqqu wan-Naaru Haqqu was-Saa'atu Haqqu, wan-Nabbiyyuwna Haqqu, wa Muhammadun Haqqu, Allaahumma Laka aslamtu, wa 'Alayka tazakkaltu, wa Bika Aamantu, wa Ilayka anabtu, wa Bika Khaaswamtu, wa Ilayka haakamtu, Anta Rabbunaa wa Ilaykal-maswiyr, fa-Ghfir liy maa qaddamtu wa maa akh-khartu, wa maa asrartu, wa maa a'lantu, wa maa Anta A'lamu bihi minniy, Antal-Muqaddimu wa Antal-Muakh-khiru Anta Ilaahiy, laa ilaaha illa Anta.*

“Ee Allaah ni Zako sifa njema, Wewe ndiye nuru<sup>(201)</sup> ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake, na ni Zako sifa njema. Wewe ndiye Mwenye kuzisimamia<sup>(202)</sup> mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake, [na ni Zako sifa njema, Wewe ni Mfalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake], na sifa njema ni Zako, Wewe ni Haqq, na ahadi Yako ni ya Haqq, na neno Lako ni Haqq, na kukutana Nawe ni Haqq, na Pepo ni Haqq, na Moto ni Haqq, na Sa'ah (Qiyaamah) ni Haqq, na Mitume ni Haqq, na Muhammad ni Haqq, Ee Mola Kwako nimejisilimisha, na Kwako nimetegemea, na Kwako nimeweka imani [yangu], na Kwako ndio nakurejelea, nimepigana kwa ajili Yako, na kwa hukumu Zako ndio nazifuata zinihukumu, [Wewe ndiye Mola wetu na Kwako ndio tunaishia, nisamehe niliyoyatanguliza na niliyoyachelewesha, na niliyoyaficha na niliyoyatangaza], [Na yote unayoyajua kutoka kwangu] Wewe Ndiye Mwenye

---

<sup>201</sup>Wewe Ndiye Mwenye kuzipa mwanga na Kwayo ndio Wanaopata uongofu kutoka Kwako.

<sup>202</sup>Mwenye kuhifadhi na Mchungaji wao.

kutanguliza na Ndiye Mwenye kuchelewesha, [Wewe ni Mola wangu] hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe<sup>(203)</sup>;

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema hivi katika Swalah ya usiku alipokuwa akisoma du'aa ifuatayo<sup>(204)</sup>:

10-

اللَّهُمَّ رَبَّ جِبْرَائِيلَ، وَمِيكَائِيلَ، وَإِسْرَافِيلَ، فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، عَالِمَ الْغَيْبِ  
وَالشَّهَادَةِ أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ. اهْدِنِي لِمَا اخْتَلَفَ فِيهِ  
مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِكَ، إِنَّكَ تَهْدِي مَنْ تَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

*Allaahumma Rabba Jibraaiyl, wa Mikaaiyl, wa Israafiyl, Faatwiras-samaawaati wal-ardhwi, 'Aalimal-Ghaybi wash-Sahaadati, Anta Tahkumu baina 'Ibaadika fiymaa kaanuw fiyhi yakhtalifuwn. IhDiniy limakhtulifa fiyhi minal-haqqi bi-Idhnika Innaka Tahdiy man Tashaau ilaa Swiraatwim-mustaqiym.*

“Ee Allaah Mola wa Jibriyl na Mikaaiyl na Israafiyl, Muumba wa mbingu na ardhi, Mjuzi wa mambo yaliojificha na yaliyowazi, Wewe unahukumu baina ya waja Wako katika mambo ambayo walikuwa wakitofautiana, niongoze mimi kwenye haki katika yale waliyotafautiana kwa ruhusa Yako. Hakika Wewe unamuongoza umtakeae kwenye njia iliyonyoka<sup>(205)</sup>”

11- Alikuwa akisema *Takbiyr*, *Tahmiyd*, *Tasbiyh*, *Tahliyl* na *Istighfaar* mara kumi kila moja na akisema:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي، وَاهْدِنِي، وَارْزُقْنِي (وَعَافِنِي)

<sup>203</sup>Al-Bukhaariy na Muslim, Abu 'Awaanah, Abu Daawuud, Ibn Nasr na Ad-Daarimiy.

<sup>204</sup> Imaam kwa khofu ya kurefusha Swalah kwa Maamuma.

<sup>205</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

*Allaahumma-ghfir liy WahDiniy Warzuqniy wa 'Aafiniy*

“Ee Allaah, nighufurie na niongoze na niruzuku [Na Nisamehe madhambi yangu]” mara kumi kisha akisema:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الضَّيْقِ يَوْمَ الْحِسَابِ

*Allaahumma inniy a'uzdhu Bika minadh-dhwiyyi yawmal-hisaabi*

“Ee Allaah, Najikinga Kwako na dhiki za Siku ya Hisabu”<sup>(206)</sup>

Mara kumi

12-

اللَّهُ أَكْبَرُ، اللَّهُ أَكْبَرُ، اللَّهُ أَكْبَرُ، ذُالْمَلَكُوتِ، وَالْجَبْرُوتِ، وَالْكِبْرِيَاءِ، وَالْعِظْمَةِ

*Allaahu Akbar, Allaahu Akbar, Allaahu Akbar Dhul-Malakuuti wal-Jabaruuti, wal'adhwamah*

“Allaah ni Mkubwa [mara tatu] Mwenye Ufalme, Nguvu, Ufakhari na Utukufu”<sup>(207)</sup>

### Kisomo (Tilaawah)

Kisha alikuwa (سبحانه صلى الله عليه وآله وسلم) akijikinga kwa Allaah (تعالى) kwa kusema:

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ مِنْ هَمَزِهِ وَنَفْخِهِ وَنَفْثِهِ

*A'uzdhu bil Llaahi minash shaytwaanir rajiiymi min hamzihii wa nafkhihii wa nafathihi*

“Najilindia na Allaah kutokana na shaytwaan aliyefukuzwa, najilinda na (kutokana na) wazimu wake<sup>(208)</sup> na kiburi chake, na ushairi [kutabana] wake<sup>209</sup>

---

<sup>206</sup> Ahmad, Ibn Abi Shaybah (12/119/2), Abu Daawuud na At-Twabaraaniy katika Mu'jam al-Awsawatw (/2) ikiwa na isnaad moja Swahiyh na nyingine Hasan.

<sup>207</sup> At-Twayaalisii na Abu Daawuud ikiwa na isnaad Swahiyh.

Mara nyingine huongeza kwa kusema,

أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمْعُ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ ...

*A'urdhu bil Llaahis Samiy'il 'Aliymi minash shaytwaanir...*

((Najikinga kwa Allaah, Mwingi wa Kusikia, Mwenye Ujuzi, kutokana na shaytwan...))<sup>(210)</sup>

Kisha husoma,

﴿ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴾

*Bismi-Llaahir Rahmaanir Rahiym*

((Kwa Jina la Allaah, Mwingi wa Rehma Mwenye Kurehemu))

Hakuwa akinyanyua au kupaza sauti<sup>(211)</sup>

**Kusoma Aayah Moja Moja**

---

<sup>208</sup> Maneno matatu ya Kiarabu; *hamz*, *nafkh* na *naft* yamefasiriwa na baadhi ya wapokezi kuwa *hamz* ni aina ya wazimu, na *nafkh* ni kiburi, na *naft* ni ushairi; yametafsiriwa hivyo hivyo na msimulizi; tafsiyir zote tatu zimepokewa (zimerudiwa pia) marfuu'an kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa isnaad Swahiyh Mursal (Ni hadiyth katika isnaad yake hakutaja Swahaba, bali kataja Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)). Na kusudio la (kwa) 'ushairi' [kutabana] hapa ni mashairi yasiyokubalika/yasiyo na heshima/yenye kudharauliwa (ina maana kwa majaribio yasiyo na mafanikio) kwani Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: **((Hakika katika baadhi ya ushairi kuna (ni) hikma))** [Al-Bukhaariy]

<sup>209</sup> Abu Daawuud Ibn Maajah, Ad-Daaraqutwny na Al-Haakim ambaye pamoja na Ibn Hibban na Adh-Dhahaabiy wamesema ni Swahiyh. Imetolewa pamoja na inayofuatia katika *Al-Irwaa Al-Ghaliyl* (342)

<sup>210</sup> Abu Daawuud na At-Tirmidhiy kwa isnaad nzuri. Ahmad ameinukuu katika *Massail* ya Ibn Haaniy 1/50

<sup>211</sup> Al-Bukhaariy, Muslim, Abu 'Awaanah, At-Twahaawiy na Ahmad.

Kisha alikuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma Suratul-Faatihah na akigawanya (kisomo chake,) kwa kuisoma Aayah moja moja; kama hivi:

﴿ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴾

*BismiLlaahir Rahmaanir Rahiym*

[Kisha hupumua/husimama, kisha husema:]

﴿ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴾

*AlhamduliLlaahi Rabbil 'Aalamiyn*

[Kisha hupumua/husimama, kisha husema:]

﴿ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴾

*Ar-Rahmaanir-Rahiym*

[Kisha hupumua/husimama, kisha husema:]

﴿ مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴾

*Maaliki Yawmid Diyn*

((Mfalme wa Siku Ya Qiyaamah))

Kisomo chake kilikuwa kama hivyo, hadi mwisho wa Surah. Na hivyo hasa ndivyo ilivyokuwa kisomo chake chote, kila anaposoma huwa anasimama/anapumua mwisho wa Aayah na wala haiunganishi na Aayah inayofuatia<sup>(212)</sup>.

---

<sup>212</sup> Abu Daawuud na Sahmiy (64-65); Al-Haakim amesema kuwa ni Swahiyh. Na Adh-Dhahabiy amakubaliana naye. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (343). Na ameipokea Abu 'Amr Ad-Daaniy katika *Al-Muktafaa* (5/2) na kasema: Hadiyth hii ina njia nyingi na ndiyo tegemeo katika mlango huu, kisha akasema: (na) Kundi la Maimamu wengi waliotangulia na

Mara nyingine alikuwa akiisoma bila ya kuivuta/bila ya kutia madda<sup>(213)</sup> (alisoma):

﴿ مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴾

*Maliki Yawmid Diyn*

((Mfalme wa Siku Ya Qiyaamah))

badala ya

﴿ مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴾

*Maaliki Yawmid Diyn*

((Mwenye kumiliki Siku Ya Qiyaamah))

### Ulazima (Ufaradhi) Wa *Al-Faatihah* Na Fadhila Zake

Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akitilia mkazo na kusisitiza kuhusiana na (Alisisitiza mno) umuhimu wa Surah hii, alikuwa akisema: **((Hakuna Swalah kwa asiyesoma [ndani yake] Ufunguo wa Kitabu))**<sup>(214)</sup>

---

Maqurraa (wasomaji wa Qur-aan) waliopita walikuwa wakipendelea kusimama katika kila Aayah hata kama (Aayah nyingine) itakuwa imefungamana katika maana na Aayah ijayo") Nasema: Sunnah hii imepuuzwa na Maqurraa (wasomaji wa Qur-aan) wengi wa nyakati hizi, achilia mbali wengineo ambao si Maqurraa.

<sup>213</sup> Tamaam Ar-Raaziyy katika Al-Fawaaid, Ibn Abu Daawuud katika Maswaahif (7/2), Abu Nu'aym katika Akhbaar Aswbahaan (1/104) na Al-Haakim ambaye amesema kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekuliana naye, qiraa/kisomo hichi 'Malik' ni mutawaatir pia kama kilivyo kile qiraa cha kwanza 'Maalik'.

<sup>214</sup> Al-Bukhaairy, Muslim, Abu 'Awaanah na Al-Bayhaqiy. Imetolewa katika Al-Irwaa (302)

Na Katika usemi mwengine: ((Swalah haitimii mtu asiposoma ndani yake Ufunguo wa Kitabu))(215)

Na wakati mwengine anasema: ((Mwenye kuswali Swalah yoyote ile bila ya kusoma ndani yake Ufunguo wa Kitabu basi hiyo Swalah ni khiddaaj<sup>(216)</sup>, ni khiddaaj, ni khiddaaj, haikukamilika))(217)

Na anasema (صلى الله عليه وآله وسلم) kuwa:

Allaah (سبحانه وتعالى) Amesema: "Nimegawa Swalah<sup>(218)</sup> baina Yangu na mja Wangu [katika] sehemu mbili; nusu ya kwanza ni Yangu na nusu nyengine iliyobaki ni ya mja Wangu, na mja Wangu atapata alichokiomba" [Kisha] Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: Someni: Mja anasema: "*Al-hamdu Llillaahi Rabbil 'Alaamiyn*", Allaah (سبحانه وتعالى) Husema "Mja Wangu amenisifu" Mja akisema: "*Ar-Rahmaanir Rahiym*", Allaah Husema: "Mja Wangu amenitukuza" Mja akisema: "*Maalik/Malik yawamid diyn*", Allaah Husema: Mja Wangu Ameniadhimisha" Mja akisema: "*Iyyaaka na'budu wa iyyaaka nasta'iyn*", [Husema]: "Hii ni baina Yangu na Mja Wangu, na Mja wangu atapata atachoomba". Mja akisema: "*Ih-dinaas swiraatal-mustaqiym, swiraattAl-Laadhiyna An'amta 'alayhim ghayril maghdhwuubi 'alayhim wala-dhwaaliyn*",

---

<sup>215</sup> Ad-Daaraqutwniy, ambae amesema kuwa ni Swahiyh, na Ibn Hibbaan katika Swahiyh yake. Pia katika *Al-Irwaa* (302)

<sup>216</sup> Kwa maana kuwa ni kasoro, Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alifasiri kwa kusema: haikutimilia

<sup>217</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>218</sup> Ina maana kuwa ni Suratul Faatihah, ni katika mifano ya kutaja kitu chote lakini kinachokusudiwa ni baadhi tu ya kitu hicho, kwa kusisitiza umuhimu/utukufu wake.



Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Allaah Aliyetukuka hakuteremsha katika Tawraat wala katika Injiyl chochote kile chenye kufanana na Ummul Qur-aan -Mama wa Qur-aan-, nayo Ni Aayah Saba zisomwazo mara kwa mara<sup>(220)</sup> [Na Qur-aan Tukufu niliyopewa]<sup>(221)</sup>)**

Alimuamrisha (صلى الله عليه وآله وسلم) "Mtu aliyeswali vibaya" aisome hiyo Faatihatul Kitaabu katika Swalah yake"<sup>(222)</sup> (Lakini) na kwa yule asiyeweza kuihifadhi alimuambia (aliyeisahau): Sema:

سُبْحَانَ اللَّهِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ

*Subhaana Allaah, Wal-Hamdu Lillaah, wala ilaaha illa Allaahu, wa Allaahu Akbar, wala Hawla wala Quwwata ila biLlaah*

---

<sup>219</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Maalik, na inayo yenye kuipa nguvu - shaahid- kutokana na Hadiyth ya Jaabir iliyothibiti kwa As-Sahmiy katika Taariykh Jurjaan (144)

<sup>220</sup>Al-Balajiy amesema: "Anakusudia maneno ya سبحانه وتعالى ((Na tumekupa

**Aayah saba zinazosomwa mara kwa mara, na Qur-aan Tukufu)) [Al-Hijr: 15:87].** Imetwa 'saba', kwa sababu ni Aayah saba, na al-Mathaaniy (inayosomwa mara kwa mara') kwa sababu inarudiwa katika kila raka, na sababu ya kuitwa (Imetwa) 'Qur-aan Tukufu' kubainisha jina hili kwa ajili yake khaswa, japokuwa kila sehemu ya Qur-aan ni Tukufu. Kama inavyosemwa kuhusiana na Ka'abah kuwa ni 'Nyumba ya Allaah' japokuwa kuwa nyumba zote ni Zake Allaah, lakini hivi ni kwa njia ya kuibainisha umahsusi na utukufu wake"

<sup>221</sup> An-Nassaiy na Al-Haakim ambae amesema kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahaabiy amekubaliana nayo.

<sup>222</sup>Al-Bukhaariy katika makala yake 'Kusoma nyuma ya Imaam' kwa isnaad Swahiyh.

“Ametakasika Allaah na sifa njema ni za Allaah na hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah, na Allaah ni Mkubwa na Hakuna uwezo wala nguvu ila za Allaah”<sup>(223)</sup>

Na (Pia) alimuambia "aliyeswali kimakosa": **((Ikiwa umehifadhi cho chote kile katika Qur-aan basi isome, vyenginevyo msifu Allaah, kiri Ukubwa Wake, na kiri kwamba hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye))**<sup>(224)</sup>

### **Kufutwa Kisomo Nyuma Ya Imaam Katika Swalah Za Jahriyyah (Swalah Za Kunyanyua Sauti)**

Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ameruhusu kwa wale waliokuwa ma-amuma kuisoma Suratul-Faatihah nyuma ya Imaam katika Swalah za jahriyyah, na mara moja alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم), "Akiswali Alfajiri na kisomo kikawa kigumu kwake. Alipomaliza alisema: **((Labda mnasoma nyuma ya Imaam wenu!))**. Tukasema: "Ndio *hadhdhan* <sup>(225)</sup> Ee Mjumbe wa Allaah". Akasema: **((Basi Msifanye hivyo isipokuwa [kwa kusoma mmoja wenu] Ufunguo wa Kitabu, kwani hakuna Swalah kwa asiyeisoma))**.<sup>(226)</sup>

Kisha aliwakataza kusoma katika Swalah za jahriyyah kabisa, na hilo lilitokea wakati,

---

<sup>223</sup> Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah (1/80/2), Al-Haakim, At-Twabaraaniy na Ibn Hibbaan ambae pamoja na Al-Haakim, wamesema ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana nayo. Imo katika *Al-Irwaa* (303)

<sup>224</sup> Abu Daawuud na At-Tirmidhiy ambae amesema ni nzuri; isnaad yake ni Swahiyh. (*Swahiyh Abi Daawuud* Namba. 807)

<sup>225</sup> *Hadhdhan*: kusoma haraka haraka, kwa kukimbilia au kuharakiza.

<sup>226</sup> Al-Bukhaariy katika kijarida, Abu Daawuud na Ahmad. At-Tirmidhiy na Ad-Daaraqutwniy wamesema ni nzuri.

"Alipomaliza Swalah ambayo alikuwa akisoma kwa sauti [katika usimulizi (mmoja) ilikuwa Swalah ya Alfajiri] basi akauliza: **((Je, kuna (yeyote) aliyekuwa akisoma pamoja nami hivi sasa?))** Mtu mmoja akajibu: "Ndio, mimi Ee Mjumbe wa Allaah". Akasema: **((Mimi Nasema: sasa kwa nini naingiliwa kati katika kisomo changu))**<sup>(227)</sup> [Abu Hurayrah alisema]: (Hivyo) watu wakaacha kusoma pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kila anapokuwa anasoma kwa sauti baada ya kusikia hivyo kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) [wakawa wanaendelea kusoma kimya kimya kila anapokuwa Imaam haisomi kwa sauti].<sup>(228)</sup>

Pia Akaufanya (صلى الله عليه وآله وسلم) ukimya katika kisomo cha Imaam kuwa ni sehemu katika kukamilisha kumfuata Imaam, kwa kusema: **((Kwa hakika amewekwa Imaam ili apatwe kufuatwa, hivyo anapoleta takbiyr, na nyinyi leteni takbiyr, na anaposoma kaeni kimya))**<sup>(229)</sup> kama alivyofanya kumsikiliza Imaam kuwa kunatosheleza na kisomo nyuma yake, kwa kusema (aliposema): **((Mwenye kuwa na Imaam, basi kisomo**

---

<sup>227</sup> Amesema al-Khattabiy: maana yake ameingilia kisomo changu, pia yawezekana ikawa ushindani kwa maana ya kushirikiana na kubadilishana, na maana ya pili ndio iliyokusudiwa hapa kwa sababu ya kuacha Swahabah (رضي الله عنهم) kusoma moja kwa moja, na kama ingelikuwa kusudio ni maana ya kwanza, basi wesingeliacha kusoma, lakini inaonyesha kuwa ni kuingilia kati tu kama ilivyodhihiri.

<sup>228</sup> Maalik, Humaydy, Al-Bukhaariy katika kijarida chake, Abu Daawuud na Mahaamaliy (6/139/1) At-Tirmidhiy amesema ni nzuri, Abu Haatim Ar-Raaziy, Ibn Hibbaan na Ibn Qayyim wamesema kuwa ni Swahiyh, na hadiyth yenye kuipa nguvu -shaahid- katika Hadiyth ya 'Umar ambayo mwisho wake: sasa kwa nini nashindaniwa Qur-aan?! Haimtoshelezeshi mmoja wenu kisoma cha Imaam wake?! Kwa hakika amewekwa Imaam ili apatwe kufuatwa, basi ataposoma kaeni kimya. Imepokewa na al-Bayhaaqiy katika kitabu ulazima wa kisomo katika Swalah, kama ilivyo katika al-Jaami' al-Kabiyr (3/344/2)

<sup>229</sup> Ibn Abi Shaybah (1/97/1), Abu Daawuud, Muslim, Abu 'Awaanah na al-Ruwayaaniy katika musnad yake, (24/119/1). Imetolewa katika *Al-Irwaa* (332,394).

## Kuwajibika Kusoma Katika Swalah Za *Sirriyyah* (Swalah Za Kimya)

Ama katika Swalah za kimya kimya, Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliwaachilia waendelea kusoma humo. Jaabir alisema: "Tulikuwa tukisoma katika (Swalah ya) Adhuhuri na 'Aswr nyuma ya Imaam katika Rak'ah mbili za mwanzo Suratul-Faatihah na Surah nyingine, na katika mbili za mwisho Suratul-Faatihah."<sup>(231)</sup>

Lakini, alichukizwa kwa tashwishi na kubabaishwa, kwa kisomo chao pale aliposwali Adhuhuri na Maswahaba akauliza: **((Nani katika nyinyi aliyesoma: "*Sabbihisma Rabbikal-A'laa*" [Suratul-A'laa, 87:1]))**. Mtu mmoja akajibu: "ni mimi" [sikuwa na kusudio lo lote lile kwa kuisoma ila kheri] Akasema: **((Nilijua kuwa kuna mtu anavutana na mimi kwayo))**<sup>(232)</sup>

Na Katika Hadiyth nyingine: "Walikuwa wakisoma nyuma ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), hivyo akasema: **((Mmenibabaisha katika kisomo changu))**"<sup>(233)</sup>

---

<sup>230</sup> Ibn Abi Shaybah (1/97/1), Ad-Daraaqutwniy, Ibn maajah, Atw-Twahaawiy. Na Ahmad kutoka njia mbali mbali, musnad na mursal. Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah amesema kuwa ina nguvu kama katika Al-Furuu' ya Ibn 'Abdil-Haadiy (48/2). Al-Buswayriy amesema kuwa baadhi ya isnaad zake kuwa ni Swahiyh. Nimejadili Hadiyth hii kwa kirefu na kuzitafiti njia zake (mbali mbali) za usimulizi katika maandishi kisha katika *Al-Irwaa Al-Ghaliyl* (Namba. 500).

<sup>231</sup> Ibn Maajah kwa isnaad Swahiyh. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (506).

<sup>232</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Siraaj.

<sup>233</sup> Al-Bukhaariy katika makala yake, Ahmad na Siraaj kwa isnaad nzuri.

Akasema: ((Anayeswali huwa ananongo'na na Mola wake, basi aangalie cha kumnongo'neza, wala msisome Qur-aan pamoja wote kwa sauti))(234)

Pia alikuwa akisema: ((Atakayesoma herufi moja katika kitabu cha Allaah atapata hasanah (jema) moja, na kila hasanah moja ni sawa na thawabu kumi, (wala) sisemi 'Alif-Laam-Miym' ni herufi moja, bali Alif ni herufi moja na Laam ni herufi moja na Miym ni herufi moja)).(235)

### Aamiyn, Imaam Kunyanyua Sauti Anapoileta

Kisha alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anapomaliza kusoma *Al-Faatihah* husema:

آمين

*Aamiyn*

kwa sauti na huku akiirefusha sauti yake(236)

---

<sup>234</sup> Maalik na Al-Bukhaariy katika Af'aal al-'Ibaad kwa isnaad Swahiyh.

#### Tanbihi:

Rai ya uthabiti wa kusoma nyuma ya Imaam katika Swalah za Sirriyah na sio za Jahriyyah, imetolewa na Imaam Ash-Shaafi'y mwanzo, na Muhammad mwanafunzi wa Abu Haniyfah katika usimulizi kutoka kwake ambao umependelewa (zaidi) na Shaykh 'Aliy al-Qaariy na baadhi ya Mashaykh (wengine) wa madhehebu. Pia (ulikuwa) ni msimamo wa Imaam Az-Zuhriy, Maalik, Ibn Al-Mubaarak, Ahmad bin Hanbal, na kundi la Muhaddithiyn na wengineo, na ni mapendeleo ya Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah.

<sup>235</sup> At-Trimidhiy na Ibn Maajah kwa isnaad Swahiyh. Imesimuliwa pia na Aajuriy katika Aadaab Hamalat al-Qur-aan. Ama Hadiyth: "Mwenye kusoma nyuma ya Imaam mdomo wake utajazwa moto" ni Hadiyth ya uzushi (mawdhwu) na hii imelezewa katika Silsilat al-Ahaadiyth Adh-Dhwa'iyfah (Namba. 569) Taz. Kiambatisho 5.

<sup>236</sup> Al-Bukhaariy katika Juz' Al-Qiraah na Abu Daawuud kwa isnaad Swahiyh.

Pia alikuwa akiwaamrisha wenye kumfuata Mamuumiyn waseme Aamiyn, kwa kusema: ((**Imaam ataposema:**

﴿ غَيْرَ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ ﴾

*Ghayril Magh-dhwuubi 'alayhim waladh dhwaaaaaalliyyyyyyn*

**((Sio waliokasirikiwa wala waliopotea))**

basi semeni: 'Aamiyn' [kwani Malaika na wao pia huwa wanasema: 'Aamiyn' na hakika Imaam anasema: 'Aamiyn']])

Katika usemi mwengine: ((**Imaam atakaposema 'Aamiyn' basi na nyinyi semeni: 'Aamiyn' - kwani itakayeafiki 'Aamiyn' yake na 'Aamiyn' ya Malaika - [katika usemi mwengine] ((Anaposema Mmoja wenu katika Swalah 'Aamiyn' na Malaika mbinguni wakasema 'Aamiyn', zikaafikiana moja na nyingine, atasamehewa madhambi yake yaliyotangulia))**<sup>(237)</sup>

Na Katika Hadiyth nyingine, ((**Semeni: Aamiyn, Allaah Atakujibuni**))<sup>(238)</sup>

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ((**Mayahudi hawakuoneeni choyo kwa jambo lolote lile zaidi kama**

---

<sup>237</sup> Ash-Shaykhaan na An-Nasaa'iy na Ad-Daarimiy. Maneno yaliyozidi yameripotiwa na wawili wa mwisho na ni dalili kuwa Hadiyth hii haiwezi kuthibitisha kuwa Imaam hasemi 'Aamiyn' kama ilivyoripotiwa na Maalik, hivyo Ibn Hajr anasema katika *Fat-h Al-Baariy*: "Inaonyesha dhahiri kwamba Imaam anasema 'Aamiyn' "Ibn 'Abdil Barr anasema katika Tamhiyd (7/13), "Ni rai ya Waislamu wengi pamoja na Maalik kama watu wa Madiynah walivyosimulia kutoka kwake, kwani ni Swahiyh kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kutokana na Hadiyth ya Abu Hurayrah (ambayo ni hii) na ile ya Waail Ibn Hujr (yaani ya nyuma yake)"

<sup>238</sup>Muslim na Abu 'Awaanah.

### Kisomo Chake (صلى الله عليه وآله وسلم) Baada Ya *Al-Faatihah*

Kisha, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma Surah nyingine baada ya *Al-Faatihah*, na alikuwa akikirefusha hicho kisomo mara nyingine, na mara nyingine akikifupisha kwa sababu ya safari, au kikohozi, au maradhi au kilio cha mtoto.

Kama alivyosema Anas Ibn Maalik (رضي الله عنه): "**Alifupisha**<sup>(240)</sup> **Mtume** (صلى الله عليه وآله وسلم) siku moja katika Swalah ya **Alfajiri**" (Na Katika Hadiyth nyingine, "**Aliswali** (صلى الله عليه وآله وسلم) Swalah ya Asubuhi akasoma Surah mbili zilizo fupi sana

---

<sup>239</sup>Al-Bukhaariy katika Al-Adaab Al-Mufrad, Ibn Maajah, Ibn Khuzaymah, Ahmad na Siraaj kwa isnaad mbili na zote ni Swahiyh.

#### **Tanbihi:**

'Aamiyn' ya Maamuumiyn nyuma ya Imaam inakuwa kwa sauti na inakuwa inaletwa pamoja na 'Aamiyn' ya Imaam, na wala hawamtangulii kama wafanyavyo waswaliji wengi, na wala hawaicheleweshi na 'Aamiyn' ya Imaam. Hii ndio iliyokuwa Raajih (na nguvu kwangu) kama nilivyoihakiki katika baadhi ya vitabu vyangu; miongoni mwake ni 'Silsilat al-Ahaadith *Adhw-Dhwa'iyfah*' (Namba. 952 Mjalada 2) ambayo imechapishwa kwa Fadhila Zake Allaah, na *Swahiyh at-Targhiyb wat-Tarhiyb* (1.205). Taz. Kiambatisho 6.

<sup>240</sup> Alifupisha Swalah kwa maana kuwa hakuirefusha, na katika Hadiyth hii na nyingine kama hii zinaonyesha kuruhusiwa watoto wadogo kuingia Misikitini. Ama Hadiyth iliyozagaa na kueleweka na wengi hadi kufikia kuwa inasemwa na kila mtu: "Watengeni mbali watoto wenu na Misikiti "ni hadiyth dhwa'iyf na haiwezi kuwa ni dalili kabisa kwa mawafikiano yaliyopo. Na Miongoni mwa walisema kuwa ni dhwa'iyf ni: Ibn Al-Jawziy, Al-Mundhiriyy, Al-Haythamiyy, Ibn Hajr Al-'Asqalaaniyy na Al-Buuswiyriyy. Na akasema 'Abdul-Haqq Al-Ishbiyyi: "Haina asili"

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Hakika mimi huingia katika Swalah hali ya kuwa ninataka kuirefusha, ninaposikia kilio cha mtoto, hufupisha Swalah yangu kwa kuelewa machungu makubwa ya mama yake kwa kilio chake))**<sup>(242)</sup>

"Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akianza kusoma kutoka mwanzo wa Surah, na aghlabu huimaliza"<sup>(243)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Ipeni kila Surah sehemu yake katika Rukuu na Sujuud))**<sup>(244)</sup>

Katika usemi mwengine: **((Kwa Kila Surah Rak'ah))**<sup>(245)</sup>

Mara nyingine huigawa Surah katika Rak'ah mbili<sup>(246)</sup> na mara nyingine huirudia yote nzima katika Rak'ah ya pili<sup>(247)</sup>

---

<sup>241</sup> Ahmad kwa isnaad Swahiyh. Na Hadiyth nyingine imepokelewa na Ibn Abi Daawuud katika al-Maswaahif (4/14/2).

<sup>242</sup> Al-Bukhaariy Na Muslim

<sup>243</sup> Linathibitishwa hili na Hadiyth nyingi zilizotajwa mbele.

<sup>244</sup> Ibn Abi Shaybah (1/100/1), Ahmad na 'Abdul-Ghaniy Al-Maqdisiy katika Sunan (9/2) kwa isnaad Swahiyh.

<sup>245</sup> Ibn Naswr na At-Twahaawiy kwa isnaad Swahiyh. Maana ya Hadiyth kwangu ni: Jaaliyeni kwa kila Rakaa Surah kamili, ili Rakaa iwe na hadhi yake kamili kwa hiyo Surah! Amri hii ni pendekezo na sio lazima utekelezaji wake kutokana na dalili inayofuatia.

<sup>246</sup> Ahmad na Abu Ya'ala kutoka njia mbili. Pia tazama "kisomo katika Swalah ya Alfajiri'

<sup>247</sup> Kama alivyofanya katitka Swalah ya Alfajiri, kama itakavyofuatia.



Mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiunganisha katika Rak'ahh baina Surah mbili au zaidi<sup>(248)</sup>

Mtu Mmoja katika Answaar alikuwa akiswalisha katika Msikiti wa Qubaa, na alikuwa kila anapoanza kuwasomea Surah<sup>(249)</sup> katika Swalah baada ya *Al-Faatihah*, huanza kwa '*Qul Huwa Allaahu Ahad*' [Suratul-Ikhlaasw: 112] hadi mwisho, kisha anasoma Surah nyingine pamoja nayo, na alikuwa akifanya hivyo katika kila Rak'ah. wenzake walimuuliza kwa kusema: "Unaanza na Surah hii, kisha huoni kama inakutosheleza mpaka unasoma nyingine, basi chagua moja; isome hiyo pekee au iache na uisome nyingine". Akasema: "Sitoiacha, ikiwa mtapenda mimi nikuswalisheni (niwe Imaam wenu) kwayo, nitaendelea, lakini ikiwa mtachukiwa, sitokuswalisheni tena", na walikuwa wakimuona kuwa yeye ni mbora miongoni mwao, na pia hawakuwa wanapendekezewa kuswalishwa na mwengine. Na pindi alipokuja Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) wakamuelezea habari hiyo, Akasema (صلى الله عليه وآله وسلم):

**((Ee fulani, kipi kinachokuzuia kutekeleza wanayokuomba watu wako? Na Kipi kinachokupelekea kuwa lazima uisome Surah hii katika kila Rak'ah?))**

Akasema: "Hakika Naipenda Surah hii" akasema (صلى الله عليه وآله وسلم): **((Mapenzi yako kwayo yatakingiza Peponi))**<sup>(250)</sup>

---

<sup>248</sup>Maelezo yake na vyanzo vyake vitafuatia karibuni.

<sup>249</sup>Yaani miongoni mwa Surah baada ya *Al-Faatihah*.

<sup>250</sup>*Al-Bukhaairy* ameipokea ta'liyyan (ni hadiyth inayoondoshwa mwanzo wa isnaad yake Msimulizi mmoja au zaidi kwa mfululizo); na *At-Tirmidhiy* ameipokea Mawswuulan (ni hadiyth inayoungana isnaad yake, iwe imemalizika kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) au kwa Swahaba), na *At-Tirmidhiy* akasema: ni Swahiyh.

## Kuchanganya Kwake (صلى الله عليه وآله وسلم) Baina Ya Surah Zinzofanana Na Nyinginezo Katika Rak'ah

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiunganisha baina ya *An-Nadhwaair*<sup>(251)</sup> miongoni mwa Surah za Mufasswal<sup>(252)</sup>, hivyo basi alikuwa akisoma jozi mojawapo za Surah zifuatazo katika Rak'ah moja<sup>(253)</sup>:

Ar-Rahmaan (55: 78) <sup>(254)</sup> na An-Najm (53: 62).

Al-Qamar (54: 55) na Al-Haaqqah (69: 52).

At-Twuur (52: 49) na Adh-Dhaariyaat (51: 60).

Al-Waaqi'ah (56: 96) na Al-Qalam (68: 52).

Al-Ma'arij (70:44) na An-Naazi'aat (79:46).

Al-Mutwaffiyn (83: 36) na 'Abasa (80: 42).

Al-Muddaththir (74: 56) na Al-Muzzammil (73: 20).

Ad-Dahr (76: 31) na Al-Qiyaamah (75: 40).

An-Nabaa (78: 40) na Al-Mursalaat (77: 50).

Ad-Dukhaan (44: 59) na At-Takwiyr (81: 29).

Mara nyingine alikuwa akiunganisha baina ya Surah kutoka *Sab'at-Twiwaal*-(Surah Saba ndefu); kama al-Baqarah, an-Nisaa na aal-'Imraan katika Rak'ah moja kwenye Swalah ya usiku kama itakavyokuja. Na alikuwa akisema:

---

<sup>251</sup> "An-Nadhwaair": Ni Surah zilizofanana katika maana. Ni kama zile ambazo zote zina nasaha, maamrishi au visa.

<sup>252</sup>Mufasswal, hizi zimekubalika kuwa zinazomalizia Qur-aan mwisho, na mwanzo wake ni Surat Qaaf (Namba 50) kwa rai iliyo sahihi zaidi.

<sup>253</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>254</sup>Namba ya mwanzo inamaanisha Surah, na ya pili ni idadi ya Aayah za hiyo Surah. Na namba zenye kumaanisha Surah, zimetuwekea wazi kuwa hakuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akifuata katika kuunganisha baina ya Surah nyingi za An-Nadhwaair utaratibu wa Surah ulivyo katika Msahafu. Hivyo

inaonyesha kuwa ni jambo lenye kuruhusiwa. Hali kama hiyo itaonekana katika Swalah ya Usiku, japokuwa ni bora zaidi kufuata mpangilio wa Qur-aan.

((Swalah bora kabisa ni yenye kisimamo kirefu)).<sup>(255)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anaposoma:

﴿ أَلَيْسَ ذَلِكَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ تُحْيِيَ الْمَوْتَىٰ ﴾

*Alaysa dhaalika biqaadirin 'alaa-an Yuhyiyal-Marwtaa*

((Je! Huyo hakuwa ni Muweza wa kufufua wafu)). [Al-Qiyaamah 75: 40]

Husema:

سُبْحَانَكَ فَبَلَىٰ

*Sub-haanak fabalaa*

“Utukufu ni Wako Ndio hapana shaka”

Na anaposoma:

﴿ سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَىٰ ﴾

*Sabbi-hisma Rabbikal-A'laa*

((Litakase Jina la Mola wako Aliye juu kabisa)). [Al-A'laa 87: 1]

Husema:

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَىٰ

*Sub-haana Rabbiyal-A'laa*

((Ametakasika Mola wangu Aliye juu)).<sup>(256)</sup>

---

<sup>255</sup> Muslim na Atw-Twahaawiy.

<sup>256</sup> Abu Daawuud na al-Bayhaqiy kwa isnaad Swahiyh. Hadiyth hii ni ya kawaida, hivyo inajumuisha kisomo kwenye Swalah na nje ya Swalah, au Swalah hiyo iwe ni ya Sunnah au ya Faradhi. Ibn Abi Shaybah (2/132/2)

## Ruhusa Ya Kusoma *Al-Faatihah* Pekee

Mu'aadh bin Jabal (رضي الله عنه) alikuwa akiswali 'Ishaa (ya mwisho) pamoja na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), kisha akirudi huwaswalisha wenzake. Usiku mmoja, aliporudi aliwaswalisha, na akaswali kijana mmoja katika watu wake [wa Banu Salamah aliyeitwa Sulaym], lakini (Swalah) ilipokuwa ndefu kwa yule kijana, [alijiondokea] na akaswali [pembezeni mwa Msikiti]. Kisha akatoka na kushika ungwe za ngamia wake na akajiondokea. Mu'aadh (رضي الله عنه) Alipomaliza kuswali alielezwa yaliyotokea, akasema: "Bila shaka ana baadhi ya unafiki! Nitamweleza Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alivyofanya". Na yule kijana naye akasema: "Nami nitamweleza Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alivyofanya". Kulipopambazuka, walikuja kwa Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم), basi Mu'aadh akamweleza yale aliyoyafanya yule kijana. Kijana akasema: "Ee Mjumbe wa Allaah! Yeye hukaa na wewe muda mrefu, kisha anarudi na kuturefushia". Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: **((Je, wewe ni mfitini ewe Mu'aadh?!))**. Na akasema kumwambia yule kijana<sup>(257)</sup>: **((Vipi unafanya unaposwali ee mtoto wa ndugu yangu?))** Akamjibu: "Nasoma Kifungulio cha Kitabu, kisha namuomba Allaah Pepo, na najikinga Kwake kutokana na moto. Na hakika mimi sielewi *dandanah*<sup>(258)</sup> yako wala *dandanah* ya Mu'aadh!" Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akamwambia: **((Hakika Mimi na Mu'aadh tuko**

---

amesimulia kutoka kwa Abu Muusa al-Ash'ariyy na al-Mughiyrah kwamba wao wawili walikuwa wakisema hivyo katika Swalah ya Faradhi. Na ameipokea kutoka kwa 'Umar na 'Aliy bila ya maelezo hayo.

<sup>257</sup> Asili ni 'Yule Kijana".

<sup>258</sup> "*Dandanah*" ni mtu anaposema maneno kwa madaha na kusikiwa mvumo wa maneno yake lakini hayafahamiki. Ni karibu kidogo na kunong'ona. (*An-Nihaayah*).

<sup>259</sup> Ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake (1634) na Al-Bayhaqiy kwa isnaad Swahiyh. Na pahala penye ushahidi kutokana na Hadiyth pako katika Abu Daawuud (Namba 758, *Swahiyh Abi Daawuud*) na asili ya kisa chenye kipo katika asw-Swahiyhayn (Al-Bukhaariy na Muslim). Nyongeza ya mwanzoni iko katika usimulizi wa Muslim. Ya pili iko katika Ahmad (5/74), na ya tatu na ya nne katika Al-Bukhaariy. Pia mlango wa hizi, ni Hadiyth iliyotolewa na Ibn 'Abbaas kwamba Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) aliswali Rakaa mbili ambazo hakusoma ndani yake isipokuwa Kifungulio cha Kitabu (*Al-Faatihah*) pekee". Imesimuliwa na Ahmad (1/282), Al-Haarith bin Abi Usaamah katika musnad yake (Uk. 38 kutoka zawaaid yake) na Al-Bayhaqiy (2/) kwa isnaad dhwa'iyf. Nilikuwa nimesema kuwa Hadiyth hii ni nzuri katika chapa zilizopita, kisha ikanibainikia kuwa nilikuwa nimekwenda kombo, kwa sababu Hadiyth yenyewe inazunguka kwa Handhwalah Ad-Dawsiy ambaye anaeleweka kuwa ni dhaifu, na sielewi kwa nini sikuweza kugundua hili?! Huenda nilifikiri kuwa ni mtu mwengine. Hata hivyo, Sifa zote ni Zake Allaah Aliyeniongoza kuweza kufikia kutambua kosa langu, na ndio maana nikakimbilia kuisahihisha katika chapa. Kisha Allaah Akanisawazisha kwa kuniruzuku Hadiyth hii bora ya Mu'aadh ambayo inahusisha yaliyoashiriwa katika Hadiyth ya Ibn 'Abbaas. Sifa zote ni Zake Allaah Ambaye kwa Neema Zake yanatimia mema.

## Kunyanyua Sauti Na Kusoma Kimya Kimya Katika Swalah Tano Na Nyenginezo

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akitoa sauti katika Swalah ya Asubuhi na katika Rak'ah mbili za mwanzo za Swalah ya Magharibi na 'Ishaa, na akisoma kimya kimya katika Swalah za Adhuhuri, Alasiri na Rak'ah ya tatu ya Swalah ya Magharibi na Rak'ah mbili za mwisho za Swalah ya 'Ishaa.<sup>(260)</sup>

Walikuwa wakiweza kuelewa kuwa anasoma kimya kimya kutokana na mtikisiko wa ndevu zake<sup>(261)</sup> na kwa kuwasikilizisha Aayah mara nyingine<sup>(262)</sup>.

Pia alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akitoa sauti katika Swalah ya Ijuma na Swalah za 'Iyd mbili<sup>(263)</sup>, na Swalah ya kuomba mvua<sup>(264)</sup>, na Swalah ya kupatwa<sup>(265)</sup> jua au mwezi.

---

<sup>260</sup> Katika hili kuna Ijmaa ya Waislamu iliyopokewa na Khalaf kutoka kwa Salaf (waliokuja kabla yetu kutoka kwa waliotangulia) pamoja na Hadiyth Swahiyh ambazo zinathibitisha hayo kama alivyosema An-Nawawiy. Na zitafuatia baadhi yake. Tazama pia *Al-Irwaa* (345).

<sup>261</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>262</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>263</sup> Tazama kisomo (sehemu ya *Tilaawah*) chake (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Swalah ya Ijuma na Swalah za 'Iyd mbili.

<sup>264</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>265</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

## Kunyanyua Sauti Na Kusoma Kimya Katika Swalah Ya Usiku <sup>(266)</sup>

Ama katika Swalah ya usiku, mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه) akisoma kimya kimya na mara nyingine kwa sauti<sup>(267)</sup>, na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anaposoma hali ya kuwa yuko nyumbani kwake, humsikia kisomo chake aliyeko barazani mwake<sup>(268)</sup>.

Huenda mara moja moja akapandisha sauti yake zaidi ya hivyo hadi akaisikia aliyelala<sup>(269)</sup>. (Yaani nje ya baraza/uwa).

Na hivyo ndivyo alivyowaamrisha Abu Bakr na 'Umar (رضي الله) wakati alipokuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) ametoka nje usiku mmoja akatahamaki kumuona Abu Bakr (رضي الله عنه) anaswali huku akiishusha sauti yake chini. Na akampitia 'Umar bin Al-Khattaab (رضي الله عنه) aliyekuwa akiswali kwa kunyanyua sauti yake juu. (Baadaye,) walipokutana pamoja kwa Mtume

---

<sup>266</sup> 'Abdul-Haqq alisema katika Tahajjud (90/1): "Ama Swalah za Sunnah za mchana, hakikusihi chochote Swahiyh kutoka kwake (صلى الله عليه وآله وسلم) chenye kuonyesha (kuhusu) kuswali kimya au kwa sauti katika Swalah hizo, Na kinachoelekea (inavyoelekea) zaidi ni kwamba alikuwa akisoma kimya kimya katika hizo Swalah. Imeripotiwa kutoka kwake (صلى الله عليه) kwamba mara moja (wakati wa mchana,) alimpitia 'Abdullaah bin Hudhaafah ambaye alikuwa akiswali mchana na kusoma kwa sauti, akamwambia: Ewe 'Abdullaah, Amesikia (mwache) Allaah (Asikie), na wala usitusikilizishe (sio) sisi)). Lakini Hadiyth hii haina nguvu"

<sup>267</sup> Muslim na Al-Bukhaariy katika *Af'aa' Al-'Ibaad*.

<sup>268</sup> Abu Daawuud na At-Tirmidhiy katika Shamaail ikiwa na isnaad nzuri.

Hadiyth ina maana kwamba yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa yu katikati baina ya ukimya na kupaza sauti.

<sup>269</sup> An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy katika Shamaail na Al-Bayhaqiyy katika Dalaail ikiwa na isnaad nzuri.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ((Mwenye kusoma Qur-aan kwa kunyanyua sauti, ni kama mfano wa mwenye kutoa sadaka kwa kuonekana na watu, na mwenye kusoma Qur-aan kimya kimya kwa kushusha sauti yake, ni kama mwenye kutoa sadaka kwa siri))<sup>(271)</sup>.

### **Aliyokuwa Akisoma (صلى الله عليه وآله وسلم) Katika Swalah Mbali Mbali**

Kuhusu Surah gani na Aayah gani aliyokuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiisoma katika Swalah, hilo linatofautiana kwa kutofautika kwa Swalah tano na Swalah nyenginezo. Basi chukua maelezo ya upambanuzi wake kwa kuanzia na Swalah ya kwanza katika Swalah tano:

---

<sup>270</sup>Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amesema kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>271</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.



## 1- Swalah Ya Alfajiri

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma Surah<sup>(272)</sup> ndefu za mufasswal<sup>(273)</sup> hivyo alikuwa (wakati mwengine) akisoma Al-Waaqi'ah (56: 96) na mfano wake katika Rak'ah mbili.<sup>(274)</sup> Alisoma kutoka Surat-Twuur (52: 49) katika Hijjatul-Wadaa' (Hijjah ya Kuaga).<sup>(275)</sup>

Mara nyingine, alikuwa akisoma Surat Qaaf [50: 45] na mfano wake [katika Rak'ah ya mwanzo].<sup>(276)</sup>

Mara nyingine alikuwa akisoma Surah fupi za mufasswal kama:

﴿ إِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ ﴾

*Idhash Shamsu kuwwirat*

((Jua litakapokunjwa)) [At-Takwiyr 81: 29]).<sup>(277)</sup>  
Na mara moja alisoma:

﴿ إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ﴾

*Idhaa zulzilatil ardhu zilzaalaha*

((Itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake!)). [Az-Zilzalah 99: 8]

---

<sup>272</sup> An-Nasaaiy na Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>273</sup> Sehemu ya saba ya mwisho ya Qur-aan, kuanzia Surah Qaaf (Namba 50) kama ilivyo rai yenye nguvu kabisa kama ilivyotangulia.

<sup>274</sup> Ahmad, Ibn Khuzaymah (1/69/1) na Al-Haakim ambaye amesema kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>275</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>276</sup> Muslim na At-Tirmidhiy. Imetolewa pamoja na inayofuatia katika *Al-Irwaa* (345).

<sup>277</sup> Muslim na Abu Daawuud.

katika Rak'ah zote mbili, jambo lililomfanya msimulizi kusema: "Sielewi kama Mjumbe wa Allaah alisahau au aliisoma kwa makusudi."<sup>(278)</sup>

Alisoma mara moja akiwa safarini:

﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴾

*Qul A'uwduhu birabbil-falaq*

((Sema: Najikinga kwa Mola wa mapambazuko)). [Al-Falaq 113: 5]  
na

﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴾

*Qul A'uwduhu birabbin Naas*

((Sema: Najikinga kwa Mola wa wanaadamu)). [An-Naas 114: 6]<sup>279</sup>

Akasema kumwambia 'Uqbah bin 'Aamir (رضي الله عنه): ((Soma Al-Mu'awwidhatayn<sup>(280)</sup> katika Swalah zako, kwani hakuna mwenye kutafuta kinga kama hiyo))<sup>(281)</sup>.

Mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma zaidi ya hivo, kwani alikuwa akisoma Aayah sitini (60) au zaidi<sup>(282)</sup>.

---

<sup>278</sup> Abu Daawuud na Al Bayhaqiy ikiwa na isnaad Swahiyh. Kinachodhihiri ni kuwa yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) alifanya hivyo kwa makusudi ili kuthibitisha kujuzu kwake.

<sup>279</sup> Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah (1/76/1), Ibn Bushraan katika Al-Amaaliy na Ibn Abi Shaybah (12/176/1). Al-Haakim amesema kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>280</sup> Surah mbili za kujikinga; yaani Surah mbili za mwisho katika Qur-aan, zote zinaanzia na Qul-A'uwduhu.... (Sema najikinga....).

<sup>281</sup> Abu Daawuud na Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>282</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma Surat Ar-Ruum [30: 60]<sup>(283)</sup> na mara nyingine akisoma Surat Yaasiyn [36: 83]<sup>(284)</sup>.

Mara moja aliswali Swalah ya Alfajiri Makkah, akaanza kusoma Suratul-Mu-minuun [23: 118] hadi alipofikia kutajwa Muusa na Haaruun au kutajwa 'Iysa<sup>(285)</sup> -Msimulizi mmoja hakuwa na hakika- alianza kukohoa hivyo akarukuu<sup>(286)</sup>.

Mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiwaswalisha katika Swalah ya Alfajiri kwa kusoma Suratu Asw-Swaaffaat [77: 182]<sup>(287)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiiswali Swalah ya Alfajiri siku ya Ijumaa kwa kusoma Surat As-Sajdah [32: 30] (katika Rak'ah ya mwanzo na Rak'ah ya pili) Surat Ad-Dahr [76: 31].<sup>(288)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akirefusha Rak'ah ya kwanza na kufupisha Rak'ah ya pili.<sup>(289)</sup>

---

<sup>283</sup> An-Nassaa'iy, Ahmad na Al-Bazzaar kwa isnaad nzuri.

<sup>284</sup> Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>285</sup> Muusa ametajwa katika Aayah ya 45: ((ثُمَّ أَرْسَلْنَا مُوسَى وَأَخَاهُ هَارُونَ بِآيَاتِنَا وَسُلْطَانٍ مُّبِينٍ)) na 'Iysa ametajwa katika Aayah ya 50: ((وَجَعَلْنَا ابْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُ آيَةً وَآوَيْنَاهُمَا إِلَى رَبْوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ )) ((وَمُعِينٍ))

<sup>286</sup> Muslim na Al-Bukhaariy katika Ta'aliyqan, nayo ni Hadiyth inayoondoshwa mwanzo wa isnaad yake msimulizi mmoja au zaidi kwa mfululizo kama ilivyoelezwa nyuma. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (397).

<sup>287</sup> Ahmad na Abu Ya'laa katika Musnad zao, na Al-Maqdisiy katika Al-Mukhtaarah.

<sup>288</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>289</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

## Kisomo katika Sunnah ya Alfajiri

Kisomo chake (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Rak'ah mbili za Sunnah ya Alfajiri, kilikuwa chepesi mno<sup>(290)</sup> hadi 'Aaishah (رضي الله عنها) alikuwa akijiuliza kwa kusema: "Je, amesoma ndani yake Kifungulio cha Kitabu (Suratul Faatihah)?"<sup>(291)</sup>.

Mara nyingine alikuwa akisoma baada ya *Al-Faatihah* katika Rak'ah ya mwanzo ya hizo mbili Aayah hii:

﴿ قُولُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْنَا... ﴾

*Quuluu Aamanna bi Llaahi wamaa un-zila ilaynaa...*

**((Semeni nyinyi: Tumemwamini Allaah na yale tuliyoteremshiwa sisi...)). [Al-Baqarah 2: 136]**

mpaka mwisho wa Aayah.

(katika Rak'ah ya kwanza,) na katika ya pili alikuwa akisoma Aayah:

﴿ قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ ﴾

*Qul yaa Ahlal-Kitaabi ta'alaw ilaa kalimatin sawaa in-baynanaa wabaynakum*

**((Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njoooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi...)) [Al-'Imraan 3: 64]** <sup>(292)</sup>

mpaka mwisho wa Aayah.

Mara nyingine husoma badala ya Aayah ya pili:

﴿ فَلَمَّا أَحَسَّ عِيسَىٰ مِنْهُمُ الْكُفْرَ ﴾

---

<sup>290</sup> Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>291</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>292</sup> Muslim, Ibn Khuzaymah na Al-Haakim.

*Falamma Ahassa 'Iysa min-humul kufra...*

**(('Iysa alipohisi kuwa kati yao pana ukafiri))** [Al-'Imraan 3: 52]<sup>(293)</sup>

mpaka mwisho wa Aayah.

Mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma Suratul-Kaafiruun [109 -6] katika Rak'ah ya kwanza, na Suratul-Ikhlaasw [112-4] katika Rak'ah ya pili.<sup>(294)</sup>

Pia alikuwa akisema: **((Hizi ni jozi bora kabisa za Surah (hizi)).**<sup>(295)</sup>

Alimsikia mtu akisoma Surah ya mwanzo - Suratul-Kaafiruun - katika Rak'ah ya kwanza, akasema: **((Huyu mja amemwamini Mola wake)).** Kisha mtu huyo akasoma Surah ya pili - Suratul-Ikhlaasw - katika Rak'ah nyingine, akasema: **((Huyu mja amemwelewa Mola wake)).**<sup>(296)</sup>

## 2- Swalah Ya Adhuhuri

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma katika Rak'ah mbili za mwanzo Suratul-Faatihah na Surah mbili, hurefusha ya kwanza kuliko ya pili.<sup>(297)</sup>

Mara nyingine alikuwa akiirefusha urefu ambao ilikuwa inaweza kufika kuqimiwa kwa Swalah ya Adhuhuri, na aliweza

---

<sup>293</sup> Muslim na Abu Daawuud.

<sup>294</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>295</sup> Ibn Maajah na Ibn Khuzaymah.

<sup>296</sup> Atw-Twahaawiy, Ibn Hibbaan katika Swahiyh yake na Ibn Bushraan. Ibn

Hajar amesema kuwa ni nzuri katika *Al-Ahaadiyth Al-'Aaliyaat* (Namba, 16).

<sup>297</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

mtu kwenda Al-Baqiy' kukidhi haja yake, [kisha aende nyumbani kwake], kutawadha, kisha aje hali ya kuwa Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akiwa bado yuko katika Rak'ah ya mwanzo, kwa namna alivyokuwa akiirefusha<sup>(298)</sup>.

(Pia) walikuwa wakidhania kwamba alikuwa akifanya hivyo ili watu waweze kuidiriki Rak'ah ya mwanzo.<sup>(299)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma katika kila Rak'ah ya hizo Rak'ah mbili, kadiri ya Aayah thelathini, kiasi cha kusoma As-Sajdah [32-30] na ikiwemo Al-Faatihah.<sup>(300)</sup> (na kufuatia As-Sajdah [32-30])

Mara nyingine alikuwa akisoma:

﴿ وَالسَّمَاءِ وَالطَّارِقِ ﴿١﴾ ﴾

*Was Samaai watw-Twaariq*

**((Naapa kwa mbingu na kinachokuja usiku!))** [At-Twaariq: 86-17],  
na

﴿ وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ ﴿١﴾ ﴾

*Was Samaai dhaatil Buruuj*

**((Naapa kwa mbingu yenye Buruji!))** [Al-Buruuj: 85-22],  
na

﴿ وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١﴾ ﴾

*Wal- Layli idhaa yagh-shaa*

---

<sup>298</sup> Muslim na Al-Bukhaariy katika *Juz-u Al-Qiraat* (Makala ya Tilaawah).

<sup>299</sup> Abu Daawuud ikiwa na isnaad Swahiyh na Ibn Khuzaymah (1/165/1).

<sup>300</sup> Ahmad na Muslim.

**((Naapa kwa usiku unapofunika!))** [Al-Layl: 92-21],  
na mfano wa Surah zilizofanana na hizi.<sup>(301)</sup>  
Na huenda akasoma



*Idhas Samaaun shaqqat*

**((Itapochanika mbingu))** [Al-Inshiqaaq: 84-25],  
na mfano wake.<sup>(302)</sup>

Walikuwa wakiweza kuelewa kwamba alikuwa anasoma katika Adhuhuri na Alasiri kutokana na mtikisiko wa ndevu zake.<sup>(303)</sup>

### **Kisomo Chake (صلى الله عليه وآله وسلم) Cha Aayaat Baada Ya Al-Faatihah Katika Rak'ah Mbili Za Mwisho**

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akizifanya Rak'ah mbili za mwisho fupi zaidi kulinganisha na Rak'ah mbili za mwanzo kiasi cha nusu yake, kiasi cha Aayah kumi na tano,<sup>(304)</sup> na pengine

---

<sup>301</sup>Abu Daawuud, At-Tirmidhiy na Ibn Khuzaymah (1/67/2). Wawili wa mwisho wamesema kuwa ni Swahiyh.

<sup>302</sup>Ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake (1/67/2).

<sup>303</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>304</sup> Ahmad na Muslim. Katika Hadiyith hii, kuna dalili kwamba kusoma Surah zaidi ya Suratul-Faatihah katika Rakaa mbili za mwisho ni Sunnah, na Maswahaba wengi walifanya hivyo. Miongoni mwao ni Abu Bakr (رضي الله عنه). (Pia) na ni rai ya Imaam Ash-Shaafi'iy, na ni sawa tu kama itakuwa katika Adhuhuri au katika Swalah nyinginezo. Maulamaa waliofuatia, Abul-Hasanaat Al-Laknawiy katika ((At-Ta'aliyq Al-Mummajad 'Alaa Muwattwa Muhammad)) (Uk. 102) (akasema:"Na baadhi ya wafuasi wetu wamekuja na rai ya ajabu, kwani waliwajibisha Sajdatus-Sahw (Sajda ya kusahau) kwa kusoma Surah katika Rakaa mbili za mwisho. Na kwa hakika wamejibiwa na wenye kutoa maelezo/ sharh ya Al-Maniyyah; Ibraahiym Al-Halabiy na Ibn Amiyr Haaj na wengineo, wamejibiwa

Alikuwa mara nyingine akiwasikilizisha Aayah.<sup>(306)</sup> Na walikuwa wakisikia kutoka kwake mvumo wa kisomo chake:

﴿ سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴾

*Sabbih-isma Rabbikal-A'laa*

((Litakase jina la Mola wako Aliye juu kabisa)) [Al-A'laa 87-19],

na

﴿ هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ ﴾

*Hal-ataaka Hadiythul Ghaashiyah*

((Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?)) [Al-Ghaashiyah 88-26].<sup>(307)</sup>

Mara nyingine husoma:

﴿ وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ ﴾

*Was Samaai dhaatil Buruuj*

((Naapa kwa mbingu yenye Buruji!)) [Al-Buruuj 85-22],

na

﴿ وَالسَّمَاءِ وَالطَّارِقِ ﴾

---

<sup>305</sup> Al-Bukhaariy Na Muslim.

<sup>306</sup> Ibn Khuzaymah katika Swahiyh yake (1.67/2) na Adh-Dhiyaa Al-Maqdsiy katika Al-Mukhtarah ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>307</sup> Al-Bukhaariy katika Makala ya Tilaawah, na At-Tirmidhiy ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh.



### *Was Samaai watw Twaariq*

**((Naapa kwa mbingu na kinacho kuja usiku!))** [Atw-Twaariq 86-17],

na Sura nyinginezo mfano wa hizi mbili.<sup>(308)</sup>  
Mara nyingine alikuwa akisoma:

﴿ وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴾

### *Wal-Layli Idhaa Yaghshaa*

**((Naapa kwa usiku unapofunika!))** [Al-Layl 92-21],  
Na mfano wake.<sup>(309)</sup>

## 3- Swalah Ya Alasiri

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma katika Rak'ah mbili za mwanzo *Al-Faatihah* na Surah mbili, hurefusha Rak'ah ya kwanza kuliko ya pili<sup>(310)</sup> na walikuwa wakidhani kuwa alikuwa akifanya hivyo ili watu waweze kuidiriki Rak'ah ya mwanzo.<sup>(311)</sup>

Alikuwa akisoma kadiri ya Aayah kumi na tano katika kila Rak'ah mbili za mwanzo, kiasi cha nusu ya kisomo alichokuwa akisoma katika Rak'ah mbili za mwanzo za Swalah ya Adhuhuri, na alikuwa akizifupisha Rak'ah mbili za mwisho kiasi cha nusu ya urefu wa Rak'ah mbili za mwanzo.<sup>(312)</sup>

---

<sup>308</sup> Muslim na At-Twayaalisiiy.

<sup>309</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>310</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>311</sup> Abu Daawuud ikiwa na isnaad Swahiyh na Ibn Khuzaymah.

<sup>312</sup> Ahmad na Muslim.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma *Al-Faatihah* katika Rak'ah mbili za mwisho.<sup>(313)</sup> Alikuwa akiwasikilizisha Aayaah (au zaidi) mara nyingine<sup>(314)</sup>, na alikuwa akisoma Surah tulizozitaja hapo nyuma katika Swalah ya Adhuhuri.

#### 4- Swalah Ya Maghrib

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma katika Swalah hii – baadhi ya nyakati -Surah fupi za Mufasswal<sup>(315)</sup>, kiasi cha “wao wanapomaliza kuswali naye, huondoka mmoja wao, na hakika mtu (angeweza kuutupa na) kuona sehemu iliyoangukia mshale wake.”<sup>(316)</sup>.

Na (Mara moja), alipokuwa safarini alisoma:

﴿ وَالَّتَيْنِ وَالزَّيْتُونَ ﴾

*Wat Tiyni waz-zaytuun*

**((Naapa kwa tini na zaytuni!))** [At-Tiyn 95: 8]

katika Rak'ah ya pili.<sup>(317)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) mara nyingine akisoma Surah ndefu za Mufasswal-na za wastani, hivyo alikuwa akisoma:

﴿ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ﴾

*Al-ladhiyna kafaruu waswadduu 'an sabiyli Llaahi*

**((Waliokufuru na wakazuilia njia ya Allaah)).** [Muhammad 47: 1].<sup>(318)</sup>

---

<sup>313</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>314</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>315</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>316</sup> An-Nasaaiy na Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>317</sup> Atw-Twayaalisy na Ahmad katika isnaad Swahiyh.

Mara nyingine akisoma Suratu-Twuur (52: 49)<sup>(319)</sup>

Na mara nyingine akisoma Suratul-Mursalaat [77: 50] ambayo aliisoma katika Swalah (yake) ya mwisho aliyoiswali (صلى الله عليه وآله وسلم).<sup>(320)</sup>

Mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma moja kati ya Surah mbili ndefu (atw-Twuulayayn)<sup>(321)</sup>; [Al-A'araaf 7: 206] (katika Rak'ah mbili).<sup>(322)</sup> Na mara nyingine akisoma Al-anfaal [8: 75] katika Rak'ah mbili.<sup>(323)</sup>

## Kisomo Katika Sunnah (Baada Ya Swalah) Ya Magharibi

Ama katika Sunnah ya baada (al-ba'diyyah) ya Maghrib, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma:

﴿ قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴾

*Qul yaa ayyuhal-kaafiruun*

**((Sema: Enyi makafiri!)).** [Al-Kaafiruun 109: 6],  
na

﴿ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴾

---

<sup>318</sup> Ibn Khuzaymah (1/166/2), Atw-Twabaraaniy na Al-Maqdisiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>319</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>320</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>321</sup> *At-Twuulayayn* ni Al-A'araaf [7] kwa makubaliano, na Al-an'aam [6] kutokana na kauli iliyo sahihi zaidi kama ilivyotajwa katika *Fat-h Al-Baariy*.

<sup>322</sup> Al-Bukhaariy, Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah (1/68/1), Ahmad, Siraaj na Mukhlisw.

<sup>323</sup> Atw-Twabaraaniy katika *Mu'jam al-Kabiyr* ikiwa na isnaad Swahiyh.

### *Qul Hurwa Allaahu Ahad*

((Sema: Yeye Allaah ni wa Pekee)). [Al-Ikhlaasw 112: 4].<sup>(324)</sup>

### 5- Swalah Ya 'Ishaa

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma Surah za kati na kati za Mufasswal-katika Rak'ah mbili za mwanzo<sup>(325)</sup>, hivyo alikuwa mara nyingine akisoma:

﴿ وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴾

*Wash shamsi wadhuhaahaa*

((Naapa kwa jua na mwangaza wake!)) (Ash-Shams 91: 15) na Surah nyingine zilizofanana na hiyo<sup>(326)</sup>. Na mara nyingine alikuwa akisoma:

﴿ إِذَا السَّمَاءُ أَنْشَقَّتْ ﴾

*Idhaas samaa-un shaqqat*

((Itapochanika mbingu)) [Al-Inshiqaaq 84: 25), na alikuwa akileta *Sajdah* humo<sup>(327)</sup>.

Pia mara moja alipokuwa safarini alisoma:

﴿ وَالزَّيْتُونَ ﴾

*Wat tiyni waz-zaytuun*

((Naapa kwa tini na zaytuni!)) (At-Tiyn 95:8) katika Rak'ah ya mwanzo.<sup>(328)</sup>

---

<sup>324</sup> Ahmad, Al-Maqdisiy, An-Nasaaiy, Ibn Naswr na Atw-Twabaraaniy.

<sup>325</sup> An-Nasaaiy na Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>326</sup> Ahmad na At-Tirmidhy ambaye amekiri ni nzuri.

<sup>327</sup> Al-Bukhaariy, Muslim na An-Nasaaiy.

Alikataza (صلى الله عليه وآله وسلم) kurefusha kisomo katika 'Ishaa, katazo hili lilikuja wakati Mu'aadh bin Jabal alipowaswalisha watu wake Swalah ya 'Ishaa akaifanya ndefu, akajiondoa mtu mmoja katika Answaar na kuswali pekee. Mu'aadh akaelezwa habari ya mtu huyo akasema: "Hakika yeye ni mnafiki". Mtu yule ilipomfikilia taarifa, alikwenda kwa Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) na kumweleza vile alivyosema Mu'aadh. Basi hapo Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akamwambia Mu'aadh: **((Je, unataka kuwa mfitini Ee Mu'aadh? Utaposwalisha watu basi soma:**

﴿ وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا ﴾

*Wash shamsi wadhuhaaha*

**((Naapa kwa jua na mwangaza wake!)) [Ash-Shams 91: 15],**  
na

﴿ سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴾

*Sabbi his-ma Rabbikal-A'laa*

**((Litakase Jina la Mola wako Mlezi Aliye juu kabisa)) [Al-A'laa 87: 19],**  
na

﴿ وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى ﴾

*Wal-layli idhaa yagh-shaa*

**((Naapa kwa usiku unapofunika!)) [Al-Layl 92: 21]**

---

<sup>328</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

[Bila ya shaka huswali nyuma yako watu wazima, wagonjwa na wenye haja zao].<sup>(329)</sup>

## 6- Swalah Ya Usiku

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) mara nyingine akifupisha<sup>(330)</sup> kisomo katika hiyo Swalah ya usiku, na mara nyingine hukirefusha, na wakati mwengine hukirefusha sana, mpaka ikampelekea 'Abdullaah bin Mas'uud kusema: "Usiku mmoja niliswali pamoja na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), basi aliendelea kusimama (kwa) muda mrefu sana mpaka nikawaza jambo baya. Pakaulizwa: "Uliwaza nini"? Akajibu: "Nilifikiria kukaa chini na kumuacha Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)!"<sup>(331)</sup>.

Hudhayfah bin Al-Yamaan pia alisema:

"Usiku mmoja niliswali na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), basi alianza kusoma Surat Al-Baqarah (2: 286). Nikasema (moyoni): "Atarukuu baada ya Aayah mia". Lakini aliendelea, nikawaza kuwa huenda ataimaliza Surah katika [Rak'ah mbili]. Lakini aliendelea na nikasema: "Atarukuu atakapoimaliza." Kisha akaanza kusoma Surat An-Nisaa (4: 176), akaisoma yote. Kisha akaanza kusoma Surat Al-Imraan (3: 200)<sup>(332)</sup>, akaisoma yote. Alikuwa akisoma polepole, anapopita kwenye Aayah zenye kumtukuza Allaah humtukuza, na anapopita kwenye Aayah zenye maombezi huomba, na anapopita kwenye Aayah za

---

<sup>329</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni. Imetolewa pia katika *Al-Irwaa* (295).

<sup>330</sup> An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>331</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>332</sup> Hivi ndivyo ilivyopokelewa kutangulizwa Surat an-Nisaa (4) kabla ya al-Imraan (3), na hiyo ni dalili kwamba inaruhusiwa kusoma kwa kuacha kufuatilia mpangilio wa Msahafu wa 'Uthmaan katika kusoma. Umekwishapita mfano kama huu.

Pia usiku mmoja alipokuwa akiumwa, alisoma Surah saba ndefu.<sup>(334)</sup>

Pia alikuwa akisoma moja ya Surah hizi saba ndefu katika kila Rak'ah.<sup>(335)</sup>

Haikupata kutokea kuwa yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) alisoma Qur-aan nzima katika usiku mmoja [abadani]<sup>(336)</sup>, na wala hakumkubalia hivyo 'Abdullaah bin 'Amru (رضي الله عنه) wakati alipomwambia: **((Soma Qur-aan nzima kila mwezi))**. Akasema: Nikamwambia: "Ninao uwezo wa kufanya zaidi ya hivyo". Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: **((Isome katika masiku ishirini))**. Akasema: Nikamwambia: "Ninao uwezo wa kusoma zaidi". Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: **((Basi isome katika siku saba na wala usipunguze zaidi ya hapo))**.<sup>(337)</sup>

Kisha Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alimruhusu kuisoma Qur-aan nzima katika siku tano.<sup>(338)</sup>

Kisha Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alimruhusu kuisoma Qur-aan nzima katika siku tatu.<sup>(339)</sup>

Kisha Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akamkataza kuisoma Qur-aan nzima chini ya hivyo<sup>(340)</sup> na akatoa sababu kwayo kwa

---

<sup>333</sup> Muslim na An-Nasaaiy.

<sup>334</sup> Abu Ya'laa na Al-Haakim ambae amesema kuwa ni Swahiy, na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye. Ibn al-Athiyr amesema: "...Surah saba ndefu ni: Al-Baqarah (2), Al-'Imraan (3), An-Nisaa (4), Al-Maaidah (5), Al-An'aam (6), Al-A'raaf (7) na At-Tawbah (9)".

<sup>335</sup> Abu Daawuud na An-Nasaaiy kwa isnaad Swahiyh.

<sup>336</sup> Muslim na Abu Daawuud.

<sup>337</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>338</sup> An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy ambaye amesema kuwa ni Swahiyh.

<sup>339</sup> Al-Bukhaariy na Ahmad.

Kisha alimwambia: ((Kwa hakika kila mwenye kuabudu huwa ana muda wa shirrah<sup>(343)</sup>, na kila shauku ina kipindi cha kupunguka, aidha ielekee kwenye Sunnah au kwenye bid'ah. Hivyo basi mwenye kuwa upungufu wake umeelekea kwenye Sunnah, huyo basi amepata uongofu, na mwenye kuwa upungufu wake umeelekea kwenye kinyume cha hivyo, basi ameangamia))<sup>(344)</sup>.

---

<sup>340</sup> Ad-Daarimiy na Sa'iyd ibn Masnuur katika Sunan yake kwa isnaad Swahiyh.

<sup>341</sup> Ahmad kwa isnaad Swahiyh.

<sup>342</sup> Ad-Daarimiy na At-Tirmidhiy ambaye amesema kuwa ni Swahiyh.

<sup>343</sup> "Shirrah" ni msisimko, hamu, shauku, nguvu. Na Shirrah ya vijana mwanzo wake ni bidii, nguvu, hamasa na raghba. Imaam Atw-Twahaawiy amesema: "Ni bidii na hamasa katika vitendo ambavyo wanavitaka Waislamu kutokana na nafsi zao wenyewe katika 'amali zao ambazo wanajikurubisha kwazo kwa Mola wao عزوجل. Na kwa hakika Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) anapenda zaidi kutoka kwao hivyo, na sio vile vitendo walivyovianza kutokana na shauku na hamasa ambayo hawana budi isipokuwa watakuwa na upungufu na kuachana navyo na kushikamana na kinyume chake. Kwa hiyo, aliwaamrisha waendeleo kushikamana na vitendo vyema ambavyo wataweza kuviendeleza na kudumu navyo hadi watakapokutana na Mola wao عزوجل. Katika kulifafanua hili, imesimuliwa kutoka kwake (صلى الله عليه وآله وسلم) kwamba amesema: ((**Vitendo vipendezavyo kwa Allaah, ni vile vyenye kudumishwa japo kuwa ni vichache**)).

Nasema: "Hadiyth hii ambayo ameitoa kwa njia ya kuonyesha kuwa msimulizi wake hajulikani (Majhuul) kama linavyomaanisha neno "imesimuliwa", ni Swahiyh na ni waliyowafikiana kwayo Al-Bukhaariy na Muslim kutokana na Hadiyth ya Mama wa Waumini 'Aaishah (رضي الله عنها).

<sup>344</sup>Ahmad na Ibn Hibbaan katika Swahiyh yake.



Kwa sababu hii, akawa (صلى الله عليه وآله وسلم) hasomi Qur-aan nzima chini ya siku tatu.<sup>(345)</sup>

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Atakayeswali katika usiku na akasoma Aayah mia mbili, basi huandikwa miongoni mwa watiifu wenye kumtakasia Allaah)).**<sup>(346)</sup>

Pia alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma Surat Bani Israaiyl (17: 111) na Surat Az-Zumar (49: 75) katika kila usiku<sup>(347)</sup>. Na alikuwa akisema: **((Atakayeswali katika usiku na akasoma Aayah mia, basi hatoandikwa miongoni mwa walioghafilika))**<sup>(348)</sup>. Mara nyingine alikuwa akisoma katika kila Rak'ah kiasi cha Aayah khamisi au zaidi<sup>(349)</sup>, na mara nyingine akisoma kiasi cha Surat Al-Muzammil (73: 20).<sup>(350)</sup>

Na wala hakuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akiswali usiku mzima<sup>(351)</sup>, isipokuwa kwa nadra, kwani mara moja 'Abdullaah

---

<sup>345</sup> Ibn Sa'ad (1/376) na Abu ash-Shaykh katika *Akhlaaq An-Nabbiyy* (صلى الله عليه وآله وسلم) (281).

<sup>346</sup> Ad-Daarimy na Al-Haakim ambaye amesema kuwa ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>347</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>348</sup> Ahmad na Ibn Naswr kwa isnaad Swahiyh.

<sup>349</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>350</sup> Ahmad na Abu Daawuud kwa isnaad Swahiyh.

<sup>351</sup> Muslim na Abu Daawuud. Nimesema: "Kwa Hadiyth hii na nyingine, inaonyesha kuwa ni makruuh kukesha usiku mzima kila siku au aghlabu, kwani ni kinyume na mwenendo wake (صلى الله عليه وآله وسلم), na lau ingelikuwa kukesha usiku mzima ni bora, basi hilo lisingelimpita Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Na uongofu bora kabisa ni uongofu wa Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم). Na wala usidanganyike na yaliyosimuliwa kuhusu Abu Haniyfah kwamba yeye alikuwa akiswali Swalah ya al-Fajr kwa wudhuu wa 'Ishaa kwa miaka arubaini!! [Maelezo ya Mfasiri: Taz. Tabliygh An-Nisaab: Fadhila za Swalah kilichoandikwa na Maulana Zakariyyah Kandhalvi kwa mifano ya dai kama hili]. Kwani usimulizi huu kutoka kwake, hauna msingi wo wote ule, bali 'Allaamah Al-Fayruuz

"Usiku wa leo umeswali Swalah sikuwahi kukuona kuswali mfano wake".

Akasema (صلى الله عليه وآله وسلم): ((Ndio, ilikuwa Swalah ya shauku na khofu, (na mimi kwa hakika) nilimuomba Mola Wangu عزوجل mambo matatu, Amenipa mawili, na Amenikatalia moja. Nilimuomba Mola wangu Asituangamize kwa kile Alichowaangamizia Ummah za kabla yetu [na katika riwaaya nyingine]: ((Asituangamize Ummah wangu kwa njaa) Akanipa hilo, Nikamuomba Mola wangu عزوجل Asitusalitisha na adui asiye kuwa miongoni mwetu, Akanipa hilo, na nilimuomba Mola wangu Asituvuruge vuruge mpaka tukawa

---

Na usiku mmoja alisimama (صلى الله عليه وآله وسلم) (katika Swalah) akawa akikariri Aayah moja hadi alfajiri. Aayah yenyewe ni:

﴿ إِن تَعَدَّيْتُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ وَإِن تَغْفِرَ لَهُمْ فإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴾

*In Tu'adh-dhibhum fainnahum 'ibaaduk wa-in Taghfir-lahum fainnaka Antal-'Aziyzul Hakiym*

**((Ukiwaadhibu, basi hao ni waja Wako. Na Ukiwasamehe, basi Wewe Ndiye Mwenye nguvu na Mwenye Hkima)). [Al-Maaidah 5: 118]**

[kwayo karukuu, na kwayo kasujudia na kwayo kaomba], [Kulipopambazuka, Abu Dharr (رضي الله عنه) alimwambia: "Ee Mjume wa Allaah! Hukusita kuisoma Aayah hii hadi kumepambazuka, umerukuu nayo, umeSujuud nayo] [na umeomba nayo] [hali ya kuwa Allaah Amekufundisha Qur-aan nzima], [lau (ingelikuwa) mmoja wetu amefanya hivi, tungelimkemea]. [Akasema: **((Hakika nimemuomba Mola wangu عزوجل kuwashufaia Ummah wangu, Akanipa hilo, na Uombezi huo utapatikana Allaah Akipenda kwa yeyote asiyemshirikisha Allaah na kitu cho chote kile))**].<sup>(353)</sup>

Mtu alimwambia: "Ee Mjumbe wa Allaah! Mimi ninaye jirani anayesimama kuswali usiku na hasomi isipokuwa:

﴿ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴾

---

<sup>352</sup> An-Nasaaiy, Ahmad na Atw-Twabaraaniy (1/187/2). At-Tirmidhiy amesema ni Swahiyh.

<sup>353</sup> An-Nasaaiy, Ibn Khuzaymah (1/70/1), Ahmad, Ibn Naswr na Al-Haakim ambaye amesema ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

### *Qul Hurwa Allaahu Ahad*

**((Sema: Yeye Allaah ni wa Pekee))** [Al-Ikhlaasw 112: 4],

(anaikariri) [haongezei nyingine] kama kwamba anaiona kuwa hadhi yake ni ndogo". Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema:

**((Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake, hakika hiyo ni sawa na thuluthi ya Qur-aan)).<sup>(354)</sup>**

### 7- Swalah Ya Witr

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma katika Rak'ah ya mwanzo:

﴿ سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴾

### *Sabbihi-sma Rabbikal-A'laa*

**((Litakase Jina la Mola wako Aliye juu kabisa))** [Al-A'laa 87: 19],

na katika Rak'ah ya pili:

﴿ قُلْ يَتَأْتِيهَا الْكُفْرُونَ ﴾

### *Qul yaa ayyuhal-kaafiyrun*

**((Sema: Enyi makafiri))** [Al-Kaafiruun 109: 6],

na katika Rak'ah ya tatu.<sup>(355)</sup>

﴿ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ﴾

### *Qul Hurwa Allaahu Ahad*

---

<sup>354</sup> Ahmad na Al-Bukhaariy.

<sup>355</sup> An-Nasaaiy na Al-Haakim ambaye amesema ni Swahiyh.

**((Sema: Yeye Allaah ni wa Pekee)) [Al-Ikhlaasw 112: 4].**

Mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiongeza katika Rak'ah ya mwisho kwa kusoma:

﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ﴾

*Qul 'auudhu bi Rabbil falaq*

**((Sema: Najikinga kwa Mola wa mapambazuko)) [Al-Falaq 113: 5],**

na

﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴾

*Qul 'auudhu bi Rabbin naas*

**((Sema: Ninajikinga kwa Mola wa wanaadamu)) [An-Naas 114: 6] <sup>(356)</sup>.**

Na mara nyingine alisoma katika Rak'ah ya tatu Aayah mia kutoka katika Surat An-Nisaa [4: 176] <sup>(357)</sup>.

Ama zile Rak'ah mbili baada ya Witr<sup>(358)</sup>, alikuwa kaisoma ndani yake:

---

<sup>356</sup> At-Tirmidhiy, Abul-'Abbaas Al-Aswam katika Hadiyih yake (Mjalada 2 Namba 117) na Al-Haakim ambaye amesema ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>357</sup> An-Nasaaiy na Ahmad kwa isnaad Swahiyh.

<sup>358</sup> Zimethibiti Rakaa mbili hizi katika Swahiyh Muslim na wengineo kama ni desturi ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Na kuthibiti kwa Rakaa mbili hizi, kunapingana na kauli yake (صلى الله عليه وآله وسلم): **((Ifanyeni Swalah yenu ya mwisho usiku kuwa ni Witr))**. Imepokelewa na Al-Bukhaariy na Muslim. Maulamaa wamekhitilafiana katika kuoanisha baina ya Hadiyithi hizi mbili, kwa maono, fikra na mitazamo tofauti. Na hakuna hata mtazamo mmoja katika mitazamo yote hiyo ulionikinaisha. Na ni busara

﴿ إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ﴾

*Idhaa zulzilatil zrdhu zil-zaalaha*

((Itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wake)) [Az-Zilzalah 99: 8], na

﴿ قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴾

*Qul yaa ayyuhal-kaafiruun*

((Sema: Enyi makafiri)) [Al-Kaafiruun 109: 6]<sup>(359)</sup>

## 8 - Swalah Ya Ijumaa

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma mara nyingine katika Rak'ah ya mwanzo Suratul-Jumu'ah [62: 11]:

---

Kisha nikakutana na Hadiyith Swahiyh ambayo ndani yake iko amri ya kuswali Rakaa mbili baada ya Witr. Kwa hiyo amri ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) imewafikiana na kitendo chake, na ikathibiti amri ya kuswali Rakaa mbili kwa watu wote. Na amri ya kwanza inaweza kuwa ni mapendekezo, hivyo basi hakuna kinachozikanusha Rakaa mbili. Hadiyith hiyo nimeiweka katika *Silsilat al-Ahaadiyith asw-Swahiyhah* (1193). Taz. Kiambatisho 7.

<sup>359</sup> Ahmad, Ibn Naswr na Atw-Twahaawiy (1/202), na Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan ikiwa na isnaad Hasan Swahiyh.

﴿ يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ الْعَزِيزِ ﴾

﴿ الْحَكِيمِ ﴾

*Yusabbihu Lillaahi maa fis samaawaati wamaa fil ardhwil-Malikal Qudduusil-Aziyzi-Hakiym...*

((Vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi vinamtukuza Allaah, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye nguvu, Mwenye Hikima.)),

na katika Rak'ah ya pili:

﴿ إِذَا جَاءَكَ الْمُتَنَفِقُونَ... ﴾

*Idhaa jaa-akal-munaafiquuna*

((Wanapokujia wanaafiki)) [63: 11]<sup>(360)</sup>,

na mara nyingine - badala yake<sup>(361)</sup>- alikuwa akisoma:

﴿ هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْعَشِيَّةِ ﴾

*Hal-ataaka hadiythul ghaashiyah*

"Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?" [88: 26],

na mara nyingine akisoma:

﴿ سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴾

*Sabbihis-sma Rabbikal-A'laa*

((Litakase Jina la Mola wako Aliye juu kabisa)) [Al-A'laa 87: 19],

---

<sup>360</sup> Muslim na Abu Daawuud. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (345).

<sup>361</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

Katika Rak'ah ya mwanzo na:

﴿ هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ ﴾

*Hal-ataaka hadiythul ghaashiyah*

**((Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?))** [88: 26],  
katika Rak'ah ya pili<sup>(362)</sup>.

### 9 - Swalah Za 'Iyd Mbili

"Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma (mara nyingine) katika Rak'ah ya kwanza

﴿ سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى ﴾

*Sabbihisma Rabbikal-A'laa*

**((Litakase jina la Mola wako Aliye juu kabisa))** [Al-A'laa 87: 19],

na katika Rak'ah ya pili:

﴿ هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْغَاشِيَةِ ﴾

*Hal-ataaka hadiythul ghaashiyah*

**((Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza?))** [88: 26]  
<sup>(363)</sup>.

Na mara nyingine "alikuwa akisoma katika hizo Rak'ah mbili:

﴿ ق وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ ﴾

*Qaaf Wal-Qur-aanil Majiyyd*

---

<sup>362</sup> Muslim na Abu Daawuud.

<sup>363</sup> Muslim na Abu Daawuud.



**((Qaaf, Naapa kwa Qur-aan Tukufu))** [Qaaf 50: 45],  
na

﴿ أَقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَنْشَقَّ الْقَمَرُ ﴾

*Iqtarabatis Saa'atu wan-shaqqal-qamar*

**((Saa imekaribia na mwezi umepasuka))** [Al-Qamar 54: 55]<sup>(364)</sup>.

## 10 -Swalah Ya Janaazah

"Sunnah ni kusoma Surat Al-Faatihah<sup>(365)</sup> [na sura nyingineyo]<sup>(366)</sup>. Pia "Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akikaa kimya kwa muda baada ya *Takbiyr* ya kwanza"<sup>(367)</sup>

## Kusoma Kisomo Vilivyo Na Kuitengeneza Sauti Unaposoma

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma - kama Alivyoamrishwa na Allaah - Qur-aan vilivyo - kama inavyotakiwa kusomwa, mtu anatakiwa achunge hukumu za kuisoma-, bila ya kwenda mbio wala kuharakiza, bali kisomo cha "Uchambuzi/ufafanuzi chenye kupelekea kubaini herufi baada ya herufi"<sup>(368)</sup> (sana)

---

<sup>364</sup> Muslim na Abu Daawuud.

<sup>365</sup> Hii ni kauli ya Imaam Ash-Shaafi'y, Ahmad na Is-haaq, na pia ni rai ya baadhi ya watafiti wa Mahanafi waliokuja baadaye. Ama kuhusu kusoma Surah baada yake, huu ni mtazamo wa baadhi ya Ma-Shaafi'y na ni mtazamo Swahiyh.

<sup>366</sup> Al-Bukhaariy, Abu Daawuud, An-Nassaiy na Ibn Al-Jaaruud. Na wala hii ziada sio ya pekee (haina mwenzake) (kitu kimoja hakina mwenzake hapa sio ajabu) kama At-Tuwayjiriy anavyodai.

<sup>367</sup> An-Nasaaiy na At-Twahaawiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>368</sup> Ibn Al-Mubaarak katika Az-Zuhd (1/1 kutoka Al-Kawaakib 575), Abu Daawuud na Ahmad kwa isnaad Swahiyh.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Itasemwa kwa mwenye kusoma Qur-aan (siku ya Qiyaamah): Soma na upande; soma (pole pole kwa mahadhi) kama ulivyokuwa ukisoma duniani; makaazi yako kwenye Aayah ya mwisho usomayo))**<sup>(370)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) "akirefusha kisomo chake (kwenye herufi za kurefushwa), alikuwa akirefusha Bismi Llaahi, na akirefusha Ar-Rahmaan na akirefusha Ar-Rahim"<sup>(371)</sup> na katika "nadhiyd" [Qaaf 50: 10]<sup>(372)</sup> na mfano wa (kama) hizo.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisimama mwisho wa kila Aayah kama ilivyoelezwa kabla.

Mara nyingine "alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma kwa sauti ya kuvutia ya kutetema<sup>(373)</sup> kama alviyofanya siku ya kufunguliwa kwa Makkah hali ya kuwa yuko juu ya ngamia wake, anasoma Surat Al-Fat-h [48: 29] [kwa sauti nyororo]<sup>(374)</sup> na 'Abdullaah bin Mughaffal amesimulia hii sauti ya kuvutia : aaa"<sup>(375)</sup>

---

<sup>369</sup> Muslim na Maalik.

<sup>370</sup> Abu Daawuud na At-Tirmidhiy ambaye amesema Swahiyh.

<sup>371</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>372</sup> Al-Bukhaariy katika *Afaal al 'Ibaad* kwa isnaad Swahiyh.

<sup>373</sup> Inatokana na neno Tarjiy', Ibn Hajr ameeleza: kuwa ni sauti ya kutetema na asli yake ni at tardiyd, watarjiy' sauti: ni kuikariri kutoka kwenye halq. Al-Manaawiy kasema, "Inakuja aghlabu kwa kuwa na hisia ya shangwe na furaha ambayo alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) siku ya Ushindi wa Makkah".

<sup>374</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>375</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Ibn Hajr amesema katika maelezo kuhusu "aaa (آء)" hii ni hamzah ikiwa na fat-haa, ikifuatia na alif ya kimya,

Alikuwa akiamrisha kuipamba sauti katika kusoma Qur-aan, alikuwa akisema: **((Ipambeni Qur-aan kwa sauti zenu (kwani sauti nzuri huzidisha kuipamba Qur-aan))**<sup>(376)</sup>

Na alikuwa akisema: **((Hakika mwenye sauti bora miongoni mwa watu katika kusoma Qur-aan ni yule ambaye mnapomsikia akiisoma, mtamdhanian ni mwenye kumkhofu Allaah))**<sup>(377)</sup>

Alikuwa pia akiamrisha kusoma Qur-aan kwa sauti ya kupendeza, alikuwa akisema: **((Jifunzeni kitabu cha Allaah, dumisheni kuisoma, ithibitisheni (kuhifadhi), na isomeni kwa (sauti ya) kughani, kwani Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, inakimbia haraka kuliko ngamia anavyochopoka katika kamba))**<sup>(378)</sup>

---

<sup>376</sup> Al-Bukhaariy ta'aliyq (kiambatisho), Abu Daawauud, Ad-Daarimiy, Al-Haakim na Tamaam Ar-Raaziy kwa isnaad mbili Swahiyh.

<sup>377</sup> Hadiyih ni Swahiyh, imesimuliwa na Ibn Al-Mubaarak katika *Az-Zuhd* (1/1 kutoka Al-Kawaakib 575), Ad-Daarimiy, Ibn Naswr, At-Twabaraaniy, Abu Nu'aym katika *Akhbaar Iswabahaan* na Adh-Dwhiyaa katika *Al-Mukhtarah*.

<sup>378</sup> Ad-Daarimiy na Ahmad kwa isnaad Swahiyh.

#### **Tanbihi:**

Hadiyih ya kwanza imegeuzwa na msimulizi mmoja, hivyo ameisimulia: **((Pambeni sauti zenu kwa (kwenye) Qur-aan))**. Haya ni makosa katika usimulizi na ufahamu, na yeyote mwenye kusema ni Swahiyh basi huyo amezama zaidi katika makosa, kwani inapingana na Simulizi Swahiyh zilizofafanuliwa katika mlango huu. Bali ni mfano bora katika Hadiyih Maqluub (iliyogeuzwa) na maelezo zaidi ya hii (tanbihi) yamo katika *Silsilatul-Ahaadiyih Adhw-Dhwa'iyfah* (Namba 5328).

Alikuwa pia akisema: ((Sio miongoni mwetu mwenye kuisoma Qur-aan bila ya kughani [kupendezesha sauti]))<sup>(379)</sup>

Na akisema:

((Allaah Hakuwahi kusikiliza kitu chochote zaidi ya jinsi ya kusikiliza [katika riwaaya nyingine: ((Kama Anavyomsikiliza))] Mtume (kwa shauku) ((kwa sauti ya kupendeza))), na [katika riwaaya nyingine: anavyosoma Qur-aan kwa sauti nzuri<sup>(380)</sup> ((ananyanyua sauti kwako))<sup>(381)</sup>

Alimuambia Abu Muusa Al-Ash'ariyy (رضي الله عنه) ((Lau ungeliniona nilipokuwa nasikiliza kisomo chako usiku wa jana, kwa Hakika umepewa zumari<sup>(382)</sup> katika mizumari ya aila ya Daawuud!)) Hivyo Abu Muusa akasema: "Lau ningelijua kuwa uko, ningelizidi kuitengeneza na kuipendesha sauti yangu kwa ajili yako"<sup>(383)</sup>

---

<sup>379</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amesema ni Swahiyh na Adh-Dhahaabiy amekubaliana naye.

<sup>380</sup> Amesema Al-Mundhiriy 'taghannaa' inamaanisha kuisoma kwa sauti ya kupendeza; Sufyaan bin 'Uyaynah na wengineo wamechukua rai kwamba ni kufanya istighnaa (yaani Qur-aan kumfanya mtu ajitenge na mapambo ya dunia) lakini hii imekanushwa.

<sup>381</sup> Al-Bukhaariy, Muslim, At-Twahaawiy na Ibn Mandah katika Tawhiyd (81/1)

<sup>382</sup> Maulamaa wamesema kuwa mizumari hapa inamaansiha: sauti nzuri, na asili ya az-zumar ni al-ghinaa: kuimba, na kwamba aila ya Daawuud inakusudiwa Daawuud mwenyewe, na aila fulani hutumika na humaanisha khaswa ya mtu mwenyewe. Daawuud (عليه السلام) alikuwa na sauti nzuri mno. Hii ameitaja An-Nawaawiy katika maelezo yake ya Swahiyh Muslim.

<sup>383</sup> Abdur-Razzaaq katika Al-Amaaliy (2/44/1), Al-Bukhaariy, Muslim, Ibn Naswr na Haakim.

## Kumsahihisha Imaam

Ametoa (صلى الله عليه وآله وسلم) mfano katika kumsahihisha Imaam anapobabaika au anapochanganyikiwa na kisomo chake. Mara moja aliswali, akasoma ndani yake kisomo, akasahau. Alipomaliza alimwambia Ubayy: **((Uliswali na sisi?))**. Alijibu: "Ndio". Akasema: **((Hivyo nini kilichokuzuia [kunisahihisha]?))**<sup>(384)</sup>.

## Kujikinga Na Shaytwaan Kwa Kutema Mate Kidogo Wakati Wa Swalah Ili Kuondosha Wasiwasi

'Uthmaan bin Abil-Aasw (رضي الله عنه) alimwambia: "Ee Mjumbe wa Allaah! Shaytwaan ameingia baina yangu na baina ya Swalah yangu na kisomo changu, ananibabaisha katika kisomo changu!" Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: **((Huyo ni Shaytwaan anayeitwa Khinzab, hivyo utakapomuhisi jikinge kwa Allaah naye, na tema mate kidogo<sup>(385)</sup> upande wa kushoto kwako mara tatu))**. Akasema: "Nikafanya hivyo, na Allaah Akamuondoshelea mbali nami".<sup>(386)</sup>

---

<sup>384</sup> Abu Daawuud, Ibn Hibbaan, Atw-Twabaraaniy, Ibn 'Asaakir (2/296/2) na Adhw-Dhwiya katika Al-Mukhtaarah kwa isnaad Swahiyh.

<sup>385</sup> "At-Tafl" ni mpulizo ikiwa na mate kidogo, hivyo ni zaidi ya kupuliza. (An-Nihaayah).

<sup>386</sup> Muslim na Ahmad. An-Nawawiy (رحمه الله) amesema: "Hadiyth hii ina mapendekezo ya kujikinga na Shaytwaan anaposhawishi, pamoja na kutema mate upande wa kushoto mara tatu".

## Kurukuu

Baada ya kumaliza kisomo chake (صلى الله عليه وآله وسلم), alikuwa akinyamaza kinyamazo kidogo<sup>(387)</sup>, kisha huinua mikono yake<sup>(388)</sup> kwa namna zilizotangulia kueleza katika 'Takbiyr Ya Kufungulia, akaleta *Takbiyr*<sup>(389)</sup> na akarukuu.<sup>(390)</sup>

Na pia alimuamrisha mambo mawili hayo aliyeswali vibaya kwa kumwambia: **((Hakika Swalah ya mmoja wenu haitotimia mpaka akamilishe wudhuu vizuri kama Allaah Alivyoamrisha... kisha alete *Takbiyr*, amsifu na kumtukuza Yeye, na asome kiasi kinachosahilika tu kwake katika Qur-**

---

<sup>387</sup>Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amesema kuwa ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>388</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Huku kuinua mikono ni jambo lililothibiti kutoka kwake (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa njia ya mutawaatir (Iliyopokelewa na idadi kubwa -ya watu- yenye kuwa muhali katika kawaida kukubaliana kusema uongo) kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Na vile vile imethibiti kutoka kwake (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa njia hiyo hiyo ya mutawaatir, kuinua mikono wakati wa kunyanyuka -wakati wa kuitadili - kutoka kwenye ruku mpaka alingane sawa hali ya kusimama. Na hivi ndivyo walivyokwenda Maimaamu watatu; Maalik, Ash-Shaafi'iy na Ahmad, na wengineo katika kundi kubwa la Maulamaa wa Hadiyith na Maulamaa wa Fiqh. Na ndio mwenendo alioshikamana nao Imaam Maalik (رحمه الله) hadi kufa kwake kama ilivyoripotiwa na Ibn 'Asaakir (15/78/2). Baadhi ya Mahanafi wamechagua kufanya hivyo. Miongoni mwao ni 'Iyswaam bin Yuusuf Abu 'Aswamah Al-Balkhiy (aliyefariki 210) ambaye ni mwanafunzi wa Imaam Abu Yuusuf (رحمه الله), kama ilivyoelezewa katika utangulizi. 'Abdullaah bin Ahmad ameripoti kutoka kwa baba yake katika Masaail yake (Uk. 60). "Imesimuliwa kutoka kwa 'Uqbah bin 'Aamir kwamba amesema kuhusiana na kunyanyua mikono miwili katika Swalah: "Anapata mema kumi kwa kila anapoinyanyua". Nikasema: Yana ushahidi - maneno ya 'Uqbah - wenye nguvu kutokana na Hadiyithul-Qudisy isemayo: ((...mwenye kutia nia ya kitendo chema na akakitekeleza, Allaah Atamuandikia mema kumi hadi mia saba)). Imesimuliwa na Ash-Shaykhaayn. Taz. *Swahiyh at-Targhiyb* Namba 16.

<sup>389</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>390</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

aan miongoni mwa Aliyofunzwa na Allaah (kwa kiasi cha wepesi) na uwezo wake, kisha alete *Takbiyr* na arukuu [na aweke mikono yake miwili juu ya magoti yake mawili] mpaka viungo vyake vitulie na vipumzike...))<sup>(391)</sup>.

## Sifa Ya Rukuu

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiweka viganja vyake juu ya magoti yake<sup>(392)</sup> na alikuwa akiwaamrisha kufanya hivyo<sup>(393)</sup> kama alivyomuamrisha mtu aliyeswali vibaya, kama ilivyoelezwa nyuma.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiimakinisha mikono yake barabara na magoti yake (kama kwamba akiyashikilia)<sup>(394)</sup>, na alikuwa akivichanua vidole vyake<sup>(395)</sup>, na alimuamrisha aliyeswali vibaya kama hivyo, kwa kumwambia: **((Utakaporukuu, weka viganja vya mikono yako juu ya magoti yako, na kisha vichanue vidole vyako, kisha bakia (hivyo) hadi kila kiungo kitue mahali pake))<sup>(396)</sup>.**

Alikuwa akijitawanya (sio kujigandamiza mkao mmoja) na akitenganisha viwiko vya mikono na ubavu wake.<sup>(397)</sup>

---

<sup>391</sup> Abu Daawuud na An-Nasaaiy. Al-Haakim amesema ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>392</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>393</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>394</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>395</sup> Al-Haakim ambaye amesema ni Swahiyh. Adh-Dhahabiy na Atw-Twayaalisy wamekubaliana naye. Imetolewa katika *Swahiyh Abi Daawuud* (809).

<sup>396</sup> Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan katika Swahiyh zao.

<sup>397</sup> At-Tirmidhiy ambaye amesema ni Swahiyh, na Ibn Khuzaymah.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anaporukuu, hutandaza mgongo wake na kuusawazisha<sup>(398)</sup> kiasi kwamba kama ungelimwagiwa maji, basi yangelitua<sup>(399)</sup>. Na pia alimwambia aliyeswali vibaya: **((Utakaporukuu, weka viwiko vyako juu ya magoti yako, na tawanya mgongo wako na makinisha madhubuti rukuu yako)).**<sup>(400)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) hainamishi kichwa chake wala hakinyanyui (zaidi ya mgongo wake),<sup>(401)</sup> bali kilikuwa baina yake.<sup>(402)</sup>

## Ulazima Wa Kutulia Katika Rukuu

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akitulia kwenye rukuu yake, na alimuamrisha awe hivyo aliyeswali vibaya, kama ilivyotajwa katika mlango wa rukuu.

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Kamilisheni rukuu na Sujuud, kwani naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu imo Mikononi Mwake, hakika mimi nakuoneni nyuma yangu<sup>(403)</sup> mnaporukuu na mnapoSujuud)).**<sup>(404)</sup>

---

<sup>398</sup>Al-Bukhaariy na Al-Bayhaqiy kwa isnaad Swahiyh.

<sup>399</sup>Atw-Twabaraaniy katika Mu'jam Al-Kabiyr na Mu'jam As-Swaghiyr, 'Abdullaah bin Ahmad katika Zawaa'id Al-Musnad na Ibn Maajah.

<sup>400</sup> Ahmad na Abu Daawuud kwa isnaad Swahiyh.

<sup>401</sup> Abu Daawuud na Al-Bukhaariy katika Juzuu Al-Qaari'ah kwa isnaad Swahiyh. Na maana ya hakinyanyui, ni kuwa hakinyanyui kichwa chake mpaka kikawa juu zaidi ya mgongo wake, bali kinakuwa usawa wa mgongo.

<sup>402</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>403</sup>Nasema na kuona huku ni kuona kwa uhakika wake kimaumbile, na ni miongoni mwa miujiza yake (صلى الله عليه وآله وسلم), nako ni katika Swalah basi. Na hakuna dalili ya kuona kwa ujumla.

<sup>404</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.



Alimuona mtu anaswali bila ya kukamilisha rukuu yake sawa sawa, akidonoa katika *Sujuud* yake, akasema (صلى الله عليه وآله وسلم): ((Lau atakufa mtu huyu katika hali yake hii, basi atakuwa amekufa katika Mila isiyokuwa ya Muhammad, [anadonoa katika Swalah yake kama adonoavyo kunguru damu]. Mfano wa yule asiyekamilisha rukuu yake na akadonoa katika *Sujuud* yake, ni kama mfano wa mwenye njaa anayekula tende moja au tende mbili, ambazo hazitomfaidisha kitu chochote))<sup>(405)</sup>

Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alisema: "Rafiki yangu mpenzi (صلى الله عليه وآله وسلم) amenikataza kudonoa katika Swalah yangu mdonowo wa jogoo na kugeuka geuka kama ageukavyo mbweha/bweha, na kuchuchumaa kama achuchumaavyo tumbili"<sup>(406)</sup>.

Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akisema: ((Mwizi muovu kabisa miongoni mwa wevi ni yule anayeiba katika Swalah yake)). Wakasema: "Ee Mjumbe wa Allaah! Vipi anaiba katika Swalah yake"? Akasema: ((Hatimizi rukuu yake na *Sujuud* yake))<sup>(407)</sup>

---

<sup>405</sup> Abu Ya'alaah katika Musnad yake (340/3491/1), Al-Aajuriy katika Al-Arba'iyn, Al-Bayhaqiyy, Atw-Twabaraaniy (1/192/1), Adhw-Dhwiyya katika Al-Muntaqaa (276/1), Ibn 'Asaakir (2/226/2, 414/1, 8/14/1, 76/2) kwa isnaad nzuri. Na Ibn Khuzaymah amesema ni Swahiyh (1/82/1). Ibn Batwtwah katika *Al-Ibaanah* (5/43/1) anao usimulizi Mursal -Hadiyth mwisho wa isnaad yake ameangushwa Swahaba- unaounga mkono sehemu ya mwanzo ya Hadiyth ukitoa ziada katika *Al-Ibaanah* (5/43/1).

<sup>406</sup> Atw-Twayaalisy, Ahmad na Ibn Abi Shaybah. Ni Hadiyth Hasan, kama nilivyoielezea katika tanbihi zangu kwenye *Al-Ahkaam* (1348) ya 'Abdul-Haqq Ishbiyliyy (1348).

<sup>407</sup> Ibn Abi Shaybah (1/89/2), Atw-Twabaraaniy na Al-Haakim ambaye amesema ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

Mara moja, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiswali, na alitupa jicho kwa mtu ambaye hokusawazisha uti wa mgongo wake katika rukuu na *Sujuud*. Alipomaliza alisema:

**((Enyi Waislamu! Hakika hakuna Swalah kwa yule asiyesawazisha uti wake wa mgongo katika rukuu na *Sujuud*)).<sup>(408)</sup>**

Akasema katika Hadiyth nyingine: **((Swalah ya mtu haihesabiwi hadi asawazishe mgongo wake katika rukuu na *Sujuud*)).<sup>(409)</sup>**

## Adhkaar Za Rukuu

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) katika nguzo hii akisoma namna mbali mbali za adhkaar na du'aa. Alikuwa akibadilisha katika kusoma kwake; mara nyingine husema hii na mara nyingine husema hii miongoni mwa zifuatazo:

1.

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ

*Sub-haana Rabbiyal-'Adhwiym*

**“Ametakasika Mola wangu Aliye Mtukufu”**

mara tatu<sup>(410)</sup>. Na mara nyingine alikuwa akiikariri zaidi ya hivyo.<sup>(411)</sup>

---

<sup>408</sup> Ibn Abi Shaybah (1/89/1), Ibn Maajah na Ahmad kwa isnaad Swahiyh.

<sup>409</sup> Abu 'Awaanah, Abu Daawuud na As-Sahmiy (61). Ad-Daaraqutwniy amesema ni Swahiyh.

<sup>410</sup> Ahmad, Abu Daawuud, Ibn Maajah, Ad-Daaraqutwniy, Atw-Twahaawiy, Al-Bazaar na Atw-Twabaraany katika Mu'jam Al-Kabiy, kutokana na Maswaha saba. Ndani yake kuna jibu kwa wale waliokataa ujio wa kutozidi mara tatu katika kuleta Tasbiyyhaat, kama Ibn Al-Qayyim na wengineo.

Mara moja, katika Swalah ya usiku, aliikariri sana hadi rukuu yake ikawa inakaribiana na kisimamo chake, alichokuwa amesoma ndani yake Surah tatu katika Surah ndefu; Al-Baqarah, An-Nisaa na Al-Imraan. Ndani yake (Swalah hii) kulijaa du'aa na kuomba Maghfirah, kama ilivyotajwa katika '(Kisomo Katika) Swalah Ya Usiku (Tahajjud).

2.

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ وَبِحَمْدِهِ

*Sub-haana Rabbiyal-'Adhwiym wabihamdihi*

“Ametakasika Mola wangu Aliye Mtukufu Na Sifa Njema Zote Ni Zake” mara tatu”.<sup>(412)</sup>

3.

سُبُّوحٌ قُدُّوسٌ، رَبُّ الْمَلَائِكَةِ وَالرُّوحِ

*Subuuhum Qudduusun Rabbul Malaikati war Ruuhi*

“Mwingi wa kutakaswa Mtakatifu<sup>(413)</sup>, Mola wa Malaika na Jibriyl”.<sup>(414)</sup>

4.

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ ، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي

*Sub-haanaka Allaahumma wa Biham-dika Allaahumma ghfir-liy*

---

<sup>411</sup> Inapatikana hii kutokana na Ahaadith zilizoweka wazi kwamba Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akifanya kisimamo chake, na rukuu yake na Sujuud zake sawa sawa kwa urefu, kama itakavyotajwa katika mlango ufuatao.

<sup>412</sup>Hadiyith Swahiyh. Imesimuliwa na Abu Daawud, Ad-Daaraqutwniy, Ahmad, Atw-Twabaraaniy na Al-Bayhaqiy.

<sup>413</sup> Abu Is-haaq amesema: "Subuuh" ina maana ya Aliyetakasika na makosa yoyote, na "Qudduus" ina maana ya Mwenye Baraka au Aliyetwahaarika". Ibn Saydah: "Subbuuh Qudduus" ni sifa za Allaah عزوجل kwa sababu Anatukuzwa na Kutakaswa". (Lisaanul-'Arab).

<sup>414</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

“Kutakasika ni Kwako, Ee Mola wangu, na sifa njema zote ni Zako, Ee Mola Nisamehe”.

Alikuwa akiileta kwa wingi hii katika rukuu yake na *Sujuud* zake, alikuwa akitekeleza amri ya Qur-aan.”<sup>(415)</sup>

5.

اللَّهُمَّ لَكَ رَكَعْتُ وَبِكَ آمَنْتُ، وَلَكَ أَسَلْتُ، (أَنْتَ رَبِّي) خَشَعْتُ لَكَ سَمْعِي، وَبَصَرِي،  
وَمُخِّي، وَعَظْمِي، (وَ فِي رِوَايَةٍ وَعِظَامِي) وَعَصَبِي، (وَمَا اسْتَقَلَّتْ بِهِ قَدَمِي لِلَّهِ رَبِّ  
الْعَالَمِينَ)

*Allaahumma laka Raka'tu, wabika Aamantu, walaka Aslamtu, [Anta Rabbii] Khasha'a laka sam'iy, wabaswariy, wamukh-khiy, wa'adhwmiy, [wa 'idhwaamiy] wa'aswabiyy, [wamas-taqallat bihii Qadamiy Lillaahi Rabbil 'Alamiyy]*

“Ee Allaah! Kwako Wewe nimerukuu, na Wewe nimekuamini, na Kwako Wewe nimejisalimisha, (Wewe Mola wangu) umenyenyekea Kwako usikizi wangu, na uoni wangu, na ubongo wangu, na mfupa wangu, (katika riwaaya mifupa yangu) na hisia zangu, (na ambacho kimesimama juu ya miguu yangu)<sup>(416)</sup> kwa ajili ya Mola Wa viumbe vyote.”<sup>(417)</sup>

<sup>415</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Na maana ya “yata-awwalul Qur-aan” ni kuwa anatekeleza yale aliyoamrisha ndani yake katika maneno Yake Allaah:

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا

((Zitakase sifa za Mola wako na umwombe msamaha, hakika Yeye Ndiye Anayepokea toba)) [An-Naswr 110: 3]

<sup>416</sup> Ina maana niliyoyabeba, kutokana na neno "*al-istiqlaal*" lenye maana "*al-irtifaa*". Ni ujumla (*ta'miyim*) baada ya ukhusuusi (*takh-swiys*), kwa maana imekuja -niliyoyabeba- baada ya khusuus -kutaja kiungo kimoja kimoja- katika viungo vya mtu).

<sup>417</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Atw-Twahaawiy na Ad-Daaraqutwniy.

6.

اللَّهُمَّ لَكَ رَكَعْتُ وَبِكَ آمَنْتُ، وَلَكَ أَسَلْتُ، وَعَلَيْكَ تَوَكَّلْتُ، أَنْتَ رَبِّي، خَشَعْتُ لَكَ  
سَمْعِي، وَبَصَرِي، وَدَمِي، وَلَحْمِي، وَعَظْمِي، وَعَصَبِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

*Allaahumma Laka Raka'tu, wa Bika Aamantu, wa Laka Aslamtu, wa'Alayka tazwakkaltu, Anta Rabbiy, Khasha'a Laka sam'iy, wabaswariy, wadamiy, walahmiy, wa'adhwamiy, wa'aswabiyy, Lillahi Rabbil 'Alamiyy*

“Ee Allaah! Kwako nimerukuu, na Wewe nimekuamini, na Kwako nimejisalimisha, Kwako nimekutegemea, Wewe Mola wangu, umenyenyekea Kwako usikizi wangu, na uoni wangu, na damu yangu, na nyama yangu, na mfupa wangu, na ubongo wangu kwa ajili ya Mola Wa viumbe vyote”.<sup>(418)</sup>

7.

سُبْحَانَ ذِي الْجَبَرُوتِ، وَالْمَلَكُوتِ، وَالْكِبْرِيَاءِ، وَالْعِظَمَةِ

*Subhaana dhil Jabaruuti wal-Malakuuti wal-Kibriyaau wal-Adhwamah*

“Ametakasika Mwenye Utawala, na Ufalme, na Ukubwa, na Utukufu”,

Hii alikuwa akiisoma katika Swalah ya usiku.<sup>(419)</sup>

---

<sup>418</sup> An-Nasaaiy kwa isnaad Swahiyh.

<sup>419</sup> Abu Daawuud, An-Nasaaiy kwa isnaad Swahiyh.

**FAIDA:**

Je, inakubalika kuchanganya baina ya hizi adhkaar (mbili au zaidi) katika rukuu moja au haikubaliki? Maulamaa wametofautiana katika hili. Ibn al-Qayyim hakuwa na msimamo kuhusu hili katika *Zaad al-Ma'aad*, na An-Nawawiy amechagua uwezekano wa mwanzo katika Al-Adhkaar, akisema: "Na lililo bora ni kuchanganya baina ya hizi adhkaar zote ikiwezekana. Na hivi ndio inavyotakikana iwe katika adhkaar za milango yote. Abu Atw-Twayyib Swiddiyq Hasan Khan katika *Nuzuul Al-Abraar* (84) hakukubaliana naye kwa kusema: "Alete adhkaar hizi mara hii, na

## Kuirefusha Rukuu

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akifanya rukuu yake, kisimamo chake baada ya rukuu, na *Sujuud* yake na kikao baina sajda mbili, karibu sawa kwa urefu.<sup>(420)</sup>

## Kukatazwa Kusoma Qur-aan Katika Rukuu

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akikataza kusoma Qur-aan katika rukuu na *Sujuud*.<sup>(421)</sup>

Alikuwa akisema: **((Hakika mimi nimekatazwa kusoma Qur-aan hali ya kuwa nimerukuu au nimesujudu. Hivyo basi**

---

alete adhkaar nyingine mara nyingine, wala sioni dalili ya kuchanganya. Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) hakuwa akizichanganya kwa mpigo mmoja, lakini alikuwa mara akisema hii, na mara nyingine akisema nyingineyo. Na kufuata ni bora kuliko kuzusha". (Rai ya mwisho hii ni rai iliyo sahihi,) na hivi ndio haki Insha Allaah. Lakini imethibitika katika Sunnah kuirefusha nguzo hii na nyingine pia (kurukuu huku), kama itakavyokuja ufafanuzi wake, hadi iwe inakaribia urefu wa kisimamo. Hivyo, mwenye kuswali akipenda kumfuata Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Sunnah hii, basi hatoweza kufanya hivyo, isipokuwa kwa njia ya kuzichanganya tu (adhkaar) ambayo amekwenda/ameifuata An-Nawawiy, na Ibn Nasr ameipokea katika *Qiyaamul-Layl* (76) kutoka Ibn Jurayj kutokana na 'Atwaa, -haitowezekana- isipokuwa kwa njia ya kukariri iliyotaja katika baadhi ya hizi adhkaar. (moja ambayo inayo maandiko ya kukariri,) na hivi ndivyo karibu na Sunnah Na Allaah Anajua zaidi.

<sup>420</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Imetolewa katika *Irwaah Al-Ghaliyl* (331).

<sup>421</sup> Muslim na Abu 'Awaanah. Makatazo ni ya ujumla, hivyo inahusisha Swalah za Faradhi na Sunnah. Ziada ya Ibn 'Asaakir (17/299/1): "Ama Swalah za Sunnah, hakuna ubaya", ni (aidha) *shaadhah au munkar*. Ibn 'Asaakir ameashiria dosari humo, hivyo haijuzu kufanyiwa kazi.

katika rukuu mtukuzeni Mola (عزوجل), na (ama) katika *Sujuud*, jitahiDini kwa du'aa, kwani ni karibu kukubaliwa humo)).<sup>(422)</sup>

### Kusimama (Kuitadili) Kutoka Katika Rukuu Na Anachokisema Ndani Yake

Kisha, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiunyanyua mgongo wake kutoka rukuu huku akisema:

سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ

*Sami'a Allaahu liman Hamidah*

“Allaah Amemsikia mwenye kumsifu”<sup>(423)</sup>

Alimuamrisha pia aliyeswali vibaya kufanya hivyo alipomwambia: ((Swalah ya mtu haitimii hadi... amesema *Takbiyr* ... kisha akarukuu .... Kisha akasema 'Allaah Amemsikia mwenye kumsifu' hadi asimame kwa kunyooka sawa sawa))<sup>(424)</sup>.

Aliponyanyua kichwa chake, alikuwa akisimama wima na kunyooka sawa sawa hadi kila pingili ya uti imerudi sehemu yake<sup>(425)</sup>

Kisha alikuwa akisema huku akiwa amesimama wima:

رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ

*Rabbanaa Walakal-Hamdu*

---

<sup>422</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>423</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>424</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amesema ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubaliana naye.

<sup>425</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud. "*Al-Faqaar*" ni uti - "mifupa inayounda uti wa mgongo kutoka mwanzo wa shingo hadi kitokono" kama ilivyo katika Kamusi. Taz. pia *Fat-h Al-Baariy* (2/308).

“Ee Mola Wetu! Na Zako Sifa njema na shukrani za dhati”<sup>(426)</sup>

Aliwaamrisha wanaoswali wote sawasawa wakiweko nyuma ya Imaam au wasiweko nyuma ya Imaam kufanya hivyo, wanapoinuka kutoka rukuu kwa kusema: **((Swalini kama mlivyoniona nikiswali))**.<sup>(427)</sup>

Alikuwa akisema pia: **((Imaam amewekwa kwa ajili ya kufuatwa ..., anaposema 'Sami'a Allaahu liman Hamidah' (Allaah Amemsikia mwenye kumsifu), basi semeni: '[Allaahumma] Rabbanaa Walakal-Hamd'. Allaah Atakusikilizeni, kwani hakika Allaah (تبارك وتعالى) Amesema katika ulimi wa Mtume Wake, (صلى الله عليه وآله وسلم), Allaah Anamsikiliza mwenye kumsifu))**.<sup>(428)</sup>

Pia ametoa sababu ya kuamrisha hivi katika Hadiyith nyingine kwa kusema: **((... kwani mwenye kuwafikiana kauli yake na**

---

<sup>426</sup> Al-Bukhaariy na Ahmad.

<sup>427</sup> Kifungu kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>428</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Ahmad na Abu Daawuud.

#### TANBIHI:

Hadiyith hii haithibitishi kwamba Maamuma hawashirikiani na Imaam katika kusema: 'Sami'a Allaahu Liman Hamidah'. Pia haithibitishi kuwa Imaam hashirikiani na Maamuuma wanaosema: 'Rabbanaa Walakal-Hamd', yote kwa kuwa Hadiyith hii haikuja kubainisha yale khaswa ambayo Imaam na Maamuma wanapaswa kuyasema katika nguzo hii, bali imekuja kueleza kwamba *tahmiyd* (Rabbana Walakal-Hamd) ya Maamuma inatakiwa isemwe baada ya *tasmiy'* (Sami'a Allaahu Liman Hamidah) ya Imaam. Hii imetiliwa nguvu kutokana na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akisema *tahmiyd* hali ya kuwa yeye ni Imaam, na pia kwa ujumla wa kauli yake: **((Swalini kama mnavyoniona nnaswali))** ambayo inaonyesha kwamba Maamuuma waseme anayoyasema Imaam kama (Sami'a Allaahu Liman Hamidah) na mengineo. Wale ndugu waheshimiwa waliorejea kwetu kuhusu mas-ala haya watilie maanani haya, labda katika tuliyotaja kuna yenye kukinaisha. Na yeyote atakayetaka kujadii zaidi mas-ala haya arejee katika makala ya Al-Haafidh As-Suyuutwiyy katika mas-ala hii kwenye kitabu chake *Al-Haawy lil Fataawa* (1/529).



**kauli ya Malaika, ataghufuriwa madhambi yake yaliyotangulia).**<sup>(429)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiinua mikono yake katika huku kusimama<sup>(430)</sup> kwa namna zilizotangulia kuelezwa katika 'Takbiyra Ya Kufungulia', na husema hali ya kuwa amesimama - kama ilivyotajwa kabla:-

1.

رَبَّنَا وَكَ الْحَمْدُ

*Rabbanaa wa Lakal-Hamd'*

“Ee Mola Wetu! Ni Zako sifa njema na shukrani za dhati”<sup>(431)</sup>.

Na mara nyingine husema:

2.

رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ

*Rabbanaa Lakal-Hamd*

“Ee Mola Wetu! Ni Zako sifa njema na shukrani za dhati”<sup>(432)</sup>.

Na mara nyingine huongezea matamshi mawili haya tamshi:

اللَّهُمَّ

*Allaahumma*

“Ee Allaah”<sup>(433)</sup>

---

<sup>429</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. At-Tirmidhiy amesema ni Swahiyh.

<sup>430</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Huku kunyanyua mikono ni *mutawaatir* kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), na ni kauli ya Maulamaa wengi na baadhi ya Mahanafi. Taz. Tanbihi za nyuma katika (mlango wa) Rukuu.

<sup>431</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>432</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

3.

اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ

*Allaahumma Rabbanaa wa Lakal-Hamd'*

“Ee Allaah! Mola Wetu! Na Zako sifa njema na shukrani za dhati”

4.

اللَّهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ

*Allaahumma Rabbanaa Lakal-Hamd'*

“Ee Allaah! Mola Wetu! Ni Zako sifa njema na shukrani za dhatii”

Alikuwa akiamrisha (wengine) kufanya hivi kwa kusema: ((Imaam anaposema 'Sami'a Allaahu Liman Hamidah' semeni: 'Allaahumma, Rabbanaa Lakal-Hamd', kwani mwenye kuwafikiana kauli yake na ya Malaika ataghufuriwa madhambi yake yaliyopita)).<sup>(434)</sup>

Mara nyingine alikuwa akiongeza:

5.

مِلْءَ السَّمَوَاتِ وَمِلْءَ الْأَرْضِ، وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ

---

<sup>433</sup>Al-Bukhaariy na Ahmad. Na kwa hakika Ibnul-Qayyim (رحمه الله) alikosea (katika nukta hii,) pale alipokanusha katika *Zaad al-Ma'aad* usahihi wa riwaayah hii yenye kukusanya baina ya 'Allaahumma' na 'wa' pamoja na kuwepo kwake katika Swahiyh Al-Bukhaariy, Musnad Ahmad, An-Nasaaiy na Ahmad tena kupitia njia mbili (za usimulizi) kutoka kwa Abu Hurayrah, na katika Ad-Daaraimiy kutokana na Hadiyth ya Ibn 'Umar, na katika Al-Bayhaqiyy kutoka kwa Abu Sa'iyd Al-Khudhriyy, na katika An-Nasaaiy tena kutokana na Hadiyth ya Abu Muusa Al-Ash'ariyy.

<sup>434</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. At-Tirmidhiy amesema ni Swahiyh.

*Mil-as Samaawaati, wamil- Al-Ardhwi, wamil-a maa shi-ita min shay-in ba'du*

“Zimejaa mbingu, na zimejaa ardhi, na zimejaa (sifa Zako) kwa Ulichokitaka baada yake”.<sup>(435)</sup>

Au:

6.

مِلْءَ السَّمَوَاتِ (وَمِلْءَ) الْأَرْضِ، وَمَا بَيْنَهُمَا، وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدَ

*Mil-as Samaawaati, [wamil-a]l Ardhwi, wamaa baynahumaa, wamil-a maa shi-ita min shayin ba'du*

“Zimejaa mbingu na (zimejaa) ardhi na vilivyomo ndani yake sifa Zako, na zimejaa (sifa Zako) kwa Ulichokitaka baada yake”.<sup>(436)</sup>

Mara nyingine aliongeza zaidi:

7.

أَهْلَ الثَّنَاءِ وَالْمَجْدِ، لَا مَانِعَ لِمَا أُعْطِيتَ، وَلَا مُعْطِي لِمَا مَنَعْتَ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ

*Ahlath - thanaai wal-Majdi, laa maani'a limaa a'twayta, wala mu'twiya lima mana'ta, walaa yanfa'u dhal-jaddi minkal-jaddu*

“Wewe ni Mstahiki wa sifa na Utukufu, hapana anayeweza kukizuia Ulichokitoa, na wala kutoa Ulichokizuia, na wala

---

<sup>435</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>436</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

haumnufaishi mwenye utajiri, kwani kwao Wewe ndio utajiri".<sup>(437)</sup>

Au mara nyingine ziada ilikuwa:

8.

مِلْءَ السَّمَوَاتِ وَمِلْءَ الْأَرْضِ، وَمَا بَيْنَهُمَا، وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ. أَهْلَ  
التَّنَاءِ وَالْمَجْدِ، أَحَقُّ مَا قَالَ الْعَبْدُ، وَكُنَّا لَكَ عَبْدًا. (اللَّهُمَّ) لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ،  
(وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ)، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ

*Mil-as Samaawaati, wamil-al Ardhi, wamaa baynahumaa, wamil-a maa shi-ita min shayin ba'du, ahlath-thanaai wal-Majdi, ahaqqu maa qaalal-'abdu, wakullunaa laka 'abdun, [Allaahumma] laa maani'a lima a'twayta, [wala mu'twiya lima mana'ta], walaa yanfa'u dhal-jaddi minkal-jaddu*

"Zimejaa mbingu na zimejaa ardhi na vilivyomo ndani yake sifa Zako, na zimejaa (sifa Zako) kwa Ulichokitaka baada yake, Wewe ni Mstahiki wa Sifa na Utukufu, ni kweli aliyoyasema mja Wako, na sote ni waja Wako, (Ee Allaah) hapana anayeweza kukizuia Ulichokitoa, (na wala kutoa Ulichokizuia), na wala haumnufaishi mwenye utajiri, kwani Kwako Wewe ndio utajiri"<sup>(438)</sup>

Mara nyingine alikuwa akisema katika Swalah ya usiku:

9.

لِرَبِّي الْحَمْدُ، لِرَبِّي الْحَمْدُ،

*Li Rabbiyal- Hamdu, li Rabbiyal Hamdu,*

---

<sup>437</sup> *Jadd:* Bahati, Utajiri, Utukufu, nguvu, yaani Mwenye mali, watoto, cheo, uwezo na nguvu katika dunia hii. Hatoweza kunufaika navyo mbele Yako; Anavyomiliki havitomuokoa kutoka Kwako, lakini kitachomnufaisha na kumuokoa ni amali njema pekee.

<sup>438</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

“Kwa Mola wangu Sifa zote, Kwa Mola Wangu Sifa zote na shukrani za dhati”

Akikariri hadi kisimamo chake kilikuwa kirefu kama rukuu yake ambayo ilikuwa inakaribiana kwa urefu na kisimamo chake cha mwanzo, na alikuwa amesoma ndani yake Suratul-Baqarah.<sup>(439)</sup>

10.

رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ، حَمْدًا كَثِيرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيهِ (مُبَارَكًا عَلَيْهِ كَمَا يُحِبُّ رَبَّنَا وَيَرْضَى)  
*Rabbanaa walakal-Hamdu, Hamdan Kathiyran Twayyiban Mubaarakan fiyh [Mubaarakan 'alayhi, kamaa Yuhibbu Rabbunaa Wayardhwaa]*

“Ee Mola wetu! Ni zako sifa njema sifa nyingi, nzuri, zenye Baraka (Baraka juu yake kama Anavyopenda Mola wetu na Kuridhika)”<sup>(440)</sup>

Matamshi haya aliyasoma mtu aliyekuwa akiswali nyuma yake (صلى الله عليه وآله وسلم). Aliyasoma baada ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kunyanyua kichwa chake kutoka kwenye rukuu na alisema: 'Sami'a Allaahu Liman Hamidah'.

Alipomaliza Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kuswali, alisema: **((Nani aliyesema hivi sasa?))** Yule mtu akasema: "Ilikuwa ni mimi Ee Mjumbe wa Allaah!"

Hivyo Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: **((Nimewaona Malaika zaidi ya thelathini wanakimbilia (kila mmoja anataka) kuwa wa kwanza kuyaandika)).**<sup>(441)</sup>

---

<sup>439</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Abu Daawuud.

<sup>440</sup> Abu Daawuud na An-Nasaaiy kwa isnaad Swahiyh. Imetolewa katika *Al-Irwaah* (335).

<sup>441</sup> Maalik, Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

## Kurefusha Kisimamo Hiki Na Wajibu Wa Kutulia Ndani Yake

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akikifanya kisimamo chake hiki kuwa kirefu, (kama) unaokaribiana na urefu wa rukuu yake kama ilivyotajwa; bali, alikuwa akisimama mara nyingine mpaka msemaji husema: "Amesahau" [kutokana na kusimama kwake muda mrefu]"<sup>(442)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiamrisha (wafanye) utulivu humo. Alimwambia aliyeswali vibaya ((...**kisha nyanyua hadi unyooke sawa sawa hali ya kuwa umesimama (kila mfupa urudi mahali pake)** [katika riwaaya nyingine] **Unapoinuka nyoosha uti wako na nyanyua kichwa chako hadi mifupa irudi katika viungo vyake**))<sup>(443)</sup>. Pia alimkumbusha kwamba: ((Swalah ya mtu haitimii kama hajafanya hivyo)).

---

<sup>442</sup> Al-Bukhaariy, Muslim na Ahmad. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (namba 307).

<sup>443</sup> Al-Bukhaariy, Muslim, Ad-Daraamiy, Al-Haakim, Ash-Shaafi'iy na Ahmad.

### TANBIHI:

Maana ya Hadiyth hii iko dhahiri na wazi, nayo ni utulivu katika kusimama huku. Ama utumiaji wa Hadiyth hii unaofanywa na baadhi ya ndugu zetu katika watu wa Hijaz na kwengineko kama ni dalili ya kuthibitisha kuweka mkono wa kulia juu ya kushoto katika kusimama, bila shaka iko mbali sana na riwaaya nyingi za Hadiyth. Bali ni hoja ni batili, kwani uwekaji uliotajwa, haukuja utajo wake katika kisimamo cha kwanza katika usimulizi wowote ule wa Hadiyth na katika matamshi yake (Hadiyth). Basi inakuaje kupelekea kutafsiri "mifupa irudi sehemu yake" iliyotajwa katika Hadiyth kuwa ni mkono wa kulia kuukumata mkono wa kushoto kabla ya rukuu?! Hii ingelitumika kama matamshi yote ya Hadiyth yangeasiriwa kumaanisha hivi. Basi vipi kuhusu wanavyohusisha maana iliyobainisha maana tofauti kabisa? Bali kuweka kwake hakuwezi kufahamika kutoka katika Hadiyth kabisa, kwa vile iliyokusudiwa 'mifupa' ni mifupa ya uti wa mgongo, kama ilivyothibitishwa katika

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Allaah عزوجل Hatazami Swalah ya mja asiyenyosha uti wake wa mgongo barabara baina ya rukuu zake na sijda zake)).<sup>(444)</sup>**

---

Sunnah, "...alikuwa akisimama kwa kunyooka barabara hadi kila mfupa ulirudi sehemu yake."

Mimi binafsi, sina shaka kwamba kuweka mikono juu ya kifua katika kusimama ni uzushi unaopotoa, kwani haikutajwa katika Hadiyth zozote za Swalah juu ya kwamba ni nyingi mno. Ingelikuwa kutendeka huko kuna asili, ingelitufikia japo katika usimulizi mmoja. Juu ya hivyo, hakuna hata Salaf mmoja aliyefanya hivyo, wala hakutaja hata mmoja wa Maulamaa wa Hadiyth niyuavyo.

Hii hailingani na alivyonukuu Shaykh At-Tuwayjiriy katika Makala yake (Uk. 18-19) kutoka kwa Imaam Ahmad (رحمه الله), "Akipenda mtu, anaweza kuacha mikono yake pembeni, au akipenda anaweza kuweka kifua ni mwake", kwani Imaam Ahmad hakuhusisha hii kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), bali alisema kutokana na ijtihaad na rai yake mwenyewe. Na rai inaweza kuwa imekosewa. Inapopatikana dalili sahihi dhidi ya uzushi inafuatwa na kuachwa hiyo ya uzushi, mfano kama hii, hivyo kauli ya Imaam yenye mapendekezo yake haikanushi uzushi wake kama alivyoandika Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله). Bali naona haya maneno yake ni ishara kwamba Imaam Ahmad hakuchukulia kuwekwa kulikotajwa juu kama ni kumethibitika katika Sunnah, kwani ameruhusu uchaguzi baina ya kutenda na kuacha kutenda. Je, anadhani Shaykh Mheshimiwa kwamba Imaam aliruhusu pia uchaguzi kuhusu uwekaji wa mikono kabla ya rukuu? Hivyo imethibitika kwamba kuweka mikono kifua ni katika kusimama baada ya rukuu sio katika Sunnah. Haya ni majadiliano mafupi ya mas-ala haya ambayo yanaweza kujadiliwa katika maelezo zaidi kwa upana, lakini kutokana na uchache wa sehemu hapa, inatosha, na badala yake, ni ubainisho wangu dhidi ya Shaykh (At-Tuwayjiriy) katika Chapa ya tano (Uk. 30) chapa mpya.

<sup>444</sup>Ahmad na Atw-Twabaraaniy katika Mu'jam Al-Kabiyr ikiwa na isnaad Swahiyh.

## Kusujudu

Kisha alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akileta *Takbiyr* na kuporomoka chini kwa kusujudu<sup>(445)</sup>, na alimuamrisha aliyeswali vibaya afanye hivyo akimwambia: **((Swalah ya mtu ye yote haikamiliki hadi ... aseme: 'Sami'a Allaahu Liman Hamidah' na mpaka anyooke sawa sawa, kisha aseme: 'Allaahu Akbar' kisha Asujudu mpaka viungo vyake (vitulizane))).**<sup>(446)</sup>

Pia alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anapotaka kusujudu, huleta *Takbiyr*, (akitenganisha mikono yake mbali na ubavu wake) kisha ndio husujudu<sup>(447)</sup>  
Mara nyingine alikuwa akiinua mikono yake anaposujudu.<sup>(448)</sup>

## Kwenda Chini Kusujudu Kwa (Kutanguliza) Mikono

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akitanguliza mikono yake ardhini kabla ya magoti yake.<sup>(449)</sup>

---

<sup>445</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>446</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amewafikiana.

<sup>447</sup> Abu Ya'laa katika Musnad (284/2) ikiwa na isnaad nzuri na Ibn Khuzaymah (1/79/2) ikiwa na isnaad tofauti iliyo Swahiyh.

<sup>448</sup> An-Nasaaiy, Ad-Daaraqutwniy na Mukhlisw katika *Al-Fawaaid* (1/2/2) ikiwa na isnaad mbili Swahiyh. Kunyanyua mikono huku kumeripotiwa na Maswahaba kumi na Masalaf wengi wameona ni muono Swahiyh. Miongoni mwao ni Ibn 'Umar, Ibn 'Abbaas, Hasan Al-Baswriy, Twaawuus, mtoto wake 'Abdullaah, Naafi' mtumwa wa Ibn 'Umar aliyeachwa huru, Saalim mtoto wa Ibn 'Umar, Qaasim bin Muhammad, 'Abdullaah bin Diyenaar na 'Atwaa. Vile vile 'Abdur-Rahmaan bin Mahdi kasema: "Hii ni kutokana na Sunnah". Imefanywa na Maimamu wa Sunnah; Ahmad bin Hanbal, na imenukuliwa kutoka kwa Maalik na Ash-Shaafi'y.



Alikuwa akiamrisha hivyo kwa kusema: **((Anaposujudu mmoja wenu, basi asiiname kama anavyoinama ngamia, bali atangulize mikono yake kabla ya magoti yake)).**<sup>(450)</sup>

---

<sup>449</sup> Ibn Khuzaymah (176/1), Ad-Daaraqutwniy na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali. Hadiyth zote zinazopinga hii si Swahiyh. Namna hii kumeidhinishwa na Maalik, na ripoti kama hiyo kutoka kwa Ahmad katika At-Tahqiq ya Ibn Al-Jawzi (108/2). Al-Marwaz pia amenukuu kwa isnaad Swahiyh. Imaam Al-Awazaa'iy katika Masaail yake (1/47/1) akisema: "Nimewaona watu wakitanguliza mikono kabla ya magoti".

<sup>450</sup> Abu Daawuud, Tamaam katika Al-Fawaaid, na An-Nasaaiy katika Sunan As-Sughraa na Sunan Al-Kubraa (47/1) ikiwa na isnaad Swahiyh. 'Abdul-Haqq amekiri ni Swahiyh katika Al-Ahkaam (54/1) na akaendelea kusema katika Kitabu At-Tahajjud (56/1), "Ina isnaad madhubuti kuliko ya nyuma yake". Yaani Hadiyth ya Waail ambayo ni kinyume (magoti kabla ya mkono). Bali Hadiyth ya mwisho, pamoja nakuwa inapinga Hadiyth hii Swahiyh na iliyotangulia, sio Swahiyh katika isnaad wala katika maana, kama nilivyoeezea katika 'Silsilatul-Ahaadiyth Adhw-Dhwa'iyfah' (Namba. 929) na katika Al-Irwaa (357). Itambulikane kwamba njia ya kutofautisha na ngamia ni kutanguliza mikono kabla ya magoti kwa sababu ngamia anaanza kutanguliza magoti kwanza; magoti ya ngamia yako katika miguu yake ya mbele kama ilivyobainishwa katika *Lisaan Al-'Arab* na vitabu vingine vya Kiarabu, na kama ilivyotajwa na Atw-Twahaawiy katika *Mushkil Al-Athaar* na *Sharh Ma'aaniy Al-Athaar*. Pia Imaam Qaasim As-Saraqutwniy (رحمه الله) katika *Gharyyb Al-Hadiyth* (2/70/1-2), ikiwa na isnaad Swahiyh, kauli ya Abu Huraryah, "Asipige magoti mtu kama afanyavyo ngamia anayekimbia". Akasema Imaam, "Hii ni katika sajdah. Anasema kwamba mtu asijitupe chini kama anavyojitupa ngamia anayekimbia (asiyefugwa) kwa haraka na bila ya utulivu, bali aende polepole chini akitanguliza kuweka mikono yake kwanza, kisha yafuatie magoti. Na maelezo ya Hadiyth marfuu' imesimuliwa kuhusu jambo hili". Kisha akataja Hadiyth za juu.

Ama kauli ya ajabu ya Ibnul-Qayyim, "Maneno haya hayaeleweki na hayafahamiki na mabingwa wa lugha", inajibiwa na vyanzo tulivyovitaja pamoja na vingi vinginevyo ambavyo maelekezo yanaweza kutafutwa. Nimelezea pia kuhusu hii katika kubainisha uongo dhidi ya Shaykh At-Tuwayjiry ambayo imechapishwa.

Na alikuwa pia akisema: **((Hakika mikono miwili inasujudu kama uso unavyosujudu, basi anapoweka mmoja wenu uso wake, aweke mikono yake na anapoinuka aiinue ))**.<sup>(451)</sup>

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) viganja vyake (akivitanua)<sup>(452)</sup>, akibana vidole vyake pamoja<sup>(453)</sup> na kuvielekeza Qiblah.<sup>(454)</sup>

Na pia alikuwa akiviweka viganja vya mikono yake usawa na mabega yake<sup>(455)</sup>, na mara nyingine usawa na masikio yake<sup>(456)</sup>. Alikuwa akiimakinisha pua yake na kipaji chake na ardhi.<sup>(457)</sup>

Alimuambia aliyeswali vibaya: **((Unaposujudu, makinisha sijda yako))**<sup>(458)</sup>. Na katika usimulizi mwingine: **((Unaposujudu, makinisha uso wako na mikono yako, hadi mifupa yako yote itulie mahali pake))**.<sup>(459)</sup>

Na alikuwa pia akisema: **((Hakuna Swalah kwa ye yote yule isiyegusa pua yake ardhi kama kinavyogusa kipaji cha uso))**.<sup>(460)</sup>

---

<sup>451</sup> Ibn Khuzaymah (1/79/2), Ahmad na Siraaj. Al-Haakim amekiri ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubali. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (313).

<sup>452</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>453</sup> Ibn Khuzaymah, Al-Bayhaqiy na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>454</sup> Al-Bayhaqiy ikiwa na isnaad Swahiyh. Ibn Abi Shaybah (1/82/2) na Siraaj wamehusisha kuelekeza vidole vya mguu katika usimulizi mwingine.

<sup>455</sup> Abu Daawuud na At-Tirmidhiy ambaye amekiri ni Swahiyh, kama alivyokir Ibn Al-Mulaqqin (27/2). Imetolewa katika *Al-Irwaa* (309).

<sup>456</sup> Abu Daawuud na An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>457</sup> Abu Dawuud na At-Tirmidhiy ambaye amekiri ni Swahiyh kama alivyokiri Ibn Al-Mulaqqin (27/2). Imetolewa katika *Al-Irwaa* (309).

<sup>458</sup> Abu Daawuud na Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>459</sup> Ibn Khuzaymah (1/10/1) ikiwa na isnaad nzuri.

<sup>460</sup> Ad-Daraqutwniy, Atw-Twabaraaniy (3/140/1) na Abu Nu'aym katika *Akhbaar Isbahaan*.

Alikuwa pia akimakinisha chini magoti yake na vidole vya miguu yake<sup>(461)</sup>, na akielekeza ncha za vidole vya mikono yake Qiblah<sup>(462)</sup>. Aliweka visigino vyake pamoja<sup>(463)</sup>. Aliweka miguu yake sawa sawa<sup>(464)</sup> na aliamrisha hivyo.<sup>(465)</sup>

Hivi ni viungo saba ambavyo (صلى الله عليه وآله وسلم) alisujudia; viganja viwili vya mikono, magoti mawili, miguu miwili, kipaji cha uso na pua.

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alivihesabu viungo viwili vya mwisho kama ni kiungo kimoja katika kusujudu kwani alisema: **((Nimeamrisha kusujudu (katika riwaaya nyingine: Tumeamrisha kusujudu juu ya viungo saba): Juu ya kipaji cha uso na akaashiria kwa mkono wake<sup>(466)</sup>, kwenye pua, na mikono, [katika riwaaya nyingine: viganja vya mikono], magoti na vidole vya miguu, na wala tusikunje<sup>(467)</sup> nguo na nywele)).<sup>(468)</sup>**

---

<sup>461</sup>Al-Bayhaqiy ikiwa na isnaad Swahiyh, Ibn Abi Shaybah (1/82/2) na Siraaj. Wamehusisha nia kuelekeza vidole vya miguu katika usimulizi mwingine.

<sup>462</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud. Ibn Sa'd (4/157) amesimulia kutoka kwa Ibn 'Umar kwamba alipenda kuelekezea Qiblah kila sehemu ya mwili wake awezavyo wakati wa kuswali hata vidole gumba.

<sup>463</sup> Atw-Twahaawiy, Ibn Khuzaymah (Namba 654) na Al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>464</sup> Al-Bayhaqiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>465</sup> At-Tirmidhy na Siraaj. Al-Haakim amekiri ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>466</sup> Kuashiria huku kwa mkono kumefasiriwa kutokana na sarufi ya matini ya Kiarabu (*Fat-h Al-Baariy*).

<sup>467</sup> Yaani kuvikusanya na kuvizuia kutawanyika, kwa maana, kukusanya nguo au nywele kwa mikono katika rukuu na Sujuud (*An-Nihaayah*). Makatazo haya si katika Swalah, bali hata kabla ya Swalah imekatazwa kama walivyoongeza Maulamaa wengi katika makatazo. Hii imetiliwa nguvu zaidi kwa kuwakataza wanaume kuswali wakiwa wamefunga nywele zao, ambayo inafuatia baadaye.

<sup>468</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (310).

Alikuwa akisema: ((Mja anaposujudu, husujudu pamoja nae viungo saba: uso wake, viganja vya mikono yake, magoti yake, na miguu yake)).<sup>(469)</sup>

Na kuhusiana na mtu aliyeswali akiwa kafunga nywele zake<sup>(470)</sup> kwa nyuma, Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ((Mfano wake hakika ni kama mfano wa mtu anayeswali huku amefunga mikono yake [nyuma ya mgongo wake]))<sup>(471)</sup>. Akasema pia: ((Hiyo ni tandiko la Shaytwaan)), yaani anapokaa Shaytwaan, akikusudia mafundo ya nywele zake.<sup>(472)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) hailazi mikono yake<sup>(473)</sup>, bali alikuwa akiinyanyua mbali na ardhi na kuiweka mbali na mbavu zake kiasi kwamba weupe wa kwapa zake huonekana nyuma yake<sup>(474)</sup>, na pia kiasi kwamba lau mbuzi mchanga angelitaka kupita chini ya mikono yake angelipita.<sup>(475)</sup>

Alikuwa akifanya hivyo sana kiasi cha kwamba baadhi ya Swahaba zake walisema: "Tulikuwa tunahisi vibaya kwa Mtume

---

<sup>469</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Ibn Hibbaan.

<sup>470</sup> Yaani kubanwa juu au kusukwa.

<sup>471</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Ibn Hibbaan. Ibn Al-Athiyr amesema: "Maana ya Hadiyth hii ni kwamba kama nywele zake ingelikuwa zimelegea, zingelianguka ardhini katika sajdah; hivyo mtu atalipwa thawabu za kusujudu nywele. Lakini nywele zikifungwa, zitamaanisha kuwa hazikusujudu, kwani kamlinganisha na mtu ambaye mikono yake imefungwa pingu pamoja, kwa vile haitogusa ardhini kusujudu. Inaelekea amri hii imewekewa mipaka kwa wanaume pekee na haiwahusu wanawake kama Ash-Shawkaaniy alivyonukuu katika *Ibn Al-'Arabi*.

<sup>472</sup> Abu Daawuud na At-Tirmidhiy ambaye amekiri ni nzuri. Ibn Khuzaymah na Ibn Hibbaan amekiri ni Swahiyh. Taz. *Swahiyh Abi Daawuud* (653).

<sup>473</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>474</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (359).

<sup>475</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Ibn Hibbaan.

(صلى الله عليه وآله وسلم) kwa sababu ya vile anavyoweka mikono yake mbali na mbavu zake anaposujudu.<sup>(476)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiamrisha hivyo kwa kusema: **((Unaposujudu, weka viganja vyako (ardhini), na inua viwiko vyako <sup>(477)</sup>. Na akisema: Kuweni sawa katika *Sujuud*, na wala asitawanye mmoja wenu mikono yake mtawanyo wa [na katika riwaaya nyingine: kama anavyoitawanya] mbwa))<sup>(478)</sup>.**

Na katika tamshi jingine na Hadiyth nyingine: **((Na wala asilaze mmoja wenu mikono yake kama mlazo wa mbwa))<sup>(479)</sup>.**

Alikuwa pia akisema: **((Msitandaze mikono yenu [kama mtandazo wa mbuai (mnyama wa kuwinda). Lazeni mikono na tandazeni mikono mbali, kwani ufanyapo hivyo, huwa kila kiungo chako kinasujudu nawe))<sup>(480)</sup>.**

### Wajibu Wa Kutulia Katika *Sujuud*

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiamrisha kutimiza rukuu na *Sujuud*, na akimlinganisha mtu asiyetimiza hivyo kuwa ni kama mtu mwenye njaa anakula tende moja au mbili ambazo hazimsaidii kitu cho chote. Pia akimuambia kuhusiana na asiyetimiza: **((Hakika yeye ni muovu kabisa miongoni mwa watu wezi))**.

Vilevile alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akihukumu kubatilika kwa Swalah ya mtu asiyenyoosha mgongo wake sawa sawa katika rukuu na *Sujuud*, kama ulivyotangulia uchambuzi wake katika

---

<sup>476</sup> Abu Daawuud na Ibn Maajah ikiwa na isnaad Hasan.

<sup>477</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>478</sup> Al-Bukhaariy, Muslim, Abu Daawuud na Ahmad.

<sup>479</sup> Ahmad na At-Tirmidhiy ambaye amekiri ni Swahiyh.

<sup>480</sup> Ibn Khuzaymah (1/80/2), Al-Maqdisy katika *Al-Mukhtaarah* na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

## Adhkaar Za Sujuud

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema katika nguzo hii namna mbali mbali za adhkaar na du'aa zozote, mara hizi na mara nyingine hizi. Kati ya du'aa hizo ni hizi zifuatazo:

1.

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى

*Subhaana Rabbiyal-'Alaa*

“Ametakasika Mola wangu Aliye juu”. (mara tatu).<sup>(481)</sup>

Mara nyingine aliikariri zaidi ya mara hizo.<sup>(482)</sup>

Mara moja aliikariri sana katika Swalah ya usiku hadi *Sujuud* yake ilikuwa inakaribiana na kisimamo chake alichokuwa amesoma ndani yake Surah tatu katika Surah ndefu; Al-Baqarah, An-Nisaa na Al-'Imraan. Ndani yake (Swalah hii) kulijaa du'aa na kuomba maghfirah, kama ilivyotajwa kabla katika Swalah ya Usiku.

2-

سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى وَبِحَمْدِهِ

*Subhaana Rabbiyal-'Alaa wa Bihamdih*

“Ametakasika Mola wangu Aliye juu Na Sifa Njema Ni Zake”. (mara tatu)<sup>(483)</sup>.

---

<sup>481</sup>Ahmad, Abu Daawuud, Ibn Maajah, Ad-Daaraqutwniy, Atw-Twahaawiy, Al-Bazaar na Atw-Twabaraaniy katika *Mu'jam Al-Kabiyr* kutoka kwa Maswahaba saba. Taz. Pia Tanbihi katika Adhkaar za Rukuu.

<sup>482</sup> Taz. Tanbihi katika Rukuu pia.

3-

سُبُوْحُ قُدُّوسٍ، رَبُّ الْمَلَائِكَةِ وَالرُّوْحِ

*Subuuhun Qudduusun Rabbul Malaaiikati war Ruuh*

“Mwingi wa kutakaswa Mtakatifu, Mola wa Malaika na Jibriyl”<sup>(484)</sup>.

4-

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي

*Sub-haanaka Allaahumma Rabbanaa wa bi Hamdika Allaahumma gh-fir-liy*

“Kutakasika ni Kwako, Ee Allaah! Mola wetu, na sifa njema zote ni Zako, Ee Allaah! Nisamehe”

Alikuwa akiileta kwa wingi hii katika rukuu yake na *Sujuud* zake, alikuwa akitekeleza amri ya Qur-aan.<sup>(485)</sup>

5-

اللَّهُمَّ لَكَ سَجَدْتُ، وَبِكَ آمَنْتُ، وَلَكَ أَسْلَمْتُ، (وَ أَنْتَ رَبِّي) ، سَجَدَ وَجْهِي لِلَّذِي خَلَقَهُ وَصَوَّرَهُ (فَأَحْسَنَ صُوْرَهُ) وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ، (فَ) تَبَارَكَ اللهُ أَحْسَنُ

الْخَالِقِينَ

*Allaahumma laka Sajad-tu, wa Bika Aamantu, wa Laka Aslamtu, [wa Anta Rabbii], Sajada wajhiy li-Lladhiy Khalaqahu wa Swawwarahu, [fa-Ahsana swuwarahu] wa Shaqqa sam'ahu wabaswarahu, [fa]-Tabaaraka Allaahu Ahsanul Khaaliqiyn.*

“Ee Allaah! Kwako nimesujudu, na Wewe nimekuamini, na Kwako nimesilimu, (Nawe ni Mola Wangu) umeSujuud uso

---

<sup>483</sup>Swahiyh, imesimuliwa na Abu Daawuud, Ad-Daaraqutwniy, Ahmad, At-Twabaraaniy na Al-Bayhaqiy.

<sup>484</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>485</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

wangu kumsujudia Yule Aliyeuumba na Akautia sura, na Akaupasua usikizi wake na uoni wake, [Basi] Ametukuka Allaah Mbora wa waumbaji”.<sup>(486)</sup>

6-

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي كُلَّهُ، وَدِقَّةَ وَجَلَّتْ، وَأَوَّلَهُ وَآخِرَهُ وَعَلَانِيَّتَهُ وَسِرَّهُ  
*Allaahumma-Ghfirliy dhambiy kullahu, wa diqqahu, wa jillahu, wa awwalahu wa aakhirahu, wa 'alaaniyyatahu wasirrahu.*

“Ee Allaah! Nisamehe dhambi zangu zote, ndogo na kubwa, za mwanzo na za mwisho, za dhahiri na za siri”<sup>(487)</sup>

7-

سَجَدَ لَكَ سَوَادِي وَخِيَالِي، وَأَمَّنَ بِكَ فُؤَادِي، أَبُوؤُ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ هَدْيِي يَدَيَّ وَمَا جَنَيْتُ  
عَلَيَّ نَفْسِي  
*Sajada Laka sawaadiy wa khayaaliy, wa aamana Bika fuaadiy, abuu-u bi-ni'matika 'alayya, haadhay yadayy wamaa janaytu 'alaa nafsiy.*

“Utu wangu na kivuli changu kimekusujudia, moyo wangu umekuamini, nakiri neema Zako kwangu, hii ni mikono yangu na yote niliyochuma dhidi yangu”<sup>(488)</sup>

8-

سُبْحَانَ ذِي الْجَبْرُوتِ، وَالْمَلَكُوتِ، وَالْكِبْرِيَاءِ، وَالْعِظْمَةِ  
*Subhaana dhil Jabaruuti wal-Malakuuti wal-Kibriyaau wal-'Adhwamah*

---

<sup>486</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Atw-Twahaawiy na Ad-Daaraqutwniy.

<sup>487</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>488</sup> Ibn Naswr, Al-Bazaar na Al-Haakim, aliyekiri kuwa ni Swahiyh lakini Adh-Dhahabiy hakukubali. Hata hivyo, inayo nguvu ambayo imetajwa katika toleo la muswada.



“Ametakasika Mwenye Utawala, na Ufalme, na Ukubwa, na Utukufu”<sup>(489)</sup>.

Hii alikuwa akiisema katika Swalah ya usiku pamoja na zifuatazo

9-

سُبْحَانَكَ (اللَّهُمَّ) وَبِحَمْدِكَ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ

*Subhaanaka Allaahumma wa Bihamdika, laa ilaaha illa Anta*

“Kutakasika ni Kwako, (Ee Allaah) na sifa njema ni Zako, hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe”<sup>(490)</sup>.

10-

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي مَا أَسْرَرْتُ وَمَا أَعْلَنْتُ

*Allaahumma-Ghfirli maa asrartu, wamaa a'lantu*

“Ee Allaah! Nisamehe (dhambi) nilizofanya kwa siri, na (dhambi) nilizofanya dhahiri”<sup>(491)</sup>.

11-

اللَّهُمَّ اجْعَلْ فِي قَلْبِي نُورًا، (وَفِي لِسَانِي نُورًا) وَاجْعَلْ فِي سَمْعِي نُورًا،  
وَاجْعَلْ فِي بَصَرِي نُورًا، وَاجْعَلْ مِنْ تَحْتِي نُورًا، وَاجْعَلْ مِنْ فَوْقِي نُورًا، وَعَنْ  
يَمِينِي نُورًا، وَعَنْ يَسَارِي نُورًا، وَاجْعَلْ أَمَامِي نُورًا، وَاجْعَلْ خَلْفِي نُورًا، (وَاجْعَلْ فِي  
نَفْسِي نُورًا) ، وَأَعْظِمْ لِي نُورًا.

*Allaahumma J'al-fiy qalbiy nuuraa, [wa fiy lisaaniy nuuraa],  
Waj'al-fiy sam'iy nuuraa, Waj'al fiy baswariy nuuraa, Waj'al-  
min tahtiy nuuraa, Waj'al-min farwqiy nuuraa, wa 'an  
yamiyniy nuuraa, wa 'an yasaariy nuuraa, Waj'al-amaamiy*

---

<sup>489</sup> Abu Daawuud na An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>490</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, An-Nasaaiy na Ibn Naswr.

<sup>491</sup> Ibn Abi Shaybah (/112/1) na An-Nasaaiy; Al-Haakim amekiri ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubali.

*nuuraa, Waj'al-khalfiy nuuraa, [Waj'al- fiy nafsiy nuura], wa a'dhwim liy nuuraa.*

“Ee Allaah! Jaalia nuru katika moyo wangu, [na katika ulimi wangu nuru], na Jaalia katika masikio yangu nuru, na Jaalia katika uoni wangu nuru, na Jaalia chini yangu nuru, na Jaalia juu yangu nuru, na kulia kwangu nuru, na kushoto kwangu nuru, na Jaalia mbele yangu nuru, na Jaalia nyuma yangu nuru (na Jaalia katika nafsi yangu nuru), na Nifanyie kubwa nuru”.<sup>(492)</sup>

12-

(اللَّهُمَّ) (إِنِّي) أَعُوذُ بِرِضَاكَ مِنْ سَخَطِكَ، وَ(أَعُوذُ) بِمَعَاذِكَ مِنْ عِقَابِكَ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْكَ، لَا أَحْصِي ثَنَاءً عَلَيْكَ، أَنْتَ كَمَا أَثْنَيْتَ عَلَيَّ نَفْسِكَ

*Allaahumma [Inniy] A'urdhuu bi-Ridhwaaka min sakhatwika, wa [A'urdhuu] bi Mu'aafatika min 'uquubatika, wa 'A'urdhuu Bika Minka, laa uhswiy thanaa-an 'Alayka Anta kamaa Ath-nayta 'alaa Na-fsika*

“Ee Allaah! Hakika [mimi] najilinda kwa Radhi Zako kutokana na hasira Zako, na [najikinga] kwa msamaha Wako kutokana na adhabu Yako, na najilinda Kwako Unihifadhi na Wewe, mimi siwezi kuzidhibiti sifa Zako, Wewe ni kama Ulivyojisifu Mwenyewe”.<sup>(493)</sup>

### **Kukatazwa Kusoma Qur-aan Katika Sujuud**

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akikataza kusoma Qur-aan katika rukuu na *Sujuud*, na alikuwa akiamrisha kujitahidi na kuleta kwa wingi du'aa humo kama ilivyoelezewa kabla katika rukuu.

---

<sup>492</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Ibn Abi Shaybah (12/106/2, 112/1).

<sup>493</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

### Kurefusha *Sujuud*

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiirefusha *Sujuud* yake kiasi cha kukaribiana na rukuu katika urefu, na mara nyingine aliifanya ndefu mno kwa kutokea jambo lisilotegemewa, kama alivyosimulia mmoja wa Maswahaba akisema:

Mjumbe wa Allaah Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alitutokea katika moja kati ya Swalah mbili za jioni (Adhuhuri na Alasiri) akiwa amembeba Hasan au Husayn. Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alitangulia mbele na akamuweka chini [karibu na mguu wake wa kulia], kisha akaleta *Takbiyr* ya Swalah, na kuanza kuswali, alisujudu -*Sajdah*- kati ya *Sajdah* za Swalah yake, *Sajdah* aliyoirefusha akasema: Hivyo nikainua kichwa changu [baina ya watu] kumbe alikuweco mtoto juu ya mgongo wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) hali ya kuwa amesujudu. (Kisha) nikarudi katika *Sajdah* yangu [hii]. Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alipomaliza Swalah, watu wakasema: "Ee Mjumbe wa Allaah! Kwa hakika ulisujudu kati ya *Sajdah* za Swalah yako, *Sajdah* uliyoirefusha, mpaka tukadhania kuwa kuna jambo limetokea au ulikuwa unapokea wahyi". Akasema: **((Haikuwa lolote katika hayo, bali mwanangu alinipandia, nikachukia kumharakisha mpaka atapomaliza haja yake))**<sup>(495)</sup>.

---

<sup>494</sup>Muslim, Abu 'Awaanah na Al-Bayhaqiy. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (456).

<sup>495</sup> An-Nasaaiy, Ibn 'Asaakir (4/257/1-2) na Al-Haakim ambaye amekiri kuwa ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

Katika Hadiyth nyingine, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiswali, aliposujudu, Al-Hasan na Al-Husayn walimrukia mgongoni kwake. Watu walipojaribu kuwazuilia, aliwaashiria wawaachilie mbali. Alipomaliza Swalah, aliwaweka katika mapaja yake na akasema: **((Yeyote anayenipenda, basi na awapende na hawa wawili))**.

### Fadhila Za Sujuud

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Hakuna yeyote katika Ummah wangu isipokuwa nitamtambua siku ya Qiyaamah))**. Wakasema: "Vipi utawatambua Ee Mjumbe wa Allaah miongoni mwa umati mkubwa wa viumbe?" Akasema: **((Huoni kama ungeliingia katika boma ambako kuna farasi mweusi tii<sup>(496)</sup> na farasi mwenye weupe katika kipaji chake na miguu<sup>(497)</sup>. Je, hutoweza kumtambua ni yupi baina yao?))**. Wakasema: "Bila shaka". Akasema: **((Basi hakika Ummah wangu siku hiyo, watakuwa na weupe katika nyuso <sup>(498)</sup> kwa sababu ya Sujuud, na wenye weupe katika mikono yao na miguu yao<sup>(499)</sup> kwa sababu ya wudhuu))**.<sup>(500)</sup>

Alikuwa akisema pia: **((Allaah Atakapotaka kumshushia Rahma Amtakaye katika watu wa motoni, Huwaamrisha**

---

<sup>496</sup> Yaani rangi nyeusi safi isiyochanganywa na rangi nyingine yoyote. (*AnNihaayah*).

<sup>497</sup> Weupe unakusudiwa sehemu ya farasi ambako minyororo na bangili zinavikwa pamoja na miguu ya chini lakini si magoti.

<sup>498</sup> Yaani zinazong'ara usoni kutokana na nuru ya Sujuud.

<sup>499</sup> Yaani sehemu zitakazong'ara kutokana na wudhuu: uso, mikono na miguu. Alama za kung'ara za wudhuu usoni, mikononi na miguuni za binaadamu kulinganisha na weupe wa uso farasi na miguu.

<sup>500</sup> Ahmad, ikiwa na isnaad Swahiyh. At-Tirmidhiy amesimulia baadhi yake na kakiri kuwa ni Swahiyh. Imetolewa katika *Silsilat al-Ahaadiyth Asw-Swahiyhah*.

Malaika wantoe yeyote aliyekuwa akimuabudu Allaah, hivyo watawatoa, kwani wanawatambua kwa alama za *Sujuud*. Kwa vile Allaah Ameuharamishia moto kuunguza alama za *Sujuud*, hivyo watatoka kutoka motoni, kila binaadamu ataunguzwa na moto isipokuwa alama za *Sujuud*).<sup>(501)</sup>

### Kusujudu Juu Ya ardhi Na Juu Ya Jamvi <sup>(502)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) sana aki*Sujuud* juu ya ardhi (tupu).<sup>(503)</sup>

Na Maswahaba zake walikuwa wakiswali pamoja naye katika joto kali, hivyo anapokuwa mmoja wao hawezi kumakinisha kipaji chake ardhini, hutandaza nguo yake na kusujudia juu yake.<sup>(504)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ((...Imejaaliwa ardhi yote kuwa ni (sehemu ya kuswalia) Msikiti - mtu anaweza kuswali popote juu ya ardhi inapomkutia Swalah kama hapana najsi - na twahara -inatwaharisha: kuitumia kwa kujitwahirisha kutayammam- kwangu na kwa Ummah wangu. Hivyo basi Swalah inapomkutia mtu yeyote katika Ummah wangu, huwa anao Msikiti (mahali pa kuswali) na anayo twahara, (Ilikuwa) kabla yangu wakidhanja kuwa ni

---

<sup>501</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Hadiyith inaonyesha kuwa wanaoswali lakini wana dhambi, hawatabakia motoni milele bali hata ambao wameacha Swalah kwa sababu ya uvivu hawatobakia motoni milele. Hii ni Swahiyh - taz. *Asw-Swahiyhah* (2054).

<sup>502</sup> *Al-Haswiyr* - jamvi au mkeka uliotengenezwa kutokana na majani ya mtende au nyasi n.k.

<sup>503</sup> Hii ni kwa sababu Msikiti wake haukutandikwa majamvi n.k. Hii ni dalili ya Hadiyith nyingi kama ifuatayo na ya Abu Sa'iyd itakayofuatia.

<sup>504</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

Mara nyingine alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) aki*Sujuud* katika matope na maji. Na yalimtokea hayo katika asubuhi ya usiku wa ishirini na moja katika Ramadhān, iliponyesha mvua, na paa la Msikiti lililojengwa na majani ya mtende liliezuliwa. Hivyo Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alisujudu katika matope na maji. Abu Sa'iyd Al-Khudriyy alisema: "Nimemuona kwa macho yangu, Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akiwa na alama za matope na maji katika kipaji chake cha uso na pua".<sup>(506)</sup>

Pia mara nyingine alikuwa akiswali katika *khumrah*<sup>(507)</sup>, au mara nyingine katika zulia/ jamvi<sup>(508)</sup>, na mara aliswali juu yake na ilikuwa ishageuka nyeusi kutokana na utumiaji wa muda mrefu.<sup>(509)</sup>

### **Kuinuka Kutoka Kwenye *Sujuud***

Kisha, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiinua kichwa chake kutoka kwenye *Sujuud* huku akileta *Takbiyr*<sup>(510)</sup> na alimuamrisha

---

<sup>505</sup> Ahmad, Siraaj na Al-Bayhaqiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>506</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>507</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni. "*Khumrah*" ni kipande cha jamvi, makumbi ya mtende, au nyenzo kama hizo za miti ambazo ni kubwa kiasi cha mtu kuweka uso wake katika Sajdah. Istilahi hiyo haitumiki kwa vipande vikubwa.

<sup>508</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>509</sup> Muslim na Abu 'Awaanah. *Al-labisa* kawaida ina maana 'kuvaa', lakini hapa imetumika kumaanisha 'kutumia', yaani kukalia n.k. Hivyo 'kuvaa' inajumuisha pia 'kuikalia'. Hii inaonyesha kwamba imekatazwa (haraam) kukalia hariri, kwa sababu ya kuharamishwa kuvaa kulikothibitishwa katika Swahiyh Al-Bukhaariy na Muslim na wengineo. Bali ni makatazo ya dhahiri kukalia hariri yamesimuliwa humo kwa hiyo asichanganywe mtu na kauli za Maulamaa wakubwa kuruhusu.

<sup>510</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

Kisha alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiutandika mguu wake wa kushoto (ardhini) na kuukalia [hali ya kuwa ametulia]<sup>(513)</sup>, na alimuamrisha aliyeswali vibaya kwa kumwambia: **((Unaposujudu, jimakinishe kwa Sujuud yako, na (kisha) unapoinuka, kalia paja lako la kushoto))**.<sup>(514)</sup>

Alikuwa akiusimamisha mguu wake wa kulia<sup>(515)</sup> na akielekeza vidole vya mguu wa kulia Qiblah.<sup>(516)</sup>

---

<sup>511</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>512</sup> Al-Bukhaariy katika Juzuu *Raf' Al-Yadayn*, Abu Daawuud ikiwa na isnaad Swahiyh, Muslim na Abu 'Awaanah. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (316).

Kunyosha mikono hapa kwa kila *Takbiyr* imetajwa na Ahmad, kama ilivyo katika Al-Badaa'i ya Ibn Al-Qayyim (3/89). Athram (ibnul Athram) amenukuu kutoka kwake (Imaam Ahmad) alipoulizwa kuhusu kunyanyua mikono, alisema: "Kwa kila harakaat ya juu na chini". Athram kasema: "Nimemuona Abu 'Abdillaah (yaani Imaam Ahmad) akinyanyua mikono katika Swalah kwa kila harakaat ya chini au ya juu".

Hii pia ilikuwa ni rai ya Ibn Al-Mundhir na Abu 'Aliy wa Ash-Shaafi'iy, na pia rai ya Maalik na Ash-Shaafi'iy mwenyewe kama ilivyo katika *Twarh At-Tathriyb*. Kunyanyua mikono hapa pia kumesimuliwa kwa usahihi kutoka kwa Anas bin Maalik, Ibn 'Umar, Naafi', Atw-Twaawuus, Hasan al-Baswriy, Ibn Siyriin na Ayyuub As-Sikhtiyaaniy, katika Muswannaf Ibn Abi Shaybah (1/106) ikiwa na usimulizi Swahiyh kutoka kwao.

<sup>513</sup> Ahmad na Abu Daawuud ikiwa na isnaad nzuri.

<sup>514</sup> Al-Bukhaariy na Al-Bayhaqiy.

<sup>515</sup> An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>516</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Abu Shaykh katika (Aliyopokea Abuz-Zubayr kutoka katika njia isiyo ya Jaabir) (Namba 104-6) na Al-Bayhaqiy.

### Kikao Baina Ya Sajdah Mbili (Kikao Cha Iftiraash)

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiutandika mguu wake wa kushoto na kuukalia [hali ya kuwa ametulia]<sup>(517)</sup>, na alimuamrisha aliyeswali vibaya kwa kumwambia: **((Unaposujudu, jimakinishe kwa *Sujuud* yako, na (kisha) unapoinuka, kalia paja lako la kushoto)).**<sup>(518)</sup>

Alikuwa akiusimamisha mguu wake wa kulia juu<sup>(519)</sup>, na akielekeza vidole vya mguu wa kulia Qiblah.

### *Al-Iq'aa*u (Kusimamisha Miguu Huku Umekalia Visigino) Baina Ya Sajdah Mbili

Alikuwa mara nyingine akifanya 'iq'aa' (kupumzika kwa kukalia visigino vyote viwili na vidole vyake [vyote]).<sup>(520)</sup>

---

<sup>517</sup> Ahmad na Abu Daawuud ikiwa na isnaad nzuri.

<sup>518</sup> Al-Bukhaariy na Al-Bayhaqiy.

<sup>519</sup> An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>520</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Abu Shaykh katika (Aliyopokea Abuz-Zubayr kutoka katika njia isiyo ya Jaabir) (Namba 104-6) na Al-Bayhaqiy.

Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni. Ibn Al-Qayyim (رحمه الله) amesahau katika hili, hivyo baada ya kutaja "Iftiraash" ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) baina ya Sajdah mbili, amesema: "Hakuna aina nyingine ya kikao cha Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kilichohifadhiwa isipokuwa hiki". Vipi hii iwe sahihi na hali 'iq'aa' imetufikia kutoka Hadiyth ya Ibn 'Abbaas katika Muslim, Abu Daawuud na At-Tirmidhiy ambaye amekiri ni Swahiyh na wengineo. (Taz. *Silsilat al-Ahaadiyith asw-Swahiyhah* 383), Hadiyth ya Ibn 'Umar ikiwa na isnaad nzuri kutoka kwa Al-Bayhaqiy na Ibn Hajr amekiri ni Swahiyh. Pia Abu Is-haaq Al-Harbiy amesimulia katika *Ghariby al-Hadiyith* (5/12/1) kutoka kwa Atw-Twaawuus, aliyemuona Ibn 'Umar na Ibn 'Abbaas wakifanya 'iq'aa', sanad yake ni Swahiyh. Allaah Amteremshie Rahma Zake Imaam Maalik ambaye amesema: "Kila mmoja wetu anaweza kukosea na kukosolewa isipokuwa mwenye kaburi hili".



## Wajibu Wa Kutulia Baina Ya *Sajdah* Mbili

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akitulia mpaka kila mfupa unarudi mahali pake sawa sawa.<sup>(521)</sup> Na alimuamrisha aliyeswali vibaya hivyo kwa kumuambia: **((Swalah ya mtu haitotimia hadi afanye hivyo)).**<sup>(522)</sup>

Pia, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akikirefusha - hichi kikao baina ya *Sajdah* mbili- kiasi cha kukaribiana na urefu wa *Sajdah* yake<sup>(523)</sup>, na mara nyingine, alibakia katika (kikao hiki) mpaka mtu akasema: "Amesahau".<sup>(524)</sup>

## Adhkaar (Utajo) Baina Ya *Sajdah* Mbili

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) katika kikao hiki akisema:

اللَّهُمَّ (رَبِّ) اغْفِرْ لِي، وَارْحَمْنِي، (وَاجْبُرْنِي)، (وَ ارْزُقْنِي)، وَاهْدِنِي، (وَ عَافِنِي)، وَارْزُقْنِي  
*Allaahumma [Rabbi] Ghfirliy wa-Rhamniy [Wajburniy], [Warfa'niy] WahDiniy, [Wa'afiniy], Warzuqniy*

---

Bila shaka, 'iq-'aa' hii ni tofauti na ile iliyokatazwa kama itakavyofuatia katika Tashahhud.

<sup>521</sup> Abu Daawuud na Al-Bayhaqiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>522</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>523</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>524</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni. Ibn Al-Qayyim amesema: Sunnah hii imeachwa na watu baada ya zama za Maswahaba. Lakini anayefuata Sunnah na haangazi kwengine kunakoipinga, hana wasiwasi wa kupinga uongofu.

“Ee Mola ((na katika mapokezi mengine akisema: Mola wangu) Nighufirie na Unirehemu na Unitie nguvu, na Uninyanyue na Unihidi na Unipe afya njema na Uniruzuku.<sup>(525)</sup>

رَبِّ اغْفِرْ لِي رَبِّ اغْفِرْ لِي

*Rabbi Ghfir-liy, Rabbi Ghfir-liy*<sup>(526)</sup>

“Mola wangu nighufirie Mola wangu nighufirie”

Na alikuwa akiomba dua hiyo hiyo katika Swalah za usiku<sup>(527)</sup> Kisha “alikuwa akifanya *takbiyrah* na kusujudu *Sajdah* ya pili”<sup>(528)</sup> na alimuamrisha hivyo aliyeswali Swalah yake vibaya akamuambia baada ya kumuamrisha kutulia baina ya *Sajdah* mbili kama ilivyotangulia, “kisha useme; Allaahu Akbar, kisha

---

<sup>525</sup> Abu Daawuud na At-Tirmidhiy na Ibn Maajah na Al-Haakim na Adh-Dhahabiy pia ameikubali.

<sup>526</sup> Ibn Maajah kwa isnadi njema. Na Imam Ahmad amezichagua du’aa kwa

mfumo huo. Na Is-haaq bin Rahaawayh amesema: “Alikuwa anapotaka akizisoma mara mara tatu tatu na anapotaka husema: “Allaahumma ghfirliy, kwa sababu zote mbili husomwa na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) baina ya sajdah mbili, na hivi ndivyo ilivyoandikwa katika Masaail ya Imaam Ahmad na Is-haaq bin Rahaawayh riwayah ya Is-haaq Al-Maruwziy (uk. 19)

<sup>527</sup> Na haya hayakanushi ulazima wa kusoma dua hizi ndani ya Swalah za ‘fardhi’, kwa sababu ya kutokuwepo tofauti baina yake na baina ya Swalah za Sunnah. Na kutokana na haya amesema Ash-Shaafi’iy na Ahmad na Is-haaq kuwa wanaona haya yanajuzu katika Swalah za Fardhi na za Sunnah pia kama alivyosema At-Tirmidhiy. Na pia Imaam Atw-Twahaawiy katika kitabu cha ‘*Mushkil al-Aathaar*’ ameona kuwa hivyo ndivyo inavyotakiwa kishari’ah. Na mtizamo sahihi unayaunga mkono hayo, kwa sababu ndani ya Swalah hapana mwahali pasiporuhusiwa kumtaja Allaah, na hayo yanapaswa kuwepo hapa pia, na hili ni bainifu lisilofichika.

<sup>528</sup> Al-Bukhaariy na Muslim

usujudu mpaka viungo vyako vitulie ; kisha fanya hivyo katika Swalah yako yote.<sup>(529)</sup>”

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) mara nyingine akinyanyua mikono yake katika *takbiyra* hii<sup>(530)</sup>

Na alikuwa akifanya katika *Sajdah* hii kama alivyofanya katika *Sajdah* ya mwanzo. Kisha “Hunyanyua kichwa chake huku akikabbir”<sup>(531)</sup> na alimuamrisha hivyo (aliyeswali Swalah yake vibaya) akamuambia baada ya kumuamrisha kusujudu *Sajdah* ya pili kama ilivyotangulia: “Kisha hunyanyua kichwa chake huku akikabbir”<sup>(532)</sup> (akisema ‘*Allahu Akbar*) “Kisha fanya hivyo katika kila Rak’ah na *Sajdah*,” na utakapotenda hivyo utakuwa umekamilisha Swalah yako, na ukipunguza jambo utakuwa umepunguza katika Swalah yako.<sup>(533)</sup> (Na alikuwa akinyanyua mikono yake) mara nyingine.<sup>(534)</sup>

### Kikao Cha Mapumziko

Kisha alikuwa “akikaa sawa sawa (akiukalia mguu wake wa kushoto sawasawa mpaka kila mfupa urudi mahali pake.”<sup>(535)</sup>

---

<sup>529</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim na amesahihisha Adh dhahabiy na yaliyozidi yamepokelewa kwa Al-Bukhaariy na Muslim

<sup>530</sup> Abu Awaanah na Abu Daawuud kwa isnadi mbili sahihi, na amesema pia juu ya unyanyuaji huu Ahmad na Maalik na Ash-Shaafi’iy katika masimulizi yao kwa hivyo soma maelezo ukurasa wa (161 nambari 1).

<sup>531</sup> Muslim na Al-Bukhaariy

<sup>532</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim na amesahihisha na aliwafikiana naye Imam Adh Dhahabiy

<sup>533</sup> Ahmad na At-Tirmidhiy na akaisahihisha.

<sup>534</sup> Abu ‘Awaanah na Abu Daawuud kwa isnadi mbili sahihi, na amezungumza juu ya unyanyuaji huu Ahmad na Maalik na na Ash-Shaafi’iy katika riwaya kutoka kwa wawili hao kwa hivyo tizama maelezo katika ukurasa wa (161-nambari 1).

<sup>535</sup> Al Al-Bukhaariy na Abu Daawuud. Na kikao hiki kinajulikana na wanavyuoni wa fiqhi kama ni kikao cha mapumziko, na amesema juu ya

## Kuitegemea Mikono Miwili Katika Kuinuka

Kisha (صلى الله عليه وآله وسلم) huinuka huku akiweka mikono yake juu ya ardhi kwa ajili ya kuanza rak'aah ya pili<sup>(536)</sup>.

“Na alikuwa akiitegemea mikono yake anaposimama katika Swalah.”<sup>(537)</sup>

Na “Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anapoinuka kwa ajili ya Rak'ah ya pili akianza kwa kusoma Alhamdulillah bila kunyamaza.”<sup>(538)</sup>

Na hufanya katika Rak'ah hii kama alivyofanya katika ya kwanza, isipokuwa alikuwa akiifanya fupi ukiilinganisha na ya kwanza kama ilivyotangulia.

## Ulazima Wa Kusoma Suratul – Faatihah Katika Kila Rak'ah

---

kikao hiki Imam Ash-Shaafi'iy na Ahmad namna hiyo hiyo katika 'Tah'qiq' (111/11) na hivyo ni bora.

<sup>536</sup> Al-Bukhaariy na Muslim

<sup>537</sup> Imesimuliwa na Abu Is-haaq Al Harbiy kwa isnaad njema na kwa Al-Bayhaqiyy maana yake ni isnadi sahihi. Ama hadithi isemayo; “Alikuwa akiinuka mfano wa upinde bila kuitegemea mikono yake” ni maudhui (haina asli) na kila kilichokuwemo ni dhaifu kisichosihhi, na nimeyabainisha hayo katika 'Adhw-Dhwai'yfah' (5,929,na 968)

<sup>538</sup> Muslim na Abu 'Awaanah. Kipumziko kilichokanushwa katika Hadiyth hii inaweza kuwa ni kipumziko cha kusoma du'aa ya kufungulia na hakijumuishi kipumziko cha kusoma isti'aadhah, au inaweza kumaanisha zaidi ya hivyo. Naona kwamba uwezekano wa kwanza unakinaisha zaidi. Kuna rai mbili baina ya Maulamaa kuhusu isti'aadhah na tunachukulia iliyo sahihi ni kuisema katika kila rakaa. Maelezo yametolewa katika *Al-Aswl*.

Alimuamrisha (صلى الله عليه وآله وسلم) aliyeswali vibaya kusoma *Al-Faatihah* katika kila Rak'ah wakati alipomwambia baada ya kumuamrisha aisome hiyo *Al-Faatihah* katika Rak'ah ya mwanzo<sup>(539)</sup>: **((...kisha fanya hivyo katika Swalah yako yote)).**<sup>(540)</sup> [katika usimulizi mwengine] **((...katika kila Rak'ah))**<sup>(541)</sup>. Na alisema: **((katika kila Rak'ah kuna kisomo)).**<sup>(542)</sup>

### Tahiyaatu (*Tashahhud*) Ya Kwanza

Kisha, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akikaa kwa *Tashahhud* baada ya kumaliza Rak'ah ya pili. Swalah ikiwa ya Rak'ah mbili kama Alfajiri, hukaa "muftarishan"<sup>(543)</sup> kama alivyokuwa akikaa baina ya *Sajdah* mbili. Na hivi hivi ndivyo anavyokaa katika *Tashahhud* ya kwanza<sup>(544)</sup> katika Swalah za Rak'ah tatu au nne.

Alimuamrisha hivyo aliyeswali vibaya kwa kumuambia: **((Utakapokaa katikati ya Swalah, jitulize, na utandaze paja lako la kushoto na lete *Tashahhud*)).**<sup>(545)</sup>

---

<sup>539</sup> Abu Daawuud na Ahmad ikiwa na isnaad iliyo na nguvu.

<sup>540</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>541</sup> Ahmad ikiwa na isnaad nzuri.

<sup>542</sup> Ibn Maajah, Ibn Hibbaan katika Swahiyh yake na Ahmad katika Masaail ya Ibn Haani (1/52). Jaabir bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) amesema: "Atakayeswali rakaa bila ya kusoma Mama wa Qur-aan hakuwali, isipokuwa akiwa nyuma ya Imaam". Imesimuliwa na Maalik katika Al-Muwatwtwa.

<sup>543</sup> An-Nasaaiy (1/173) ikiwa na isnaad Swahiyh. "Muftarishan" ni kukalia tumbo la mguu wa kushoto na kuusimamisha unyayo wa mguu wa kulia kama ilivyotangulia.

<sup>544</sup> Al-Bukhaariy na Abu Daawuud.

<sup>545</sup> Abu Daawuud na Al-Bayhaaqiy ikiwa na isnaad nzuri.

Abu Huraryah (رضي الله عنه) amesema: "Rafiki yangu (صلى الله عليه وآله وسلم) amenikataza kuchutama (iq'aa) mchutamo wa mbwa."<sup>(546)</sup> [katika riwaaya nyingine] Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akikataza kuchutama kama Shaytwaan.<sup>(547)</sup>

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anapokaa katika *Tashahhud* huweka kiganja chake cha mkono wa kulia juu ya paja [katika usimulizi mwingine: goti] la kulia, na huweka kiganja chake cha kushoto katika paja [katika usimulizi mwingine: goti] la kushoto<sup>(548)</sup>. Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiweka kisugudi cha mkono wake wa kulia katika paja lake la kulia.<sup>(549)</sup>

Pia (صلى الله عليه وآله وسلم) alimkataza mtu aliyekaa katika Swalah hali ya kuwa anaategemea mkono wake wa kushoto akamwambia: **((Hakika hiyo ni Swalah ya Mayahudi))**<sup>(550)</sup>. Na katika kauli nyingine: **((Usikae hivi, kwani hakika hiki ni kikao cha wale wanaoadhibiwa))**<sup>(551)</sup>. Katika Hadiyth nyingine: **((Ni kitako cha wale walioghadhikiwa [Na Allaah]))**<sup>(552)</sup>.

---

<sup>546</sup> Atw-Twayaalisiiy, Ahmad na Ibn Abi Shaybah. Kuhusu "iq'aa", Abu 'Ubaydah na wengineo wamesema: "Ni mtu anapogandamiza kikatio chake ardhini, akiweka muundi wake wima, na kuegemeza mikono yake ardhini kama mbwa anavyofanya". Hii ni tofauti na "iq'aa" baina ya Sajdah ambayo imekubaliwa katika Sunnah kama ilivyotangulia kabla.

<sup>547</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na wengineo. Imetolewa katika *Al-Irwaa* (316).

<sup>548</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>549</sup> Abu Daawuud na An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh. Inayokusudiwa ni kwamba hakutenganisha viwiko vyake na ubavu wake kama alivyofafanua Ibn Al-Qayyim katika *Zaad al-Ma'aad*.

<sup>550</sup> Al-Bayhaqi na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali. Imetolewa pamoja inayofuatia katika *Al-Irwaa* (380).

<sup>551</sup> Ahmad na Abu Daawuud ikiwa na isnaad nzuri.

<sup>552</sup> 'Abdur-Razaq; 'Abdul-Haqq amekiri ni Swahiyh katika *Ahkaam* yake (Namba 1284 katika utafiti wangu).

## Kutikisa Kidole Katika *Tashahhud*

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akitandaza kiganja chake cha mkono wa kushoto juu ya goti la mkono wa kushoto, na akikunja vidole vyake vya mkono wa kulia vyote, huku akiashiria kinachofuatia kidole cha gumba -kidole cha Shahada-upande wa Qiblah huku akikitupia jicho lake.<sup>(553)</sup>

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anapoashiria kwa kidole chake, huweka kidole cha gumba juu ya kidole cha kati<sup>(554)</sup>, na mara nyingine alikuwa akifanya duara kwa hivyo viwili.<sup>(555)</sup>

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) - anaponyanyua kidole chake - akikitikisa (huku) akiomba du'aa nacho<sup>(556)</sup> akisema: **(Hakika**

---

<sup>553</sup> Muslim, Abu 'Awaanah na Ibn Khuzaymah. Al-Humaydiy (13/1) na Abu Ya'laa (275/2) wameongeza katika isnaad Swahiyh kutoka kwa Ibn 'Umar, ((Na hii ni kumdunga Shaytwaan, hakuna atakayesahau akifanya hivi)). Na Al-Humaydiy alinyosha kidole chake. Al-Humaydiy pia alisema kwamba Muslim bin Abi Maryam amesema: "Mtu alisimulia Hadiyth kwangu katika kanisa la Syria, aliona Surah za Mitume wakiwa katika taswira kama hii",

na Al-Humaydiy akanyosha kidole chake. Hii ni kauli ya ajabu lakini sanad yake hadi kwa 'huyo mtu' ni Swahiyh.

<sup>554</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>555</sup> Abu Daawud, An-Nasaaiy, Ibn Al-Jaruud katika Al-Muntaqaa (208), Ibn Khuzaymah (1/86/1-2) na Ibn Hibbaan katika Swahiyh yake (485) ikiwa na isnaad Swahiyh. Ibn Al-Mulaqqin amekiri ni Swahiyh (28/2), na inayo usimulizi madhubuti kutoka kwa Ibn 'Addiy (287/1).

<sup>556</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni. Kuhusu 'kuomba du'aa nacho', Imaam Atw-Twahaawiy amesema: "Hii ni dalili kwamba ilikuwa ni mwisho wa Swalah". Hivyo kuna dalili kwamba Sunnah ni kuendelea kukielekeza na kukitikisa hadi katika Tasliym, kwani du'aa huwa hadi hapo. Hii ni rai ya Maalik na wengineo. Imaam Ahmad aliulizwa: "Je mtu akitikise kidole chake katika Swalah"? Akajibu: "Ndio, kwa nguvu" (Imetajwa na Ibn Haaniy katika Masaail yake Imaam Ahmad 1/80). Kutokana na hii, ni dhahiri kwamba kutikisa kidole ni Sunnah iliyothibiti ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na ni desturi ya Ahmad na Maimamu

Kadhalika, Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) walikuwa wakikumbushana baina yao, yaani, kuhusu kuashiria kwa kidole wakati wa kuomba du'aa.<sup>(558)</sup>

---

Jambo la ajabu ni kwamba wengine watamtetea Imaam katika mas-ala mengine, japo kama rai yake inapingana na Sunnah, kwa hoja kwamba kudhihirisha makosa ya Imaam ina maana ni kufanya dhihaka na kumdharau. Kisha wanasahau hii na kukanusha Sunnah hii iliyothibiti na huku wakifanya istihzai kwa wanaoitekeleza. Ikiwa wanatambua au hawatambui, istihzai zao pia zinajumuisha wale Maimaam ambao kwa kawaida yao wanawatetea kwa yaliyo batili, na ambao wako sahihi katika Sunnah mara hii! Bali wanambeza Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) mwenyewe, kwani yeye ndiye aliyetuletea Sunnah hii. Kwa hiyo kuifanyia mzaha ni sawa na kumfanyia yeye ((فَمَا جَزَاء مَنْ يَفْعَلُ ذَلِكَ مِنْكُمْ إِلَّا...))

**((Basi hana malipo mwenye kutenda hayo miongoni mwenu ila....))** [Al-Baqarah: 85] Ama kukiweka kidole chini baada ya kukielekeza, au kupunguza kutikisa na kukithibitisha (katika kusema 'Laa ilaaha [Hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki...] na kukanusha (kusema 'illa-Allaahu ...' [isipokuwa Allaah']) vyote hivi hakuna asili katika Sunnah; bali ni kinyume na Sunnah, kama Hadiyth hii inavyothibitisha.

Juu ya hivyo, Hadiyth ambayo inasema hakutikisa kidole chake haina isnaad Swahiyh, kama nilivyoelezea katika *Dhwa'iyf Abi Daawuud* (175). Hata kama ingelikuwa ni Swahiyh, inakanusha na Hadiyth ya juu inathibitisha. Uthibitisho unapewa kipaumbele juu ya ukanushaji kama inavyojulikana kwa Maulamaa.

<sup>557</sup> Ahmad, Al-Bazaar, Abu Ja'far, Al-Bukhtiriy katika Al-Amaail (60/1), 'Abdul-Ghaniy Al-Maqdisiy katika Sunan yake (12/2) ikiwa na isnaad nzuri, Ar-Ruuyaaniy katika musnad yake (249/2) na Al-Bayhaqiy.

<sup>558</sup> Ibn Abi Shaybah (2/123/2) ikiwa na isnaad nzuri.



Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akifanya hivyo katika *Tashahhud* zote mbili.<sup>(559)</sup>

Wakati mmoja, alimuona mtu akiomba du'aa kwa vidole vyake viwili akasema: **((Pwekesha (Kimoja, [kimoja]))** na akaashiria kidole chake cha shahada.<sup>(560)</sup>

### Wajibu Wa *Tashahhud* Ya Kwanza Na Hukumu Ya Du'aa Ndani Yake

Kisha alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisoma *At-Tahiyyaatu* kila baada ya *Rak'ah* mbili<sup>(561)</sup>.

Na alikuwa kitu cha kwanza anachokisema anapokaa ni: **((*At-Tahiyyaatu liLlaah*))**.<sup>(562)</sup>

Na anapoisahau *Tashahhud* katika *Rak'ah* mbili za mwanzo, husujudu *Sajdatus-Sahw*-.<sup>(563)</sup>

Alikuwa akiamrisha - *Tashahhud* - kwa kusema: **((Mtakapokaa katika kila *Rak'ah* mbili, semeni: 'At-Tahiyaatu ...na kila mmoja wenu ajichagulie du'aa anayoipenda zaidi amuombe Allaah (عز وجل) [kwayo]))**<sup>(564)</sup>. Katika riwaaya nyingine:

---

<sup>559</sup> An-Nasaaiy na Al-Bayhaqiyy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>560</sup> Ibn Abi Shaybah (12/40/1, 2/123/2) na An-Nasaaiy. Al-Haakim amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali. Kuna usimulizi unaotilia nguvu kutoka kwa Ibn Abi Shaybah.

<sup>561</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>562</sup> Al-Bayhaqiyy amesimulia katika usimulizi kutoka kwa 'Aaishah ikiwa na isnaad nzuri kama ilivyohakikishwa na Ibn Al-Mulaqqin (28/2).

<sup>563</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Imetolewa katika *Al-Irwaa Al-Ghaliyl* (338).

<sup>564</sup> An-Nasaaiy, Ahmad na Atw-Twabaraaniy katika *Mu'jam Al-Kabiyr* (3/25/1)

ikiwa na isnaad Swahiyh. Maana halisi ya Hadiyth ni dalili ya kuamrisha

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiwafundisha *Tashahhud* kama alivyokuwa akiwafundisha Surah katika Qur-aan<sup>(566)</sup> na "Sunnah ni kuisema kimya kimya."<sup>(567)</sup>

### Matamshi Mbali Mbali Ya *Tashahhud*

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) aliwafundisha matamshi mbali mbali ya *Tashahhud*:

1- *Tashahhud* ya Ibn Mas'uud ambaye amesema: "Amenifundisha Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) *Tashahhud*, viganja vyangu baina ya viganja vyake (صلى الله عليه وآله وسلم) kama anavyonifundisha Surah katika Qur-aan:

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ،  
السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ. أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ  
مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

*At-Tahiyyaatu liLlaahi, wasw-Swalawaatu, watw-Twayyibaatu, Assalaamu 'alayka ayyuhan-Nabbiyyu WarahmatuLlaahi WaBarakaatuh, Assalaamu 'alaynaa wa'ala 'IbaadiLlaahi Swaalihiy. Ash-hadu Al-laa ilaaha*

---

du'aa katika kila *Tashahhud* hata isiyongana na Tasliym. Na hii ni rai ya Ibn Hazm (رحمه الله).

<sup>565</sup> An-Nasaai ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>566</sup> Al-Bukhaari na Muslim.

<sup>567</sup> Abu Daawuud na Al-Haakim aliyekiri kuwa ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amewafikiana.

*illa-Allaah wa ash-hadu anna Muhammadan 'Abduhu wa Rasuuluhu.*

“Maamkuzi mema,<sup>(568)</sup> na rehema<sup>(569)</sup> na mazuri yote<sup>(570)</sup>, ni kwa Allaah, amani<sup>(571)</sup>, zishuke juu yako Ee Mtume na Rehema za Allaah, na Baraka Zake<sup>(572)</sup>, amani ishuke juu yetu, na juu ya waja wa Allaah walio wema, (kwani mtu anaposema hivi, inajumuisha kila mja mwema mbinguni na ardhini) nashuhudia kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah, na nashuhudia kwamba Muhammad ni mja Wake na ni Mjumbe Wake”

[Na hali ya kuwa yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) yu pamoja nao (Hivi alivyokuwa na sisi, lakini) alipofariki tukawa tunasema:

السَّلَامُ عَلَى النَّبِيِّ

*Assalaamu 'alan-Nabbiyyi*

“Amani ishuke juu ya Mtume”<sup>(573)</sup>

---

<sup>568</sup> "At-Tahiyyaatu" yaani, maneno yote yanayoambatana na amani, ufalme na kudumu ni kwa ajili ya Allaah. (*An-Nihaayah*)

<sup>569</sup> "As-Swalawaatu" yaani, 'du'aa zote zinazotumika kumtukuza Allaah Ta'ala, kwani Yeye ni Mwenye kustahiki nazo, na hakuna apasaye kustahiki nazo isipokuwa Yeye. (*An-Nihaayah*)

<sup>570</sup> "At-Twayyibaatu" yaani, maneno mazuri na masafi yote yanayofaa kumsifu Allaah, na sio yale ambayo yasiyofanana na sifa Zake ambayo hutukuzwa kwazo wafalme. (*Fat-hul-Baariy*)

<sup>571</sup> Maana, kujikinga na Allaah na kutiwa nguvu Naye kwa vile *As-Salaam* (amani) ni Jina la Allaah khasa. Hivyo maamkizi yanamaanisha: Allaah Awe Muwakilishaji na Mlinzi wako. Kama inavyosemwa: '*Allaah Ma'ak*' (Allaah Awe nawe) yaani Ulinzi Wake, msaada na ihsani.

<sup>572</sup> Ni neno linalotumika kwa mazuri yote yanayotoka kwa Allaah.

<sup>573</sup> Al-Bukhaariy, Muslim, Ibn Abi Shaybah (1/90/2) Sirraaj na Abu Ya'laa katika Musnad yake (258/2). Imetolewa katika *Al-Irwaa* (321).

Kauli ya Ibn Mas'uud: "Tulisema: 'Amani ishuke juu ya Mjumbe', inabainisha kwamba Maswahaba (رضي الله عنهم) walikuwa wakisema: Amani ishuke juu yako ewe Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Tashahhud

Ibn Hajr amesema: 'Ziada hii inaonyesha dhahiri kwamba walikuwa wakisema: 'Amani ishuke kwako ewe Mtume' wakimuelekezea yeye wakati wa uhai wake, lakini alipofariki Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) waliacha kumuelekezea hivyo wakimtaja kama ni mtu wa nafsi ya tatu badala yake wakisema: 'Amani ishuke juu ya Mtume'. Amesema pia sehemu nyingine, 'As-Subkiy amesema katika *Sharh Al-Minhaaj* baada ya kutaja usimulizi kutoka kwa Abu 'Awaanah pekee, 'ikiwa usimulizi huu ni Swahiyh kutoka kwa Maswahaba, inathibitisha kwamba baada ya (kufariki) Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), sio lazima kumuelekezea Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) maamkizi ya amani, hivyo mtu aseme: 'Amani ishuke juu ya Mtume'. (Ibn Hajr anaendelea: "Hii ni Swahiyh bila ya shaka (kwa sababu imethibitishwa katika Swahiyh Al-Bukhaariy) na pia nimepata dalili ya kutilia nguvu". 'Abdur-Razzaaq amesema: "Ibn Jurayj ameniarifu: 'Atwaa amenijulisha kwamba Maswahaba walikuwa wakisema 'Amani ishuke kwako ewe Mtume' alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) yuhai, lakini baada ya kufariki walikuwa wakisema: 'Amani ishuke juu ya Mtume', na hii ni isnaad Swahiyh. Ama usimulizi wa Sa'iyd bin Manswuur kutoka kwa 'Ubaydah bin 'AbdiAllaah bin Mas'uud, ambaye ameripoti kutoka kwa baba yake kwamba Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) amemfundisha Tashahhud kisha yeye ('Abdullaah bin Mas'uud) akaisema (Tashahhud), Ibn 'Abbaas amesema: "Tulikuwa tukisema 'Amani ishuke juu yako ewe Mtume' alipokuwa yuhai pekee", ambayo Ibn Mas'uud amejibu akisema: "Hivi ndivyo tulivyofundishwa na hivi ndivyo tunavyofundisha". Inavyoelekea ni kwamba Ibn 'Abbaas amesema kuwa hili ni jambo la kujadiliana lakini Ibn Mas'uud hakulikubali. Lakini usimulizi wa Abu Ma'mar (yaani usimulizi katika Al-Bukhaariy) ndio ulio Swahiyh zaidi, kwa vile Abu 'Ubaydah hakisikia (Ahaadiyith) kutoka kwa baba yake, na juu ya hivyo, isnaad inavyoelekea hadi kwa Abu 'Ubaydah ni dhaifu" (mwisho wa kunukuu kutoka kwa Ibn Hajr).

2- *Tashahhud* ya Ibn 'Abbaas, amesema: "Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akitufundisha *Tashahhud* kama anavyotufundisha [Suraah katika] Qur-aan. Alikuwa akisema:

التَّحِيَّاتُ الْمُبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ الطَّيِّبَاتُ لِلَّهِ (ال)سَلَامٌ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، (ال)سَلَامٌ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ. أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، (و) أَشْهَدُ أَنْ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، (وفي رواية: عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ)

*At-Tahiyyaatu Al-Mubaarakatu Asw-Swalawaatu, Atw-Twayyibaatu LiLlaahi, [as] Salaamu 'alayka ayyuhan-Nabbiyyu WarahmatuLlaahi WaBarakaatuh, [as] Salaamun 'alaynaa wa'ala 'IbaadiLlaahis Swaalihiyin. Ash-hadu al-laa ilaaha illa-Allaah, [wa] ash-hadu anna Muhammadan Rasuulu Allaah, ['Abduhu Wa Rasuuluhu].*

“Maamkuzi mema, maneno ya Baraka, Swalah, mazuri yote ni ya Allaah, amani ishuke juu yako Ee Mtume na Rehma za Allaah na Baraka Zake. Amani ishuke juu yetu na waja wema wa Allaah, nashuhudia kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allaah, na (nashuhudia) kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allaah, [na katika riwaaya ...mja wake na Mjumbe wake”]<sup>(574)</sup>

3- *Tashahhud* au *Tahiyyaatu* ya Ibn 'Umar ambaye ameripoti kwamba Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema katika *Tashahhud*:

---

Maneno haya ya Ibn Hajr yamenukuliwa na Maulamaa wengi katika utafiti wao, mfano; Al-Qastwalaaniy, Az-Zarqaaniy, Al-Laknaawiy n.k. Wote wamechagua kutoa maneno yake bila ya kutoa tanbihi zaidi. Hoja hizi zimetajwa kikamilifu zaidi katika *Al-Aswl*.

<sup>574</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Ash-Shaafi'iy na An-Nasaaiy.

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ (وَ) الصَّلَوَاتُ (وَ) الطَّيِّبَاتُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ  
وَبَرَكَاتُهُ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ. أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا  
شَرِيكَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

*At-Tahiyyaatu liLlaahi [Wa] SSwalawaatu, [Wa] Twayyibaatu, Assalaamu 'alayka ayyuhan-Nabbiyyu WarahmatuLlaahi WaBarakaatuh, Assalaamu 'alaynaa wa'ala 'TbaadiLlaahis Swaalihiyn. Ash-hadu al-laa ilaaha illa-Allaah, Wahdahu laa shariyka Lahuu, wa ash-hadu anna Muhammadan 'Abduhu wa Rasuuluhu.*

“Maamkuzi mema ni ya Allaah, (na) Swalah (na) mazuri, amani ishuke juu yako Ee Mtume na Rehma za Allaah - Ibn 'Umar amesema: "Nimeongezea<sup>(575)</sup> .... na Baraka Zake - Amani ishuke juu yetu na waja wema wa Allaah, nashuhudia kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila ni Allaah - Ibn 'Umar amesema: "Nimeongozea<sup>(576)</sup> - ... Pekee Hana mshirika - na nashuhudia kwamba Muhammad ni mja Wake na ni Mjumbe Wake”<sup>(577)</sup>.

4- *Tashahhud* ya Abu Muusa Al-Ash'ariyy ambaye amesema kwamba, Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ((... **Mnapokaa, kauli ya mwanzo ya kila mmoja wenu iwe:**

---

<sup>575</sup> Taz. Tanbihi inayofuatia.

<sup>576</sup> Ziada mbili hizi zimethibitika kuwa ni sehemu ya Tashahhud kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Ibn 'Umar hakuziongeza kwa upendekezo wa nafsi yake (hasa ameeepukana na hayo); bali amejifunza hayo kutoka kwa Maswahaba ambao wameziripoti kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), kisha ndio akaziongeza katika Tashahhud ambayo amesikia moja kwa moja kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).

<sup>577</sup> Abu Daawud na Ad-Daaraqutniy ambaye amekiri ni Swahiyh.

التَّحِيَّاتُ الطَّيِّبَاتُ، الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ،  
السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ. أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ (وَوَحْدَهُ لَا شَرِيكَ  
لَهُ)، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

*At-Tahiyyaatu At-Twayyibaatu As-Swalawaatu liLlaahi, Assalaamun 'alayka ayyuhan-Nabbiyyu WarahmatuLlaahi WaBarakaatuh, Assalaamun 'alaynaa wa'alaa 'IbaadiLlaahi Swaalihyyn. Ash-hadu al-laa ilaaha illa-Allaah [Wah-dahu laa shariyka Lahu] wa ash-hadu anna Muhammadan 'Abduhu wa Rasuuluhu.*

“Maamkizi, mazuri, Swalah ni kwa ajili ya Allaah, amani ishuke juu yako Ee Mtume na Rehma za Alalh na Baraka Zake, amani ishuke juu yetu na juu ya waja wema, nashuhudia kwamba hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah, [Pekee Hana mshirika] na nashuhudia kwamba Muhammad ni mja Wake na Mjumbe Wake”.<sup>(578)</sup>

Matamshi saba ndio Tahiyyaatu.<sup>(579)</sup>

5- *Tashahhud* ya ‘Umar bin Al-Khattwaab ambaye alikuwa akiwafundisha watu *Tashahhud* huku akiwa juu ya Minbar akisema: “Semeni:

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ، الرَّكَائِيَّاتُ لِلَّهِ، الطَّيِّبَاتُ (لِلَّهِ)، الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا  
النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ. أَشْهَدُ أَنْ لَا  
إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

*At-Tahiyyaatu liLlaahi, Az-Zaakiyaatu liLlaahi, Atw-Twayyibaatu [liLlaahi], Asw-Swalawaatu LiLlaahi, Assalaamun 'alayka ayyuhan-Nabbiyyu WarahmatuLlaahi WaBarakaatuh, Assalaamun 'alaynaa wa'alaa 'IbaadiLlaahi*

<sup>578</sup> Muslim, Abu ‘Awaanah, Abu Daawuud na Ibn Maajah.

<sup>579</sup>Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

*Swaalihin. Ash-hadu al-laa ilaaha illa-Allaah, wa ash-hadu anna Muhammadan 'Abduhu wa Rasuuluhu.*

“Maamkizi ni ya Allaah, kutakasika kote ni kwa Allaah, mazuri [ni kwa ajili ya] Allaah, Swalah ni kwa ajili ya Allaah, amani ishuke kwako Ee Mtume na Rahma za Allaah na Baraka Zake, amani ishuke kwetu na kwa waja wema wa Allaah, nashuhudia kwamba hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah, na nashuhudia kwamba Muhammad ni mja Wake na Mjumbe wake”.<sup>(580)</sup>

### **Kumswalia Mtume Pahala Pake Na Matamshi Yake Mbali Mbali**

---

<sup>580</sup> Maalik na Al-Bayhaqi ikiwa na isnaad Swahiyh. Ingawa Hadiyth hii ni Mawquuf, lakini ina hukmu ya Marfuu' kwani inajulikana kuwa haisemwi tu kutokana na rai ya mtu, na lau kama ingelikuwa ni rai, basi kauli hii isingelikuwa ni dhikr bora miongoni mwa adhkaar nyingine kama alivyosema 'Ibn 'Abdil-Barr.

#### **TANBIHI:**

Hakuna ziada ya 'wa maghfiratu...' (na magfirah Yake) katika Tashahhud yoyote katika hizi, kwa hiyo isiwe desturi ya mtu kusema. Kwa ajili hiyo baadhi ya Masalaf wameikanusha kutokana na usimulizi ufuatao:

Atw-Twabaraaniy (3/56/1) ameripoti ikiwa na isnaad Swahiyh kutoka kwa Twalha bin Muswarrif ambaye amesema: "Rabiy' bin Khaytham ameongeza katika Tashahhud, '...wa Barakaatuhu, wa Maghfiratu!' Hivyo 'Alqamah akasema: "Tumesita tulipofundishwa: 'amani ishuke juu yako ewe Mtume, na Rahma za Allaah na Baraka Zake". 'Alqamah alikuwa akifuata khaswa mfano wa Mwalimu wake 'Abdullaahi bin Mas'uud ( رضي الله عنه ) ambaye kutoka kwake imeripotiwa kuwa ni Swahiyh. Alikuwa akimfundisha mtu Tashahhud, na alipofika katika neno: 'Nakiri kwamba hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah...', yule mtu alisema: "Pekee, Hana mshirika", na 'Abdullaah akasema: "Yeye ni hivyo lakini tunakomea pale tulipofunzwa". [Imesimuliwa na Atw-Twabaraaniy katika Mu'jam Al-Awsat Namba. 2848 ikiwa na isnaad Swahiyh].



Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akijiswalia mwenyewe katika *Tashahhud* ya kwanza na nyingineo<sup>(581)</sup>. Na akaifanya kuwa ni amrisho kwa Ummah wake, kwani aliwaamrisha kumswalia yeye baada ya kumuomba amani<sup>(582)</sup>, na aliwafundisha matamshi mbali mbali ya kumswalia.

1-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى أَهْلِ بَيْتِهِ وَعَلَى أَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ. وَ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ بَيْتِهِ وَعَلَى أَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ.

<sup>581</sup> Abu 'Awaanah katika Swahiyh yake (2/324) na An-Nasaaiy.

<sup>582</sup> Wamesema, "Ewe Mjumbe wa Allaah! Tumefundishwa kukuomba amani (yaani katika *Tashahhud*) lakini vipi tukuswalia?" Akasema: "Semeni Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad..." n.k. Hivyo hakubainisha kuwa khaswa kwa *Tashahhud* moja na bila ya nyingine. Hivyo kuna dalili hapa ya kuamrisha kumswalia katika *Tashahhud* ya kwanza pia. Hii ni madhehebu ya Imaam Ash-Shaafi'iy kama alivyonukuu katika kitabu chake *Al-Umm*, nayo ni Swahiyh kwa wafuasi wake kama alivyoeleza An-Nawawiy katika *Al-Majmuu'* (3/460) na ikatiliwa nguvu na *Rawdhwah At-Twaalibiyn* (1/263). Ni rai pia ya Al-Waziyr bin Hubayrah Al-Hanbaliy katika *Al-Ifswaah* kama Ibn Rajab alivyonukuu na akaipa nguvu katika *Dhayl Twabaqaat* (1/280). Hadiyth nyingi zimekuja kuhusu kumswalia (صلى الله عليه وآله وسلم) katika *Tashahhud*. Hakuna hata mojawapo iliyoeleza bayana kuhusu yaliyotajwa, bali Hadiyth hizo ni za ujumla zimejumuishwa *Tashahhud* zote. Na nimetaja hii katika *Al-Aswl* kama ni ta'liyy (kiambatisho) lakini sio katika matni kuu kwani haziridhishi shuruti zetu za (kutambulisha) usahihi. Lakini zinakubaliana katika maana, na wale wanaokanusha na kupinga hii, hawana dalili sahihi kutumia kama ni ushahidi, kama nilivyopambanua katika *Al-Aswl*. Kama kauli ya kuonyesha kuongeza chochote katika '*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad*' ni Makruuh (inachukiza), pia haina asili katika Sunnah, wala hakuna dalili inayokinaisha. Bali tunaona kwamba anayesema hivi hafuati maamrisho ya nyuma ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), '*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad ...'* na hoja zaidi za hii zipo katika *Al-Aswl*.

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammadin, wa 'alaa ahli baytihi, wa 'alaa azwajihii wa dhurriyaatihi, kamaa Swallayta 'alaa aali Ibraahiyma, Innaka Hamiydun Majiydun. wa Baarik 'alaa Muhammadin, wa 'alaa aali baytihi, wa 'alaa Azwajihii wa dhurriyaatihi, kamaa Baarakta 'alaa aali Ibraahiyma, Innaka Hamiydun Majiydun*

“Ee Allaah! Mswalie Muhammad<sup>(583)</sup> na watu wa nyumbani kwake, na wake zake, na kizazi chake kama Uliyowaswalia jamaa zake Ibraahiym, hakika wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu. Na Mbariki Muhammad<sup>(584)</sup> na jamaa wa nyumba yake, na wake zake, na kizazi chake kama Uliyowabariki jamaa zake Ibraahiym, hakika wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu”

Du'aa hii alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiitumia kwa kuomba yeye mwenyewe<sup>(585)</sup>.

2-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى (إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى) آلِ  
إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ. اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ  
عَلَى (إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى) آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ .

---

<sup>583</sup> Rai ya mwanzo kabisa kuhusu maana ya 'kumswalia Mtume Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ni ya Abu Al-'Aaliyah (kwa marejeo ya Suratul-Ahzaab 33: 56), 'Swalah ya Allaah kwa Mtume ina maana kudhibiti na kumpa utukufu; Swalah ya Malaika na wengineo ni kuomba hivyo kwa Allaah, na hapa inamaanisha kuomba Swalah zizidishwe na sio asili ya Swalah yenyewe". Ibn Hajr amenukuu katika *Fat-h Al-Baariy*, na amepinga kauli mashuhuri kwamba Swalah ya Mola ni Rahmah, akaipambanua hii Ibn Al-Qayyim katika *Jalaa Al-Ahkaam*, akiacha nafasi ndogo kwa maoni zaidi.

<sup>584</sup>Kutokana na barakah: ukuaji, uongezaji na kukua, kubarikika. Hivyo du'aa hii inamdhani Muhammad mema ambayo Allaah Amewajaalia familia ya Ibraahiym, kumdumishia na kumthibitishia na pia kumuongezea maradufu.

<sup>585</sup> Ahmad na Atw-Twahaawiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammadin, wa 'alaa aali Muhammadin, kamaa Swallayta 'alaa [Ibraahiyma, wa 'alaa] aali Ibraahiyma, Innaka Hamiydun Majiydun, Allaahumma Baarik 'alaa Muhammadin, wa 'alaa aali Muhammadin, kamaa Baarakta 'alaa [Ibraahiyma wa 'alaa] aali Ibraahiyma, Innaka Hamiydun Majiydun*

“Ee Allaah! Mswalie Muhammad, na jamaa wa Muhammad, kama Ulivyomswalia [Ibraahiym na juu ya]<sup>(586)</sup> jamaa zake Ibraahiym, hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu. Ee Allaah! Mbariki Muhammad na jamaa zake Muhammad kama Ulivyombariki [Ibraahiym na juu ya]<sup>(587)</sup>, jamaa zake Ibraahiym, hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu”.<sup>(588)</sup>

3-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ (وَأَلِ إِبْرَاهِيمَ)،  
إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ. وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى (إِبْرَاهِيمَ  
(و) آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ.

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammadin, wa 'alaa aali Muhammadin, kamaa Swallayta 'alaa Ibraahiyma [wa aali Ibraahiyma], Innaka Hamiydun Majiydun, wa Baarik 'alaa Muhammadin, wa 'alaa aali Muhammadin, kamaa Baarakta*

<sup>586</sup> Taz. Tanbihi ifuatayo.

<sup>587</sup> Nyongeza hizi mbili ni ushahidi wenye kuthibitika katika Al-Bukhaariy, Atw-Twahaawiy, Al-Bayhaqiy, Ahmad na An-Nasaaiy. Pia zimekuja katika njia mbali mbali za usimulizi katika aina nyinginezo za du'aa (Taz. Namba 3, 7). Hivyo usichanganywe na rai ya Ibn Al-Qayyim katika *Jalaa Al-Afhaam* (Uk. 198) akifuata nyayo za Mwalimu wake mkuu Ibn Taymiyyah katika *Al-Fataawa* (1/16). "Hakuna Hadiyth Swahiyh kuhusu ibara 'Ibraahiym wa aali Ibraahiym' pamoja". Hapa tumekuonyesha Hadiyth zilizo Swahiyh. Kosa la Ibn Al-Qayyim limebainika kutokana na mwenyewe kukiri kuwa (aina ya kumswalia) Namba 7 (inayofuatia) ni Swahiyh ambayo imetaja aliyokanusha kabla!

<sup>588</sup> Al-Bukhaariy, Muslim, Al-Humaydiy (138/1) na Ibn Mandah (68/2) ambaye amesema kuwa kuna makubaliano kuwa Hadiyth hii ni Swahiyh.

*'alaa [Ibraahiyma wa] aali Ibraahiyma, Innaka Hamiydun Majiydun*

“Ee Allaah! Mswalie Muhammad na jamaa zake Muhammad kama Ulivyomswalia Ibraahiyhm [na jamaa zake Ibraahiym], hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu. Na Mbariki Muhammad na jamaa zake Muhammad kama Ulivyombariki [Ibraahiym na] jamaa zake Ibraahiym hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu”.<sup>(589)</sup>

4-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ (النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ)، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى (آلِ) إِبْرَاهِيمَ. وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ (النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ)، وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى (آلِ) إِبْرَاهِيمَ، فِي الْعَالَمِينَ. إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammadin [an-Nabbiyyil Ummiyyi], wa 'alaa aali Muhammadin, kamaa Swallayta 'alaa [aali] Ibraahiyma, wa Baarik 'alaa Muhammadin [an Nabbiyyil Ummiyyi], wa 'alaa aali Muhammadin, kamaa Baarakta 'alaa [aali] Ibraahiyma fil 'aalamiyna, Innaka Hamiydun Majiydun*

“Ee Allaah! Mswalie Muhammad [Nabii Ummiy (Asiyejua kusoma au kuandika)] na jamaa zake Muhammad kama Ulivyowaswalia [jamaa zake] Ibraahiym, na Mbariki Muhammad [Nabii Ummiy] na jamaa zake Muhammad kama Ulivyowabariki [jamaa zake] Ibraahiym miongoni mwa walimwengu, hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu”.<sup>(590)</sup>

5-

---

<sup>589</sup> Ahmad, An-Nassaiy na Abu Ya'laa katika Musnad yake (44/2) ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>590</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Ibn Abi Shaybah (2/132/1) na Abu Daawuud, na Al-Haakim amekiri ni Swahiyh.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى (آلِ) إِبْرَاهِيمَ. وَبَارِكْ عَلَى  
مُحَمَّدٍ (عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ)، (وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ) كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ (وَعَلَى آلِ  
إِبْرَاهِيمَ)

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammadin 'Abdika wa  
Rasuulika, kamaa Swallayta 'alaa [aali] Ibraahiyma, wWa  
Baarik 'alaa Muhammadin ['Abdika wa Rasuulika], [wa 'alaa  
aali Muhammadin], kamaa Baarakta 'alaa Ibraahiyma [wa  
'alaa aali Ibraahiyma]*

“Ee Allaah! Mswalie Muhammad Mja Wako na Mjumbe Wako kama Ulivyowaswalia [jamaa zake] Ibraahiym, na Mbariki Muhammad [Mja Wako na Mjumbe Wako] [na jamaa zake Muhammad] kama Ulivyowabariki jamaa zake Ibraahiym [na jamaa zake Ibraahiym”]<sup>(591)</sup>

6-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ(عَلَى) أَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى (آلِ) إِبْرَاهِيمَ. وَ  
بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ (عَلَى) أَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى (آلِ) إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ  
مَجِيدٌ.

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammadin, wa ['alaa] azwaaajih  
wa dhurriyaatih, kamaa Swallayta 'alaa [aali] Ibraahiyma,  
wa Baarik 'alaa Muhammadin, wa ['alaa] azwaaajih wa  
dhurriyaatih, kamaa Baarakta 'alaa [aali] Ibraahiyma, Innaka  
Hamiydun Majiydun*

“Ee Allaah! Mswalie Muhammad na wake zake na kizazi chake, kama Ulivyowaswalia [jamaa zake] Ibraahiym, na Mbariki Muhammad na wake zake na kizazi chake kama

<sup>591</sup> Al-Bukhaariy, An-Nasaaiy, Atw-Twahaawiy, Ahmad na Ismaa'iy Al-Qaadhwi katika *Fadhwl asw-Swalaat 'alaa an-Nabbiyy* (صلى الله عليه وآله وسلم) (Uk. 28 Chapa ya mwanzo, Uk. Chapa ya pili ikiwa na utafiti wangu).

Ulivyowabariki [jamaa zake] Ibraahiym, hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu”.<sup>(592)</sup>

7-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ. وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ وَبَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَآلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammadin wa 'alaa aAl-Muhammaadin, wa Baarik 'alaa Muhammadin, wa 'alaa aAl-Muhammadin, kamaa Swallayta wa Baarakta 'alaa Ibraahiyma wa 'alaa aali Ibraahiyma Innaka Hamiydin Majiydun*

“Ee Allaah! Mswalie Muhammad na jamaa zake Muhammad, na Mbariki Muhammad na jamaa zake Muhammad kama Ulivyomswalia na Ukambariki Ibraahiym na jamaa zake Ibraahiym, hakika Wewe ni Mwenye Kusifika Mtukufu”.<sup>(593)</sup>

## Faida Muhimu Za Kumswalia Mtume Wa Ummah 'Swalaatu 'Alan Nabbiy

### Faida Ya Kwanza

Kinachoonekana ni kuwa nyingi katika hizi namna mbali mbali za kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), hakuna utajo wa Ibraahiym pekee bila ya jamaa zake, lakini imo ndani yake:

---

<sup>592</sup> Al-Bukhaariy, Muslim na An-Nasaaiy.

<sup>593</sup> An-Nasaaiy, Atw-Twahaawiy, Abu Sa'iyd bin Al-'Araabiy katika *Al-Mu'jam* (79/2) ikiwa na isnaad Swahiyh. Ibn al-Qayyim ametoa chanzo chake katika *Al-Jalaa Al-Afhaam* (Uk. 14-15) ya Muhammad bin Is-haaq As-Siraaj na akakiri kuwa ni Swahiyh. Kauli hii inajumuisha zote mbili 'Ibraahiym na jamaa zake Ibraahiym' jambo lililokanushwa na wote wawili; Ibn Al-Qayyim na Mwalimu wake Ibn Taymiyyah, kama ilivyoelezwa juu.

﴿ إِنَّ اللَّهَ أَصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴾



((Hakika Allaah Alimteua Aadam na Nuuh na kizazi cha Ibraahiym na kizazi cha 'Imraan juu ya walimwengu wote))<sup>594</sup>

﴿ إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَاصِبًا إِلَّا آءَالَ لُوطٍ حَجَّيْنَاهُمْ بِسَحَرٍ ﴾

((Hakika Sisi Tuliwapelekea kimbunga cha vijiwe, isipokuwa wafuasi wa Luutw. Hao Tuliwaokoa karibu na Alfajiri))<sup>595</sup>

Na katika hayo pia, ni kauli yake (صلى الله عليه وآله وسلم) : ((**Ee Allaah! Waswalie jamaa zake Abu Awfaa**)). Pia lipo tamshi la Ahlul-Bayt (watu wa nyumba), kama kauli ya Allaah (تعالى):

﴿ رَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ إِنَّهُ حَمِيدٌ مَّجِيدٌ ﴾

((Rehma ya Allaah na Baraka Zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii!))<sup>596</sup>

---

<sup>594</sup> Al-'Imraan 3:33

<sup>595</sup> Al-Qamar 54: 34.

<sup>596</sup> Huud 11: 73.

Hivyo basi Ibraahiym ni katika wao. (amejumuishwa katika 'jamaa zake Ibraahiym) "

Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah amesema:

"Na kwa sababu hiyo, ndio ikaja katika matamshi mengi: '*Kamaa Swallayt 'alaa Aali Ibraahiym'* [Kama Ulivyowaswalia jamaa zake Ibraahiym], na '*Kamaa Baarakta 'alaa Aali Ibraahiym'* [Kama Ulivyowabariki jamaa zake Ibraahiym]. Na ikaja katika baadhi yake Ibraahiym mwenyewe, na hii ni kwa kuwa, yeye ndiye shina katika Swalah na Utakaso, na waliobakia katika watu wa nyumbani kwake wanapata hayo kufuatana na hilo. Na imekuja katika baadhi yake kutaja haya, na hii ni kutanabahisha juu ya yote mawili.

Ukisha elewa hayo, kumezagaa maulizano baina ya Maulamaa kuhusiana na namna ya kushabihisha katika kauli yake: '*Kamaa Swallayta 'alaa... mpaka mwisho wake'* (kama Ulivyomswalia mpaka mwisho wake), kwani ki kawaida katika kushabihisha ni kuwa anayeshabihishwa huwa si bora kuliko anayeshabihishwa naye. Na kwa hakika, hali hii hapa ni kinyume kabisa na ile ya kawaida, kwani Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) ni mbora zaidi kuliko Ibraahiym, na kwa kuwa yeye ni mbora, basi Swalah zinazombwa zinakuwa ni bora zaidi kuliko Swalah zilizopatikana au zitakazopatikana. Maulaamaa wametoa majibu mengi kuhusu haya yanayopatikana katika *Fat-h Al-Baariy* na *Al-Jalaa al-Ifhaam*.

Majibu hayo yamefikia kumi. Baadhi yake ni dhaifu sana kupita kiasi kulinganisha na mengineyo, isipokuwa kauli moja tu ambayo ina nguvu na imependezeshwa na Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyyah na Ibn al-Qayyim kwa kusema ni nzuri. Nayo ni ile kauli ya aliyesema:

"Hakika kizazi cha Ibraahiym kinajumuisha Mitume ndani yake, Mitume ambao kama wao hakuna katika jamaa zake Muhammad. Hivyo, inapombwa Swalah kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na jamaa zake kama Swalah aliyoswaliwa Ibraahiym



Ibn Al-Qayyim amesema:

"Hii ni rai bora kuliko zote (za nyuma), na kilicho bora zaidi ya hii ni kusemwa kwamba Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) ni katika jamaa zake Ibraahiym, bali yeye ni mbora wao kama alivyosimulia 'Aliy bin Twalhah kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kuhusu kauli yake تعالى :

﴿ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴾



**((Hakika Allaah Alimteua Aadam na Nuuh na kizazi cha Ibraahiym na kizazi cha 'Imraan juu ya walimwengu wote))<sup>597</sup>**

Ibn 'Abbaas amesema:

"Muhammad ni katika jamaa zake Ibraahiym". Na hii ni Matini ikiwa wataingia Mitume wengine ambao ni vizazi vya Ibraahiym katika jamaa zake, basi kuingia kwa Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) kunafaa zaidi. Hivyo kauli yetu huwa: "... Kama Swallayta 'alaa ali Ibraahiym [kama Uliyowaswalia jamaa zake Ibraahiym]", inajumuisha kuswaliwa yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) na kuswaliwa Mitume wote

---

<sup>597</sup> Al-'Imraan 3: 33

Akasema: Wala hakuna shaka kwamba (jumla ya) Swalah wanayoipata jamaa zake Ibraahiym (pamoja) na Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) huwa pamoja nao ila Swalah iliyo bora zaidi na kamilifu kuliko zote huipata Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) pekee. Kwa hiyo, anayoombewa yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Swalah -kuswaliwa- ni hili jambo tukufu ambalo nalo ndilo lililo bora zaidi kuliko anayoombewa Ibraahiym bila ya shaka yo yote ile.

Na hapo ndipo inapodhihiri ile faida ya kushabihisha na kwamba inakwenda sambamba na asli -kawaida- yake, na kwamba Swalah anayoombewa yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa maneno haya ni ile iliyo tukufu na iliyo bora zaidi kuliko anayoombewa mwengine. Basi ikiwa kusudio la du'aa ni kuwa yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) kashabihiana na yule anayeshabihishwa naye na kwamba Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) anayo sehemu iliyo kubwa zaidi, basi huwa kwake yeye aliyeshabihishwa kusudio zaidi ya aliyopewa Ibraahiym na mwengineo.

Na ikiongezewa hayo ni kuwa yule aliyeshabihishwa naye anapata mambo ambayo hawayapati wengineo.

Kwa hivyo, imedhihirisha fadhila za Muhammad (صلى الله عليه) (صلى الله عليه وآله وسلم) na utukufu wake juu ya Ibraahiym na juu ya kila jamaa zake wakiwemo miongoni mwao Mitume kama anavyostahiki (utukufu). Ndio ikawa Swalah hii inathibitisha ubora huu na ni kitu kilichoshikamana naye. Na hivyo ndivyo itakiwavyo, kwani hayo ni katika masharti na matakwa yake.

*'Swalla Allaahu 'alayhi wa 'alaa aalihi wa Sallam Tasliyman kathyran, wa Jazaahu 'annaa afdhwal maa Jazaa Nabbiyyan 'an Ummatihi. Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad, kamaa Swallayta 'alaa aali Ibraahiym Innaka Hamiydum-Majiyd. Wa Baarik 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad kama Baarakta 'alaa aali Ibraahiym Innaka Hamiydum-Majiyd'.*

'Basi Allaah Amswalie pamoja na jamaa zake, na Amshushie amani juu yake, maamkizi mengi ya amani, na Ampe jazaa njema kutokana na sisi (du'aa zetu) jaza bora kuliko zote Alizompa Mtume yeyote kutokana na Ummah wake. Ee Allaah! Mswalie Muhammad na jamaa zake Muhammad kama Ulivyowaswalia jamaa zake Ibraahiym, hakika Wewe ni Mwenye kusifika Mtukufu. Na Mbariki Muhammad na jamaa zake Muhammad kama Ulivyowabariki jamaa zake Ibraahiym, hakika Wewe ni Mwenye kusifika Mtukufu.'

## Faida Ya Pili

Msomaji mtukufu ataona kwamba matamshi haya yote ya Swalah juu ya tofauti ya aina zake, yote yana kuswaliwa kwa jamaa zake Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), wake zake, kizazi chake pamoja na yeye mwenyEe (صلى الله عليه وآله وسلم). Kwa hiyo basi,

Na katika maajabu ya zama hizi na katika fujo za kielimu ni kuwa baadhi ya watu - naye ni Ustaadh Muhammad Is-'aaf An-Nashaashiyby katika kitabu chake 'Al-Islaamus-Swahiyh' (Uislamu Sahihi),- wana ushupavu wa kukanusha kuwaswalia jamaa zake Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) wakati wa kumswalia yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) juu ya kuthibiti hayo katika Swahiyhayn (Al-Bukhaariy na Muslim), na kwengineko na kutoka kwa kundi la Maswahaba mbali mbali wakiwemo Ka'ab bin 'Ujrah, Abu Humayd As-Saa'idy, Abu Sa'iyd Al-Khudriyy, Abu Mas'uud Al-Answaariy, Abu Hurayrah na Twalha bin 'Ubaydullaah. Na katika Hadiyth zao (imeonekana kwamba) walimuuliza Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم): "Vipi tukuswalie?" Akawafundisha (صلى الله عليه وآله وسلم) aina hizi. Na hoja ya An-Nashaashiyby katika kukanusha ni kwamba Allaah تعالى Hakutaja katika kauli Yake mtu mwingine yeyote yule pamoja na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم):

﴿ إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ

وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴾

**((Hakika Allaah na Malaika Wake wanamswalia Mtume. Enyi mliaoamini! Mswalieni na muombeani Rehma))<sup>598</sup>**

Kisha akaendelea kukanusha bali alipindukia mipaka katika kukanusha kwamba Maswahaba wamemuuliza (صلى الله عليه وآله) (swali kama hilo, kwa sababu ya maana ya 'Swalah' ilijulikana kwao, nayo ni 'du'aa'. Hivyo, itakuwaje wamuulize?!

Huku ni kuchanganyikiwa kuliko wazi kabisa, kwani swali lao - Maswahaba- halikuwa kuhusu maana ya kumswalia yeye (صلى) (صلى الله عليه وآله) hata akajibu alivyotaja, bali lilikuwa ni vipi kumswalia yeye (صلى الله عليه وآله وسلم), kama ilivyothibiti katika riwayah zote zilizotangulia kuashiriwa. Na wakati huo hapatokuwa na la kushangaza, kwani walimuuliza (صلى الله عليه) (صلى الله عليه وآله) kuhusu namna ya utekelezaji kishari'ah - kama ilivyo katika Shari'ah- jambo ambalo hawawezi kulielewa isipokuwa kwa njia ya uongofu kutoka kwa Mjuzi na Mwenye Hikima na Muwekaji wa Shari'ah. Na hii ni kama lau walimuuliza kuhusu vipi utekelezaji wa Swalah ya Faradhi kutokana na kauli ya Allaah تعالى:

﴿ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ ﴾

**((Na simamisheni Swalah))<sup>599</sup>**

---

<sup>598</sup> Al-Ahzaab: 56

Kwani elimu yao ya maana ya asili ya Swalah katika lugha haiwatoshelezi kuuliza kuhusu vipi unakuwa utekelezaji wake kishari'ah, na hii ni dhahiri kabisa.

Ama hoja yake -An-Nashaashiyby- iliyohusishwa si lolote, kwani ni jambo linaloelekea vizuri miongoni mwa Waislamu kwamba Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ndie mbainishaji wa maneno ya Mola wa Walimwengu kama Anavyosema:

﴿ وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴾

**((Nasi Tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kutafakari))<sup>600</sup>**

Hivyo Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) amebainisha wazi namna gani aswaliwe na ndani yake imejumuisha kutaja jamaa zake. Hivyo ni wajibu kukubali hivyo kutokana na yeye (صلى الله عليه وآله وسلم), na kwa kauli yake Allaah:

﴿ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ ... ﴾

**((Na anachokupeni Mtume chukueni, ...))<sup>601</sup>**

Na kwa kauli yake (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Hadiyth Swahiyh mash-huur<sup>(602)</sup>: **((Nimepewa Qur-aan pamoja na iliyofanana nayo)).<sup>(603)</sup>**

---

<sup>599</sup> Al Baqarah:110

<sup>600</sup> An-Nahl: 44

<sup>601</sup> Al-Hashr: 7

<sup>602</sup> Ni Hadiyth ambayo idadi ya wapokezi wake haijafikia idadi ya wapokezi wa Hadiyth ya *Mutawaatir*.

<sup>603</sup> Abu Daawuud na Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

Nashangazwa na wala sielewi ni nini hasa anachotaka kusema An-Nashaashiyby na kila aliyedanganyika na uongo wa maneno yake yenye majivuno. Itakuwaje kwa anaekanusha *Tashahhud* katika Swalah kabisa, au kukanusha mwanamke mwenye hedhi kuacha kuswali na kufunga akiwa katika masiku yake, yote kwa hoja kwamba Allaah (تعالى) Hakutaja *Tashahhud* kwenye Qur-aan; bali Ametaja kisimamo na kusujudu tu, na kwamba Yeye (تعالى) katika Qur-aan Hakumuondoshea mwanamke mwenye hedhi kuswali na kufunga, bali ni wajibu juu yake -mwenye hedhi- kuzitekeleza! Hivyo, wanakubali na hoja kama hizi ambazo zinakwenda sambamba na hoja zake za asili au sivyo. Je, wanakubaliana naye huyu mkanushaji katika kukanusha kwake, au wanapingana nae? Wakiwa wanakubaliana naye jambo ambalo hatulitarajii, basi watakuwa kwa uhakika wamepotea upotofu wa mbali, na wamefarikiana na Waislamu. Na ikiwa wanapingana naye, basi watakuwa wamewafikishwa na wamesibu na walichomjibu mkanushaji. Na sisi ndio jawabu letu kwa An-Nashaashiyby, na tumekubainishia hivyo.

Basi tahadhari Ee Muislamu kujaribu kufahamu Qur-aan bila ya kurejea kwenye Sunnah, kwani hakika hutoweza kufanya hivyo hata kama utakuwa katika lugha (Ya Kiarabu) ni Siybawayh<sup>(604)</sup> wa zama zako. Huu hapa mfano mbele yako. Huyu An-Nashaashiyby alikuwa ni mmoja kati ya Wataalamu bingwa na wakubwa wa lugha ya Kiarabu wa zama hizi, nawe unamuona namna alivyopotoka baada ya kughururika kwa elimu yake katika lugha bila ya kutafuta msaada wa Sunnah katika kuweza kuifahamu Qur-aan, bali yeye ameikanusha hiyo Sunnah kama unavyoelewa. Na kuna mifano mingi tu kwa haya tuyasemayo,

---

<sup>604</sup> Mwanasarufi mashuhuri na bingwa wa lugha ya Kiarabu katika karne ya pili Hijriyah.

lakini hakuna nafasi ya kuitaja, (lakini) na katika tuliyoyataja yatatosheleza. Na Allaah Ndie Muwafiqishaji.

### Faida Ya Tatu

Msomaji pia atagundua kuwa katika aina zote hizi za kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), hakuna neno la 'as siyad' (bwana), na kwa sababu hiyo Maulama waliokuja mwisho wamekhitilafiana kuhusu hukmu ya kuingiza neno hili - Sayyidinaa/Bwana wetu- katika Swalah ya Ibraahimiyyah. Kutokana na upungufu wa nafasi, hatutoingia katika kuchambua kauli wala kutaja waliokataa jambo hili kwa kushikamana na kufuata mafunzo kamili ya Mtume (صلى الله عليه) kwa Ummah wake alipoulizwa vipi kumswalia (صلى الله) (عليه وآله وسلم). Akajibu hali kuwa anaamrisha kwa kusema: **((Semeni, Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad..))**. Lakini napenda kuwanukulia wasomaji rai ya Al-Haafidhw Ibn Hajr Al-'Asqalaaniy katika hayo, tukizingatia kuwa yeye ni mmoja wa Maulamaa wakubwa wa Ki-Shaafi'iy waliokusanya baina ya Hadiyth na Fiqh. Imeenea kwa waliokuja mwisho katika ash-Shaafi'iyyah kwenda kinyume na mafunzo haya ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).

Al-Haafidhw Muhammad bin Muhammad bin Muhammad Al-Ghuraabiyy (790-835 AH) mwenziwe Ibn Hajr amesema na nimenukuu kutoka mswada wake.<sup>(605)</sup>

Aliulizwa (Ibn Hajr) - Allaah Atunufaishe kwa maisha yake - kuhusu namna ya kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Swalah au nje ya Swalah, sawa sawa kama imesemwa ni wajibu au inapendekezeka. Je, ni sharti mojawapo kuwa Mtume (صلى الله)

---

<sup>605</sup> Iliyohifadhiwa katika Maktaba ya *Adhw-Dhwaahiriyyah* Damascus.



(Ibn Hajr رضي الله عنه) akajibu:

"Ndio, kushikamana na matamshi yaliyopokewa, ndio ni bora zaidi, na wala pasisemwe kuwa labda Mtume (صلى الله عليه وآله) ameacha hivyo -hakujiita mwenyewe sayyid- kwa sababu ya unyenyekevu wake (صلى الله عليه وآله وسلم), kama alivyo الله (صلى الله عليه وآله وسلم) anapotaja jina lake, ingawa Ummah wake wamehimizwa kufanya hivyo kila anapotajwa (صلى الله عليه وآله وسلم). Kwani sisi tunasema, kama ingelikuwa hivyo ni bora, basi ingelipokelewa kutoka kwa Maswahaba kupitia Mataabi'yna, lakini hatukupata hata kukutana na cho chote kile katika yaliyopokewa kutokana na mmoja miongoni mwa Maswahaba wala Mataabi'yna waliowafuata. Akasema: Juu ya wingi wa hayo yaliyopokewa kutokana na wao kuhusiana na hilo. Na huyu hapa Imaam Ash-Shaafi'iy, Allaah Ampandishe daraja yake, ni miongoni mwa watu wenye kumuheshimu Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) zaidi. Amesema katika utangulizi wa kitabu chake ambacho ni tegemezi kwa watu wa madhehebu yake: 'Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad...!' hadi mwisho wa ilipomfikisha juhudi yake, nayo ni kauli yake: 'kila wanapomkumbuka wanaomkumbuka, na kila wanapoghafilika kumkumbuka wanaoghafilika', kama kwamba ametoa hayo kutokana na Hadiyth Swahiyh ambayo ndani yake kuna: "Subhaana Allaahi 'adada Khalqih". Imethibiti kuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)

Al-Qaadhwi 'Iyaadhwi ameweka mlango katika namna za kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika kitabu chake Ash-Shifaa (Kitabu cha Tiba). Amenukuu ndani yake mapokezi mar-fuu'an -usimulizi wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) - kutoka kwa kundi la Maswahaba na Mataabi'iyin. Na hakuna katika yote hayo au kutoka kwa yeyote yule miongoni mwa Swahaba na wengineo tamshi la 'sayyidinaa'. Miongoni mwa hayo mapokezi ni:

a) Hadiyth ya 'Aliy kwamba alikuwa akiwafundisha namna ya kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa kusema:

اللَّهُمَّ دَاجِي الْمَدْحُورَاتِ وَبَارِي الْمَسْمُوكَاتِ اجْعَلْ سَوَابِقَ صَلَوَاتِكَ وَنَوَامِي بَرَكَاتِكَ زَائِدَ تَحَنُّنِكَ عَلَيَّ مُحَمَّدَ عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ الْفَاتِحِ لِمَا أُغْلِقُ

*Allaahumma Daahiy al-Mad-huwaat, wa Baari al-Masmuukaat, Ij-'Al-Sawaabiq Swalawaatak, wa Nawaamiy Barakaatak, wa Zaa'id Tahiyyaatak 'alaa Muhammad 'Abduka wa Rasuulak, Al-Faatih Limaa Ughliq'*

“Ee Allaah! Mtandazaji wa ardhi, Mwanzishi wa mbingu, Zijaalie Swalah Zako bora kabisa zilizojaa rutuba ya Baraka Zako na yote mema yaliyozidi, kwa Muhammad, Mja (wako) na Mjumbe (wako), mfunguaji wa yaliyofungwa”.

b) Na kutoka kwa 'Aliy pia, alikuwa akisema:

صلواتُ اللهِ البرِّ الرحيمِ والملائكةِ المقربينِ والنبِيِّينَ والصِدِّيقِينَ والشهداءِ الصَّالِحِينَ،  
وما سبح لك من شيء يا رب العالمين، على محمد بن عبد الله خاتم النبيين وإمام  
المتقين

*'Swalawaatu-LLaahil-Barrur-Rahiym, wal-Malaaikatil-Muqarrabiyn, wan-Nabbiyyiyn was-Swiddiyqiyn was-Shuhadaais-Swaalihiyn, wa Maa Sabaha Laka min shayin Yaa Rabbal-'Aalamiyn, 'alaa Muhammad Ibn 'Abdillaahi Khaatamin-Nabbiyyiyn wa Imaamil-Mutaqqiyn...' n.k.*

“Swalah za Allaah Mhisani Mkunjufu wa rehemu, na za Malaika walio karibu Naye, na Mtume na Wasema kweli na Mashahidi na watu wema, na kila kinachosababisha kwa ajili Yako ewe Mola wa walimwengu wote, juu ya Muhammad bin 'Abdillaah mwisho wa Manabii na kiongozi wa wamchao Mungu”.

c) Kutoka kwa 'Abdullaah bin Mas'uud ambaye alikuwa akisema:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ صَلَوَاتِكَ وَبَرَكَاتِكَ وَرَحْمَتَكَ عَلَى مُحَمَّدٍ إِمَامِ الْخَيْرِ وَرَسُولِ الرَّحْمَةِ  
*Allaahummaj'al Swalawaatika wa Barakaatik, wa Rahmataka 'alaa Muhammad 'Abdika wa Rasuulik, Imaamil-Khayr wa Rasuulir-Rahmah...*

“Ee Mola zijaalie Swalah Zako na Baraka Zako na Rehma Zako juu ya Muhammad kiongozi wa wema na Mtume wa Rehma”.

d) Kutoka kwa Hasan Al-Baswri ambaye alikuwa akisema:  
"Anayetaka kunywa katika kikombe kinachokata kiu kutoka hawdh (chemchem) ya Mustwafaa, aseme:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِهِ وَأَصْحَابِهِ وَأَزْوَاجِهِ وَأَوْلَادِهِ وَذُرِّيَّاتِهِ وَأَهْلِ بَيْتِهِ  
وَأَصْنَاهُ وَأَنْصَارِهِ وَأَشْيَاعِهِ وَمُحِبِّبِهِ

*'Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad wa 'alaa aailihi wa Aswahaabihi, wa azwaajihi, wa awlaadihi wa dhurriyaatihi wa ahli baytihi wa aswahaarihi wa answaarihi wa ashyaa'ihii wa muhibbihi'*

“Ee Mola Mswalie Muhammad na Aali zake na Swahaba zake na Wake zake na Wanawe na Vizazi vyake na Watu wa nyumba yake na Shemeji na wakwe zake na Waliomnusu na Wenzake na Wapenzi wake”

Hivyo ndivyo (Al-Qaadhiy 'Iyaadhw) alivyoandika katika Ash-Shifaa kuhusu namna ya kumswalia Mtume kutoka kwa Maswahaba na waliowafuatia na akataja mengineyo.

Ndio, imesimuliwa katika Hadiyth ya Ibn Mas'uud kwamba kumswalia kwake kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alikuwa akisema:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ فَضَائِلَ صَلَوَاتِكَ وَرَحْمَتِكَ وَبَرَكَاتِكَ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ

*'Allaahummaj'al fadhwaail Swalawaatika wa Rahmatika wa Barakaatika 'alaa Sayyidil-Mursaliyn...*

Imesimuliwa na Ibn Maajah, lakini isnaad yake ni dhaifu kwa hiyo Hadiyth ya 'Aliy iliyosimuliwa na At-Twabaraaniy ikiwa na isnaad inayokubalika inaongoza. Hadiyth hii ina maneno magumu ambayo nimeyataja na kuelezea katika kitabu *Fadhwal An-Nabbiy* (Ubora wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)) cha Abu al-Hasan bin Al-Faaris. Baadhi ya Mashaafi'iy wamesema kwamba mtu akiapa kwa kumswalia Swalah Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) Swalah bora kabisa ili kutekeleza kiapo chake iwe:

اللَّهُمَّ صَلِّ اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ كُلَّمَا ذَكَرَهُ الذَّاكِرُونَ وَسَهَا عَنْ ذِكْرِهِ الْعَافُونَ

*'Allaahuuma Swalli 'alaa Muhammad kullamaa dhakarahuudh-dhaakiruun, wa sahaa 'an dhikrihil-ghaafiluun'*

An-Nawawiy kasema: "Inayopasa kutekelezwa ni kusema:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ.....

*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad wa 'alaa aali Muhammad, kamaa Swallayta 'alaa Ibraahiym ...*

Maulamaa wengi wa mwishoni wamejibu hii, kwa kusema kwamba hakuna dalili inayothibitisha kuhusu aina mbili zilizotajwa kuhusu ubora katika usimulizi. Ama kuhusu maana basi ya mwanzo ndio bora.

Mas-ala haya ni mashuhuri katika vitabu vya Fiqh, na Maulamaa wote wa Fiqh waliozungumzia mas-ala haya kwa pamoja hawajanukuu neno la 'sayyid'. Ingelikuwa neno hili limependekezwa, lisingeliwakwepa wote hata wawe wameghafilika. Mazuri yote ni kufuata waliosimulia na Allaah Anajua zaidi"

Rai ya Ibn Hajr ya kutokukubali kumsifia Mtume (صلى الله عليه وآله) (وسلم) kwa 'usayyid' (ubwana) ni kutokana na amri ya Qur-aan, na hii pia ni rai ya Maulamaa wa Kihanafi. Ni rai ipasayo kufuatwa kwani ndio udhihirisho mkweli wa mapenzi yake (صلى الله عليه وآله وسلم),

﴿ قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ ﴾

**((Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Allaah basi nifuateni mimi, Allaah Atakupendeni))<sup>606</sup>**

---

<sup>606</sup> Aal-'Imraan 3: 31

Kwa sababu hii, Imaam An-Nawawiy amesmea katika Rawdhwatut-Twaalibiyn (1/265): "Swalah iliyo kamilifu kabisa ya kumswaliwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ni:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ

'*Allaahumma Swalli 'alaa Muhammad...* "

inayowafikiana aina ya 3 iliyotajwa ambayo haikutajwa sayyid.

### Faida Ya Nne

Itambulike kwamba aina ya 1 na ya 4 ndizo Mjume wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alizowafundisha Maswahaba walipomuuliza kuhusu vipi kumswalia, kwa hiyo hii imetumika kama ni dalili kwamba hizi ndizo bora kabisa za kumswalia kwani asingeliwachagulia au kujichagulia mwenyewe isipokuwa kilicho bora na utukufu. Imaam An-Nawawiy kama ilivyotajwa, amenukuu (katika *Radhwatut-Twaalibiyn*) kwamba kama mtu anataka kuapa kwa kumswalia Swalah bora kabisa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), basi haiwezi kutimizwa isipokuwa kwa njia hizi.

As-Subkiy ametoa sababu nyingine: "Yeyote anayemswalia kwa Swalah hizi basi amemswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa yakini na atakayemswalia kwa maneno mengine, ameingia katika mashaka au hakutimiza kumswalia kama ipasavyo kwa sababu waliuliza: "Vipi tukuswalie?" Alijibu: "Semeni: ...". Hivyo wakiilezea Swalah yao kwake kama kauli yao kadhaa na kadhaa. Hii imetajwa na Al-Haytamiy katika *Ad-Durr Al-Mandhwuud* (25/2) kisha akasema, (27/1) kwamba lengo linapatikana katika aina zote zilizokuja katika Ahaadiyth Swahiyh.

## Faida Ya Tano

Ijulikane kwamba sio sheria kuunganisha aina zote hizi kuwa ni aina moja ya Swalah, hali kadhalika *Tashahhud* zote zilizotolewa kabla, kwani hiyo itakuwa ni bid'ah (uzushi) katika Dini; Sunnah ni kusema mara hivi mara vile katika nyakati mbali mbali kama Shaykhul-Islam Ibn Taymiyyah alivyoelezea katika utafiti wake wa *Takbiyr* za 'Iyd mbili (*Majmuu' Al-Fataawa* 29/253/1)

## Faida Ya Sita

'Allaamah Swiddiyq Hasan Khaan amesema katika kitabu chake *Nuzuul Al-Abraar bil 'Ilm Al-Manthuur minal-Ad'iyah wal-Adkhaar*, baada ya kutoa Hadiyith nyingi kuhusu fadhila za kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na kukithiri katika kumswalia (Uk. 161):

"Hakuna shaka kwamba wengi miongoni mwa Waislamu wanaomswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) ni Ahlul-Hadiyith (wenye kufuata hadiyth sahihi) na wasimulizi wa Sunnah iliyotwahirika, kwani ni mojawapo wa kazi yao katika elimu hii sharifu kumswalia kablaa ya kila Hadiyith, kwa hiyo ndimi zao zimerutubika daima kwa kumtaja (صلى الله عليه وآله وسلم). Hakuna kitabu cha Sunnah au mkusanyo wa Hadiyith; ikiwa ni *Jaami'*, *Musnad*, *Mu'jam*, *Juz'u* n.k ila imekusanya maelfu ya Hadiyith, hata kilichokuwa cha chini yao kabisa kwa uzito; *Jaami' As-Saghiyr* cha As-Swuyutiy, kilichokuwa na Hadiyith elfu kumi na hivyo ndivyo ilivyo katika vitabu vyote vya elimu ya hadiyth. Hivyo hawa ni makundi waliookoka, na Jamaa wa Hadiyith ambao watakaokuwa karibu kabisa na Mjumbe wa

Namuomba Allaah Anifanye miongoni wa watu hawa wa Hadiyth, ambao ni miongoni mwa watu waliokaribu kabisa na Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) , na labda kitabu hiki kitakuwa ni ushahidi kwayo. Allaah Amerehemu Imaam Ahmad aliyesema:

Dini ya Muhammad iko katika usimulizi  
Kipando bora kwa vijana ni Sunnah athari zake  
Usizigeukie nyuma Hadiyth na watu wake  
Kwani rai ni usiku na Hadiyth ni mchana  
Kijana anaweza kuwa mjinga wa uongofu....  
Ingawa jua linang'ara katika mwanga wake!

### **Kusimama Kwa Ajili Ya Rak'ah Ya Tatu, Kisha Ya Nne**

Kisha, alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akinyanyuka kwa ajili ya Rak'ah ya tatu pamoja na *takbiyr*<sup>(607)</sup> na alimuamrisha

---

<sup>607</sup>Al-Bukhaariy na Muslim.



tangulia”

Na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) anaposimama kutoka kikao alisema *takbiyr*, kisha akasimama<sup>(608)</sup> na "Alikuwa akinyanyua (صلى الله عليه وآله وسلم)mikono yake<sup>(609)</sup> pamoja na *takbiyr* mara nyingine.

Na alikuwa anapotaka kusimama kwa ajili ya Rak'ah ya nne, akisema: ((*Allaahu Akbar*))<sup>(610)</sup> na alimuamrisha "aliyeswali vibaya" hivyo kama kabla na alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akinyanyua mikono yake<sup>(611)</sup> pamoja na *takbiyr* mara nyingine.

Alikuwa akiketi barabara juu ya mguu wake wa kushoto, kwa utulivu hadi kila mfupa ulirudi sehemu yake kisha akisimama, akijisaidia kwa mikono yake, alikunja ngumi<sup>(612)</sup> na kutegemea mikono yake katika kuinuka.<sup>(613)</sup>

Alikuwa akisoma Suratul-Faatihah kaitika Rak'ah zote mbili na alimuamrisha "aliyeswali vibaya" kufanya hivyo. Katika Swalah ya adhuhuri aliongeza mara nyingine Aayah chache kama ilivyoelezwa katika 'Kisomo cha Swalah ya Adhuhuri'.

### ***Qunuut An-Naazilah Katika Swalah Tano (Qunuut Wakati Waislamu Inapowafikia Janga, Au Maafa)***

---

<sup>608</sup>Abu Ya'alaah katika Musnad yake (284/2) ikiwa na isnaad nzuri. Imetolewa katika *Silsilat al-Ahaadiyih Asw-Swahiyhah* (604).

<sup>609</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

<sup>610</sup>Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>611</sup>Abu 'Awaanah na An-Nasaa'iy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>612</sup>Ina maana 'kama mtu anayekanda unga'.

<sup>613</sup> Al-Harbiy katika *Hadiyih Al-Ghariyb*. Maana yake inapatikana katika Al-Bukhaariy na Abu Daawuud. Ama kuhusu Hadiyih kuwa 'alimkataza mtu kujisaidia kwa mikono yake anapoinuka katika Swalah', ni Munkar na sio Swahiyh kama nilivyoelezea katika *Silsilat al-Ahaadityh adhw-Dhwa'iyfah* (967).

Alipotaka (صلى الله عليه وآله وسلم) kuomba dhidi ya mtu, au kumuomba mtu, alifanya *Qunuut* <sup>(614)</sup> katika Rak'ah ya mwisho baada ya rukuu, na baada ya kusema: '*Sami'a Allaahu Liman Hamidah, Allaahumma Rabbana lakal Hamd*'<sup>(615)</sup> "Aliomba kwa sauti"<sup>(616)</sup> "alinyanyua mikono"<sup>(617)</sup> "ya walionyuma yake walisema Aamiyn"<sup>(618)</sup>

"Alikuwa akifanya *Qunuut* katika Swalah zote tano"<sup>(619)</sup> lakini "hakuwa akifanya *Qunuut* humo ispokuwa alipoomba dhidi ya watu au kuwaomba watu"<sup>(620)</sup> Mfano, mara alisema: ((**Ee Allaah! Muokoe Al-Waliyd Ibn Al-Waliyd na Salamah Ibn Hishaam na 'Ayyaash Ibn Abi Rabiya'ah. Ee Allaah! Zidisha adhabu Yako kwa (kabila la) Mudhwar, na wajalie miaka (ya ukame) kama miaka ya Yuusuf. [Ee Allaah! Malaani Lahyaan na Ru'lan, na Dhakwaan, na 'Uswayyah waliomuasi Allaah na Mjumbe Wake]**))<sup>(621)</sup>

---

<sup>614</sup> "*Qunuut*" inabeba maana nyingi kama unyenyekevu na uchaji. Na ilivyokusudiwa hapa ni du'aa khaswa wakati wa kusimama katika Swalah.

<sup>615</sup> Al-Bukhaariy na Ahmad.

<sup>616</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni.

<sup>617</sup> Ahmad na Atw-Twabaraaniy ikiwa na isnaad Swahiyh. Kunyanyua mikono katika *Qunuut* ni madhehebu ya Ahmad na pia Is-haaq bin Raahawaih kama ilivyo katika Masaail ya Al-Marwazy (Uk. 23). Ama kufuta uso kwa mikono, hili halikuripotwa katika hali hii, hivyo ni bid'ah. Ama nje ya Swalah, haikusimuliwa kuwa ni Swahiyh. Yote yaliyosimuliwa kuhusu hili, ni dhaifu au dhaifu sana kama nilivyohakikisha katika *Dhwa'iyf Abi Daawuud* (2) na *Silsilat al-Ahaadiyith Asw-Swahiyhah* (597). Hii ndio maana Al-'Izz bin 'Abdis-Salaam amesema katika fatwa zake, "Mtu mjinga tu ndiye anayefanya" Taz. Kiambatisho 8.

<sup>618</sup> Abu Daawuud na Siraaj. Al-Haakim amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy na wengineo wamekubali.

<sup>619</sup> Abu Daawuud, Siraaj na Ad-Daaraqutwniyy ikiwa na isnaad mbili Hasan.

<sup>620</sup> Abu Khuzaymah katika Swahiyh yake (1/78/2) na Al-Khatwiyb katika Kitabu Al-*Qunuut* ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>621</sup> Al-Bukhaariy na Ahmad, ziada kutoka kwa Muslim.

Kisha "alikuwa akisema: 'Allaahu Akbar' anapomaliza *Qunuut* na kusujudu"<sup>(622)</sup>

### ***Qunuut* Katika Swalah Ya Witr**

"Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akifanya *Qunuut* katika Rak'ah za witiri kwenye Swalah ya Witr"<sup>(623)</sup> mara nyingine<sup>(624)</sup> na "alifanya kabla ya rukuu"<sup>(625)</sup>

Alimfundisha Al-Hasan bin 'Aliy (رضي الله عنه) kusema [baada ya kumaliza kisomo chake katika Witr]:

اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيمَنْ هَدَيْتَ، وَعَافِنِي فِيمَنْ عَافَيْتَ، وَتَوَلَّنِي فِيمَنْ تَوَلَّيْتَ، وَبَارِكْ لِي  
فِيمَا أَعْطَيْتَ، وَقِنِي شَرَّ مَا قَضَيْتَ، (فَ) إِنَّكَ تَقْضِي وَلَا يُقْضَى عَلَيْكَ، (وَ) إِنَّهُ لَا

---

<sup>622</sup> An-Nasaaiy, Ahmad, Siraaj (109/1) na Abu Ya'laa katika Musnad yake ikiwa na isnaad nzuri.

<sup>623</sup> Ibn Naswr na Ad-Daaraqutwniy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>624</sup> Tumesema, "... Mara nyingine", kwa sababu Maswahaba waliosimulia Swalah ya Witr, hawakutaja *Qunuut* humo, kwani ingelikuwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) alifanya daima humo wangelitaja wote. Lakini 'Ubayy Ibn Ka'ab pekee amesimulia *Qunuut* katika Witr, hivyo inaonyesha kwamba alikuwa akifanya mara nyingine. Kwa hiyo, ni dalili kwamba *Qunuut* katika Witr sio wajibu, na hii ni rai ya Maulamaa wengi. Kwa sababu hii, Mwanachuoni mtafiti wa Hanafi Ibn Al-Humaam, ametambua katika Fath Al-Qadiyr (1/306/ 359, 360) kwamba rai ya kuwa ni wajibu haikuthibiti kwa dalili na ni dhaifu. Na hivi ni katika kusahilisha mambo na sio kufanya magumu, kwani rai hii aliyoipa nguvu ni kinyume na madhehebu yake.

<sup>625</sup> Ibn Abi Shaybah (12/41/1), Abu Daawuud, An-Nasaaiy katika Sunan Al-Kubraa (218/1-2), Ahmad, At-Twabaraaniy, Al-Bayhaqiyy na Ibn 'Aasakir (4/244/1) amesimulia hii pamoja na du'aa inayofuatia, ikiwa na isnaad Swahiyh. Ibn Mandah amesimulia du'aa katika Tawhiyd (70/2) pekee ikiwa na isnaad tofauti ya Hasan. *Takhriyy* yake imetolewa katika *Al-Irwaa* (426).

*Allaahumma-hdiniy fiyman Hadayta, wa 'Aafiniy fiyman 'Aafayta, wa Tawallaniy fiyman Tawwallayt, wa Baarik liy fiymaa A'twayta, wa Qiniy sharra maa Qadhwayta, [fa] Innaka Taqdhwiyy wa laa yuqdhwaa 'Alayka, [wa] innahu la yadhwillu man Walayta, (wa laa yai'izzu man 'Aadayta) Tabarakta Rabbanaa wa Ta'aalayta [La manjaa Minka illa Ilayka]*

“Ee Allaah, Niongoze pamoja na Uliowaongoza, na Unipe afya njema pamoja na Uliowapa afaya njema, na Nifanye kuwa ni mpenzi Wako pamoja na Uliowafanya wapenzi na Nibariki katika Ulichonipa na Nikinge na shari ya Ulilolihukumu kwani] Wewe Unahukumu wala Huhukumiwi. [Na] Hakika hadhaliliki Uliemfanya mpenzi [wala hatukuki Uliyemfanya adui] Umetakasika Ee Mola wetu na Umetukuka [Hakuna mahali pa kuokoka isipokuwa Kwako]”<sup>(626)</sup>

---

<sup>626</sup> Ibn Khuzaymah (1/119/2) na pia Ibn Abi Shaybah n.k kwa Hadiyith ya mwisho.

#### **TANBIHI:**

An-Nasaa'iy ameongeza katika mwisho wa *Qunuut*: ‘Wa Swalla Allaahu ‘alaan-Nabbiyyil-Ummiyy’ (Allaah Amswalie Mtume asiyejua kusoma na kuandika), imesimuliwa ikiwa na isnaad Dhwa’iyf. Miongoni mwa waliokiri ni dhaifu ni Ibn Hajr Al-‘Asqalaaniy na Az-Zurqaaniy. Hivyo hatukuitia katika muundo wetu wa kuunganisha usimulizi unaokubalika. Al-‘Izz bin ‘Abdus-Salaam amesema katika Al-Fataawa (66/1/19): “Kumswalia Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) katika *Qunuut* sio sahihi, wala haifai kuongeza kitu katika Swalah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kwa vyovyote. Rai hii inaonyehsa kwamba hakuipanua kwa hoja ya kuingiza fikra ya bid’ah hasanah (uzushi mzuri) kama Maulamaa wa mwishoni wanavyodai. Lakini, imethibitika katika Hadiyith kuhusu ‘Ubayy bin Ka’ab akiswalisha watu katika Swalah za masiku ya Ramadhaan kwamba alikuwa akimswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika mwisho

## Tashahhud Ya Mwisho

### Wajibu Wa Tashahhud Hii

Kisha baada ya kumaliza Rak'ah ya nne, alikuwa (صلى الله عليه وآله) (صلى الله عليه وآله وسلم) akikaa kwa ajili ya Tashahhud ya mwisho. Aliwaamrisha kuhusu hii na akifanya kama alivyofanya katika Tashahhud ya kwanza isipokuwa "alika mutawarrikan"<sup>(627)</sup> "paja lake la kushoto likiwa ardhini na miguu yake yote miwili ikitokeza kutoka upande mmoja (yaani upande wa kulia)"<sup>(628)</sup> "Aliweka mguu wake wa kushoto chini ya paja (la kulia) na muundi"<sup>(629)</sup> "mguu wake wa kulia akiuinua"<sup>(630)</sup> au mara nyingine "akiulaza pamoja ardhini"<sup>(631)</sup> "paja lake la kushoto lilifunika goti lake (kushoto) akiliegemeza"<sup>(632)</sup>

Ameweka mfano wa kumswalia yeye (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Tashahhud, kama Tashahhud ya kwanza. Njia za kumswalia (صلى الله عليه وآله وسلم) zimetajwa kabla katika sehemu yake.

---

<sup>627</sup> Al-Bukhaariy.

<sup>628</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni. Ama katika Swalah ya rakaa mbili kama Alfajiri, Sunnah ni kukaa muftarishan. Tofauti hii imeelezwa kirefu kutoka kwa Imaam Ahmad katika *Masaail* ya Ibn Haaniy kutoka kwa Imaam Ahmad (Uk. 79)

<sup>629</sup> Abu Daawuud na Al-Bayhaqiyy ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>630</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

<sup>631</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni

<sup>632</sup> Kifungu kile kile kilichotajwa hapo mbeleni

### Wajibu Wa Kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)

Alimsikia mtu (صلى الله عليه وآله وسلم) akiomba du'aa bila ya kumtukuza Allaah تعالى, wala kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) hivyo akasema: **((Huyu mtu ameharakiza))**. Kisha akamwita na kumwambia yeye na wengineo: **((Anaposwali mmojawenu, aanze kwa kumsifu Mola wake, (عزرجل) na kumtukuza kisha amswalie [katika usimulizi mmoja: amswalie Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) kisha aombe anayotaka]))**.<sup>(633)</sup>

Pia, "alimsikia mtu akimtukuza na kumsifu Allaah na kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Swalah, hivyo Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akamwambia: **((Omba na utaitikiwa, uliza utapewa))**"<sup>(634)</sup>

### Wajibu Wa Kujikinga Kutokana Na Mambo Manne Kabla Ya Kuomba Du'aa

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: **((Atakapomaliza mmoja wenu Tashahhud (ya mwisho) aombe kujikinga kwa Allaah kutokana na mambo manne: [aseme]:**

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ جَهَنَّمَ، وَمِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَمِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا  
وَالْمَمَاتِ، وَمِنْ شَرِّ الْمَسِيحِ الدَّجَالِ

---

<sup>633</sup>Ahmad, Abu Daawuud, Ibn Khuzaymah (1/83/2) na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh na Adh-Dhahabiy amekubali.

<sup>634</sup> An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh.

*“Allaahumma inniy a’uwdhu Bika min ‘adhaabi Jahannam, wamin ‘adhaabil qabri, wa min fitnatil mahyaa wal-mamaat, wamin sharri [fitnati]l masiyhid-Dajjal”*

“Ee Allaah, mimi najikinga Kwako] na adhabu za moto (wa Jahannam) na adhabu za kaburi na fitna ya uhai, na ya kufa, na shari ya [fitna] ya Masihi-dajjal)) [Kisha ajiombe mwenyewe kinachompata]<sup>(635)</sup> Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiomba (du’aa) katika *Tashahhud* yake”<sup>(636)</sup>

Pia alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akiwafundisha Maswahaba (رضي الله عنهم) hivyo kama alivyowafundisha Surah za Qur-aan”<sup>(637)</sup>

### **Kuomba (Du’aa) Kabla Ya Kutoa Salaam Na Aina Zake**

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) katika Swalah yake akiomba aina mbali mbali za du’aa.”<sup>(638)</sup> Akiomba wakati mwingine kwa du’aa hizi na wakati mwingine zile, na akazikubali du’aa nyingine na “akamuamrisha mwenye kuswali achague azipendazo”<sup>(639)</sup> Nazo ni:

---

<sup>635</sup> Muslim, Abu ‘Awaanah, An-Nasaaiy na Ibn Al-Jaruud katika Al-Muntaqaa (27). Imetolewa katika *Al-Irwaa* (350).

<sup>636</sup> Abu Daawuud na Ahmad ikiwa na isnaad Swahiyh.

<sup>637</sup> Muslim na Abu ‘Awaanah.

<sup>638</sup> Hatukusema “...katika *Tashahhud* yake”, kwa sababu matini ni “...katika Swalah yake”, bila ya kuelezea kama *Tashahhud* au sehemu nyingine. Hivyo inajumuisha sehemu zote zifaazo kwa du’aa mfano katika *Sujuud* na *Tashahhud*. Amri ya kuomba du’aa katika vikao viwili zimetajwa kabla.

<sup>639</sup> Al-Bukhaariy na Muslim. Amesema Al-Athram: “Nilimuuliza Ahmad: Niombe na nini baada ya *Tashahhud*? Akasema: Kama ilivyosimuliwa. Nikasema: Kwani Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) hakusema: ((Achague du’aa zozote azipendazo?)) Akasema: Achague katika zilizosimuliwa. Nikakariri swali, akasema: Kutoka zilizosimuliwa. Hii imenukuliwa na Ibn Taymiyyah (*Majmuu’a Al-Fataawa* 69/218/1),

1-

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَسِيحِ الدَّجَالِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْمَأْثَمِ وَالْمَغْرَمِ

*Allaahumma inniy a'uwduh Bika min 'adhaabil qabri, wa a'uwduh bika min fitnatil Masiyhid Dajaal wa a'uwduh bika min fitnatil mahyaa wal- mamaat, Allaahumma inniy 'a'uwduh bika minal ma-athami wal-maghrami*

“Ee Allaah! Hakika mimi najikinga Kwako kutokana na adhabu ya kaburi, na najikinga Kwako kutokana na fitna ya Masihid-dajjaal, na najikinda Kwako kutokana na fitna ya uhai na ya mauti, Ee Allaah, hakika mimi najikinda Kwako kutokana na dhambi<sup>(640)</sup> na deni<sup>(641)</sup> (642)

2-

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا عَمِلْتُ، وَمِنْ شَرِّ مَا لَمْ أَعْمَلْ (بَعْدُ)

*Allaahumma inniy a'uwduh Bika min sharri ma 'amiltu wamin sharri ma lam a'amal (ba'ad)*

---

<sup>640</sup> "Ma-tham" ni yale yanayomsababisha mtu kutenda dhambi au dhambi yenyewe.

<sup>641</sup> "Maghram" ni mzigo. Hapa ina maana deni kama ilivyothibiti katika Hadiyith nyingine ambayo 'Aaishah amesema: "Mtu alimwambia: "Kwa nini kila mara unajikinga kutokana na maghram ewe Mjumbe wa Allaah?" Akajibu: ((Hakika mtu anapokuwa na deni, husema uongo na anaaahidi na kuvunja ahadi yake)).

<sup>642</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.



“Ee Allaah, hakika mimi najikinga Kwako kutokanan na shari nilizozitenda na shari nisizozitenda<sup>(643)</sup> [bado]<sup>(644)</sup>”

3-

اللَّهُمَّ حَاسِبِنِي حِسَاباً يَسِيراً

*Allaahumma Haasibniy hisaabani yasiyran*

“Ee Allaah, nihesabie hisabu nyepesi”<sup>(645)</sup>

4-

اللَّهُمَّ بِعِلْمِكَ الْغَيْبِ وَقُدْرَتِكَ عَلَى الْخَلْقِ، أَحْيِنِي مَا عَلِمْتَ الْحَيَاةَ خَيْرًا لِي، وَتَوَفَّنِي إِذَا كَانَتِ الْوَفَاةَ خَيْرًا لِي، اللَّهُمَّ وَأَسْأَلُكَ خَشْيَتَكَ فِي الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ، وَأَسْأَلُكَ كَلِمَةَ الْحَقِّ (وَفِي رِوَايَةٍ: الْحُكْم) وَالْعَدْلَ فِي الْعُضْبِ وَالرِّضَى، وَأَسْأَلُكَ الْقَصْدَ فِي الْفَقْرِ وَالْغِنَى، وَأَسْأَلُكَ نَعِيمًا لَا يَبِيدُ، وَأَسْأَلُكَ قُرَّةَ عَيْنٍ (لَا تَنْفَدُ وَ) لَا تَنْقَطِعُ وَأَسْأَلُكَ الرِّضَى بَعْدَ الْقَضَاءِ، وَأَسْأَلُكَ بَرْدَ الْعَيْشِ بَعْدَ الْمَوْتِ، وَأَسْأَلُكَ لَذَّةَ النَّظَرِ إِلَى وَجْهِكَ (وَأَسْأَلُكَ) الشُّوقَ إِلَى لِقَائِكَ، فِي غَيْرِ ضَرَاءٍ مُضِرَّةٍ، وَلَا فِتْنَةٍ مُضِلَّةٍ، اللَّهُمَّ زَيِّنَا بِزِينَةِ الْإِيمَانِ، وَاجْعَلْنَا هُدَاةً مُهْتَدِينَ

*Allaahumma bi 'ilmikal-ghaybi, wa Qudratika ala khalqi. Ahyiniy maa 'alimtal-hayaata khayran liy wa Tawafaniy idhaa kaanatil wafaatu khayran liy. Allaahumma wa As-aluka Khashyataka fil ghaybi wash-shahaadah, wa As-aluka*

<sup>643</sup> Yaani kutokana na shari ya vitendo viovu nilivyovitenda, na kutokana na shari ya maovu ya kutokutenda vitendo vyema.

<sup>644</sup> An-Nasaaiy ikiwa na isnaad Swahiyh na Ibn Abi 'Aaswim katika kitabu

chake *As-Sunnah* (Namba. 370- ikiwa na utafiti wangu). Ziada ni kutoka kwake.

<sup>645</sup> Ahmad na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

*kalimatal haqqi, [al-hukmu], wal-'adla fil ghadhwabi war-ridhwaa, wa As-alukal qaswda fil faqri wal-ghinaa, wa As-aluka na'iyman laa yabiydu, wa As-aluka quratan 'aynin [laa tanfadhu wa] la tanqatwi'u, wa As-alukar-ridhwaa ba'dal-qadhwai, wa As-aluka bardal-'aysha ba'dal mawti, wa As-aluka ladhatan nadhwari ilaa Wajhika, wa [As-aluka] ash-shawqa ilaa Liqaaika, fiy ghayri dhwaraa'in mudhwirratin, wa la fitnaatin mudhwillah. Allaahumma Zayinnaa bi ziynatil iymaani, wa J'alnaa hudaatan muhtadiyn.*

“Ee Allaah, Kwa ujuzi Wako wa mambo yaliyofichikana, na uwezo Wako wa kuumba, niweke hai iwapo Unajua kwamba uhai ni bora kwangu, na nifishe iwapo kufa ni bora kwangu, Ee Allaah, nakuomba pia khofu yako kwa siri na dhahiri na ninakuomba neno la haki [na katika riwaaya: hukmu], na uadilifu wakati nimefurahi na wakati nimekasirika, na ninakuomba matumizi ya wastani wakati wa utajiri na wakati wa umaskini, na ninakuomba neema isiyokwisha na ninakuomba kituliza jicho (moyo) [kisicho toweka na] kisichokatika, na ninakuomba kuridhia baada yakuwa umeshanipangia, na ninakuomba maisha ya utulivu baada ya kufa, na ninakuomba ladha ya kukutizama uso Wako, [na nakuomba] shauku ya kukutana Nawe, pasina madhara yanayodhuru, wala fitna yenye kupoteza. Ee Allaah, Tupambe kwa kipambo cha imani, na Tujaalie tuwe waongozi wenye kuongoka”<sup>(646)</sup>

5- Amemfundisha Abu Bakr As-Swiddiyq (رضي الله عنه) kusema:

اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْمًا كَثِيرًا وَلَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ، فَاعْفِرْ لِي مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ وَارْحَمْنِي، إِنَّكَ أَنْتَ الْعَفْوُ الرَّحِيمُ

---

<sup>646</sup> An-Nasaaiy na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

*Allaahumma Inniy dhwalamtu nafsiy dhwalman kathiyran walaa yaghfirudh-dhunuuba illa Anta, fa-Ghfirliy maghfiratan min 'indika, wa-Rhamniy Innaka Antal-Ghafuurur-Rahiym*

“Ee Allaah, hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu, dhulma nyingi, na hasamehe madhambi ila Wewe, basi Nisamehe msamaha kutoka Kwako, na Unirehemu, hakika Wewe ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu”<sup>(647)</sup>

6- Amemuamrisha 'Aaishah (رضي الله عنها) aseme:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنَ الْخَيْرِ كُلِّهِ (عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ) مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الشَّرِّ كُلِّهِ، (عَاجِلِهِ وَآجِلِهِ) مَا عَلِمْتُ مِنْهُ وَمَا لَمْ أَعْلَمْ، وَأَسْأَلُكَ (وَفِي رَوَايَةٍ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ) الْجَنَّةَ وَمَا قَرَّبَ إِلَيْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّارِ وَمَا قَرَّبَ إِلَيْهَا مِنْ قَوْلٍ أَوْ عَمَلٍ، وَأَسْأَلُكَ (وَفِي رَوَايَةٍ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ) مِنَ (الْ) خَيْرِ مَا سَأَلَكَ عَبْدُكَ وَرَسُولُكَ (مُحَمَّدٌ وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا اسْتَعَاذَكَ مِنْهُ عَبْدُكَ وَرَسُولُكَ مُحَمَّدٌ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) (وَ أَسْأَلُكَ) مَا قَضَيْتَ لِي مِنْ أَمْرٍ أَنْ تَجْعَلَ عَاقِبَتَهُ (لِي) رُشْدًا

*Allaahumma inniy As-aluka minal-khayri kullihi 'aajilihi wa aajilihi maa `alimtu minhu wa maa lam a`lam, wa a`uwdhu Bika mina-sharri kullihi `aajilihi wa aajilihi maa `alimtu minhu wa maa lam a`lam. Wa As-aluka [Allaahumma inniy As-aluka] Al-Jannata wamaa qarraba ilayhaa bi qawlin au `amal. Wa a`uwdhu Bika minan-naari wamaa qarraba ilayhaa min qawlin au `amal. Wa As-aluka [Allaahumma inniy As-aluka] minal-khayri ma sa-alaka 'Abduka wa Rasuuluka Muhammadun, wa a`uwdhu Bika min sharri ma sta'aadhaka minhu 'Abduka wa Rasuuluka Muhammadun Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam. [Wa As-aluka] maa qadhwayta liy min amrin an Taj'ala 'aqibatahu [liy] rushdaa.*

<sup>647</sup> Al-Bukhaariy na Muslim.

“Ee Allaah hakika mimi nakuomba mema yote [karibu na mbali] ninayoyajua na nisyoyajua, na najikinga Kwako na shari zote [karibu na mbali] ninazozijua na nisizozijua, na nakuomba [na katika riwaaya: Ee Allaah hakika mimi nakuomba] Pepo na kila kauli au kitendo kinachokaribisha nayo, na najikinga Kwako na moto na kila kauli na kitendo kinachokaribisha nao, na nakuomba [na katika riwaaya: Ee Allaah, hakika hakika mimi nakuomba] kutokana na kheri alizokuomba Mja Wako na Mjumbe Wako [Muhammad na najikinga Kwako na shari alizojikinga nazo Mja Wako na Mjumbe Wako Muhammad SwallaLlaahu ‘alayhi wa sallam], [na nakuomba] kwa mambo yote uliyonikidhia Ujaalie matokeo yake [kwa ajili yangu] yawe ya uongofu<sup>(648)</sup>

7- Alimuuliza mtu: **((Unasema nini katika Swalah?))** Akasema: “Nakiri kwamba (yaani nashuhudia) kisha nauomba Allaah Pepo, na najikinga Naye kutokana na moto. Lakini Naapa, hakuna dandana (mnong’ono)<sup>(649)</sup> mzuri kama wako au wa Mu’aadh”. Hivyo akasema: **((Dandanah [mnong’ono] wetu ni kama wako))<sup>(650)</sup>**

8- Amemsikia mtu akisema katika *Tashahhud* yake:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ يَا اللَّهُ (وَفِي رِوَايَةٍ: بِاللَّهِ) (الْوَاحِدُ) الْأَحَدُ، الصَّمَدُ الَّذِي لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ، وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ - أَنْ تَغْفِرَ لِي ذُنُوبِي إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ  
*Allaahumma inniy As-aluka yaa Allaah [BiLlahi] [Al-Waahidu] Al-Ahad As-Swamadu Alladhiy lam Yalid walam*

---

<sup>648</sup> Ahmad, Atw-Twayaalisiy, Al-Bukhaariy katika *Al-Adaab Al-Mufrad*, IbnMaajah na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali. Nimetoa takhirij yake katika *Silsilat al-Ahaadiyith asw-Swahiyhah* (1542).

<sup>649</sup> "Dandanah" ni kusema kwa sauti ndogo isiyosikika, lakini maneno yasiyofahamika – katika hali hii ni maneno ya kimya ya du’aa. Kauli ya mwisho ina maana: “Maneno yetu ni kama yako”.

<sup>650</sup> Abu Daawuud, Ibn Maajah na Ibn Khuzaymah (1/87/1) ikiwa na isnaad Swahiyh.

*Yuwlad walam Yakun Lahu kufuwan ahad-an Taghfira liy dhunubiy Innaka Antal-Ghafuwrur Rahiym.*

“Ee Allaah! Hakika mimi nakuomba Ee Allaah, [na katika riwaayah: Naapa kwa Allaah] [Wewe ni Mmoja] Uliye Pekee, Mwenye kutegemewa kwa haja zote, Ambaye Hakuzaa wala Hakuzaliwa, na wala hakuna mfano Wake na kitu chochote, Unisamehe makosa yangu, hakika Wewe ni Mwingi wa Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.

Hii (صلى الله عليه وآله وسلم) alisema: ((**Amesamehewa, Amesamehewa**))<sup>(651)</sup>

9- Alimsikia mtu mwingine akisema katika *Tashahhud* yake:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِأَنَّ لَكَ الْحَمْدُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ (وَحَدَّكَ لَا شَرِيكَ لَكَ) (الْمَنَّانُ) (يَا)  
بَدِيْعَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ، يَا حَيُّ يَا قَيُّوْمُ (إِنِّي أَسْأَلُكَ) (الْجَنَّةَ  
وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّارِ)

*Allaahumma inniy As-aluka bianna Lakal-hamdu, laa ilaaha illa Anta [Wahdaka laa shariyika Lak], [Almannaan], [yaa] Badiy'a s-samawati wal-ardhwi, yaa Dhal-Jalaali wal-Ikraami, yaa Hayyu yaa Qayyuum, [inniy as-aluka] [al-Jannata, wa a'urdhu Bika minan-Naari]*

“Ee Allaah! Hakika mimi nakuomba, kwa vile sifa njema zote ni Zako, hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, [Peke Yako Huna mshirika] [mwingi wa kuneemesha]. [Ee] Mwanzishi (muumbaji) wa mbingu na ardhi, Ee mwenye Utukufu na Ukarimu, Ee Uliye Hai Mwenye kusimama kwa dhati Yako, [hakika mimi nakuomba] [Pepo, na najilinda Kwako kutokana na moto”].

---

<sup>651</sup> Abu Daawuud, An-Nasaaiy, Ahmad na Ibn Khuzaymah. Al-Haakim amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali.

Hivyo Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) akawaambia Maswahaba: **((Mnajua kaomba nini?))** Wakasema: “Allaah na Mjumbe Wake wanajua zaidi”. Akasema: **((Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, amemuomba Allaah kwa Jina Lake tukufu))**

[katika riwaaya nyingine: **Tukufu kabisa**]<sup>(652)</sup> **ambalo Anapoombwa Anajibu na Anapoombwa Hutoa**].<sup>(653)</sup>

10- Kitu cha mwisho alichokuwa akisema baina ya *Tashahhud* na *Tasliym* ilikuwa ni:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي مَا قَدَّمْتُ وَمَا أَخَّرْتُ، وَمَا أَسْرَرْتُ وَمَا أَعْلَنْتُ، وَمَا أَسْرَفْتُ، وَمَا  
أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي. أَنْتَ الْمُقَدِّمُ، وَأَنْتَ الْمُؤَخِّرُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ

*Allaahumma-Ghfirliyi maa qaddamtu wamaa akhartu, wa maa asrartu, wamaa a'lantu, wamaa asraftu, wamaa Anta A'lamu*

---

<sup>652</sup> Tawassul hii (kujikurubisha) kwa Allaah kwa kutumia Majina Yake mazuri na sifa Zake, ni amri ya Allaah تعالى ((وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا)) [Al-A'raaf 7: 180]. Ama kumuomba Allaah kwa kukurubia vitu vingine mfano, 'kwa kumtaja fulani na fulani' au 'kwa makarama ya fulani na fulani' au 'masharifu' n.k - matini ya Imaam Abu Haniyfaah (رحمه الله) na Maswahaba zake, wametaja kuwa desturi hii ni makruuh (inachukiza). Kwa ujumla imeharamishwa. Hivyo inasikitisha kwamba watu wengi miongoni mwao Mashaykh, wamedharau tawassul zilizokubaliwa-hutowasikia wakijikurubisha kwa Allaah kwa tawassul hizo, bali wamebobeza katika aina za tawassul za bid'ah ambazo angalau kwa uchache zinasemwa kuwa zimekhitilafiana - wanazidumisha kama kwamba nyinginezo hazifai. Shaykhul-Islam Ibn Taymiyyah ameandika makala ndefu kuhusu maudhui hii yenye kichwa cha habari: *At-Tawassul Wal-Wasiyilah* (Kujikurubisha kwa Allaah na njia zake) ipasayo kufuatwa, kwani ni muhimu sana hakuna mfano wake katika maudhui hii. Pia kuna makala yangu "*Tawassul Anwaa'uhaa wa Ahkaamuhaa*" ambayo pia ni muhimu katika maudhui yake na mfumo wake, na pia inakanusha shubuhaat mpya kutoka kwa baadhi ya Madaktari wa kisasa wa Dini. Allaah Atuongoze pamoja nao.

<sup>653</sup> Abu Daawud, An-Nasaaiy, Ahmad, Al-Bukhaariy katika *Al-Adaabu Al-Mufrad*, At-Twabaraaniy na Ibn Mandah katika *Tawhiyd* (44/2, 67/1, 70/1-2) ikiwa na isnaad Swahiyh.

*bihi minniy, Antal Muqaddimu, wa Antal Muakhiru, laa ilaaha illa Anta.*

“Ee Allaah! Nisamehe niliyoyatanguliza, na niliyoyachelewesha, na niliyoyafanya kisiri, na niliyoyafanya kwa dhahiri na niliyoruka mipaka, na ambayo Wewe Unayajua zaidi kuliko mimi, Wewe Ndiye Mwenye kutanguliza na Wewe Ndiye Mwenye kuchelewesha, hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe”.<sup>(654)</sup>

### **Tasliym (Kutoa Salaam)**

Kisha, “Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akitoa salaam upande wa kulia:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ

*Assalaamu 'Alaykum wa RahmatuLlaah*

“Amani na Rahma iwe juu yenu” (akigeuka hadi weupe wa shavu lake la kulia ukionekana)

Na upande wa kushoto:

---

<sup>654</sup> Muslim na Abu 'Awaanah.

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ

*Assalaamu 'Alaykum wa RahmatuLlaah*

“Amani na Rahma iwe juu yenu”

(Akigeuka hadi weupe wa shavu lake la kushoto ukionekana)”<sup>(655)</sup> Mara nyingine aliongeza katika maamkizi upande wa kulia:

وَبَرَكَاتُهُ

*Wa Barakaatuh*

...Na Baraka Zake (zishuke kwenu)<sup>(656)</sup>

"Aliposema

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ

*Assalaamu 'Alaykum wa RahmatuLlaahi*

“Amani na Rahma ya Allaah iwe juu yenu”

Upande wa kulia, alipunguza mara nyingine alipatoa salamu upande wa kushoto;

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ

*Assalaamu 'Alaykum*

“Amani iwe juu yenu”<sup>(657)</sup>

---

<sup>655</sup> Abu Daawuud, An-Nasaaiy na At-Tirmidhiy ambaye amekiri ni Swahiyh.

<sup>656</sup> Abu Daawuud na Ibn Khuzaymah (1/82/2) ikiwa na isnaad Swahiyh. 'Abdul-Haqq pia amekiri kuwa ni Swahiyh katika *Ahkaam* (56/2) kama alivyokiri An-Nawawiy na Ibn Hajr. Pia imesimuliwa kupitia njia nyingine na 'Abdur-Razzaaq katika *Muswannaf* (2/219). Abu Ya'ala katika *Musnad* yake (3/1253), At-Twabaraaniy katika *Mu'jam Al-Kabiy*r (3/67/2) na *Mu'jam Al-Awsawatw* (Namba: 4476 - Nambari zangu) na Ad-Daaraqutwniy.

<sup>657</sup> An-Nasaaiy, Ahmad na Siraaj ikiwa na isnaad Swahiyh.



Mara nyingine, "aliambia mara moja tu:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ

*Assalaamu 'Alaykum*

“Amani iwe juu yenu”

(Mbele ya uso wake akigeuza upande wake wa kulia kidogo) [au kidogo tu]<sup>(658)</sup>

"Walikuwa wakiashiria mikono yao walipotoa slaamu upande wa kulia na kushoto; Alipowaona Mjumbe wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alisema: ((Mna nini nyinyi? Mnaashiria mikono yenu kama kwamba ni mikia ya farasi mwitu?! Anapotoa salamu mmoja wenu, atazame mbele ya mwenziwe na sio kuashiria kwa mikono yake))

Hivyo waliposwali naye, hawakuashiria) [katika riwaaya nyingine: ((Inatosheleza kila mmoja wenu kuweka mkono wake pajani kisha kutoa slaamu kwa nduguye aliyoko upande wa kulia kwake au kushoto))<sup>(659)</sup>

---

<sup>658</sup> Ibn Khuzaymah, Al-Bayhaqi, Adh-Dhwiyya katika Al-Mukhtarah na 'Abdul-Ghaaniy Al-Maqdisiy katika Sunan yake (243/1) ikiwa na isnaad Swahiyh; Ahmad, At-Twabaraaniy katika *Mu'jam Al-Awsawatw* (32/2), Al-Bayhaqi, Ibn Al-Mulaqqin (29/1) na Al-Haakim ambaye amekiri ni Swahiyh, na Adh-Dhahabiy amekubali. *Takhriyy* yake imetolewa katika *Al-Irwaa Al-Ghaliyl* katika Hadiyth Namba 327.

<sup>659</sup> Muslim, Abu 'Awaanah, Siraaj, Ibn Khuzaymah na At-Twabaraaniy.

#### TANBIHI:

Ibaadhwiyyah wamegeuza Hadiyth hii. 'Aalim wao Rabiy' amesimulia katika Musnad isiyotegemewa ikiwa na kauli mbali mbali kuthibitisha rai zao kwamba kunyanyua mikono pamoja na *takbiyr* inatengua Swalah! Kauli hiyo ni uongo, kama nilivyoelezea katika *Adhw-Dhwa'iyfah* (6044).

## Wajibu Wa *Tasliym* (Kutoa Salaam)

Alikuwa (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ((...na inamalizika (yaani Swalah) kwa *Tasliym*))<sup>(660)</sup>

### Hitimisho

Yote yaliyotangulizwa humu kuhusu sifa ya Swalah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) yanawahusu wanamume na wanawake, na wala haikuthibiti katika Sunnah kwamba kuna baadhi ya mambo yanamtofautisha (inayomtenga) mwanamke, bali inahikisha kauli ya ujumla ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم): ((Swalini kama mlivyoniwa nikiswali)).

Hivyo imejumuisha wanawake wote, na kauli ya Ibraahiym An-Nakha'iy amesema: "Mwanamke anafanya kama anavyofanya mwanamume katika Swalah" [Imetoka kwa Ibn Abi Shaybah (1/75/2) ikiwa na isnaad Swahiyh kutoka kwake]

Al-Bukhaariy amesimulia katika At-Tariykh As-Saghiyr (Uk. 95) ikiwa na isnaad Swahiyh kutoka kwa Umm Ad-Dardaa: "Alikuwa akikaa katika Swalah yake kikao cha wanaume na alikuwa ni faqihi"

Ama Hadiyth inayosema mwanamke ajikunje katika *Sujuud* na kwamba yeye sio sawa na mwanamume, ni Hadiyth Mursal haina hoja. [Amesimulia Abu Daawuud katika *Al-Maraasil*] (117/87) kutoka kwa Yaziyd Ibn Abi Habiyb ambaye ametolewa katika *Adh-Dwa'iyfah* (2652).

Ama ile aliyosimulia Imaam Ahmad katika Masaail (ya mwanawe) Ibn 'Abdullaah kutoka kwake, (Uk.71) kutoka kwa

---

<sup>660</sup> Al-Haakim, na Adh-Dhahabiy amekiri Swahiyh. Imeshatolewa kikamilifu katika '*Takbiyr*' ya kufungulia.

Ibn 'Umar kwamba alikuwa akiwaamrisha wanawake waketi kimarufaa, (hadithi hii) haisihi isnaad yake kwa sababu yumo 'Abdullaah bin Al-'Amriy ambaye dhaifu.

\*\*\*\*\*

Haya ndiyo yaliyowezekana kukusanya pamoja katika kuelezea Sifa Ya Swalah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) Kutoka *Takbiyr Hadi Tasliym*. Natumai kwamba Allaah Ataijaalia iwe yenye ikhlaasw mbele ya Uso Wake Mkarimu na uongofu kwa Sunnah ya Mtume Wake Raufur-Rahiym (...Mpole)

سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ أَسْتَغْفِرُكَ  
وَأَتُوبُ إِلَيْكَ. اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ. وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ  
مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ وَبَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَآلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

*Subhaana-Llaahi wa-Bihamdihi, Subhaanaka Llaahumma wa-Bihamdika, ash-hadu an laa ilaaha illa Anta, Astaghfiruka wa atuwbu Ilayka, Allaahumma swalliy 'alaa Muhammad, wa 'alaa aali Muhammad, wa Baarik 'alaa Muhammad, wa 'alaa aali Muhammad, kama Swallayta wa Baarakta 'alaa Ibraahiyma, wa aali Ibraahiyma, Innaka Hamiydum-Majiyd.*

“Ametakasika Allaah, na sifa njema zote ni zake. Kutakasika ni kwako Ee Allaah, na sifa njema zote ni Zako. Nakiri kwamba hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe, nakuomba msamaha na ninarejea Kwako.

Ee Allaah, Mswalie Muhammad na jamaa zake Muhammad, na Mbariki Muhammad na jamaa zake Muhammad kama Ulivyomswalia na Ukambariki Ibraahiym na jamaa zake Ibraahiym hakika Wewe ni mwenye kusifika Mtukufu”<sup>(661)</sup>

---

<sup>661</sup> Du'aa ya mwanzo ni du'aa kamili inayojulikana kama *Kaffaaratul-Majlis* (Kafara ya kikao): ((Atakayeisema katika mkusanyiko wa kumkumbuka (Allaah) itakuwa kama ni mhuri wa kuchapia, na atakayesema katika

## Vitabu Alivyotumia Mwandishi Kwa Marejeo

### A) Qur-aan

### B) Vitabu Vya Tafsiyr

2. Ibn Kathiyr (701-774 AH): *Tafsiyr al-Qur-aan al-`Adhwiym*, Chapa ya Muhammad Mustafa, 1365.

---

mkusanyiko wa maneno ya kipuuzi, itakuwa kama ni kafara yake)). [Imeripotiwa na Al-Haakim na Atw-Twabaaraniy ikiwa Swahiyh]. Du'aa ya pili ni Sunnah kumswalia Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Du'aa hizi mbili hivyo ni njia bora kabisa katika kutekeleza miongozo ya Kiislamu. ((Hapana watu wowote wale wanaokaa kikao chochote bila ya kumtaja Allaah, wala kumswalia Mtume ila itakuwa dhambi kwao, Allaah Akipenda Atawaadhibu, au Akipenda Atawasamehe)). [Imesimuliwa na At-Tirmidhy, Al-Haakim, Ahmad ikiwa Swahiyh] Taz. *Silsilat al-Ahaadiyth asw-Swahiyhah* cha Shaykh Al-Albaaniy (74/81) kwa maelezo.

### C) Vitabu Vya Hadiyth/Sunnah

3. Maalik bin Anas (93-179): *Al-Muwattwaa'*, Daar Ihyaa' Kutub al-`Arabiyyah, 1343.
4. Ibn al-Mubaarak, `Abdullaah (118-181): *Az-Zuhd*.
5. Muhammad bin al-Hasan Shaybaaniy (131-189): *Al-Muwattwa'*, *al-Mustafaa'i*, 1297.
6. Twayaalisiy (124-204): *Al-Musnad*, Daairah al-Ma`arif, Hyderabad Deccan, 1321.
7. `Abdur-Razzaaq bin Humaam (126-211): *Al-Amaaliy*.
8. Humaydiy, `Abdullah bin az-Zubayr (...-219): *Al-Musnad*.
9. Ibn Sa`d, Muhammad (168-230): *At-Twabaqaat al-Kubraa*, Ulaya.
10. Ibn Ma`iyn, Yahya (...-233): *Taariykh ar-Rijaal wal-`Ilal*.
11. Ahmad bin Hanbal (164-241): *Al-Musnad*, Chapa ya al-Maymaniyyah, 1313; Chapa ya al-Ma`arif, 1365.
12. Ibn Abi Shaybah, `Abdullaah bin Muhammad Abu Bakr (...-235): *Al-Muswannaf*.
13. Ad-Daarimiy (181-255): *As-Sunan*, Chapa ya al-I`tidaal, Damascus, 1349.

14. Al-Bukhaariy (194-256): *Al-Jaami` as-Swahiyyh*, Chapa ya al-Bahiyyah al-Misriyyah, 1348. Iliyochapwa na maelezo, *Fat-h Al-Baariy*.
15. Al-Bukhaariy (194-256): *Al-Adab al-Mufrad*, Chapa ya al-Khaliliy, India, 1306.
16. Al-Bukhaariy (194-256): *Khalq Afaal al-Ibaad*, Chapa ya al-Answaar, India.
17. Al-Bukhaariy (194-256): *At-Taariykh as-Swaghiyr*, India.
18. Al-Bukhaariy (194-256): *Juz' al-Qiraa'ah*.
19. Abu Daawuud (202-275): *As-Sunan*, Chapa ya at-Ta'aziah, 1349.
20. Muslim (204-261): *Asw-Swahiyyh*, Chapa ya Muhammad 'Aliy.
21. Ibn Maajah (209-273): *As-Sunan*, Chapa ya at-Taaziyah, 1349.
22. At-Tirmidhiy (209-279): *As-Sunan*, toleo. Ahmad Shaakir, Halab, 1356.
23. At-Tirmidhiy: *Shamaa'il Muhammadiyyah*, pamoja na maelezo ya 'Aliy al-Qaariy na `Abdur-Ra'uuf al-Manaawiy, Chapa ya al-Adabiyyah, Misr, 1317.
24. Al-Haarith bin Abi Usaamah (176-282): *Al-Musnad - Zawaaaiduh*.
25. Abu Is-haaq al-Harbi, Ibraahiym bin Is-haaq (198-285): *Ghariyb al-Hadiyth*.
26. Al-Bazaar, Abu Bakr Ahmad bin `Amr al-Basri (...-292): *Al-Musnad - Zawaaaiduh*.

27. Muhammad bin Nasr (202-294): *Qiyaam al-Layl*, Chapa ya Rifaah `Aamm, Lahore, 1320.
28. Ibn Khuzaymah (223-311): *Asw-Swahiyyh*, al-Maktab al-Islaamiy.
29. An-Nasaaiy (225-303): *As-unan - Al-Mujtabaa*, Chapa ya al-Maymaniyyah.
30. An-Nasaaiy: *As-Sunan al-Kubraa*.
31. Al-Qaasim al-Sarqastiy (255-302): *Ghariyb al-Hadiyth* au kwa jina lingine *ad-Dalaa'il*.
32. Ibn al-Jaarud (...-307): *Al-Muntaqaa*, Misri.
33. Abu Ya`laa al-Muusiyyiy (...-307): *Al-Musnad*.
34. Ar-Ruuyaani, Muhammad bin Haaruun (...-307): *Al-Musnad*.
35. Siraaj, Abul-`Abbaas Muhammad bin Ishaq (216-313): *Al-Musnad*, mijaladi kadhaa katika maktaba ya Dhwaahiriyyah, Damascus.
36. Abu `Awaanah (...-316): *Asw-Swahiyyh*, Daa'irah al-Ma`aarif, Hyderabad Deccan, 1326.
37. Ibn Abi Daawuud, `Abdullaah bin Sulaymaan (230-316): *Al-Maswaahif*.
38. Atw-Twahaawiy (239-321): *Sharh Ma`aani al-Aathaar*, al-Mustafaa'i, India, 1300.
39. Atw-Twahaawiy: *Mushkil al-Aathaar*, Daar al-Ma`aarif, India, 1333.
40. `Uqayliy, Muhammad bin `Amr (...-322): *Adh-Dhwu`afaa'*.

41. Ibn Abi Haatim (240-327): *Al-Jarh wat-Ta`diyl*, India.
42. Ibn Abi Haatim (240-327): *`Ilal-al-Hadiyth*, As-Salafiyyah, Misri, 1343.
43. Abu Ja`far al-Bukhturi, Muhammad bin `Amr ar-Razaaz (...-329): *Al-Amaaliy*.
44. Abu Sa`iyd bin al-A`raabi, Ahmad bin Ziyaad (246-340): *Al-Mu`jam*.
45. Ibn as-Sammaak, `Uthmaan bin Ahmad (...-344): *Hadiyth*.
46. Abul-`Abbaas al-Asamm, Muhammad bin Ya`quub (247-346): *Hadiyth*.
47. Ibn Hibbaan (...-354): *Asw-Swahiyyh*, Daar al-Ma`aarif, Misri.
48. Atw-Twabaraaniy (260-360): *Al-Mu`jam al-Kabiyr*, mijaladi kadhaa, Maktaba ya Dhwaahiriyyah, Damascus.
49. Atw-Twabaraaniy (260-360): *Al-Mu`jam al-Awsawat min al-jam` baynahu wa bayn as-Swaghiyr*.
50. Atw-Twabaraaniy (260-360): *Al-Mu`jam as-Swaghiyr*, Chapa ya al-Answaari, Delhi, 1311.
51. Abu Bakr al-Aajuriy (...-360): *Al-Arba`iyn*.
52. Abu Bakr al-Aajuriy (...-360): Aadaab Hamlah al-Qur-aan.
53. Ibn as-Sunni (...-364): *`Amal al-Yawm wal-Laylah*, Daa'irah al-Ma`aarif, India, 1315.
54. Abu ash-Shaykh Ibn Hayyaan (274-369): *Twabaqaat al-Isbahaaniyyiyn*.



55. Abu ash-Shaykh Ibn Hayyaan (274-369): *Maa Rawaahu Abu az-Zubayr `an Ghayr*.

56. Abu ash-Shaykh Ibn Hayyaan (274-369): *Akhlaaq an-Nabbiy* (صلى الله عليه وآله وسلم), Misr.

57. Ad-Daaraqutwniy (306-385): *As-Sunan*, India.

58. Al-Khattwaabiy (317-388): *Ma`aalim as-Sunan*, Answaar as-Sunnah, Misri.

59. Al-Mukhlis (305-393): *Al-Fawaa'id*, Maktaba ya Dhwaahiriyyah, Damascus.

60. Ibn Mandah, Abu `Abdillaah Muhammad bin Is-haaq (316-395): *At-Tawhiyd wa Ma`rifah Asmaa' Allaah Ta`aalaa*.

61. Al-Haakim (320-405): *Al-Mustadrak*, Daairah al-Ma`arif, Hyderabad, 1340.

62. Tammaam ar-Raaziyy (330-414): *Al-Fawaa'id*, kopi mbili zilizokamilika, Maktaba ya Dhwaahiriyyah, Damascus.

63. Sahmi, Hamzah bin Yuusuf al-Jurjaaniy (...-427): *Taariykh Jurjaan*.

64. Abu Nu`aym al-Isbahaaniy (336-430): *Akhbaar Iswbahaan*, kilichochapishwa Ulaya.

65. Ibn Bushraan (339-430): *Al-Amaaliy*, Maktaba ya Dhwaahiriyyah, Damascus.

66. Al-Bayhaqiy (384-458): *As-Sunan al-Kubraa*, Daa'irah al-Ma`arif, Hyderabad, 1352.

67. Al-Bayhaqiy (384-458): *Dalaail an-Nubuwwah*, Maktaba ya Ahmadiyyah, Halab.

68. Ibn `Abdil-Barr (368-463): *Jaami` Bayaan al-`Ilm wa Fadhwlih*, Chapa ya al-Muniyriyyah.
69. Ibn Mandah, Abul-Qaasim (381-470): *Ar-Radd `alaa man Yunfi al-Harf min al-Qur-aan*, Maktaba ya Dhwaahiriyyah, Damascus.
70. Al-Baajiy (403-477): *Sharh al-Muwattwaa'*.
71. `Abdul-Haqq al-Ishbiyliy (510-581): *Al-Ahkaam al-Kubraa*.
72. `Abdul-Haqq al-Ishbiyliy (510-581): *At-Tahajjud*.
73. Ibn al-Jawziy (510-597): *At-Tahqiq `alaa Masaa'il at-Ta`liyyq*.
74. Abu Hafsw al-Mu-adib, `Amr bin Muhammad (516-607): *Al-Muntaqaa min Amaali Abil-Qaasim as-Samarqndiy*.
75. `Abdul-Ghaniy bin `Abdil-Waahid al-Maqdisiy (541-600): *As-Sunan*.
76. Adh-Dhwiyyaa' al-Maqdisi (569-643): *Al-Ahaadiyth al-Mukhtaarah*, mijaladi kadhaa, Maktaba ya Dhwaahiriyyah, Damascus.
77. Adh-Dhwiyyaa' al-Maqdisi (569-643): *Al-Muntaqaa min al-Ahaadiyth as-Swihaah wal-Hisaan*.
78. Adh-Dhwiyyaa' al-Maqdisi (569-643): *Juz' fi Fadhwil al-Hadiyth wa Ahlih*.
79. Al-Mundhiriyy (581-656): *At-Targhiyb wat-Tarhiyb*, Chapa ya al-Muniyriyyah, Misr.
80. Az-Zayla`iy (...-762): *Naswb ar-Raayah*, Daar al-Ma'muun, Misri, 1357.
81. Ibn Kathiyr (701-774): *Jaami` al-Masaaniyd*.

82. Ibn al-Mulaqqin, Abu Hafsw `Amr bin Abil-Hasan (723-804): Khulaasah al-Badr al-Muniyr.
83. Al-`Iraaqiy (725-806): *Takhriy Ihyaa' Twaba' al-Halabiy*, Misri, 1346.
84. Al-`Iraaqiy (725-806): *Twarh at-Tathriyb*, Jam`iyyah an-Nashr wat-Ta-aliyf al-Azhariyyah, 1353.
85. Al-Haythamiy (735-807): *Majma` az-Zawaa'id*: Husaam ad-Diyn al-Qudsiy, 1352.
86. Al-Haythamiy (735-807): *Mawaarid adh-Dhwam'aan fiy Zawaa'id Ibn Hibbaan*, chapa ya Muhibud-Diyn.
87. Al-Haythamiy (735-807): *Zawaa'id al-Mu`jam as-Swaghiyr wal-Awswat lit-Twabaraaniy*.
88. Ibn Hajr al-`Asqalaaniy (773-852): *Takhriyj Ahaadiyth al-Hidaayah*, India.
89. Ibn Hajr al-`Asqalaaniy (773-852): *Talkhiysw al-Khabiyr*, Chapa ya al-Muniyriyyah.
90. Ibn Hajr al-`Asqalaaniy (773-852): *Fat-h Al-Baariy*, Chapa ya al-Bahiyyah.
91. Ibn Hajr al-`Asqalaaniy (773-852): *Al-Ahaadiyth al-`Aaliyaat*.
92. As-Suyuutwiyy (889-911): *Al-Jaami` al-Kabiyr*.
93. `Aliy al-Qaariy (...-1014): *Al-Ahaadiyth al-Mawdhwu`ah*, Istanbul.
94. Al-Manaawiy (952-1031): *Faydhw al-Qadiyr Sharh al-Jaami` asw-Swaghiyr*, Chapa ya Mustafa Muhammad.

95. Az-Zurqaaniy (1055-1122): *Sharh al-Mawaahib al-Ladunniyyah*, Misri.
96. Ash-Shawkaaniy (1171-1250): *Al-Fawaa'id al-Majmuu'ah fil-Ahaadiyith al-Mawdhwuuh*, India.
97. `Abdul-Hayy al-Laknawiy (1264-1304): *At-Ta'liyyq al-Mumajjid `alaa Muwattwa' Muhammad*, al-Mustafaa'i, 1297.
98. `Abdul-Hayy al-Laknawiy (1264-1304): *Al-Aathaar al-Marfuu'ah fil-Akhbaar al-Mawdhwuuh*, India.
99. Muhammad bin Sa`iyd al-Halbi (...-...): *Musalsalaat*.
100. Al-Albaaniy, Muhammad Naaswirud-Diyn: *Takhriyy Swifat asw-Swalaat an-Nabbiy*, chanzo cha asili cha kitabu hiki, kijulikanacho kama *al-Aswl*.
101. Al-Albaaniy, Muhammad Naaswirud-Diyn: *Irwaa' al-Ghaliyl fi Takhriyy Ahaadiyith Manaar as-Sabiyl*, mijaladi 8, al-Maktab al-Islaamiy.
102. Al-Albaaniy, Muhammad Naaswirud-Diyn: *Swahiyh Abi Daawuud*.
103. Al-Albaaniy, Muhammad Naaswirud-Diyn: *At-Ta'aliyyq `alaa Ahkaam `Abdil-Haqq*.
104. Al-Albaaniy, Muhammad Naaswirud-Diyn: *Takhriyy Ahaadiyith 'Sharh `Aqiydat atw-Twahaawiyyah'*, al-Maktab al-Islaamiy.
105. Al-Albaaniy, Muhammad Naaswirud-Diyn: *Silsilat al-Ahaadiyith adhw-Dhwa`iyfah*, mijaladi 4, al-Maktab al-Islaamiy.

## D) Vitabu Vya Fiqh

106. Maalik bin Anas (93-179): *Al-Mudawwaanah* (Fiqh ya Ki-Maalikiy), Chapa ya as-Sa`adah, 1323.
107. Ash-Shaafi`iy, Muhammad bin Idriys (150-204): *Al-Umm*, Chapa ya al-Amiyriyyah, 1321.
108. Al-Marwaziyy, Ishaq bin Mansuur (...-251): *Masaail al-Imaam Ahmad wa Ishaq bin Raahawayh*.
109. Ibn Haani, Ibraahiym Naisaaburiy (...-265): *Masaail al-Imaam Ahmad*.
110. Al-Muzaniy (175-264): *Mukhtaswar Fiqh ash-Shaafi`iy*.
111. Abu Daawuud (202-275): *Masaail al-Imaam Ahmad* (Fiqh ya Ki-Hanbaliy), al-Manaar, 1353.
112. `Abdullaah bin al-Imaam Ahmad (203-290): *Masaail al-Imaam Ahmad*.
113. Ibn Hazm (384-456): *Al-Muhallaa* (Fiqh ya Ki-Dhwaahiriyy), Chapa ya al-Muniyriyyah.
114. `Izz bin `Abd as-Salaam (578-660): *Al-Fataawaa*.
115. An-Nawawiy (631-686): *Al-Majmuu` Sharh al-Muhadhdhab* (Ki-Shaafi`iy), Chapa ya al-Muniyriyyah.
116. An-Nawawiy (631-686): *Rawdhwah at-Twaalibiyn* (Ki-Shaafi`iy), al-Maktab al-Islaamiy.

117. Ibn Taymiyyah (661-728): *Al-Fataawaa*, Chapa ya Farj ad-Diyn al-Kurdi.
118. Ibn Taymiyyah (661-728): *Min Kalaam lahu fit-Takbiyr fil-`Iydayn wa ghayruh*.
119. Ibn al-Qayyim (691-751): *I`laam al-Muwaqqi`iyn*.
120. As-Subkiy (683-756): *Al-Fataawaa* (Ki-Shaafi`iy).
121. Ibn al-Humaam (790-869): *Fat-h al-Qadiyr* (Ki-Hanafiy), toleo la Buulaaq.
122. Ibn `Abdil-Haadiy, Yuusuf (840-909): *Irshaad as-Saalik* (Ki-Hanbaliy).
123. Ibn `Abdil-Haadiy, Yuusuf (840-909): *Al-Furuu`* (Ki-Hanbaliy).
124. As-Suyuutwiyy (809-911): *Al-Haawiy lil-Fataawi* (Ki-Shaafi`iy), al-Qudsi.
125. Ibn Nujaym al-Misriy (...-970): *Al-Bahr ar-Raa'iq* (Ki-Hanafiy), Chapa ya al-`Ilmiyyah.
126. Ash-Sha`raaniy (898-973): *Al-Miyzaan* (Fiqh ya madhehebu manne).
127. Al-Haytamiy (909-973): *Ad-Durr al-Mandhuuud fis-Swalaat was-Salaam `alaa Swaahib al-Maqaam al-Mahmuud*.
128. Al-Haytamiy (909-973): *Asmaa al-Matwaalib*.
129. WaliyuLlaah ad-Dahlawiy (1110-1176): *Hujjat-uLlaah al-Baalighah*, al-Muniyrah.

130. Ibn `Aabidiyn (1151-1203): *Al-Haashiyah 'alaa ad-Durr al-Mukhtaar* (Ki-Hanafiy), Istanbul.
131. Ibn `Aabidiyn (1151-1203): *Haashiyah al-Bahr ar-Raa'iq* (Ki-Hanafiy).
132. Ibn `Aabidiyn (1151-1203): *Rasm al-Muftiy* (Ki-Hanafiy).
133. `Abdul-Hayy al-Laknawiy (1264-1304): *Imaam al-Kalaam fiymaa yata`allaq bil-Qiraa'ah Khalf al-Imaam*, Chapa ya Al-Baladi, India.
134. `Abdul-Hayy al-Laknawiy (1264-1304): *An-Naafi` al-Kabiyir liman Yutwaali` al-Jaami` asw-Swaghiyr*, Chapa ya Al-Yuusufi, India, 1349.

**E) Vitabu Vya Siyrah Ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) Na  
Taraajum (Historia Ya Wasimulizi Wa Hadiyth)**

135. Ibn Abi Haatim, `Abdur-Rahmaan (240-327): *Taqaddamah al-Ma`rifah li Kitaab al-Jarh wat-Ta`diyl*, India.
136. Ibn Hibbaan (...-354): *Ath-Thiqaat*.
137. Ibn `Adiy (277-365): *Al-Kaamil*.
138. Abu Nu`aym (336-430): *Hilyat al-Azwwiyaa'*, Chapa ya as-Sa`aadah, Misri, 1349.
139. Al-Khatwiyb Al-Baghdaadiy (392-463): *Taariykh Baghdaad*, Chapa ya as-Sa`aadah, Misr.

140. Ibn `Abdil-Barr (368-463): *Al-Intiqaa' fi Fadhwaa'il al-Fuqahaa'*.
141. Ibn `Asaakir (499-571): *Taariykh Dimashq*.
142. Ibn al-Jawziy (508-597): *Manaaqib al-Imaam Ahmad*, kimeshachapishwa.
143. Ibn al-Qayyim (691-751): *Zaad al-Ma`aad*, Chapa ya Muhammad `Aliy, 1353.
144. `Abdul-Qaadir al-Qurashiy (696-775): *Al-Jawaahir al-Madhwiyyah*, India.
145. Ibn Rajab al-Hanbaliy (736-795): *Dhayl atw-Twabaqaat*, Misri.
146. `Abdul-Hayy al-Laknawiy (1264-1304): *Al-Fawaa'id al-Bahiyyah fiy Taraajum al-Hanafiyyah*, Chapa ya as-Sa`adah, Misri, 1324.

## F) Vitabu Vya Lugha Ya Kiarabu

147. Ibn al-Athiyr (544-606): *An-Nihaayah fi Ghariyb al-Hadiyth wal-Athar*, Chapa ya al-`Uthmaaniyyah, Misri, 1311.
148. Ibn Mandhwuur (630-711): *Lisaan al-`Arab*, Daar Swaadir, Beirut, 1955 M.
149. Al-Fayruuz `Aabaadiy (729-817): *Al-Qaamuus al-Muhiytw*, chapa ya 3, 1353.



### G) Vitabu Vya Uswuul Al-Fiqh

150. Ibn Hazm (384-456): *Al-Ihkaam fi Uswuul al-Ahkaam*, Chapa ya as-Sa`aadah, Misri, 1345.

151. As-Subkiy (683-856): *Ma`naa Qawl ash-Shaafi`i al-Matwlabi, "idhaa swahhal-hadiyth fahuwa madh-habiy"*, Majmuu`ah ar-Rasaa'il al-Muniyriyyah.

152. Ibn al-Qayyim (691-856): *Badaa'i` al-Fawaa'id*, Chapa ya al-Muniyriyyah.

153. WaliyuLlaah ad-Dahlawiy (1110-1176): *Iqd al-Jiyd fi Ahkaam al-Ijtahaad wat-Taqliyd*, India.

154. Al-Fulaaniy (1166-1218): *Iyqaadhw al-Himam*, Chapa ya al-Muniyriyyah.

155. Az-Zurqaa', Shaykh Mustwafaa: *Al-Madkhal ilaa `Ilm Uswuul al-Fiqh*, kimechapishwa.

### H) Vitabu Vya Adhkaar

156. Ismaa`iyl al-Qaadhwiy al-Jahdhwamiy (199-282): *Fadhwl as-Swalaat `alaa an-Nabbiy* (صلى الله عليه وآله وسلم), pamoja na uhakiki wangu, Al-Maktab al-Islaamiy.

157. Ibn al-Qayyim (691-751): *Jalaa' al-Ifhaam fi as-Swalaat `alaa Khayr al-Anaam*, Chapa ya al-Muniyriyyah.

158. Swiddiyq Hasan Khaan (1248-1307): *Nuzul al-Abraar*, Chapa ya Al-Jawaaib.

## J) Vitabu Vinginevyo

159. Ibn Battwah, `Abdullaah bin Muhammad (304-387): *Al-Ibaanah `an Shariy`at al-Firqat an-Naajiyah*.

160. Abu `Amr ad-Daaniy, `Uthmaan bin Sa`iyd (371-444): *Al-Muktafaa fi Ma`rifah al-Waqf at-Taamm*.

161. Al-Khatwiyb al-Baghdaadiy (392-463): *Al-Ihtijaa' bi ash-Shaafi`iy fiymaa asnada ilayh....*

162. Al-Haraawiy, `Abdullaah bin Muhammad al-Answaariy (396-481): *Dhamm al-Kalaam wa Ahlah*.

163. Ibn al-Qayyim (691-751): *Shifaa al-`Aliyl fi Masaa'il al-Qadhwaaw' wal-Qadar wat-Ta`liyl*.

164. Al-Fayruuz `Aabaadiy (729-817): *Ar-Radd `alaa al-Mu`taridhw `alaa Ibn `Arabiy*.

